# MUUNDO NA RUWAZA YA VIVUMISHI KATIKA TUNGO ZA KIIMENTI

**KENNETH KINYUA THURANIRA**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Idara ya Lugha, Isimu na Utamaduni ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili.**

**CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA**

**2023**

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya stashahada au digrii.

Saini ________________ Tarehe_________________

Kenneth Kinyua Thuranira

AP04/JP/KE/3849/2017

### IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo kikuu.

Saini_____________________________ Tarehe_____________________

Dkt James Omari Ontieri

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Rongo

Saini_______________________________ Tarehe_____________________

Dkt Nancy K. Ayodi

Idara ya Lugha, Isimu na Utamaduni

Chuo Kikuu cha Maasai Mara

## HAKIMILIKI

© Kenneth Kinyua Thuranira 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupiga chapa, kutafsiri au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa mfumo wowote ule bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu mpendwa Anne K. Kinyua na wanangu wapendwa Linah Nkirote na Collins Murithi.

## SHUKRANI

Shukrani za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusoma hadi ngazi hii. Sina budi kuwashukuru wazazi wangu, Bw. Julius K. Thuranira (marehemu) na Bi. Georgina M. Thuranira kwa kunilea, kunisomesha na kunihamasisha kusomea shahada ya uzamifu.

Shukrani za kipekee ni kwa wasimamizi wangu na wahadhiri wangu, (marehemu) Prof. Mwenda Mukuthuria, Dkt James Ontieri na Dkt Nancy Ayodi kwa kuniongoza na kurekebisha kazi hii hadi ikafikia kiwango hiki bila kuchoka. Nawashukuru kwa hisani na mapenzi yenu mliyonionyesha na kunikwamua nilipokwama nikifanya kazi hii. Bila msaada wenu adhimu ndoto yangu ya kukamilisha shahada yangu isingalitimia. Pia, mlinifaa kwa kazi mbalimbali nilizorejelea katika utafiti huu. Napenda kuwashukuru wahadhiri wangu wengine ambao ni Prof. Miriam Mwita na Dkt Meitamei kwa kunitia moyo kuendelea na masomo nilipokosa ari ya kuendelea nayo, pamoja na kuniongoza katika masomo ya shahada yangu ya uzamifu.

Nawajibika kumshukuru kwa dhati sana, marehemu Profesa Mwenda Mukuthuria kwa kunitia moyo katika masomo yangu na kwa kunisaidia kupata kazi mbalimbali za kurejelea zilizonifanya kupiga hatua katika utafiti wangu. Kamwe, siwezi kuwasahau wazamifu wenzangu ambao tulifaana kwa mengi. Hawa ni Japheth Ndolo, Nelly Kitonga, Esther Nthenya na Agnes Mulewa kwa kunisaidia kwa mawaidha, makala, majarida na kazi zinginezo nilipokuwa nikisoma. Mlinitia moyo nikapata ghera kuendelea na masomo yangu na kuyakamilisha.

Vilevile nawashukuru ndugu zangu ambao walinifaa kwa hali na mali katika masomo yangu. Hawa ni Jane C. Mwendwa, James E. Kimathi (marehemu), Dkt. Martin A. Mwenda (marehemu), Nicholas R. Kinoti (marehemu) na Mary A. Kirumba. Siwezi kumsahau mke wangu, Ann K. Kinyua na watoto wangu Linah Nkirote na Collins Murithi kwa kunivumilia nilipokuwa nikifanya kazi hii. Nawashukuru kwa kujitwika baadhi ya majukumu yangu ili kuendeleza familia wakati wote nilipokuwa nikifanya utafiti.

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia muundo na ruwaza ya kivumishi cha lahaja ya Kiimenti kinapotumika katika tungo za Kiimenti. Kiimenti ni lahaja mojawapo ya lugha ya Kimeru inayozungumzwa katika kaunti za Meru na Tharaka Nithi. Lahaja hii haijafanyiwa utafiti mwingi. Kwa hivyo, utafiti huu ni jitihada za kuongezea maarifa katika lahaja hii. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha aina za vivumishi katika lahaja ya Kiimenti; kuchunguza miundo ya vivumishi vya Kiimenti na jinsi usarufi unavyowakilishwa katika maumbo ya vivumishi; kupambanua ruwaza za usarufi katika vivumishi vya Kiimenti na kutathmini sheria za mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi (Chomsky, 1957; 1965) na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (Hooper, 1976). Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi ilisaidia kuchanganua maumbo ya vivumishi kimofemiki huku miundo ya nje na ndani ya vivumishi husika ikichunguzwa. Vivumishi vya Kiimenti hupitia michakato mingi ya kifonolojia vinapodhihirisha muundo wa nje kutoka muundo wa ndani. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilitumika kuchunguza michakato hiyo na sheria zinazohusika. Uchunguzi wa nyanjani na maktabani ulifanyika. Nyanjani, utafiti ulifanywa katika wadi ya Abothũgũchi ya Magharibi katika kaunti ndogo ya Meru ya Kati. Mbinu ya sampuli makusudi ilitumiwa kuteua eneo la utafiti na wasailiwa walioshirikishwa katika utafiti huu. Walengwa wa utafiti huu walikuwa wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti ili kuhakikisha uthabiti wa data. Mtafiti alihudhuria mikutano ya machifu, kanisa na ya wazazi shuleni ili kukusanya data ya vivumishi ambayo ilichanganuliwa. Mbinu za utafiti zilizotumiwa ni kurekodi mazungumzo ya wasailiwa katika mikutano hii kwa kutumia kalamu na karatasi pamoja na kinasa sauti cha rununu. Aidha, tasnifu, makala mahsusi na vitabu hasa vya hadithi katika lahaja ya Kiimenti na vingine vilivyohusu mada ya utafiti huu vilisomwa katika maktaba za vyuo vikuu vya Kenyatta, Nairobi, Moi, Egerton na Chuka. Kazi zaidi zilisomwa katika maktaba ya Wizara ya Elimu iliyoko jijini Nairobi ambapo tasnifu nyingi za vyuo vikuu mbalimbali zimehifadhiwa. Data ya vivumishi vya Kiimenti iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kupanga aina mbalimbali za vivumishi katika majedwali na kuondoa uradidi uliojitokeza. Kisha vivumishi husika vilifanyiwa unukuzi wa kifonetiki na kutafsiriwa. Aidha, vilichanganuliwa ili kuamua utendakazi wa kisarufi ulioainishwa. Hatua nyingine ilihusu kupangilia sentensi zenye mpangilio sawa wa vivumishi pamoja na kuzifanyia unukuzi wa kifonetiki. Kisha zilitafsiriwa na sheria kuandikwa zilizodhibiti kila ruwaza ya vivumishi katika sentensi. Utafiti ulibainisha kuwa kivumishi cha Kiimenti huwasilisha muundo mahsusi wenye mofimu zinazotekeleza kazi za kisarufi. Inatarajiwa kwamba utafiti huu utakuwa mchango mkubwa wa kiisimu kwa kuwasaidia wanafunzi, walimu na watafiti wengine wakichunguza lugha za kiasili. Pia, utafiti utasaidia katika uhifadhi wa lahaja ya Kiimenti kwa vizazi vijavyo.

## ABSTRACT

This research investigated the adjective structure of Kiimenti dialect and inherent patterns arising from its arrangement when used in sentences together with other adjectives. Kiimenti is one of the major dialects of Kimeru language which is spoken in counties of Meru and Tharaka Nithi. To date, few scientific studies have been done on this dialect. Hence, the impetus to initialize this study. The main objectives of this study were to investigate the types of adjectives found in Kiimenti dialect; to investigate structure of Kiimenti adjectives and grammatical categories marked in them; to identify pattern of morpheme arrangement marked in Kiimenti adjective and lastly to analyse rules that guide arrangement of Kiimenti adjectives when they are used in sentences. Transformation Generative Theory proposed by Noam Chomsky (1957; 1965) is one of the theories that informed this study. This theory was preferred because it assisted in analyzing the surface and deep structures of the adjectives by use of morphemic analysis. Natural Generative Phonology theory (Hooper, 1976) was also used in this study to assist in analysing phonological processes that affect the structure of Kiimenti adjectives. Later phonological rules which are inherent in each process were written. Kiimenti dialect speakers are found in Abothũgũchi West Ward of Imenti Central Sub County in Meru County which was purposively selected for this study because of limited interferences from other Kimeru dialects. The study targeted Kiimenti dialect speakers so as to enhance data validity. Data for this research was collected in the context of public meetings which included parents' meetings in selected primary schools, chiefs meetings and church gatherings where lengthy discussions feature. Methods used to collect data in these meetings comprised of note taking on Kiimenti dialect adjectives and their arrangement in various sentences. The researcher also used his own mobile phone to record discussions in these meetings. To gather more data, the researcher visited various university libraries like Kenyatta, Nairobi, Moi, Egerton and Chuka where theses, journals and books relevant to the study were read. Also, story books and other Kiimenti works were read from these libraries. More research works were read from Ministry of Education library in Nairobi where theses from various universities are preserved. Data collected was used to arrange Kiimenti adjectives into tables, each table comprising of one type of adjective. Then duplicated adjecties were removed; the ones left were phonetically transcribed and interpreted. Lastly they were analysed to determine grammatical categories marked in them and rules guiding arrangement of grammatical categories written. On the other hand Kiimenti sentences with the same arrangement of adjectives were grouped together, transcribed and interpreted. An attempt was made to write rules that guided each arrangement of adjectives in similar sentences. The research found out that Kiimenti adjective has a structure that is marked by various grammatical cateogories. It is expected that the findings from this study will make great linguistic contribution by assisting students, teachers and researchers to carry out in-depth scientific studies on indigenous languages. Also, the research will assist in preserving Kiimenti dialect for posterity.

# YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** .......... **ii**

**UNGAMO** .......... **ii**

**IDHINI** .......... **ii**

**HAKIMILIKI** .......... **iii**

**TABARUKU** .......... **iv**

**SHUKRANI** .......... **v**

**IKISIRI** .......... **vii**

**ABSTRACT** .......... **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **xvii**

**ISHARA NA VIFUPISHO** .......... **xix**

1.7 Maelezo ya Istilahi .......... xxi

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**UTANGULIZI** .......... **1**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 3

1.4 Maswali ya Utafiti .......... 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 4

1.6 Upeo wa Utafiti .......... 5

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI** .......... **6**

2.1 Utangulizi .......... 6

2.2 Maana ya Kivumishi .......... 6

2.2.1 Kazi za Karne ya 20 na 21 Kuhusiana na Vivumishi .......... 8

2.2.2 Aina za vivumishi ........................................ 8
2.2.3 Miundo ya Vivumishi ........................................ 15
2.2.4 Usarufi Unaoainishwa katika Maneno mbalimbali ........................................ 27
2.2.5 Ruwaza ya Usarufi katika Maneno Mbalimbali ........................................ 30
2.2.6 Mpangilio wa vivumishi katika Tungo ........................................ 33
2.3 Misingi ya Nadharia ........................................ 40
2.3.1 Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi ........................................ 41
2.3.2 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ........................................ 46
2.3.3 Hitimisho ........................................ 50
**SURA YA TATU ........................................ 51**
**MBINU ZA UTAFITI ........................................ 51**
3.1 Utangulizi ........................................ 51
3.2 Muundo wa Utafiti ........................................ 51
3.3 Eneo la Utafiti ........................................ 51
3.4 Kundi Lengwa ........................................ 52
3.5 Uteuzi wa Sampuli ........................................ 53
3.6 Vifaa vya Utafiti ........................................ 53
3.7 Utafiti wa Awali ........................................ 54
3.8 Utegemeo ........................................ 55
3.9 Uthabiti ........................................ 55
3.10 Utafiti wa Maktabani ........................................ 55
3.11 Ukusanyaji wa Data Nyanjani ........................................ 56
3.12 Uchanganuzi wa Data ........................................ 58
3.13 Hitimisho ........................................ 60
**SURA YA NNE ........................................ 61**

**UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO........................................................ 61**
4.1 Utangulizi ........................................................................................... 61
4.2 Fonimu za Kiimenti.............................................................................. 61
4.2.1 Fonimu za Irabu ................................................................................ 62
4.2.2 Wakaa katika Irabu ........................................................................... 64
4.2.3 Fonimu za Nusu Irabu ...................................................................... 65
4.2.4 Fonimu za Konsonanti za Kiimenti ................................................. 65
4.3 Umuhimu wa Fonimu katika Lugha..................................................... 70
4.4 Miundo ya Silabi za Kiimenti .............................................................. 71
4.4.1 Irabu Pekee (I) .................................................................................. 72
4.4.2 Nusu Irabu (½ I) na Irabu (I) ............................................................ 73
4.4.3. Konsonanti (K) na Irabu (I) ............................................................. 73
4.4.4 Konsonanti (K), Konsonanti (K) na Irabu (I) ................................... 74
4.4.5 Konsonanti (K) Nusu Irabu (½I) na Irabu (I) ................................... 75
4.4.6 Konsonanti (K), Konsonanti (K), Nusu Irabu (½ I) na Irabu (I) .................... 75
4.5 Dhana ya Mofu...................................................................................... 76
4.5.1 Mofu, Alomofu na Mofimu katika Lahaja ya Kiimenti ................................ 77
4.5.2 Mofimu katika Lahaja ya Kiimenti .................................................. 78
4.5.3 Aina za Mofu katika Lahaja ya Kiimenti ......................................... 82
4.5.3.1 Mofu Huru katika Lahaja ya Kiimenti ........................................... 83
4.5.3.2 Mofu Funge katika Lahaja ya Kiimenti ......................................... 83
4.5.3.3 Mofu Tata katika Lahaja ya Kiimenti ............................................ 84
4.5.3.4 Mofu Mseto katika Lahaja ya Kiimenti ......................................... 85
4.5.3.5 Mofu Kapa katika Lahaja ya Kiimenti ........................................... 86
4.6 Dhana ya Mzizi katika lahaja ya Kiimenti .......................................... 87
4.6.1 Mizizi Huru katika Lahaja ya Kiimenti ............................................ 89

4.6.2 Mizizi Tegemezi katika Lahaja ya Kiimenti ................................................ 89
4.6.3 Miundo ya Mizizi ya Vivumishi vya Kiimenti............................................. 90
4.7 Uamilifu wa Viambishi katika Kivumishi cha Kiimenti...................................... 93
4.8 Aina ya Vivumishi vya Kiimenti ...................................................................... 102
4.8.1 Vivumishi vya Sifa ........................................................................................ 102
4.8.2 Vivumishi vya Idadi ....................................................................................... 103
4.8.2.1 Vivumishi vya idadi halisi ........................................................................ 104
4.8.2.2 Vivumishi vya idadi jumla......................................................................... 104
4.8.3 Vivumishi Viulizi ........................................................................................... 107
4.8.3.1 Mzizi wa kiulizi -ng'ana (kiasi /-ngapi)................................................ 107
4.8.3.2 Mzizi wa Kiulizi –rĩku (-ipi).............................................................. 108
4.8.3.3 Mzizi wa Kiulizi –au? (kina nani?)....................................................... 108
4.8.4 Vivumishi Vimilikishi ..................................................................................... 109
4.8.4.1 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya Kwanza ....................................... 110
4.8.4.2 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya pili ............................................... 111
4.8.4.3 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya Tatu ............................................. 111
4.8.5 Vivumishi vya Pekee ...................................................................................... 112
4.8.5.1 Mzizi –ngĩ [-nge] (-ingine) .................................................................. 112
4.8.5.2 Mzizi –ene [-ɛnɛ] (-enye)..................................................................... 113
4.8.5.3 Mzizi –ngwa [-ŋgwa] (-enyewe)........................................................... 113
4.8.5.4 Mzizi –nthe [-nθɛ] (-ote)..................................................................... 113
4.8.5.5 Mzizi -nka [-nka] (bila kuhusisha mtu/kitu/hali fulani)......................... 113
4.8.6 Vivumishi Viradidi ......................................................................................... 114
4.8.6.1 Viradidi Visisitizi.................................................................................. 114
4.8.6.2 Viradidi Vilinganishi ............................................................................ 115
4.9.7 Vivumishi Vionyeshi....................................................................................... 116
4.9.7.1 Vivumishi Vionyeshi vya Karibu ......................................................... 116
4.9.7.2 Vivumishi Vionyeshi vya Mbali kidogo................................................ 116
4.9.7.3 Vivumishi Vionyeshi vya mbali zaidi................................................... 116

4.10 Vivumishi vya A - unganifu ........ 116
4.10.1 Nomino, a –unganifu na nomino ........ 117
4.10.2 Nomino, a –unganifu na kitenzi ........ 117
4.10.3 Nomino, a –unganifu na kielezi ........ 117
4.11 Vivumishi vya Majina ........ 118
4.12 Vivumishi vya Mkopo ........ 118
4.13 Sifa za Vivumishi vya Kiimenti ........ 118
4.14 Uamilifu wa Vivumishi vya Lahaja ya Kiimenti ........ 120
4.15 Ngeli za Mofolojia za Lahaja ya Kiimenti ........ 126
4.16 Muundo ya Vivumishi vya Kiimenti ........ 136
4.16.1 Muundo wa Mzizi Pekee ........ 136
4.16.2 Muundo wa Viambishi Awali na Mzizi ........ 137
4.16.2.1 Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip+Mz) ........ 138
4.16.2.2 Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip+Kip+Mz) ........ 139
4.16.2.3 Muundo wa Vivumishi vya Pekee Katika Kiimenti. ........ 140
4.16.2.4 Muundo wa Vivumishi Vionyeshi Katika Kiimenti ........ 141
4.16.2.5 Muundo wa Vivumishi vya A – Unganifu vya Kiimenti ........ 143
4.16.2.6 Muundo wa Vivumishi Viulizi vya Kiimenti ........ 145
4.16.2.7 Muundo wa Vivumishi Vimilikishi vya Kiimenti ........ 145
4.16.2.8 Muundo wa Vivumishi vya Majina vya Kiimenti ........ 146
4.16.2.9 Muundo wa Vivumishi vya Sifa vya Kiimenti ........ 148
4.16.2.9.1 Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip + KiN + Mz) ........ 148
4.16.2.9.2 Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip+ Kip+Mz) ........ 151
4.16.3 Muundo wa Viashiria vya Karibu (VA+Mz+VT) ........ 153
4.17 Usarufi Unaobainika katika Vivumishi vya Kiimenti ........ 155
4.18 Ruwaza ya Mofimu katika Vivumishi vya Kiimenti ........ 165
4.19 Hitimisho ........ 171

**SURA YA TANO ... 172**

**MICHAKATO YA KIFONOLOJIA, MOFOLOJIA NA RUWAZA ZA VIVUMISHI KATIKA TUNGO ZA KIIMENTI ... 172**

5.1 Utangulizi ... 172

5.2 Michakato ya Kifonolojia inayoathiri Vivumishi vya Kiimenti ... 172

5.2.1 Uyeyushaji ... 173

5.2.2 Uimarikaji wa Fonimu ... 178

5.2.3 Usilimisho Nyuma ... 179

5.2.4 Udondoshaji wa Irabu ... 181

5.2.5 Udondoshaji na Uchopekaji wa Vokali ... 183

5.2.6 Mvutano wa Irabu ... 186

5.2.7 Uwiano wa Irabu ... 190

5.2.8 Udondoshaji wa Konsonanti ... 191

5.2.9 Uchopekaji wa Konsonanti ... 195

5.2.10 Ukaakaishaji ... 196

5.2.11 Sheria ya Dahl ... 197

5.3 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Kiimenti ... 200

5.3.1 Dhana ya Uradidi ... 200

5.3.2 Aina za Uradidi Katika Vivumishi vya Lahaja ya Kiimenti ... 201

5.3.2.1 Uradidi Kamili wa Vivumishi ... 202

5.3.2.2 Uradidi Nusu wa Vivumishi ... 203

5.3.3 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Sifa ... 208

5.3.4 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi Viashiria ... 210

5.3.5 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Pekee ... 211

5.3.6 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Idadi ... 213

5.3.7 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya mkopo ... 215

5.3.8 Dhima ya Uradidi katika Vivumishi vya Kiimenti......215
5.4 Uhusiano wa Fonetiki na Mofolojia katika Uchanganuzi wa Vivumishi vya Kiimenti......217
5.5 Ruwaza za Vivumishi Mbalimbali katika Tungo za Kiimenti......219
5.5.1 Ruwaza za Kivumishi cha Pekee na Kivumishi kingine......219
5.5.2 Ruwaza za Kimilikishi na Kivumishi Kingine......229
5.5.3 Ruwaza za Kivumishi cha Idadi na Kivumishi Kingine......235
5.5.4 Ruwaza za Kiulizi na Kivumishi Kingine......242
5.5.5 Ruwaza za Kivumishi cha Sifa na Kivumishi Kingine......244
5.5.6 Ruwaza za Kivumishi cha Jina na Kivumishi Kingine......246
5.5.7 Ruwaza za Kiashiria na Kivumishi Kingine......247
5.6 Hitimisho......258
**SURA YA SITA......259**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO......259**
6.1 Utangulizi......259
6.2 Muhtasari wa Utafiti......259
6.3 Mahitimisho......263
6.4 Mapendekezo ya Utafiti......264
6.5 Hitimisho......265
**MAREJELEO......266**
**KIAMBATISHO A: AINA ZA VIVUMISHI NA MUUNDO UNAOBAINIKA......279**
**1 (a). VIVUMISHI VYA SIFA......279**
**(b). VIVUMISHI VYA SIFA......281**
**2 (a). VIVUMISHI VYA IDADI......281**
**(b). VIVUMISHI VYA IDADI......283**

**4. VIVUMISHI VIULIZI ........ 284**

**5.VIVUMISHI VIMILIKISHI ........ 285**

**6 (a). VIVUMISHI VIONYESHI VYA KARIBU ........ 286**

**(b). VIVUMISHI VIONYESHI VYA MBALI KIDOGO ........ 287**

**(c). VIVUMISHI VIONYESHI VYA MBALI ........ 288**

**7. VIVUMISHI VYA A – UNGANIFU ........ 289**

**8 (a). VIVUMISHI VYA MAJINA ........ 290**

**9.VIVUMISHI VYA MKOPO ........ 291**

**10.VIVUMISHI VYA PEKEE ........ 292**

**11.VIVUMISHI VIRADIDI - VISISITIZI ........ 293**

**VIVUMISHI VIRADIDI – VILINGANISHI ........ 294**

**KIAMBATISHO B: Wilaya ya Eneo Bunge la Meru ya Kati, Maeneo ya Kiutawala na Kata Zake ........ 295**

**KIAMBATISHO C: Cheti cha Idhini ya Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Maasai Mara ........ 296**

**KIAMBATISHO D: Cheti cha Idhini kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi ........ 298**

**KIAMBATISHO E: Cheti cha Idhini kutoka kwa Mkuu wa Kaunti ya Meru ........ 299**

**KIAMBATICHO F: Cheti cha Idhini kutoka Mkuu wa Elimu Kaunti ya Meru 300**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali la 1: Utamkaji wa Irabu za Kiimenti ........ 63
Jedwali la 2: Irabu za Kiimenti na Unukuzi Wake ........ 64
Jedwali la 3: Konsonanti za Kiimenti ........ 69
Jedwali la 4: Jozi za Mlinganuo Finyu ........ 71
Jedwali la 5: Mofu Kapa ........ 86
Jedwali la 6: Mizizi ya Vivumishi vya Kiimenti ........ 88
Jedwali la 7: Mnyambuliko Sarufi (Vivumishi kutokana na Vivumishi) ........ 94
Jedwali la 8: Mnyambuliko geuzi (Vivumishi kutokana na Vitenzi) ........ 96
Jedwali la 9: Mnyambuliko geuzi (Vitenzi kutokana na Vivumishi) ........ 97
Jedwali la 10: Mnyambuliko geuzi (Nomino kutokana na Vivumishi) ........ 98
Jedwali la 11: Mnyambuliko Geuzi (Vielezi kutokana na Vivumishi) ........ 99
Jedwali la 12: Matumizi ya Vivumishi katika Virai Nomino ........ 101
Jedwali la 13: Nafsi na Vivumishi Vimilikishi vya Kiimenti ........ 110
Jedwali la 14: Jinsi Nomino Hudhibiti Viambishi Awali vya Vivumishi ........ 120
Jedwali la 15: Ngeli Mbalimbali za Kiimenti ........ 128
Jedwali la 16: Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip + Mz) ........ 139
Jedwali la 17: Muundo wa Vivumishi vya Idadi (Kip+Kip+Mz) ........ 140
Jedwali la 18: Muundo wa Vivumishi vya Pekee vya Kiimenti (Kip + Mz) ........ 141
Jedwali la 19: Muundo wa Vivumishi vya Mbali Kidogo vya Kiimenti (Kip + Mz) ... 142
Jedwali la 20: Muundo wa Vivumishi vya Mbali vya Kiimenti (Kip + Mz)oro ........ 143
Jedwali la 21: Muundo wa Vivumishi vya A – Unganifu vya Kiimenti (Kip + Mz) ... 144
Jedwali la 22: Muundo wa Vivumishi Viulizi vya Kiimenti (Kip + Mz) ........ 145
Jedwali la 23: Muundo wa Vimilikishi vya Kiimenti (Kip + Mz) ........ 146
Jedwali la 24: Muundo wa Vivumishi vya  Majina vya Kiimenti (KiN + Mz) ........ 147
Jedwali la 25: Muundo wa Vivumishi vya Sifa vya Kiimenti (Kip+KiN + Mz) ........ 150
Jedwali la 26: Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip + Kip + Mz) ........ 152
Jedwali la 27: Muundo wa Vivumishi Vionyeshi vya Karibu (Kip + Mz + I- (KiP) ... 154
Jedwali la 28: Muhtasari wa Ruwaza za Mofimu katika Vivumishi vya Kiimenti ...... 170
Jedwali la 29: Uchopekaji wa Konsonanti ........ 196
Jedwali la 30: Uradidi Kamili wa Vivumishi vya Kiimenti ........ 202

Jedwali la 31: Vivumishi vya Sifa Vilivyoundwa na Uradidi ...................................... 209
Jedwali la 32: Vivumishi Viashiria Vilivyoundwa Kutokana na Uradidi .................... 210
Jedwali la 33: Uradidi katika Uundaji wa Vivumishi vya Pekee.................................. 212
Jedwali la 34: Uundaji wa Vivumishi vya Idadi Kupitia Uradidi................................. 214

## ISHARA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| { } | Mabano mbinuko yanayofungia mofu zinazosetiri mofimu katika lahaja ya Kiimenti. |
| [ ] | Mabano mraba ya kufungia abjadi za kifonetiki. |
| ⟶ | Ishara hii huonyesha uhusiano wa vipengele vya kushoto na vile vya kulia. |
| / / | Mistari yombo inayotumika kufungia fonimu pamoja na maneno yaliyochanganuliwa kimofemiki. |
| * | Alama ya kinyota ya kuonyesha kuwa neno au sentensi ina makosa ya kisarufi au maendelezo. |
| + | Alama chanya ambayo huonyesha muungano wa mofimu katika ruwaza. |
| Ø | Mofu kapa |
| (**$**) | Alama (**$**) hutumia kuonyesha mpaka wa silabi katika isimu. |
| > | Alama yenye dhana ya hubadilika kuwa. |
| AIPCA | African Independent Pentecostal Church of Africa |
| E | Kielezi |
| FZA | Fonolojia Zalishi Asilia |
| EAPC | East African Pentecostal Church |
| KA | Kiambishi Awali |
| Mz | Mzizi wa Kivumishi |
| N | Nomino |
| SMV | Sarufi Miundo Virai |
| SGUZ | Sarufi Geuza Umbo Zalishi |

| | |
|---|---|
| T | Kitenzi |
| V | Vivumishi |
| VA | Viambishi Awali |
| VT | Viambishi Tamati |

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

**Lahaja**: Lugha moja kati ya lugha mbalimbali za Wameru na hutofautiana katika lafudhi na msamiati.

**Mofolojia**: Uchanganuzi wa mofimu zinazounda maneno ya kategoria mbalimbali kama vivumishi vya Kiimenti na usarufi unaowasilishwa katika maumbo hayo ya maneno.

**Muundo wa vivumishi**: Uchanganuzi wa maumbo ya vivumishi na usarufi unaoainishwa.

**Mzizi:** Umbo la kimsingi la neno kama la kivumishi au kitenzi ambalo hubeba maana ya kileksia katika kategoria mbalimbali za maneno ya Kiimenti.

**Ruwaza:** Mpangilio au mfumo maalumu wa vipashio vya lugha kama vivumishi au mofu zinazaounda vivumishi.

**Sheria**: Kanuni au kaida ambazo zinazingatiwa kupangilia mofimu katika vivumishi na tungo mbalimbali za Kiswahili au Kiimenti.

**Tungo za Kiimenti:** Dhana hii inamaanisha sentensi zenye mfuatano wa vivumishi katika lahaja ya Kiimenti.

**Usarufi:** Maana inayowakilishwa na mofu zinazopatikana katika kategoria mbalimbali za maneno. Maana hii ndiyo hujulikana kama mofimu.

**Muundo wa ndani**: Huu ni muundo wa tungo kama neno, kirai, kishazi au sentensi ambao umejificha na hudhihirika kama muundo mwingine katika uandishi na usemaji.

**Muundo wa nje**: Huu ni muundo wa tungo kama neno, kirai, kishazi au sentensi ambao hudhihirika katika uandishi na usemaji.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Kivumishi ni kipashio muhimu katika sarufi ya lugha yoyote ile. Hii ni kwa sababu ndiyo sehemu ambayo hueleza zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi chake katika sentensi. Vivumishi mbalimbali huweza kueleweka na hupitisha ujumbe kulingana na usarufi unaoainishwa katika kivumishi husika.

Uchunguzi wa kiisimu kuhusu lahaja mbalimbali za Kimeru umewahi kuvutia wasomi kama vile (Gacunku, 2005; Kanake, 2013; Kinyua, 2011; Mukuthuria, 1997; 2004; Nguma, 2012; Rukenya, 2014; Salesio, 2011; Wa Mberia, 1981;1993). Watafiti wote hawa walijikita katika kuchunguza lahaja zingine za Kimeru na hawakushughulikia lahaja ya Kiimenti hasa kivumishi chake. Utafiti unaofahamika kuhusu lahaja ya Kiimenti ni ule wa Kanana (2016). Utafiti huu ulichunguza jinsi mchakato wa uradidi hutumika katika uundaji wa maneno ya kategoria mbalimbali za Kiimenti. Mpaka hapa ni wazi kuwa lahaja ya Kiimenti haijachunguzwa sana na utafiti wake wa kiisimu si mwingi. Ni vizuri kufahamu kuwa utafiti wa kiisimu kuhusu lahaja mbalimbali za Kimeru uliangazia masuala mengine ya kiisimu na kupuuza kivumishi cha Kiimenti. Kwa mfano, utafiti kuhusu kategoria za maneno kama nomino na kitenzi katika lahaja ya Kichuka, Kimwimbi, Kitigania na Kitharaka umewahi kufanywa. Hata hivyo, hakuna uchunguzi wowote wa kiisimu unaofahamika kuhusu lahaja ya Kiimenti uliojikita katika masuala ya muundo wa kivumishi ili kubainisha usarufi unaoainishwa. Jambo hili lilitia ari ya kufanyia lahaja hii utafiti wa kiisimu. Uhaba wa utafiti wa kiisimu katika lahaja za

Kimeru ulimfanya Mukuthuria (1997) kutoa rai kuwa lahaja za Kimeru zifanyiwe uchunguzi wa kiisimu.

Lugha ya Kimeru huzungumzwa katika Kaunti za Meru na Tharaka Nithi. Sensa ya 2019 ilithibitisha kuwa wazungumzaji wa lugha hii katika kaunti ya Meru ni watu 1,545,714 na katika kaunti ya Tharaka Nithi ni watu 393, 177. Jumla ya wazungumzaji wa lugha ya Kimeru ni 1,938,891 (KNBS, 2019). Lugha hii ina lahaja zifuatazo: Kiimenti, Kitigania, Kiĩgembe, Kiĩgoji, Kimĩĩtĩne, Kimuthambĩ, Kimwĩmbĩ, Kitharaka na Kichuka. Utafiti huu ulishughulikia lahaja ya Kimenti ambayo huzungumzwa katika maeneo mbalimbali ya kaunti ya Meru. Kwa mujibu wa sensa ya 2019 wazungumzaji wa Kiimenti ni takriban watu 542,384 ambao huishi katika kaunti ndogo za kaunti ya Meru ambazo ni Bũũri Mashariki, Bũũri Magharibi, Imenti Kaskazini, Imenti Kusini na Imenti ya Kati. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika wadi ya Abothũgũchi ya Kati katika Imenti ya Kati ambayo ni kaunti ndogo ya kaunti ya Meru. Wazungumzaji wa Kiimenti wanaoishi katika wadi ya Abothuguchi Magharibi ni 133,818 ambao wanaishi katika eneo la 381.8 kilomita mraba. Kaskazini, eneo hili linapakana na kaunti ndogo za Imenti Kaskazini na Bũũri. Upande wa Kusini eneo hili linapakana na kaunti ndogo ya Imenti Kusini. Magharibi linapakana na msitu wa Mlima Kenya.

Suala la kuwepo kwa lugha ya Kitharaka badala ya lahaja ya Kimeru limevutia wasomi mbalimbali. Baadhi yao ni kama Wa Mberia (1981; 1993). Kwa maoni yake Watharaka ni jamii tofauti na Wameru. Maoni yake yanapingwa na inadaiwa kuwa Kitharaka ni mojawapo ya lahaja za Kimeru (Fadiman, 2012; Irea, 2005; Kanake, 2013; Kobia, 2008; M'Imanyara, 1992; M' Ngaruthi, 2008; Mpungu, 1984; Rimita,1988; Nyaga, 1996). Mukuthuria (1997) akichangia mjadala huu alitoa maoni kuwa Wa Mberia (1981; 1993)

alipofikia uamuzi wake hakutilia maanani uhusiano wa muundo na kileksia kati ya lahaja ya Kitharaka na lahaja nyingine za Kimeru. Aidha, hakutilia maanani uelewano na ukuruba wa mazingira ambamo lahaja hii na nyingine za Kimeru hupatikana. Haja ya utafiti huu haikuwa kujihusisha na mjadala huu. Utafiti huu ulinuia kuchunguza muundo wa kivumishi cha Kiimenti ili kueleza sheria zinazodhibiti ruwaza ya mofimu katika kivumishi husika na jinsi kinavyouhusiana na vingine katika sentensi za Kiimenti ili kuibua ruwaza mbalimbali.

## 1.2 Suala la Utafiti

Ingawa kivumishi ni kategoria muhimu ya lugha, hakuna utafiti wowote uliofanyiwa kategoria hii ya maneno katika lahaja ya Kiimenti, kuainisha utendakazi wake kisarufi pamoja na kubainisha ruwaza ya mpangilio wa maneno ya kategoria hii katika tungo za Kiimenti na kuweka wazi sheria za kimiundo zinazouelekeza; masuala haya ndiyo yaliyozingatiwa katika utafiti huu.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

i) Kubainisha aina za vivumishi zinazopatikana katika lahaja ya Kiimenti.

ii) Kuchunguza miundo ya vivumishi vya Kiimenti na jinsi usarufi unavyowakilishwa katika maumbo ya vivumishi.

iii) Kupambanua ruwaza za usarufi katika vivumishi vya Kiimenti.

iv) Kutathmini sheria za mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

i) Je, lahaja ya Kiimenti ina aina gani za vivumishi?

ii) Je, vivumishi vya lahaja ya Kiimenti vinawasilisha muundo upi na usarufi unaobainika unawakilishwaje?

iii) Je, usarufi unaowakilishwa katika maumbo ya vivumishi unabainisha ruwaza gani?

iv) Je, ni sheria zipi huelekeza ruwaza ya vivumishi katika tungo za Kiimenti?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Vivumishi vya lahaja ya Kiimenti havijafanyiwa utafiti wa kiisimu. Kwa hivyo, utafiti huu wa vivumishi utafanikisha uelewa wa muundo wa kundi hili la maneno kiisimu. Pia, utendakazi wa mofimu zinazoainishwa katika maneno hayo utabainishwa. Vilevile, inatazamiwa kwamba utafiti huu utakuwa kichocheo cha tafiti zingine katika lahaja ya Kiimenti na lugha zingine za Kibantu.

Kiswahili ni lugha ya Kibantu sawa na lahaja ya Kiimenti. Kwa hivyo, lugha hizi mbili huweza kushabibiana kwa mambo kadha kama muundo. Kwa hivyo, uelewa wa masuala ya muundo wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti utasaidia anayejifunza Kiswahili kuyaelewa anaposoma na kuyachunguza katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, uelewa wa muundo wa vivumishi vya Kiimenti utasaidia anayejifunza na kuchanganua muundo wa vivumishi vya Kiswahili pamoja na lugha nyingine za Kiafrika. Pia, utafiti huu utaweka wazi sheria zinazodhibiti mpangilio wa vivumishi katika tungo mbalimbali za lahaja ya Kiimenti. Hali hii itasaidia katika kuchunguza na kuandika sheria zinazozingatiwa katika kupangilia vivumishi vya Kiswahili katika tungo zake.

Aidha, utakuwa mchango mkubwa kwa wanafunzi, walimu na wanaisimu wa lugha ili kuendeleza utafiti katika lugha zingine za Kibantu hasa watakapokuwa wakitafitia mofolojia na sintaksia ya lugha hizo. Hii ni kwa sababu utawapatia msingi wa kiisimu

utakaowasaidia kutafitia masuala ya kiisimu. Inatarajiwa kwamba data kutoka kwa utafiti huu itakuwa kanzi kubwa katika uandishi wa sarufi ya lugha ya Kimeru.

Vilevile, utafiti huu utasaidia waandishi wa vitabu vya Kimeru. Hii ni kwa sababu watapata kanzi ya baadhi ya vivumishi vya Kimeru na hivyo itakuwa rahisi kuviainisha katika kazi zao. Uandishi kama huu utasaidia walimu na wanafunzi katika ufunzaji wa lugha ya Kimeru katika shule za msingi. Hii ni kwa sababu mtaala mpya wa elimu hapa nchini unatilia maanani ufunzaji wa lugha za kiasili kama Kimeru.

**1.6 Upeo wa Utafiti**

Lugha ya Kimeru ina lahaja takriban tisa ambazo huainisha kategoria mbalimbali za maneno. Lahaja hizo ni Kiimenti, Kitigania, Kiĩgembe, Kiĩgoji, Kimĩĩtĩne, Kimũthambĩ, Kimwĩmbĩ, Kitharaka na Kichuka. Hata hivyo, utafiti huu haukuchunguza lahaja hizo zote. Ulichunguza lahaja ya Kiimenti ukizingatia muundo wa kategoria ya kivumishi katika lahaja husika. Utafiti huu ulinuia kuweka wazi vipashio vya kimaumbo vinavyounda vivumishi na kuchunguza ruwaza ya vivumishi katika tungo za Kiimenti na kutunga kanuni zinazotawala ruwaza hizo. Lahaja ya Kiimenti huzungumzwa katika maeneo mengi ya Kaunti ya Meru. Hata hivyo, si eneo lote la kaunti hiyo lililozingatiwa katika utafiti huu. Utafiti huu ulichunguza lahaja ya Kiimenti inayozungumzwa katika wadi ya Abothũgũchi ya Magharibi, kaunti ndogo ya Meru ya Kati katika Kaunti ya Meru ili kupunguza athari za lugha zinazopatikana katika maeneo ya mipaka ya Meru.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia kazi za wataalamu mbalimbali kuhusu mada ya utafiti. Kazi zilizorejelewa kwenye sehemu hii ni pamoja na kazi za kijumla zilizofafanua maana ya kivumishi na kuelezea vivumishi mbalimbali. Aidha, majarida na kazi zingine zilizoshughulikia utafiti wa kiisimu pamoja na nadharia zilizoongoza utafiti huu zilirejelewa.

## 2.2 Maana ya Kivumishi

Neno kivumishi ni nomino ambayo imeundwa kutokana na kitenzi *vuma*. Kitenzi hiki kina maana ya kufanya habari nzuri au mbaya za mtu kujulikana (BAKITA, 2015). Kwa hivyo, neno hilo linavumisha sifa hizo ili zijulikane zaidi na hivyo likaitwa kivumishi. Hali hii inapelekea kutoa fasili ya kivumishi kama neno ambalo hutoa habari zaidi kuhusu nomino ili ijulikane au ieleweke zaidi. Katika ufafanuzi wa nomino hatutajikita katika mtu pekee. Hii ni kwa sababu nomino ni za aina nyingi.

Kivumishi ni kipashio chenye uamilifu wa kutoa maelezo zaidi kuhusu nomino (Massamba na wenzie, 2001; Mbaabu, 1992; Mohamed, 2001; Steere, 1934). Nomino hutangulia kivumishi katika kirai au sentensi. Hali hii huenda isiwe ya kweli kila wakati. Hii ni kwa sababu katika sentensi kama: *Kila mwanafunzi anunue kitabu kingine*, *kila* huweza kuwa kivumishi ambacho kinafafanua mwanafunzi na huja kabla ya nomino.

Kapinga (1981) anaeleza kivumishi kama maneno yanayotoa habari ya mtu alivyo au kitu kilivyo, jinsi kinavyoonekana au kinavyofikiriwa kwamba kina tabia fulani au kipo katika idadi fulani. TUKI (1990) vivyo hivyo, hueleza kivumishi kama kipashio kinachotoa

maelezo zaidi juu ya nomino. Maelezo mengine kutoka kwa kamusi hii ni kuwa kivumishi ni neno au kirai kinachoeleza zaidi kuhusu nomino au kikundi cha maneno. Maelezo haya yana udhaifu katika kufafanua kivumishi. Hii ni kwa sababu sio lazima kila kikundi cha maneno kuwa na nomino. Kuna uwezekano wa kuwa na kikundi cha maneno cha kitenzi, kielezi au aina nyingine ya maneno, na hivi si vivumishi.

Kivumishi au sifa ni maneno yanayotoa habari zaidi au yanayosifu mtu au kitu kinachozungumziwa (Ndalu, 1993). Ufafanuzi zaidi wa kivumishi unaotolewa na Ndalu (1997) ni kuwa kivumishi ni neno linaloongezea jina, kivumishi au sifa maana. Mfano anaotoa wa kivumishi kuvumisha kingine ni kama katika kirai kivumishi hiki, *nguo nzuri nzuri* ambapo anasema kuwa *nzuri* ya pili inafafanua 'nzuri' ya kwanza. Hali ya kivumishi kufafanua jina tunakubaliana nayo, lakini kauli ya kivumishi kufafanua kivumishi kingine hatukubaliani nayo. Hii ndiyo kazi ya kwanza tuliyopitia inayoangazia hali ya kivumishi kuelezea kingine. Kasoro nyingine katika kazi zake ni kutambua kivumishi kama sifa. Kivumishi si sawa na sifa bali sifa ni aina mojawapo ya vivumishi.

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2011) kivumishi ni kundi la maneno ambayo hufafanua nomino na kudokeza sifa za nomino hiyo. Baadhi ya sifa za nomino ni kama – kali, -fupi, -refu, -eupe na kadhalika. Katika kutoa maelezo ya kivumishi maelezo haya ni finyu sana. Ikiwa yatazingatiwa basi ni vivumishi vya sifa ambavyo vingeainishwa pekee. Ingekuwa vigumu kuainisha aina zingine za vivumishi. Kwa mfano, vile vya idadi vingehusishwaje na sifa za nomino?

Baada ya kutalii maelezo mbalimbali kuhusu ufafanuzi wa kivumishi kinaweza kuelezwa kama neno au fungu la maneno ambalo hufafanua/hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi cha nomino.

Maelezo ya watalaamu mbalimbali hapo juu yalisaidia kuelewa kwa uwazi maana ya kivumishi. Maelezo ya wataalamu hao yalijikita katika kivumishi cha Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia kivumishi cha lahaja ya Kiimenti na si cha Kiswahili. Aidha, utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza uamilifu wa mofimu zinazopatikana katika vivumishi vya Kiimenti.

### 2.2.1 Kazi za Karne ya 20 na 21 Kuhusiana na Vivumishi

Utafiti huu umeangazia kazi zilizoandikwa karne iliyopita hadi sasa kuhusu vivumishi vya Kiswahili. Baadhi ya kazi za zamani za karne iliyopita ni zile zilizoandikwa na wageni. Kazi zao ziliweka msingi wa sarufi ya Kiswahili na ziliathiri wasomi na waandishi wa baadaye wa sarufi ya Kiswahili.

### 2.2.2 Aina za vivumishi

Kuhusiana na aina za vivumishi Wilson (1970) alishughulikia aina zifuatazo za vivumishi:

i) Vivumishi vya pekee

Yeye hakuvipa vivumishi vya pekee jina maalumu. Aliviita tu vivumishi –ote, -o-ote, -enye na –enyewe. Upungufu katika kazi hii ni kuwa hakuhusisha mzizi –ingine ambao umeainishwa na watalaamu wengine kama kivumishi cha pekee. Aliuainisha mzizi huo kama kivumishi cha idadi.

ii) Vivumishi ambatani huweza kudhihirika katika sentensi zifuatazo:

a) Mtoto *wa kifalme* amekuja. b) Mtoto amekula chakula *cha kutosha*.

Kwa maoni yetu, mifano ya sentensi iliyotolewa hapo juu na Wilson (mtaje), ni kuwa vivumishi ambatani vimechanganya vivumishi vya a - unganifu na vile vya ‘ki’ ya mfanano. Mawazo haya ni sawa na ya Steere (mtaje) kuonyesha kuwa kulikuwa na

uwezekano wa kazi ya Steere (mtaje) kuathiri ile ya Wilson (mtaje) katika kueleza vivumishi.

iii) Vivumishi viashiria

Wilson (mtaje) alitambua viashiria mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Upungufu wake ni kwamba hakuwa wazi na kuvieleza kama vivumishi au vivumishi viashiria. Lakini kulingana na mifano ya vishazi tegemezi aliyoitoa, ni wazi kuwa alikuwa akielezea vivumishi viashiria. Kwa mfano alitoa mifano ya vishazi tegemezi kama mpishi mzuri *yule*, miti mirefu *hii* na mkate mbovu *huu.* Kwa hivyo, *yule, hii* na *huu* ni vivumishi viashiria.

iv) Vivumishi vya idadi

Wilson (mtaje) ameainisha vivumishi vya idadi dhahiri kama alivyofanya Ashton (mtaje). Hii ni kuonyesha kwa namna fulani aliathiriwa na kazi ya mtangulizi wake katika uandishi wa sarufi ya Kiswahili. Hata hivyo, amepiga hatua na kubainisha mizizi ya vivumishi vya jumla kama – ‘*chache’* na – *‘ingi’.*

Upungufu wa kazi hii ni kuwa kuna vivumishi vingine vya idadi isipokuwa vivumishi alivyoainisha. Vivumishi hivi vinaundwa kutoka kwa mizizi kama, *kidogo* na *kiasi* (Mgullu, 1999). Upungufu mwingine katika kazi yake unahusiana na mzizi ‘*–ngapi*?’ Alitambua mzizi huu kama kivumishi cha idadi na pia kama kivumishi kiulizi. Kwa hivyo, hakuwa wazi ‘*–ngapi*’ ni kivumishi cha aina gani. Hata hivyo, wasomi wa baadaye wameainisha mzizi *‘–ngapi*’ kama kivumishi kiulizi. Kazi ya Wilson (mtaje) ni muhimu kwa kuwa ilifaa kuweka wazi aina mbalimbali za vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Kwa mfano, ilielekeza kuchunguza vivumishi ambatani katika lahaja ya Kiimenti. Kazi hiyo iliangazia vivumishi vya Kiswahili, hii ilijikita katika lahaja ya Kiimenti

inayozungumzwa katika eneo la Abothũgũchi Magharibi katika kaunti ndogo ya Meru ya Kati katika Kaunti ya Meru.

Akizungumzia vivumishi zaidi, Mbaabu (mtaje) alidai vivumishi hugawanywa katika makundi kadha. Haya ni kama:

i) Maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kibantu na Kiarabu. Kutoka lugha za Kibantu kuna maneno kama: *pia*, *kakamavu, marakaraka* na *kama*. Hata hivyo, kulingana na mtaalamu huyu pamoja na Philipo (2017), vivumishi vya aina hii ni vichache katika lugha ya Kiswahili. Aidha, vivumishi vingine vilivyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu ni kama: *ghali, sawa, kamili, safi, hodari, rahisi, dhaifu* na *sahihi.*

ii) Vivumishi ambavyo ni maneno ya kuhesabu kama *moja, kumi, laki* na mengineyo.

iii) Vivumishi vinavyoundwa kwa kutumia nomino, ambapo nomino ya pili huvumisha nomino ya kwanza. Mfano ni kama *askari kanzu, punda milia,* na *simba marara*. Mbaabu (mtaje) alieleza kuwa katika nomino '*askari kanzu*', nomino '*kanzu*' ni kivumishi cha kuvumisha nomino *askari.*

iv) Vivumishi vya 'a' ya uhusiano ambavyo ni kama *la*, *wa*, *cha, za* na hata *vya*. Virai vifuatavyo huweza kutumiwa kuonyesha jinsi 'a' ya uhusiano hutumika kuhusisha nomino mbili: Gari *la* mwalimu, magari *ya* walimu, kiatu *cha* mtoto na viatu *vya* mtoto.

v) Vivumishi vya 'o' rejeshi ambapo mawazo ya Mbaabu (mtaje) kuhusu aina hii ya vivumishi yanaoana na ya Ashton (1944) kuonyesha kwa kiasi aliathiriwa na kazi ya mtangulizi wake katika uwanja wa isimu.

vi) Vivumishi vinavyoundwa kutokana na mzizi '*-enye*' kama *mwenye, chenye, lenye* na hata *wenye*. Vivumishi vya aina hii hutumiwa kutoa dhana ya kumiliki.

vii) Vivumishi Viradidi. Mfano wa vivumishi hivi ni kama *fupifupi* na hata *sawasawa*. Vivumishi vya aina hii hutumiwa wakati wa kutoa msisitizo.

Kwa ujumla aina ya vivumishi vilivyoangaziwa ni kama vile vya idadi, 'a' –unganifu, mkopo, majina, virejeshi, viradidi na pekee. Kazi ya Mbaabu (mtaje) ni miongoni mwa kazi za mwanzo za sarufi ya Kiswahili kuandikwa na wasomi wenye ujuzi wa kiisimu hapa nchini. Kwa hivyo, kazi hii ilisaidia kuweka msingi wa sarufi ya Kiswahili na utafiti wa kiisimu hapa nchini. Hata hivyo, ilikabiliwa na upungufu kwa jinsi alivyoshughulikia baadhi ya masuala ya vivumishi vya Kiswahili. Kwa mfano, katika kuainisha vivumishi vya pekee, aliainisha kimoja tu ambacho ni '–enye'. Wataalamu wa baadaye kama Mohamed (mtaje); Habwe na Karanja (2004) waliongezea vivumishi vingine vya pekee. Aidha, aliainisha vivumishi vya idadi kamili na kukosa kuhusisha vivumishi vya idadi ya jumla vinavyoundwa kwa kutumia mizizi kama '–ingi' na '–chache'. Pia kazi hiyo haikuweka wazi tofauti kati ya aina mbalimbali za vivumishi na muundo wa vivumishi. Hii ni kwa sababu vivumishi vinavyoambishwa viambishi vya ngeli viliainishwa kama kundi moja la vivumishi.

Hata hivyo, kazi ya Mbaabu (mtaje) ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu ilielekeza katika kuchunguza aina mbalimbali za vivumishi vinavyopatikana katika lahaja ya Kiimenti; hasa vivumishi viradidi ambavyo havikuangaziwa na wataalamu wengine ambao kazi zao zilirejelewa. Utafiti huu ulitofautiana na kazi hiyo kwa sababu ulijikita katika vivumishi vya Kiimenti na si Kiswahili kama yake. Pia, kazi Mbaabu (mtaje) iliangazia kategoria nyingine za maneno na utafiti huu haukuzichunguza. Upeo wa utafiti huu ulihusu uchunguzi wa vivumishi vya Kiimenti pekee.

Mgullu (1999) alishughulikia aina sita za vivumishi. Hivi ni vya sifa, vionyeshi, viulizi, visisitizi, idadi na vimilikishi. Kuhusiana na vivumishi vya idadi ameainisha idadi dhahiri na isiyo dhahiri. Maelezo ya idadi dhahiri ni kama ilivyoelezwa na wataalamu wengine kama Mbaabu (mtaje). Hata hivyo, katika maelezo ya idadi isiyo dhahiri mizizi ya vivumishi inayoainishwa kama vivumishi vya pekee na wataalamu kama Mohammed (mtaje) imejumlishwa hapa. Hii ni mizizi kama *–ot e, o-te na –ingine.* Mizizi mingine ya vivumishi iliyoainishwa kama idadi isiyo dhahiri ni *–ingi, -chache, kidogo* na *kiasi*. Kwa hivyo, vivumishi vinavyotambuliwa na wasomi wengine kama vya pekee haviainishwi hapa. Hata ufafanuzi wa vivumishi visisitizi unatofautiana na ule wa wasomi wengine. Hii ni kwa sababu Mgullu (1999) aliainisha mzizi *–enyewe* kama kivumishi kisisitizi ilhali kazi nyingine zimeuainisha kama kivumishi cha pekee. Aidha, kazi hiyo haisemi chochote kuhusu mzizi *–enye* ulioainishwa na wasomi wengine kama kivumishi cha pekee. Kuhusiana na vivumishi vionyeshi aliainisha aina tatu kulingana na umbali kama: vivumishi vionyeshi vya karibu kama *huyu* na *hawa*, vivumishi virejeshi vya mbali kidogo kama *hao* na *huyo* na vivumishi vionyeshi vya mbali kama *ile* na *yule.* Kazi hii ya Mgullu (1999) ilielekeza kuainisha vivumishi mbalimbali vya lahaja ya Kiimenti. Inatofautiana na hii kwa sababu imepiga hatua na kuchunguza uamilifu unaoainishwa katika vivumishi vya Kiimenti. Utafiti huu ulichunguza lahaja ya Kiimenti na si Kiswahili. Aidha, umepiga hatua na kuchunguza masuala ya miundo ya vivumishi kama ruwaza ya mofimu katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti na si aina ya vivumishi vya Kiswahili viliyoangaziwa katika kazi ya Mgullu (1999).

Aidha, Kihore na wenzie (2001) walishughulikia aina mbalimbali za vivumishi vya Kiswahili. Uainishaji wao ulizingatia kigezo cha maana ya kivumishi badala ya kile cha

umbo kuainisha vivumishi. Katika kigezo cha maana waliongozwa na maana kuhusu vivumishi iliyotolewa katika TUKI (1990). Maelezo ya kamusi hii ni kuwa kivumishi hueleza jinsi nomino huonekena, hufikiriwa kuwa, tabia au idadi yake. Katika hali hii aina nne za vivumishi vya Kiswahili ambavyo ni vile vya sifa, idadi, viulizi na vya pekee vimeainishwa. Maelezo yametolewa kuwa vivumishi vya kumiliki, vionyeshi, 'a' unganifu na vya majina si vivumishi. Kwa kuzingatia kigezo cha maana ya kivumishi kutoka kwa kamusi TUKI (1990); kuna ukweli fulani kuwa hivi si vivumishi. Hata hivyo, kwa kuna upungufu wa kutoainisha vivumishi vya majina kama aina nyingine ya vivumishi ikiwa kigezo cha maana kilizingatiwa. Kwa mfano, kivumishi kama *bahili* katika kirai '*mtu bahili'* kinaeleza jinsi nomino 'mtu' hufikiriwa, huonekana au tabia yake. Vivumishi vya kumiliki na vionyeshi viliainisha kama viwakilishi. Vile vya 'a'-unganifu na majina vikaainishwa kama virai vivumishi. Vivumishi vya idadi vilivyoainishwa ni kama *haba, kidogo, chache, pungufu, lukuki, -ingi* na *maridhawa.* Vingine ni nambari za kuhesabu. Vile vya kuuliza ni *–ngapi?* na *gani*? Vya pekee ni *–enye* na *–enyewe*. Mzizi *-ingine* uliainishwa kama kivumishi cha kawaida ilhali *-ote* na *o-ote* ni viwakilishi. Muainisho huu wa vivumishi uliofanywa na Kihore na Wenziwe (wataje) ni tofauti na wasomi wengine hasa walipoainisha aina fulani ya maneno kuwa si vivumishi. Waandishi na wasomi walioandika kuhusu vivumishi baada ya Kihore na Wenziwe (wataje) hawaonyeshi kukubali au kuathiriwa na mawazo yao. Kwa hivyo kuna kazi za waandishi kama Habwe na Karanja (wataje) na hata *Kamusi ya Karne ya 21* (2011) ambazo zimeainisha vivumishi vilivyopuuzwa na Kihore na Wenziwe (wataje) kama aina nyingine za vivumishi. *Kamusi ya Karne ya Ishirini na 21* (2011) iliandikwa chini ya uangalizi na uelekezi wa wasomi wenye tajriba ya kina katika nyanja mbalimbali

za lugha ya Kiswahili, ikiwemo sarufi yake. Kwa hivyo hawaonekani kukubali madai ya Kihore na Wenziwe (wataje) kuhusu uainishaji wa vivumishi vya Kiswahili.

Kazi ya Kihore na wenziwe (wataje) inazua dhana ya kugawa vivumishi kwa misingi ya maana. Kazi hiyo ilielekeza uchunguzi wa jinsi kigezo cha maana hutumiwa kuainisha vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Kazi hiyo ilishughulikia vivumishi vya Kiswahili ilhali hii ilichunguza vile vya Kiimenti. Pia, hii ilichunguza mofimu mbalimbali kwenye vivumishi vya Kiimenti na uamilifu wake. Utafiti huu ulielekezwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA ilhali kazi ya Kihore na wenziwe (wataje) haikuongozwa na misingi yoyote ya kinadharia.

*Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja* (2011) ilianisha vivumshi vya sifa, idadi, pekee, vionyeshi, a – unganifu, virejeshi, visisitizi, nomino, viulizi na vimilikishi. Muainisho huu wa vivumishi uliongoza uainishaji wa vivumishi vya Kiimenti katika utafiti huu. Licha ya kuangazia vivumishi vya Kiswahili katika kazi hiyo, ilishughulikia kategoria nyingine za maneno pamoja na masuala mengine ya kiisimu. Utafiti huu ni tofauti na kazi hiyo kwa sababu ulichunguza vivumishi vya Kiimenti na si vya Kiswahili. Aidha, haukuchunguza kategoria nyingine za maneno isipokuwa vivumishi pekee.

*Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) iliandikwa na wataalamu wa Kiswahili chini ya uongozi wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Kamusi hii imeainisha aina saba za vivumishi vya Kiswahili. Hivi ni vivumishi vya sifa, idadi, vimilikishi, vionyeshi, virejeshi, pekee na viulizi. Muainisho kama huu pia ulituelekeza katika harakati zetu za kugawa vivumishi vya Kiimenti katika aina zake. Utafiti huu utatofautiana na kazi ya BAKITA kwa sababu ulijikita katika vivumishi vya Kiimenti na si Kiswahili. Aidha, kazi hiyo imeshughulikia masuala mengi ya kisarufi kuhusiana na majukumu ya kamusi kama umoja, wingi,

mnyambuliko, etimolojia ya maneno, aina za maneno na mengineyo. Utafiti huu haukuchunguza masuala kama hayo kwa sababu yalikiuka upeo wa uchunguzi huu.

### 2.2.3 Miundo ya Vivumishi

Kuhusiana na muundo wa vivumishi Ashton (mtaje) alisema kuna:

i). Mashina na mizizi ya vivumishi inayochukua viambishi vya ngeli kama*-bovu –refu, -fupi –kali*. Aidha, alidhihirisha upatanisho wa nomino na vivumishi kwa kuchukua viambishi vya mwanzo katika ngeli mbalimbali. Vilevile, aliangazia tarakimu au rakamu mbalimbali ambazo huchukua viambishi vya ngeli. Hizi ni kama *moja, mbili, tatu, nne, tano* na *nane.* Aliongezea na kusema kuwa mzizi *–ngapi* huweza kuambishwa ili kuunda vivumishi.

ii). Vivumishi ambavyo havichukui viambishi vya upatanisho wa kisarufi katika ngeli mbalimbali. Mfano wa vivumishi hivi ni kama vile vya mkopo kutoka Kiarabu kama *safi, kamili, tele na hodari*. Katika kuelezea maneno ya tarakimu, Ashton (mtaje) alibainisha kuwa vivumishi kama *sita, saba, kumi na tisa* havichukui viambishi vya upatanisho vya ngeli mbalimbali. Kauli hii inaungwa mkono na Habwe na Karanja (wataje). Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa vivumishi vya idadi dhahiri hasa nambari 1 hadi 5 pamoja na 8 huchukua viambishi vya ngeli mbalimbali. Ashton (mtaje) aliendelea kusema kuwa vivumishi vingine vya idadi vilikopwa kutoka lugha nyingine kama Kiarabu. Baadhi ya vivumishi hivyo ni kama *edashara (*kumi na moja), *thenashara* (kumi na –wili), *thelatashara* (kumi na – tatu) na vingine. Vivumishi hivi vya mkopo kutoka lugha ya Kiarabu hadi kwa Kiswahili na havichukui viambishi vya upatanisho katika ngeli mbalimbali. Miundo mingine ya vivumishi iliyoangaziwa ni kama:

iii). Vivumishi vya – ‘a’ unganifu

Hivi huundwa kwa kutumia mofu ‘a’ na vipatanishi vya nomino kama: gari *la* baba, mtoto *wa* mwalimu, kiatu *cha* mwanafunzi na nguo *ya* mtoto.

iv). Vivumishi vya ‘o’ rejeshi

Hivi huundwa kutokana na kiwakilishi rejeshi ‘o’ na vipatanishi vya nomino katika vitenzi. Kwa mfano, mwizi ali***ye***iba, wezi wali***o***iba, kiti kili***cho***vunjika. Hapa kirejeshi ‘o’ kinarejelea nomino iliyotajwa kwa nia ya kuifafanua zaidi. Kwa ufupi kazi ya Ashton (mtaje) iliangazia muundo wa vivumishi vya lugha ya Kiswahili. Kazi hiyo iliongoza uchunguzi wa hali ya vivumishi vya lahaja ya Kiimenti kuzingatia muundo kama huo. Aidha, kazi hii ilijikita katika vivumishi vya Kiswahili pamoja na kategoria nyingine za maneno. Utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza muundo wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti pekee kwa sababu upeo wake haukuhusisha kategoria nyingine za maneno.

Mtaalamu mwingine ambaye amezungumzia muundo wa vivumishi vya Kiswahili ni Wilson (mtaje). Alieleza kuhusu aina za vivumishi vya Kiswahili kwa kutumia muundo wavyo. Hivyo, alibainisha makundi matatu ya vivumishi. Makundi haya ni:

1). Mashina yenye konsonanti na huchukua vipatanishi vya nomino inayoelezwa. Mashina hayo ni kama *–fupi, -refu, -baya, -zuri* na mengine ya vivumishi yanayoanza kwa konsonanti.

2). Mashina yenye irabu na huchukua vipatanishi vya nomino inayoelezwa kama *–eusi, -eupe, -ekundu -epesi* na mengine ya vivumishi yanayoanza kwa irabu.

3). Mashina ya mkopo kutoka lugha ya Kiarabu ambayo hayachukui vipatanishi vya nomino inayoelezwa. Mifano ya vivumishi vilivyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu ni

kama: *tele, sawa, laini, bora, tayari, hodari, safi, bora, maridadi, wazi, kamili, rahisi* na *kila*.

Mawazo ya Wilson (mtaje) kuhusu muundo wa vivumishi hayatofautiani sana na ya Ashton (mtaje). Hii ni kwa sababu wataalamu hawa wawili walielezea jinsi mashina ya vivumishi huchukua viambishi mbalimbali ili kuleta upatanisho. Aidha, wote walishughulikia vivumishi vya mkopo ambavyo havichukui vipatanishi vya ngeli au vya nomino zinazofafanuliwa. Hata hivyo, Ashton (mtaje) alidhihirisha aina mbili za mashina ya vivumishi ilhali Wilson (mtaje) alieleza kuhusu aina tatu. Jambo linalojitokeza kuhusiana na kazi za wataalamu hawa wawili ni kuwa kazi ya Ashton (mtaje) kwa kiasi ilikuwa na athari kubwa kwa kazi ya Wilson (mtaje).

Aidha, Wilson (mtaje) aliangazia muundo wa vivumishi ambatani ambavyo alisema huundwa kwa kutumia mofu ‘a’ pamoja na maneno kama ya nomino na vitenzi pamoja. Hapa mofu ‘a’ inapotumika pamoja na maneno hayo huchukua vipatanishi vya maneno; na hivyo, kuunda vivumishi ambatani. Kwa mfano, *wa kifalme* na *cha kutosha* katika sentensi zifuatazo:

a) Mtoto *wa kifalme* amekuja. b) Mtoto amekula chakula *cha kutosha*.

Jambo jingine linalodhihirika katika kazi ya Wilson (mtaje) ni mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati vipatanishi vya nomino zinazovumishwa huungana na mizizi ya vivumishi mbalimbali. Ametoa mifano ifuatayo kuonyesha mabadiliko haya:

wa + ema → wema  wa + ingi → wengi

wa + ingine → wengine  mi + eusi → myeusi

Hata kama mabadiliko haya ya sauti hayakuelezwa vizuri na Wilson (mtaje), yanahusu mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia. Kwa mfano kuna muungano wa irabu katika

kuunda vivumishi *wema*, mvutano wa irabu unatokea katika kuunda vivumishi *wengi* na *wengine* ilhali uimarishaji wa irabu umetokea katika kuunda *myeusi*. Mifanyiko kama hiyo ya kifonolojia imeangaziwa hata katika kazi ya awali kama ile ya Ashton (mtaje).

Kazi ya Wilson (mtaje) ilifaa katika kuchunguza muundo wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti hasa vile vya mkopo kutoka lugha zingine hadi Kiimenti. Aidha, ilielekeza uchunguzi wa miundo ya vivumishi vya Kiimenti wakati viambishi ngeli huambishwa mizizi ya vivumishi na mifanyiko ya kifonolojia inayotokea. Utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza hata utendakazi wa maumbo ya vivumishi vya Kiimenti na ruwaza ya vivumishi hivyo katika tungo za Kiimenti, ambayo hayakuchunguzwa katika kazi hiyo.

Kazi za tafsiri zilizoandikwa na wageni zilichangia ukuaji wa sarufi ya Kiswahili. Mfano wa kazi hizo ni kama ya Myachina (1981) iliyotafsriwa na E. N. Campell. Katika kazi hiyo masuala ya mofolojia ya aina za maneno ya Kiswahili kama nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na hata viunganishi yameangaziwa. Kazi hii imepiga hatua kuangazia suala la sintaksia katika Kiswahili kwa kuchunguza sentensi za Kiswahili. Haja ya utafiti huu haikuwa kushughulikia masuala haya yote, bali ulijikita katika sehemu inayohusu mada ya uchunguzi huu ambayo ni mofolojia ya vivumishi. Hii ni kwa sababu sehemu hii ilielekeza uchunguzi wa usarufi katika kivumishi cha Kiimenti. Kazi hiyo ilieleza kuwa vivumishi hutanguliwa na nomino inayovumishwa. Kisha iliendelea kudai kuwa kuna upatanisho wa kisarufi kati ya ngeli, nomino na kivumishi katika lugha ya Kiswahili. Ili kuleta upatanisho huu mzizi wa kivumishi huambatishwa kiambishi awali kinachofanana na ngeli ya nomino inayovumishwa. Mfano uliotolewa ni katika ngeli ya kwanza M ambapo nomino mtu huweza kuvumishwa na kivumishi mwema. Kwa hivyo kirai nomino kinachopatikana ni *mtu mwema*. Katika kivumishi *mwema*, mzizi ni *–ema*

ambao umetanguliwa na kiambishi ‘*m*’ cha ngeli ya kwanza M- (umoja). Hali hii kimofolojia inaweza kuelezwa hivi: *mu* + *ema* inakuwa *mwema*. Mchakato unaotokea hapa ni uimarikaji wa irabu, hivi kwamba irabu /*u*/ kwenye kiambishi ngeli inaimarika na kuwa nusu irabu. Hivyo basi viambishi awali vya nomino na kivumishi vinakuwa sawa na vinafanana na vile vya ngeli. Hata hivyo, Myachina (mtaje) alidai kuwa hali hii ni tofauti katika ngeli ya 11 ambapo mizizi ya vivumishi vinavyovumisha nomino huanza na kiambishi awali *m*. Mfano wa nomino katika ngeli hii ni *ufunguo*, inapovumishwa tunapata kirai nomino kama *ufunguo mzito.* Kazi hii ilifaa utafiti huu katika kuchunguza mofolojia ya vivumishi vya Kiimenti. Utafiti huu utatofautiana na kazi ya Myachina (mtaje) kwa sababu ulichunguzi huu ulishughulikia muundo wa vivumishi vya Kiimenti na si vya Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA ilhali kazi ya Myachina (mtaje) haikuongozwa na nadharia yoyote. Aidha, kazi hiyo haikuangazia uamilifu wa maumbo ya vivumishi, jambo ambalo pia lilichunguzwa katika utafiti huu.

Mbaabu (mtaje) aliangazia suala la vivumishi vya lugha ya Kiswahili na kueleza jinsi vinavyochukua viambishi vya ngeli mbalimbali za kimofolojia. Alieleza kuwa vivumishi vingi vyenye asili ya Kibantu hupatikana katika kundi hili. Mifano ya mizizi ya vivumishi hivi ni kama *-eusi, -pya, -refu, -fupi, -eupe* na mizizi mingine. Kwa mfano, katika ngeli ya kwanza huweza kuwa na nomino kama *mtoto*. Nomino hii huweza kuvumishwa na kivumishi *mzuri*. Kiambishi *m* katika *mtoto* cha ngeli ya kwanza hutangulia mzizi wa kivumishi *–zuri* na hivyo kuwa na kivumishi *mzuri* ili kuleta upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya kwanza. Hali hii huweza kubainika katika ngeli mbalimbali. Hata hivyo, si katika ngeli zote ambapo vivumishi huchukua viambishi vya ngeli.

Suala jingine lililoangaziwa na Mbaabu (mtaje) na lilikuwa muhimu katika utafiti huu lilihusu mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea wakati viambishi ngeli huungana na mizizi ya vivumishi ili kuunda vivumishi. Mifano aliyotoa ni:

i) pa + eusi ⟶ peusi ii) Ji + ekundu ⟶ jekundu

Aliendelea kusema kuwa viambishi ngeli vingeambishwa mizizi ya vivumishi iliyo hapo juu, basi tungepata *paeusi* na *jiekundu.* Lakini haikutokea hivyo bali vivumishi vilivyopatikana baada ya kuwekwa viambishi vya ngeli ni *peusi* na *jekundu*. Hali hii inaitwa na Mbaabu (mtaje) mabadiliko ya sauti badala ya kuieleza kama mchakato wa kifonolojia kama inavyoelezwa na Mgullu (mtaje). Mchakato huu unahusu muungano wa irabu. Utafiti huu ulinufaika na kazi ya Mbaabu (mtaje) katika kuchunguza muundo wa vivumishi vya Kiimenti na michakato ya kifonolojia inayotokea katika vivumishi hivyo baada ya mizizi ya vivumishi husika kuambishwa mwanzoni. Hata hivyo, kazi ya Mbaabu (mtaje) ni ya kijumla sana kuhusu vivumishi vya Kiswahili na haikuongozwa na nadharia yoyote ilhali utafiti huu uliongozwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA. Utafiti huu haukuchunguza kategoria yoyote ya maneno katika lugha ya Kiswahili bali ulijikita katika kuchunguza muundo wa vivumishi vya Kiimenti na usarufi unaoainishwa. Aidha, ulichunguza jinsi usarufi huo huzingatia ruwaza mahsusi.

Kazi ya mwanaisimu kama Mgullu (1999) imeangazia mofolojia ya vivumishi mbalimbali. Kwa mfano, mofolojia ya vivumishi vya sifa vyenye asili ya Kibantu kama *mrefu* huundwa kwa kutumia kiambishi awali *m* ambacho hufanana na kiambishi awali cha nomino inayovumishwa na mzizi *-refu* unaobeba maana ya kileksia ya kivumishi. Uundaji wa vivumishi kwa kutumia kiambishi cha upatanisho wa kisarufi cha nomino inayovumishwa unasisitizwa hata na TUKI (2004). Mfano mwingine unahusu mofolojia

ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri ambavyo huundwa kwa kiambishi awali na mzizi wa kivumishi (KA + Mz → V). Hii ni kusema kuna sehemu mbili ambazo ni kiambishi awali au kipatanishi cha wingi cha nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi na mzizi wenyewe. Hii ni mifano ya mofolojia ya vivumishi iliyojadiliwa. Kazi ya Mgullu (1999) ilihusu hata mofolojia ya vivumishi vingine kwa kina. Kazi hiyo ilikuwa muhimu katika kuchunguza mofolojia ya vivumishi vya Kiimenti. Hata hivyo, utafiti huu haukuchunguza vivumishi vya Kiswahili bali vya Kiimenti. Utafiti huu haukujikita kwenye masuala ya mofolojia ya vivumishi vya Kiimenti pekee bali ulipiga hatua na kuchunguza masuala ya sintaksia ya vivumishi husika. Pia, kazi Mgullu (1999) haikuongozwa na misingi ya kinadharia ilhali utafiti huu ulitegemea nadharia ya SGUZ na ile ya FZA ili kuuelekezwa.

Kihore na Wenziwe (wataje) walizungumzia mofolojia ya vivumishi vya Kiswahili kwa kuonyesha vinavyoambishwa na visivyoambishwa. Walieleza kuwa vivumishi vya mkopo, hasa vile vya Kiarabu haviambishwi ilhali vile vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu huambishwa. Walitoa mifano ya vivumishi vilivyoambishwa kama *to-vu, pungu-fu, badhiri-fu, pe-vu* na hata *cho-vu*. Viambishi *vu* na *fu* vinavyopatikana katika vivumishi hivyo huwakilisha sifa. Aidha, kutokana na kivumishi *cho-vu* tunaweza kuunda *m-cho-vu*, kwa mfano *mtu mchovu*. Hapa inaonyesha kuwa kivumishi hiki kina viambishi viwili ambapo kiambishi awali kinawakilisha jina katika ngeli ya kwanza. Miundo miwili ya vivumishi inaainishwa hapa. Hii inaweza kuwasilishwa hivi: (Mz + KT → V) na (KA + Mz + KT → V). Kazi hii ilitufaa kuchunguza mofolojia ya vivumishi vya Kiimenti na utendakazi wa mofimu katika maumbo ya vivumishi vya Kiimenti. Inatofautiana na hii kwa sababu yake ilikuwa ya kijumla sana bila hata ya kuongozwa na

nadharia yoyote. Hii ilijikita katika ukusanyaji wa vivumishi katika lahaja ya Kiimenti na kuchunguza miundo yavyo pamoja na kueleza usarufi uliopatikana katika mofimu zake tukiongozwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA.

Mtaalamu mwingine ambaye aliandika kuhusu muundo wa vivumishi vya Kiswahili ni Mohamed (mtaje). Mwanasarufi huyu aliangazia michakato ya kifonolojia ambayo inaathiri maneno ya Kiswahili kama vivumishi na nomino. Hali hii inaweza kuonyeshwa hivi:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /a/+/a/ → | (wa+ana) | wana | /a/+/e/ → | (wa+enzi) | wenzi |
| /a/+/o/ → | (wa+ote) | wote | /a/+/i/ → | (ma+ingi) | mengi |
| /u/+/u/ → | (mu+ume) | mume | /i/+/i/ → | (vi+ingi) | vingi |

Baadhi ya michakato ya kifonolojia inayojitokeza vivumishi vya Kiswahili vinapoundwa ni kama muungano wa irabu, mvutano wa irabu na udondoshaji wa irabu. Kazi ya Mohamed (mtaje) ilitufaa kuchunguza michakato ya kifonolojia inayotokea vivumishi vya Kiimenti vinapoundwa. Kazi hii haikuongozwa na misingi ya nadharia yoyote. Ilikuwa kazi ya kijumla ambayo iliangazia hata kategoria zingine za maneno pamoja na masuala mengine ya kisarufi. Utafiti huu ulichunguza muundo wa vivumishi vya Kiimenti ili kuainisha mofimu zake huku ukiongozwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA. Aidha, ulijikita katika vivumishi vya Kiimenti katika lahaja ya Kiimenti na si Kiswahili.

Baadhi ya utafiti wa awali wa kiisimu kuhusu lahaja za Kimeru tuliokumbana nao ni ule wa Wa Mberia (1981;1993). Mtaalamu huyu alichunguza konsonanti ya lahaja ya Kitharaka na mofofonolojia arudhi akitafitia kitenzi na nomino katika lahaja husika. Wa Mberia (1981; 1993) aliweka msingi wa kiisimu kuhusu utafiti wa baadaye wa lahaja za

Kimeru kuzingatia mfumo wa kisayansi wenye uwazi na uyakinifu. Katika utafiti aliofanya hakuna pahali ambapo kategoria ya kivumishi cha lahaja ya Kiimenti imezingatiwa. Uchunguzi wa kwanza ulitalii konsonanti na kudhihirisha kuwa lahaja ya Kitharaka ina konsonanti 15 na mbili kati ya hizi ni nusu irabu. Vilevile, alieleza kuwa vokali katika lahaja hiyo ni 7. Utafiti wa pili ulichunguza muundo wa nomino na kitenzi cha Kitharaka. Aidha katika kazi zote mbili alipiga hatua na kueleza michakato ya kifonolojia inayoathiri fonimu za irabu na konsonanti katika lahaja ya Kitharaka. Hali hii ilisaidia utafiti huu kuchunguza michakato hiyo katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Utafiti wa mwanaisimu huyo ulitofautiana na huu kwa sababu ulichunguza lahaja ya Kitharaka ilhali huu ulijikita katika lahaja ya Kiimenti.

Utafiti kuhusu kuathiriana kwa Kiswahili na Kitigania ulifanywa na Mukuthuria (2004). Utafiti wake ulibainisha kuwa lugha ya Kiswahili na lahaja ya Kitigania huathiriana. Utafiti huo ulifaa huu hasa katika sura ya nne ya tasnifu yake. Sehemu hiyo imejikita katika muundo wa nomino za Kiswahili na vitenzi vya Kitigania. Baadhi ya mambo aliyozungumzia katika sura hiyo yalipatia utafiti huu mwelekeo zaidi. Kwa mfano, alidai kuwa kitenzi cha Kitigania hugawika mara tatu. Sehemu ya kwanza inahusu mofu zinazotangulia mzizi, kisha mzizi na mofu ambazo zinatanguliwa na mzizi wa kitenzi. Hivyo, kitenzi kina viambishi awali, mzizi na kisha viambishi tamati kama hivi:

(T $\longrightarrow$ VA + Mz + VT). Katika maelezo yake alieleza uamilifu wa mofu zinazoambishwa mzizi wa kitenzi. Katika sura hiyo pia alieleza mofolojia ya nomino za Kiswahili. Alifafanua kuwa kuna nomino ambazo huambishwa na zingine haziambishwi. Zinazoambishwa ni za aina mbili. Aina ya kwanza ni zile huambishwa mwanzoni mwa mzizi wa nomino. Muundo kama huu hujitokeza (N $\longrightarrow$ VA+Mz). Aina ya pili ni zile

ambazo huundwa kwa mzizi wa nomino kuambishwa mwanzoni na mwishoni kama hivi: (N ⟶ VA+Mz+VT). Aina nyingine ya maumbo ya nomino ni yale ambayo hayaambishwi viambishi vyovyote na husimama kama mzizi huru (N ⟶ Mz). Kwa ujumla Mukuthuria (2004) aliangazia mofolojia ya vitenzi vya Kitigania na nomino za Kiswahili. Utafiti huo ulikuwa muhimu kwa huu katika kuchunguza muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Ulielekeza ugawaji wa kivumishi cha Kiimenti kulingana na mofu zake na kuchunguza usarufi unaowakilishwa na mofu hizo. Hii ni kwa sababu Kiswahili, Kitigania na Kiimenti ni lugha za mpachiko na hufanana kwa mambo fulani ya kimuundo. Utafiti huu ni tofauti na wa Mukuthuria (2004) ulioshughulikia hali ya lugha kuathiriana. Huu ulijikita katika muundo na ruwaza ya mofimu zinazounda vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Aidha, maeneo ya utafiti ni tofauti kwa sababu utafiti huu ulifanyika katika eneo la Imenti ya Kati ukilenga lahaja ya Kiimenti na si Kitigania. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya SGUZ na ile ya FZA ilhali ule wa Mukuthuria (2004) uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na ile ya Mawasiliano. Hizi ni nadharia tofauti za kiisimu.

Lahaja ya Kimwimbi ilitafitiwa na Gacunku (2005) akichunguza upatanisho wa kisarufi unaodhihirika katika lahaja hiyo. Katika utafiti huo alichunguza muundo wa nomino na jinsi inavyodhibiti maneno mengine kama vitenzi na vivumishi (upatanisho wa kisarufi). Kuhusiana na muundo wa kivumishi alieleza kuwa kinaweza kuundwa kwa kutumia viambishi ngeli mbalimbali. Kwa hivyo muundo unaoweza kudhihirika ni:

V ⟶ KA + Mz. Alizidi kueleza kuwa mzizi wa kivumishi huambishwa konsonanti, voweli au konsonanti na voweli ili kuunda kivumishi kamilifu kutegemea ngeli mbalimbali. Kwa kutumia mzizi wa kivumishi **{-kue}** (-fupi) aliibuka na vivumishi

hivi kulingana na ngeli: **omokue** (mfupi) /o-mo-kue/, **babakue** (wafupi) /ba-ba-kue/, **emekue** (mifupi) /e-me-kue/, **rerekue** (fupi) /re-re-kue/, **mamakue** (mafupi) /ma-ma-kue/. Mifano hii inaonyesha kuwa mizizi ya vivumishi vya Kimwimbi huweza kuambishwa viambishi awali vingine isipokuwa vya ngeli. Utafiti huu ulielekeza uchunguzi wa muundo wa kivumishi cha Kiimenti na jinsi unavyoathiriwa na viambishi ngeli katika ngeli mbalimbali. Aidha, utafiti wa Gacunku (mtaje) uliongozwa na nadharia ya FZA ambayo ni mojawapo ya nadharia zilizoongoza utafiti huu. Utafiti huu haukuchunguza lahaja ya Kimwimbi bali ulijikita katika lahaja ya Kiimenti. Aidha, eneo ambamo utafiti huu uliendeshwa ni tofauti na alilo shirikisha Gacunku (mtaje).

Utafiti wa kiisimu ambao unahusu lahaja ya Kiĩgembe ni kama ule wa Kanake (2013). Msomi huyu alichunguza jinsi Kiswahili huathiriwa na Kiigembe kwa wanafunzi wa jamii ya Waĩgembe ambao hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Alibainisha kuwa Kiĩgembe huathiri Kiswahili kwa kuchopeka baadhi ya sauti na kudondosha zingine. Sura ya mwisho ya utafiti wake ndiyo ina umuhimu katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu mtafiti alipendekeza uchunguzi ufanywe kuhusu masuala ya mofolojia katika lahaja za Kimeru. Jambo hili lilitia ghera ya kuchunguza mofolojia ya vivumishi vya Kiimenti na hata sintaksia yavyo. Utafiti wa Kanake (mtaje) ni tofauti na huu ambao ulijikita katika lahaja ya Kiimenti ambayo ni tofauti na Kiĩgembe na huzungumzwa katika maeneo tofauti. Aidha, huu hautukutafiti masuala ya kuathiriana kwa lugha kama katika utafiti wa Kanake (mtaje). Utafiti aliofanya uliongozwa na misngi ya nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ambayo ni tofauti na ile ya SGUZ na FZA ambazo zilielekeza utafiti huu.

Utafiti wa kiisimu kuhusu lahaja ya Kiimenti ni ule wa Kanana (2016). Msomi huyu alichunguza jinsi mchakato wa uradidi hutumika katika uundaji wa nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi vya Kiimenti. Katika utafiti huo aligundua uradidi wa sehemu fulani za neno kama mzizi huweza kutumika kuunda neno lingine la Kiimenti. Haja ya utafiti huu si kuchunguza jinsi uradidi hutumika kuunda maneno ya kategoria mbalimbali za Kiimenti bali ulijikita katika vivumshi vya lugha husika pekee. Katika utafiti huo mtaalamu huyu aligundua kuwa vivumishi vya sifa kama *ũmũraja* [omoraja] (mrefu), *ũmũkuĩ* [omokue] (mfupi), *ũmũthongi* [omoθɔŋgi] (mrembo) na *intune* [intunɛ] (nyekundu) huweza kuunda vivumishi vingine kama *ũmũrajaraja* (mrefu zaidi), *ũmũkuakuĩ* [omokuakue] (mfupi zaidi), *ũmũthongathongi* [omoθɔŋgaθɔŋgi] (mrembo zaidi) na *intunatutune* [intunatunɛ] (nyekundu zaidi). Utafiti huo ulikuwa muhimu kwa sababu ulielekeza huu kuchunguza muundo wa vivumishi viradidi vyenye dhana ya ulinganishi katika Kiimenti. Utafiti huu ulipiga hatua na kuainisha usarufi unaopatikana katika vivumishi hivyo.

Makala ya Biwott na Ong'onda (2020) ni kazi inayoangazia mchakato wa uradidi katika uundaji wa maneno ya kategoria mbalimbali katika lahaja ya Kipsigis. Wataalamu hawa wametumia nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi kueleza aina za uradidi katika lahaja ya Kipsigis. Aidha, wameonyesha jinsi mchakato wa uradidi nusu na kamili hubainika katika lahaja husika. Kazi hiyo ilisaidia utafiti huu kueleza mchango wa uradidi katika uundaji wa vivumishi vya Kiimenti. Tofauti ya utafiti huu na kazi hiyo ni kuwa, huu ulichunguza uradidi katika muundo wa vivumishi vya Kiimenti na si kategoria zote za maneno ambazo walichunguza. Pia, utafiti huu ulizingatia lahaja ya Kiimenti na si Kipsigis. Hatimaye utafiti huu ulifanyika katika eneo tofauti na walilofanyia utafiti wao.

### 2.2.4 Usarufi Unaoainishwa katika Maneno mbalimbali

Usarufi ni dhana ambayo hujeleza maana inayowakilishwa na mofu zinazopatikana katika kategoria mbalimbali za maneno. Maana hii ndiyo hujulikana kama mofimu. Mofu katika vitenzi vya Kiswahili huweza kuwakilisha njeo, nafsi, mtenda au usarufi mwingine.Utafiti wa kiisimu ulioangazia usarufi katika vitenzi vya Kitigania ni kama ule wa Mukuthuria (1997). Kwa kufanya hivyo msomi huyu alitoa mchango adhimu kuhusu isimu ya lahaja ya Kitigania na lugha za Kiafrika kwa ujumla. Katika utafiti wake mtaalamu huyu alijikita katika njeo za lahaja ya Kitigania. Kazi hiyo ina uhusiano na utafiti huu. Hii ni kwa sababu imechanganua vitenzi vya lahaja ya Kitigania kimofemiki na kudhihirisha utendakazi wa mofimu za njeo na usarufi wa zingine. Mukuthuria (1997) alisema kuwa kitenzi cha Kitigania huainisha mofimu za nafsi ya mtenda, njeo, ukanushi, nafsi ya mtendwa, mzizi wa kitenzi, kauli mbalimbali za mnyambuliko na kiishio. Hali hii huweza kubainika kwa kuchanganua vitenzi vifuatavyo vya Kitigania:

**ũkathoma** /ũ -ø-ka-thom-a/ [okaθɔma] (utasoma)

{ũ -} mofimu ya nafsi ya pili ya mtenda

{-ø-} mofimu ya wakati uliopo

{-ka-} mofimu ya ukanushi

{-thom-} mzizi wa kitenzi

{-a} kiishio

**ũkamũrĩmĩra** /ũ -ø-ka-mũ-rĩm-ĩr-a/ [okamoremera] (usimlimie)

{ũ -} mofimu ya nafsi ya pili ya mtenda

{-ø-} mofimu ya wakati uliopo

{-ka-} mofimu ya ukanushi

{-mũ -} mofimu ya nafsi ya mtendewa

{-rĩm-} mzizi wa kitenzi

{-ĩr-} mofimu ya mnyambuliko – hali ya kutendea

{-a} kiishio

Hali ya vitenzi vya Kitigania kuchanganuliwa kimofemiki ilitutia ari kuchunguza kupatikana kwa kategoria mbalimbali za kisarufi katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Hii ni kwa sababu lahaja ya Kiimenti tuliyoichunguza na Kitigania zinahusiana kimuundo. Aidha, utafiti wa Mukuthuria (1997) ni muhimu kwa upande wa nadharia. Utafiti aliofanya ulipendekeza nadharia ya SGUZ aliyotumia ijaribiwe kuongoza utafiti katika ngazi za fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki katika lugha za Kibantu. Hii ni baada ya kugundua ufaafu wa nadharia hiyo katika kuongoza utafiti wa lahaja ya Kitigania. Kwa hivyo, nadharia ya SGUZ ilizingatiwa kuelekeza utafiti huu ili kudhihirisha mofimu zinazopatikana katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti na jinsi zilivyopangiliwa katika maneno hayo. Aidha, nadharia ya FZA ilitumika kuchunguza michakato ya kifonolojia inayobainika katika muundo wa vivumishi husika.

Totauti ya utafiti huu na wa Mukuthuria (1997) ni kwamba, huu haukuchunguza muundo wa kitenzi ili kubainisha njeo bali ulijikita katika muundo wa kategoria nyingine ya maneno ambayo ni kivumishi. Aidha, ulipiga hatua zaidi na kuchunguza mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti na kuandika sheria zinazotawala mpangilio huo.

Utafiti uliofanywa na Salesio (2010) kuhusu usarufi katika kitenzi cha Kichuka ulibainisha kuwa kitenzi hicho huweza kuainisha mofimu mbalimbali. Hizi ni kama mofimu za kuainisha wakati kitendo hutokea, nafsi, njeo, ukanushi, mzizi, mofu jenzi,

mnyambuliko na kiishio. Vitenzi hivi kutoka lahaja ya Kichuka hudhihirisha usarufi huo vikichanganuliwa kimofemiki.

**nĩmagũtũrĩmĩra** /nĩ-ma-gũ-tũ-rĩm- ĩr-a/[nemagotoremera] (wanatulimia)

{nĩ -}mofimu ya kibainishi

{-ma-} mofimu ya nafsi ya mtenda (wingi)

{-gũ -} mofimu ya wakati uliopo

{-tũ-} mofimu ya mtendewa (wingi)

{-rĩm-} mzizi wa kitenzi

{-ĩr-} mofimu ya mnyambuliko wa kitenzi (jinsi ya kutendea)

{-a} kiishio

**ntĩgakũrugĩra** /n-tĩ-ga-kũ-rug-ĩr-a/[ntegakorugera] (sitakupikia)

{n-}mofimu ya nafsi ya kwanza (umoja)

{-tĩ-} mofimu ya ukanushi

{-ga-} mofimu ya wakati ujao

{-kũ -} mofimu ya kitenzi jina

{-rug-} mzizi wa kitenzi

{-ĩr-} mofimu ya mnyambuliko wa kitenzi (jinsi ya kutendea)

{-a} kiishio

Utafiti wa Salesio (mtaje) ulitufaa kuchunguza usarufi katika vivumishi vya Kiimenti. Hii ni kwa sababu Kichuka na Kiimenti ni lahaja za Kimeru na hushabihiana kwa mambo fulani kama mofolojia ya maneno yake. Nadharia ya SGUZ iliyotumiwa na mwanaisimu huyu ndiyo ilielekeza utafiti huu. Utafiti wa Salesio (mtaje) ulitofautiana na huu ambao ulichunguza ruwaza ya mofimu katika vivumishi vya Kiimenti na si vitenzi vya Kichuka.

Aidha, huu ulielekezwa na nadharia ya FZA kubainisha michakato ya kifonolojia katika vivumishi husika.

### 2.2.5 Ruwaza ya Usarufi katika Maneno Mbalimbali

Ruwaza ya usarufi hurejelea mpangilio wa mofimu mbalimbali katika maneno ya lugha yoyote ile. Hali hii imeangaziwa na Mukuthuria (1997) akiangazia ruwaza ya mofimu zinazopatikana katika vitenzi vya Kitigania. Amethibitisha kuwa mofimu katika lahaja hiyo hupangwa kwa kuzingatia ruwaza maalumu. Kazi yake inaonyesha kuwa kila mofimu huwa na mazingira yake katika kitenzi. Kwa mfano, katika kitenzi kama **akũrĩra** [akorera] (amelia) kuna mofimu mbalimbali zinazotokea katika mazingira tofauti kwenye kitenzi hicho. Mofimu katika kitenzi hicho ni kama **{a-}, {-kũ-}, {-rĩr-}** na **{-a}.** Katika mazingira ya kwanza **{a-}** ni mofimu ya nafsi ya tatu ya mtenda katika umoja. Mazingira ya pili ni**{-kũ-}** ambayo ni mofimu ya njeo iliyopita lakini si muda mrefu sana. **{-rir-}** huwakilisha mofimu ya mzizi wa kitenzi na imechukua nafasi ya tatu katika kitenzi hicho. Kiishio huwakilishwa na mofimu **{-a}.** Kitenzi **akũrĩra** [akorera] (amelia) huweza kuwa na nafsi ya mtendwa na mnyambuliko. Ikifanyika hivi tutakuwa na kitenzi **akũmũrĩrĩra** [akomorerera] (amemlilia) ambapo mofimu ya nafsi ya tatu ya mtenda katika umoja itatokea katikati ya mofimu ya njeo na mzizi wa kitenzi. Mofimu hii ni {**-mũ-**}. Mofimu ya mnyambuliko nayo itatokea kati ya mzizi na kiishio. Mofimu hii ni**{-ĩr-}.** Hali hii inaweza kueleweka zaidi katika uchanganuzi wa kitenzi hiki kimofemiki hapa chini.

**akakũmũrĩrĩra** [akomorerera] /a-kũ-mũ-rĩr-ĩr-a/ (anamlilia)

{a-} mofimu ya mtenda/nafsi ya tatu/umoja

{-kũ-} mofimu ya njeo iliyopita lakini si muda mrefu sana

{-mũ- } mofimu ya mtenda/nafsi/umoja

{-rĩr-} mzizi wa kitenzi

{-ĩr-} mofimu ya mnyambuliko (kauli ya kutendea)

{-a} kiishio.

Kitenzi **ũkarĩra** [okarera] (usilie) /u-ø-ka-rĩr-a/ kiko katika hali ya kukanusha. Mpangilio wa mofimu katika kitenzi hicho huzingatia ruwaza maalumu. Kitenzi hicho kikichanganuliwa kinaweza kuwa na mofimu **{ũ-}** ambayo ni nafsi ya mtenda (umoja), mofimu kapa **{ø}** huwakilisha njeo, **{-ka-}**ni mofimu ya kukanusha, {**-rĩr-}** ni mofimu ya mzizi wa kitenzi na **{-a}** kiishio.

Utafiti wa Mukuthuria (1997) ulielekeza uchunguzi wa jinsi mpangilio wa mofimu za vivumishi vya Kiimenti huzingatia mpangilio mahsusi. Aidha, utafiti huo ulifaa zaidi kwa sababu nadharia iliyoongoza utafiti huo ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu haukuchunguza kitenzi cha lahaja ya Kitigania bali kivumishi cha lahaja ya Kiimenti. Pia, ulitumia nadharia ya FZA ili kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayoathiri muundo wa vivumishi vya Kiimenti.

Salesio (mtaje) alichunguza usarufi katika kitenzi cha Kichuka. Aliweza kubainisha kuwa mpangilio wa mofimu katika kitenzi hicho huzingatia mpangilio mahsusi huku kila mofimu ikipangiliwa katika mazingira yake. Mpangilio huo huweza kubainika katika kitenzi kama **nĩararĩmĩre** [neararemerɛ] (alilima) ambacho kinaweza kuchangunuliwa kimofemiki na kuwa **nĩ-a-ra-rĩm-ĩr-e**. Katika kitenzi hicho **{nĩ-}** ni mofimu ya kwanza ambayo ni kibainishi kinachoelekeza njeo ya utendekaji wa kitendo. Nafasi ya pili huchukuliwa na mofimu **{-a-}** ambayo ni nafsi ya mtenda (umoja) na hata ngeli ya sintaksia ya 1 (**A)** katika lahaja hiyo. Nafasi ya tatu ni mofimu **{-ra-}** ambayo ni mofimu ya njeo iliyopita. Mzizi wa kitenzi huwakilishwa na **{-rĩm-}** na huwa katika nafasi ya nne.

**{-ĩr-}** ni mofimu ya mnyambuliko na huwa katika nafasi ya tano ilhali mofimu ya mwisho ni **{-e**}na ni kiishio. Inafaa ieleweke kuwa si wakati wote ambapo kitenzi cha Kichuka kitakuwa na kibainishi. Ikitokea hivyo, basi nafasi ya kwanza katika kitenzi hicho huwa na mofimu ya nafsi/mtenda/ngeli. Katika lahaja hiyo alomofu **{-tĩ-}**na**{-ta-}** hutumika kukanusha katika kitenzi cha Kichuka na hupatikana katika ruwaza ya pili. Uchanganuzi wa vitenzi vifuatavyo katika lahaja hiyo unaweza kubainisha hali hiyo.

**atĩruga** [ateruga] /a-tĩ-rug-a/ (hatapika)

{a-} nafsi/mtenda/ngeli

{-tĩ-} mofimu ya ukanushaji

{-rug**-}** mzizi wa kitenzi

{-a} kiishio

**atiramũringa** [ateramoringa] /a-tĩ-ra-mũ-riŋg-a/ (hajampiga)

{a-} nafsi/mtenda/ngeli

{-tĩ-} ukanushaji

{-ra} wakati timilifu

{-mũ-} mtendwa

{-ring-} mzizi wa kitenzi

{-a} kiishio

**ntarĩma** [ntarema] /n-ta-rĩm-a/ (sitalima)

{n-} nafsi

{-ta-} ukanushaji

{-rĩm-} mzizi wa kitenzi

{-a} kiishio

**ntakinya** [ntakiɲa] /n-ta-kiny-a/ (sijafika)

{n-}nafsi

{-ta-} ukanushaji

{-kiny-} mzizi wa kitenzi

{-a} kiishio

Utafiti wa Salesio (mtaje) ulisaidia uchunguzi wa ruwaza ya usarufi katika vivumishi vya Kiimenti. Hata hivyo, ni tofauti na huu ambao ulichunguza lahaja ya Kiimenti bali si Kichuka. Aidha, ulichunguza vivumishi vya Kiimenti na si vitenzi vya Kichuka.

#### 2.2.6 Mpangilio wa vivumishi katika Tungo

Kuhusiana na mpangilio wa vivumishi katika sentensi Ashton (mtaje) alionyesha mipangilio mbalimbali. Hali hii inadhihirika katika mifano ifuatayo:

i) Kitu namna *gani hiki*? (kiulizi, kiashiria)

ii) Macho *yangu mawili* yanauma. (kimilikishi, idadi)

iii) Safari *yote hii* imekuwa ya taabu. (pekee, kiashiria)

iv) Mashamba *yangu haya mawili* hayana rotuba. (kimilikishi, kiashiria, idadi)

v) Ndugu *zake wawili wa kike* wameondoka. (kimilikishi, idadi, ‘a’ unganifu)

Mifano ya sentensi iliyotolewa inaonyesha mipangilio mbalimbali. Sentensi ya kwanza inaonyesha kuwa kivumishi kiulizi hutangulia kivumishi kiashiria katika sentensi iwapo vyote vitatumika katika sentensi moja. Sentensi ya pili inaonyesha mpangilio ambapo kivumishi kimilikishi hutangulia kile cha idadi iwapo vyote viwili vitatokea pamoja katika sentensi. Katika sentensi ya tatu kivumishi cha pekee kinatangulia kile cha kuashiria vikitokea vyote viwili katika sentensi moja. Aidha, sentensi ya nne inaonyesha safu ya vivumishi vya kumiliki, kiashiria na idadi vikifuatana katika hali hiyo. Sentensi

ya mwisho inaonyesha mpangilio wa kivumishi kimilikishi, idadi na a -unganifu vikifuatana katika mpangilio huo iwapo vitatokea katika sentensi moja. Kazi ya Ashton (mtaje) ilifaa katika uchunguzi wa mpangilio wa vivumishi katika sentensi za lahaja ya Kiimenti. Hata hivyo, ni tofauti na utafiti huu ambao ulijikita katika Kiimenti na si Kiswahili.

Katika safu ya vivumishi, Wilson (mtaje) alisema vivumishi vya idadi ndivyo huja mwisho; na huweza kutanguliwa na vivumishi vingine kama vya sifa. Hata hivyo, katika kirai cha tatu katika mifano ifuatayo inaonekana kivumishi cha idadi huweza kutangulia kiashiria. Mpangilio huu unadhihirika katika mifano hii:

i) Mikate *mitamu michache*… (sifa, idadi)

ii) Wanyama *wakubwa wanne* … (sifa, idadi)

iii) Watoto *wadogo kumi* na *wanne hawa*… (sifa, idadi, idadi, kiashiria)

iv) Mpishi *hodari mmoja* … (sifa, idadi)

Aidha, Wilson (mtaje) ameainisha vivumishi viulizi mbalimbali ambavyo hutokea kuzingatia mpangilio maalumu kwenye sentensi. Hivi ni kama:

a) ‘Gani’ ambacho hujitokeza kikiwa cha mwisho kwenye safu ya vivumishi kwenye sentensi. Kwa mfano: *Mti mrefu gani ulianguka*? Gani hutokea hata mwisho wa sentensi kama: *Unataka gari gani*? Sentensi ya kwanza pia inaonyesha kuwa kivumishi cha sifa huweza kufuatwa na kiulizi kwenye sentensi.

b). ‘Ngapi’ – Hutumika mwisho wa safu ya vivumishi kwenye sentensi. Kwa mfano, *Watu weusi wangapi walifika*? Hii inaonyesha ruwaza ya kivumishi kiulizi kutanguliwa na kile cha sifa iwapo vyote viwili vitatokea pamoja kwenye sentensi.

Maoni ya Wilson (mtaje) ni kuwa vivumishi vimilikishi huwa na mpangilio wa kufuata nomino inayoelezwa. Anasisitiza kuwa vivumishi hutanguliwa na nomino katika sentensi huku kivumishi kimilikishi kikitangulia safu ya vivumishi vingine. Katika safu ya vivumishi kwenye sentensi anaendelea kusema kuwa vivumishi viashiria ndivyo huwa vya mwisho. Hali hii inadhihirika katika mifano ya virai vifuatayo ambapo kuna ruwaza ya kivumishi kiashiria kutanguliwa na kile cha sifa katika sentensi iwapo vitatumika vyote pamoja.

a). Mpishi *mzuri yule* … (sifa, kiashiria)  b). Miti *mirefu hii*… (sifa, kiashiria)

c). Mkate *mbovu huu*… (sifa, kiashiria)

Kazi ya Wilson (mtaje) iliongoza uchunguzi wa ruwaza mbalimbali za vivumishi katika sentensi za lahaja ya Kiimenti. Kazi hiyo ilihusu mpangilio wa vivumishi katika sentensi za Kiswahili na kategoria nyingine za maneno. Utafiti huu haukushughulikia hayo bali ulijikita katika mpangilio wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti.

Kazi ya mwanaisimu kama Mbaabu (mtaje) imeangazia matumizi ya nomino katika ngeli mbalimbali. Ametunga sentensi akitumia nomino za ngeli mbalimbali pamoja na vivumishi vya Kiswahili. Sentensi alizotunga zinadhihirisha mpangilio fulani katika matumizi ya vivumishi. Mifano ya sentensi ni kama:

i). Mtoto *yule mfupi* anaruka. (kiashiria, sifa)

N V V T

ii). Watoto *wale wafupi* wanaruka. (kiashiria, sifa)

N V V T

iii). Kisu *kile kikali* kimemkata. (kiashiria, sifa)

N V V T

iv). Visu *vile vikali* vimewakata. (kiashiria, sifa)

N V V T

Hali inayojitokeza hapa ni kuwa kivumishi cha kuashiria kinatangulia kile cha sifa katika sentensi ikiwa vyote vimetumika katika sentensi pamoja. Ruwaza nyingine inayodhihirika katika kazi ya Mbaabu (mtaje) inahusu matumizi ya vivumishi vya kumiliki na vile vya sifa. Iwapo vivumishi hivi viwili vimetumika pamoja katika sentensi, kimilikishi hutangulia kile cha sifa. Kwa mfano:

i). Kiti *changu kizuri* kimevunjika. (kimilikishi, idadi)

N V V T

Kazi ya Mbaabu (mtaje) ilifaa kuchunguza ruwaza mbalimbali za vivumishi vinapotumika katika tungo za Kiimenti. Kazi hiyo iliangazia mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti. Pia, ulipiga hatua zaidi na kuandika sheria zinazotawala mpangilio huo tofauti na ya Mbaabu (mtaje) ambayo haikuzama katika suala hili.

Kazi ya Mochiwa (2000) imeangazia ruwaza mbalimbali zinazozingatiwa katika kupangilia vivumishi katika sentensi za Kiswahili. Ruwaza moja ni ile ya mkururo wa vivumishi vya sifa katika sentensi moja. Mfano mmoja ni kama huu: *Mwalimu mzuri mrefu na mwembamba anazungumza*. Maoni ya mwanasarufi huyu ni kuwa mpangilio wa vivumishi vya sifa katika sentensi hii vinadhibitiwa na maana inayowasilishwa na vivumishi vilivyotumika. Anadai kuwa katika muktadha wa semantiki uzuri wa kitu huweza kuchangiwa na kukamilishwa na vivumishi vingine kama *mrefu* na *mwembamba* katika mfano tuliotoa hapo juu. Aidha, uzuri wa mti huweza kuchangiwa na *urefu* na *wembamba*, au *urefu* na *unene* wake. Anasisitiza kuwa mawazo kama haya humfanya

mtumiaji wa lugha kupangilia kivumishi *mzuri* kikitangulia vivumishi vingine vya sifa katika sentensi kama tuliyodokeza hapo juu. Mawazo sawa na haya yalitolewa na Wales (2014) anaposema kuwa vivumishi vya sifa huzingatia mpangilio maalumu katika sentensi na havipangwi kiholela. Anasisitiza kuwa maana inayoibushwa au masuala ya semantiki kama saizi, rangi na umri inafaa kutiliwa maanani. Kwa maoni yake ili maana inayofaa kuwasilishwa isionekane kuwa na dosari, kivumishi cha sifa ambacho kinaangazia saizi au kiwango kinafaa kutangulia kile cha rangi katika sentensi. Katika muktadha huu basi, *Mtu* ***mdogo mweusi*** *amekuja* ingefaa kuliko *Mtu* ***mweusi mdogo*** *amekuja*.

Ruwaza zingine za mfuatano wa vivumishi katika sentensi ambazo Mochiwa (mtaje) aliangazia ni kama kivumishi kimilikishi kutangulia kivumishi cha sifa katika sentensi. Kwa kuzingatia ruwaza hii tunaweza kupata sentensi kama hii.

Gari langu zuri limeibwa.

*Gari zuri langu limeibwa.

Aidha, alisema kivumishi cha sifa hutanguliwa na kile cha idadi katika sentensi. Kwa mfano:

Watu watatu wazuri wameondoka.

* Watu wazuri watatu wameondoka.

Vilevile, alisema kuwa kivumishi kimilikishi hutangulia kile cha idadi katika sentensi. Kwa mfano:

Magari yangu mawili yamefika.

*Magari mawili yangu yamefika.

Hatimaye, Mochiwa (mtaje) aliibuka na ruwaza hii ambayo ni sheria ya jumla ya kuelezea ruwaza hizi tatu.

**Kivumishi kimilikishi; kivumishi cha idadi; kivumishi cha sifa.**

Sheria hii ina maana kuwa kivumishi kimilikishi kinaweza kutangulia kivumishi cha sifa katika sentensi kama katika mfano wa kwanza. Pia, kivumishi cha idadi huweza kutangulia kile cha sifa kama katika mfano wa pili. Vilevile, kivumishi kimilikishi huweza kutangulia kile cha idadi katika sentensi kama katika mfano wa tatu.

Mochiwa (mtaje) pia amebainisha kuwa kivumishi cha sifa huweza kutumika pamoja na a-unganifu katika sentensi moja. Inapotokea hivi kivumishi cha sifa ndicho hutanguliwa na nomino na kisha a - unganifu. Hali hii inaweza kudhihirishwa kupitia mfano wa sentensi ufuatao:

Gari zuri la baba limeharibika.

*Gari la baba zuri limeharibika.

Sentensi ya pili katika mifano iliyo hapo juu ina kasoro. Ruwaza kama hiyo haifai. Neno zuri katika hali hiyo halivumishi gari.

Kazi ya Mochiwa (mtaje) ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ilifaa uchanganuzi wa ruwaza mbalimbali za vivumishi vya Kiimenti katika sentensi na kuibuka na sheria zinazodhibiti hali hiyo. Hata hivyo, kazi hiyo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu ulijikita katika lahaja ya Kiimenti na si Kiswahili. Aidha, kazi hiyo haikuongozwa na misingi ya nadharia yoyote ilhali utafiti huu ulielekezwa na nadharia ya SGUZ na nadharia ya FZA.Vilevile, utafiti huu ulichunguza sentensi zaidi za Kiimenti na kuibuka na ruwaza mbalimbali katika utafiti huu.

Kulingana na Philipo (mtaje); Philipo na Kuyenga (2017) vivumishi vitatu vya sifa hupangiliwa katika sentensi moja kuvumisha nomino. Wanaendelea kudai kuwa hii ni sifa moja ya vivumishi vya Kiswahili. Hali ya vivumishi zaidi ya viwili kufuatana katika sentensi yaelekea kupingwa na Wilson (mtaje). Kwa maoni yake si rahisi kwa vivumishi zaidi ya viwili kufuatana katika sentensi moja. Hili ni dai ambalo lina ukweli kiasi kwa sababu watumiaji wengi wa lugha hutumia kivumishi kimoja au viwili vikifuatana. Hata hivyo anakiri kuwa kuna uwezekano wa kupata ruwaza ya vivumishi zaidi ya viwili katika sentensi moja alipotoa mfano wa kirai kama hiki:

Watoto *wadogo wazuri wachache hawa*… (sifa, sifa, idadi, kiashiria)

Kuhusu mpangilio wa vivumishi katika sentensi Mgullu (1999) alidokeza kuwa kivumishi kiulizi na kiashiria vikitumika pamoja katika sentensi, basi kiulizi hutangulia kiashiria. Hali hii inadhihirika katika sentensi hii:

i). Gari *gani hili*? (kiulizi, kiashiria)

Kazi ya Mgullu (1999) ilifaa katika uchunguzi wa ruwaza mbalimbali za matumizi ya vivumishi vya Kiimenti kwenye utafiti huu. Utafiti huu ulijikita katika ruwaza nyingine mbalimbali zilizodhihirika katika lahaja ya Kiimenti na si Kiswahili. Maelezo ya Mgullu (1999) ni ya kijumla sana na hayakuongozwa na misingi yoyote ya kinadharia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya SGUZ na FZA ili kuafikia malengo ya utafiti.

Kuhusiana na mpangilio wa vivumishi katika sentensi, Habwe na Karanja (wataje) wameonyesha ruwaza fulani inayozingatiwa na vivumishi walipokuwa wakieleza jinsi nomino huleta upatanisho kwa maneno mengine katika sentensi. Wametoa mfano huu:

i). Wachezaji *wale wawili warefu* walishinda vikombe *viwili vipya* vilivyonunuliwa.

N V V V T N V V T

Katika sentensi hiyo, ruwaza mbili zinajitokeza. Kwanza nomino ikitangulia katika sentensi huweza kufuatwa na kivumishi kiashiria, kisha cha idadi na hatimaye kile cha sifa iwapo vyote vitatu vitatumika katika sentensi moja. Ruwaza ya pili ni katika kishazi tegemezi cha pili ambapo nomino vikombe inafuatwa na kivumishi cha idadi na kisha cha sifa. Hii inaonyesha kuwa iwapo kivumishi cha idadi na sifa vitatumika katika sentensi na nomino ikivitangulia, basi kile cha idadi kitatangulia kile cha sifa. Kazi hiyo iliongoza uchunguzi wa ruwaza kama hizo katika lahaja ya Kiimenti. Utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza ruwaza hizo ukitumia data kutoka lahaja ya Kiimenti.

## 2.3 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umetumia nadharia mbili. Hizi ni nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi (SGUZ) (Chomsky, 1957; 1965) na ile ya Fonolojia Zalishi Asilia (Hooper, 1976). Nadharia ya SGUZ ndiyo nadharia kuu ilhali nadharia ya FZA inasaidia katika kuelekeza utafiti huu pale ambapo nadharia kuu haikuweza. Nadharia ya SGUZ ilifaa kueleza mofimu na ruwaza zake katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa jinsi hii ilijaribu kueleza muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Hata hivyo, katika mipaka ya mofu kunapatikana michakato mbalimbali ya kifonetiki inayoathiri irabu na konsonanti katika mofu husika. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kujumuisha nadharia ya FZA ili kueleza kikamilifu muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Licha ya nadharia hii kushughulikia michakato ya kifonolojia katika kivumishi cha Kiimenti inabainisha muundo wa nje na wa ndani wa kivumishi husika. Ifahamike kuwa muundo wa ndani huonyesha mofu zenye usarufi kuliko muundo wa nje ambao umepata athari nyingi za michakato ya kifonolojia. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kutumia nadharia mbili kwa sababu moja haingeweza

kuongoza utafiti huu kikamilifu. Nadharia zilizotumika zinakamilishana na kuchangiana ili kuongoza utafiti huu.

### 2.3.1 Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi

Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi (SGUZ) iliasisiwa na Chomsky (1957; 1965) ili kukabili baadhi ya matatizo ya uchanganuzi hasa wa sentensi yaliyozuka baada ya Sarufi Miundo Virai. Hii ndiyo sababu Sarufi Miundo Virai husemekana kuwa msingi wa SGUZ. Sarufi miundo virai ilishughulikia uchanganuzi wa vijenzi vya sentensi au tungo bila kuonyesha uhusiano wa vijenzi hivyo. Aidha, Sarufi Miundo Virai haikutambua kuwa sentensi moja huweza kuwa na umbo la ndani na umbo la nje. Mambo haya yote yaliweza kuelezwa kwa kuzingatia nadharia ya SGUZ.  Kwa mujibu wa sarufi miundo virai sentensi kama: *Mama anamchapa mtoto* na *Mtoto anachapwa na mama* zilionekana kama sentensi tofauti zenye upekee na zisizohusiana. Hata hivyo, SGUZ hutambua kuwa sentensi hizo zina uhusiano na zinatokana na umbo moja la ndani. Nadharia ya SGUZ hudokeza kuwa ili kupata umbo la nje kutoka umbo la ndani, kuna sheria za kuzingatiwa zinazojulikana kama sheria za ugeuzi. Mafanikio makubwa ya SGUZ baada ya kuasisiwa ni kuwa iliwezekana kuonyesha uhusiano kati ya maumbo mbalimbali ya sentensi au tungo na uhusiano kati ya sentensi na nyingine. Aidha, iliwezekana kueleza utata wa sentensi kwa kuzingatia maumbo yake ya ndani (Massamba na Wenzie, 2001).

Chomsky (1965) katika kitabu chake ‘*Aspects of* the *Theory Syntax’* alihimiza ujuzi wa mzungumzaji mzawa wa lugha na kupunguza hali ya kutilia sarufi mkazo. Aliendelea kudai kuwa lugha inahusu msemaji mmoja na hapo akatofautiana na Ferdinand de Saussure aliyesema mfumo lugha unahusu jamii nzima. Sheria ambazo mzungumzaji mzawa anazijua aliziita umilisi na hali ya kutumia sheria hizo akaiita utendaji. Alizidi

kudai kuwa wanaisimu walipaswa kutafiti umilisi wa msemaji mzawa kwa sababu utendaji huweza kuathiriwa na mambo mengine kama ugonjwa, ghadhabu, hofu na uchovu. Kwa hivyo, utendaji una makosa mengi; na hivyo, hali halisi ya lugha haionyeshwi. Baadhi ya sifa za nadharia hii ni kuwa sheria chache huweza kutumika kuzalisha sentensi nyingi ambazo haziwezi kuhesabika. Aidha, huonyesha sentensi sahihi na zisizo sahihi na msemaji mzawa wa lugha fulani (Habwe na Karanja, wataje).

Nadharia ya Sarufi Geuza Umbo Zalishi ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu licha ya kutumika kuchambua sentensi na kueleza muundo wazo, pia iliweza kutumika kuchambua muundo wa vipashio vidogo vya sentensi kama vivumishi vya Kiimenti tulivyozingatia katika utafiti huu.

Nadharia ya SGUZ ina mihimili mbalimbali. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya SGUZ ni kueleza hali ya kuwepo kwa uhusiano wa nje na wa ndani wa vipashio mbalimbali vya kisarufi. Baadhi ya vipashio hivi ni vivumishi vya lahaja ya Kiimenti ambavyo huwa na umbo la ndani na nje. Katika kueleza mofu za vivumishi vya lahaja ya Kiimenti umbo la ndani ni muhimu ili kuchanganua mofu za maneno hayo na kueleza usarufi wa kila mofu. Kauli hii inashadidiwa na Mgullu (1999) aliposema kuwa ili kubainisha mofu na alomofu za neno, umbo la ndani la neno hutumika kwa sababu umbo la nje huweza kuwa na athari za mikondo ya kifonolojia au ya kimofofonolojia. Aidha, maumbo ya ndani huonyesha mofu kuliko yale ya nje. Kauli ya nadharia ya SGUZ kueleza kuwa neno huwa na muundo wa ndani na nje imejadiliwa zaidi na Mukuthuria na Chimerah (2004). Aidha, SGUZ husisitiza utumiaji wa umbo la ndani katika uchanganuzi wa mofimu zinazounda neno (Mukuthuria, 1997; Mukuthuria na wenziwe, 2016). Kwa hivyo, kwa kuzingatia nadharia ya SGUZ inawezekana kuchambua vivumishi vya lahaja ya Kiimenti

kimofemiki. Kwa mfano kivumishi cha lahaja ya Kiimenti kama **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi) huchanganuliwa hivi: **/ ũ-mw-irũ /** ambapo,

**ũ** – mofimu ambayo ni kiwakilishi cha ngeli/kipatanishi/idadi (umoja)

**mw** – mofimu ya ngeli/idadi (umoja)

**irũ** – mofimu inayowakilisha maana ya kimsingi (kileksia) au mzizi wa kivumishi.

Uchanganuzi kama huu wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti ulisaidia kuelewa zaidi umbo la ndani la maneno hayo na usarufi wa mofimu mbalimbali zinazoyaunda. Aidha, uelewa wa mfuatano au mpangilio wa mofimu za vivumishi vya Kiimenti na ruwaza zilizotokea kwa jinsi mofimu za maneno hayo hupangiliwa ulifahamika.

Hivyo basi, nadharia ya SGUZ iliwezesha uchanganuzi wa vivumishi vya Kiimenti kimofemiki kutekelezwa na kudhihirishwa kwa mofimu mbalimbali zinazoainishwa. Mofimu huweza kuwakilisha maana za kisarufi na za kileksia. Hali hii inaweza kudhihirishwa katika mfano uliotolewa wa kivumishi cha lahaja ya Kiimenti **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi).

Katika kivumishi **ũmwirũ** [omwiro] kategoria mbalimbali za kisarufi kama ngeli, idadi na mzizi hubainika. Kwa hivyo, inawezekana kutunga sheria zinazotawala muundo wa kivumishi cha lahaja ya Kiimenti na kubainika kwa mpangilio wa mofimu zinazounda kivumishi hicho.

Hivyo, nadharia ya SGUZ iliwezesha kutumiwa kwa sheria za kimofemiki na kuchambua vivumishi vya lahaja ya Kiimenti na kupata mofimu mbalimbali kutegemea usarufi wake katika vivumishi. Aidha, ilisaidia katika uainishaji wa mofimu zote za viambishi awali na mzizi wa kivumishi cha lahaja ya Kiimenti na kueleza usarufi unaowakilishwa. Kwa

mujibu wa nadharia ya SGUZ maneno huwakilishwa na mofimu ambazo ni vipashio vidogo vya maneno. Mofimu hizi huwa na usarufi katika maneno hayo. Kwa hivyo, nadharia hiyo ilisaidia katika kugawa kivumishi katika vipashio vidogo. Iliwezekana kugawa kivumishi cha lahaja ya Kiimenti na kupata vipashio kama mzizi wa kivumishi hicho na pia mofimu zinazoambishwa mzizi huo. Aidha, iliwezekana kuonyesha jinsi kila mofimu huwakilisha kazi ya kisarufi na ya kileksia katika umbo la nje.

Mhimili wa pili wa nadharia ya SGUZ ni kutambua mzizi kama kiini cha ujumbe katika muundo wa maneno. Kutokana na hali hii kuna uwezekano wa mzizi kuambishwa mwanzoni, mwishoni au mwanzoni na mwishoni. Katika hali hii miundo kama hii ya vivumishi vya Kiimenti huweza kupatikana.

i) V → VA + Mz  ii) V → Mz + VT  iii) V → VA + Mz + VT

Hali hii ilisaidia uchunguzi wa miundo mbalimbali ya vivumishi vya Kiimenti na usarufi wa mofu awali na tamati katika mizizi mbalimbali ya vivumishi. Aidha, iliwezekana kueleza ruwaza za usarufi huo na ufafanuzi wa sheria zilizodhibiti ruwaza husika. Miundo kama hiyo ya vivumishi imeelezwa pia na Mukuthuria na Chimerah (wataje) walipoangazia jinsi nadharia ya SGUZ inavyoweza kutumika katika uchanganuzi wa maneno mbalimbali katika lugha za Kibantu kimofolojia.

Mhimili wa tatu wa nadharia hii ni kukubali matumizi ya mofimu kapa {Ø} katika uchanganuzi wa maneno. Matumizi ya mofimu kapa katika nadharia ya SGUZ yameshadidiwa zaidi na Mukuthuria na Chimerah (wataje) katika uchanganuzi wa lugha za Kibantu. Hali hii ilisaidia kuchanganua vivumishi vya Kiimenti. Ilifaa zaidi kuchanganua kimofemiki vivumishi ambavyo hudhihirisha maumbo fulani kwa muundo

wa nje lakini muundo huo ukakosa kuainishwa katika muundo wa ndani katika vivumishi husika. Kwa mfano, kivumishi cha mkopo kama **maritati** [maritati] (maridadi) kinadhihirisha muundo wa nje jinsi kilivyo. Hata hivyo, katika muundo wa ndani kitakuwa na mofu kapa{Ø katika mwanzo wake. Uchanganuzi wa kivumishi hicho utakuwa /ø-maritati/. Mofu kapa hapa huwakilisha ngeli ya kimofolojia ambapo kivumishi hicho hupatikana na idadi. Vivumishi vingi vya mkopo hukosa maumbo fulani katika muundo wa nje, hivyo basi mofu kapa hutumika kuyaainisha katika muundo wa ndani.

Mhimili wa nne wa nadharia ya SGUZ ni kutambua umilisi wa lugha wa mzungumzaji mzawa wa lugha fulani. Kwa mujibu wa Chomsky (1965) umilisi anaokuwa nao msemaji wa lugha asilia humwezesha kutofautisha maumbo ambayo ni kamili na yale si kamili. Kwa hivyo, katika utafiti huu ujuzi wa mtafiti kama mzungumzaji asilia wa lahaja ya Kiimenti ulifaa katika uibuaji wa data. Data ambayo mtafiti aliibua aliilinganisha na ile ya wasailiwa wake. Kwa hivyo, ujuzi wa mtafiti kama mzungumzaji wa lahaja ya Kiimenti ulikuwa jambo la msingi katika utafiti huu. Umilisi anaokuwa nao msemaji wa lugha fulani asilia huandamana na utendaji ambapo huitumia lugha hiyo katika mazungumzo. Aidha, umilisi wa mzungumzaji mzawa wa lugha fulani humwezesha kuelewa na kutunga sentensi za lugha husika hasa kwa kuzingatia kategoria za maneno zinazotumika kuziunda. Kwa hivyo, nadharia hii ilifaa kutathmini mpangilio wa vivumishi mbalimbali vya Kiimenti katika sentensi za lahaja hiyo. Hali hii ilifaa katika utafiti huu hasa katika mazungumzo ya nyanjani.

Mhimili wa tano wa nadharia ya SGUZ ni kusisitiza kuwa kila lugha huwa na sarufi tofauti na nyingine. Kwa hivyo, sheria za muundo wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti

hutofautiana na sarufi za lugha zingine zote. Hali hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ilisaidia kukusanya data kutoka kwa wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti.

### 2.3.2 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia

Aidha, Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilitumika kuchanganua data katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu ilifaa kueleza michakato mbalimbali ya kifonolojia ambayo vivumishi vya Kiimenti hupitia kutoka muundo wake wa ndani hadi wa nje. Nadharia hii iliasisiwa na Theo Vennemann katika kazi zake mwaka wa 1971 ili kukabiliana na matatizo ya Fonolojia Zalishi (FZ) iliyoasisiwa na Chomsky (1950). Baadhi ya matatizo hayo ni kama udhahania uliyojitokeza katika FZ. Mwaka wa 1968 Chomsky na Halle walitoa kazi nyingine iliyojulikana kama *Sound Patterns of English* ambayo ilipata nafasi ya kuchunguzwa na kuhakikiwa na mwanafunzi wa Vennemann aliyejulikana kama Joan Bybee Hooper. Mwanafunzi huyu aliifanyia FZ marekebisho na kuiendeleza katika tasnifu yake ya Uzamifu iliyojulikana kama *Aspects of General Phonology* mwaka wa 1971. Kazi hii ilikuja kuchapishwa 1976 ikijulikana kama *Introduction to Natural Generative Phonology*.

Vivumishi vya Kiimenti hupitia mabadiliko mengi ya sauti ambayo yanahusishwa na michakato ya kifonolojia. Nadharia ya FZA huhusisha vipengele vya fonolojia na mofolojia katika uchangunuzi wa lugha. Nadharia hii ina kanuni mbalimbali ambazo hubainika katika lugha mbalimbali za ulimwengu. Mojawapo ya kanuni hizi ni zile za kifonetiki zinazofanya kazi katika mazingira mahsusi zikizingatia maumbo ya kifonetiki. Kanuni hizi ni bia na hivyo hupatikana katika lugha nyingi za ulimwengu. Hii ni kwa sababu zinahusisha ala za utamkaji ambazo hufanana kote ulimwenguni. Kanuni hizi

hazibanwi au kuzuiliwa na hufanya kazi hata katika vivumishi vya Kiimenti. Baadhi ya kanuni hizi ni michakato ya kifonolojia kama usilimisho, uimarikaji na udhoofikaji wa fonimu (Gacunku, mtaje; Jumwa, 2008; Nyaucho, 1988). Aidha, ukaakaishaji ambapo sauti zisizo za kaakaa hutamkiwa katika kaakaa gumu hujumuishwa katika kanuni hizo (Hyman, 1975; Wa Mberia, 1981). Curr (2008) anabainisha kuwa usilimisho nyuma pia ni kanuni ya kifonetiki. Anaeleza kuwa katika kanuni hii sauti ya nazali hutangulia konsonanti ya kipasuo, kikwamizwa au kizuiwa kwamizwa na hutamkiwa mahali pa konsonanti inayoifuata. Kanuni hizi za kifonetiki zilisaidia uchunguzi wa mabadiliko ya sauti ambayo huathiri vivumishi vya Kiimenti. Hii ni kwa sababu zilibainika katika vivumishi husika. Aidha, zilifaa kuandika sheria ambazo zinajitokeza wakati wa mabadiliko ya sauti katika kuunda vivumishi vya Kiimenti hasa kutoka muundo wa ndani hadi muundo wa nje.

Pia kuna kanuni za mofofonemiki ambazo si bia kama kanuni zile za kifonetiki. Kanuni hizi huonyesha mabadiliko zaidi katika muundo wa maneno huku zikihusisha vipengele vya mofolojia, sintaksia na leksia. Hii ni kwa sababu zinahusu mipaka ya mofimu pamoja na kategoria za kileksia. Curr (mtaje) anasema mipaka ya mofimu ni ile ambayo hupatikana kati ya mofimu na huonyeshwa kutumia alama ‘+’. Anaendelea kudai kuwa mipaka ya mofimu huweza kuchangia michakato mbalimbali ya kifonetiki. Kanuni hizi ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu katika mipaka ya mofimu za vivumishi vya Kiimenti kunatokea mabadiliko mengi ya maumbo ya maneno. Kwa mfano, kivumishi **ũmwega** [omwɛga] kina kivumishi **ũmũega**/ũ –mũ–ega/ (mzuri) kikionyesha muundo wa ndani. Hapa irabu /u/ imeyeyushwa katika mazingira ya kutangulia irabu /e/. Sheria hii inaweza kutumika kueleza hali hii: o $\longrightarrow$ w / ___ ɛ.

Lakini irabu /ũ/ ikitangulia mzizi wa kivumishi wenye konsonanti haiyeyushwi. Hali hii inapatikana katika kivumishi **ũmũkũrũ** [omokoro] / ũ–mũ–kũrũ / (mzee). Aidha, vivumishi vingine ambavyo huonyesha irabu /ũ**/** ikikosa kuyeyushwa ikikutana na konsonanti ni kama **ũmũraja** [omoraɟa] / ũ–mũ–raja / (mrefu), **ũmũkuĩ** [omokue] / ũ–mũ–kuĩ / (mfupi), **ũmũthũku** [omoθoku] / ũ–mũ–thũku / (mbaya), **ũmũtune** [omotunɛ] / ũ–mũ–tunɛ / (mwekundu). Pia irabu /a/ ikikutana na konsonanti, kuna uwezekano wa kukosa kuyeyushwa. Mifano inapatikana katika vivumishi vifuatavyo; **bathũku** [βaθoku] /ba-thũku/ (wabaya), **baraja** [βaraɟa] /ba-raja (warefu) na **batune** [βatunɛ] /ba-tune/ (wekundu). Hali kama hii huweza kuelezwa kutumia kanuni za mofofonemiki. Kanuni hizi pia zilikuwa muhimu katika kueleza miundo mbalimbali ya vivumishi vya Kiimenti.

Vilevile, kuna kanuni za Sandhi. Neno hili ni la lugha ya Sanskrit ambayo ni lugha moja ya Kihindi likiwa na maana ya kuweka pamoja kutokana na San (pamoja) na dhi (weka). Neno hili lilitumiwa kwa mara ya kwanza na wanasarufi wa Kihindi kuelezea michakato inayopatikana katika mipaka ya kimofolojia na kisintaksia ya maneno. Mipaka hii ni kama ile ya maneno na mofimu. Mipaka ya maneno ni mipaka inayojitokeza kati ya maneno kama katika maneno ya Kiingereza "far away" ambapo sauti /r/ inapatikana ikiwa ya mwisho katika neno "far", ikiwa neno linalolifuatia "away" linaanza kwa irabu (Curr, mtaje). Wa Mberia (1993) alipochanganua nomino na kitenzi cha Kitharaka akitumia nadharia ya FZA alisema kuwa kanuni za Sandhi hufanana na zile za fonetiki kwa sababu mpaka wa neno huweza kukutana na mpaka wa silabi au mpumuo. Anaendelea kusema kuwa kanuni za Sandhi hufanana na zile za mofofonemiki kwa sababu mipaka ya maneno inahusishwa katika sheria za Sandhi. Kwa maoni yake mipaka ya maneno haiamuliwi na fonetiki za lugha bali sintaksia pamoja na semantiki yake. Hali

hii hufanya mipaka ya maneno kutambuliwa kama mipaka ya sintaksia (Hooper, mtaje). Kanuni hizi hupatikana kati ya sheria za kifonetiki na zile za mofofonemiki.

Kwa hivyo, kanuni za Sandhi hufanya kazi katika mipaka ya maneno na mofimu. Otiende (2013) akimnukuu Lass (1984) anasema kuwa mchakato wa mvutano wa irabu ni mfano wa sheria za Sandhi. Anatoa mfano kama huu /ma+ingi/ ⟶ [mɛŋgi].

Meitamei na Wenzie, 2014 wakitumia nadharia ya FZA kuchanganua michakato ya kifonolia katika nomino za Kimaasai wameeleza jinsi muungano wa vokali huweza kuelezwa kupitia sheria za Sandhi. Mchakato huu hutokea katika mipaka ya maneno, sentensi au wakati maneno changamani yanaundwa. Kwa mfano, nomino mbili “erubata enkejuni” ni nomino changamani ambapo irabu /a/ ya mwisho katika “erubata” huungana na irabu /ɛ / ya kwanza katika “enkeju” na kuunda irabu unganifu /ae/ ambayo ni ya mbele na haijaviringwa (Meitamei na Wenzie, wataje). Muungano wa irabu hutokea hata katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, kivumishi/**ja**–**me**–**thĩ**/ [ɟamɛθe] (mabichi) kina muundo wa ndani kama huu /ɟa-ma-eθe / (mabichi). Ili kuunda kivumishi /**ja**–**me**–**thĩ**/[ɟamɛθe] muungano wa irabu /a/ na /ĩ / unatokea na kuunda irabu /ɛ / ya kati. Mchakato huu wa kifonolojia unaweza kuelezwa kupitia sheria hii.

[a] > [ɛ] ___ #/___

$$\begin{bmatrix} \text{+mbele} \\ \text{+chini} \\ \text{-mviringo} \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} \text{+mbele} \\ \text{+kati juu} \\ \text{-mviringo} \end{bmatrix} / ____ \; \#____$$

Kwa hivyo, kanuni za Sandhi zilikuwa muhimu katika utafiti huu hasa kwa kuonyesha mabadiliko ya sauti katika vivumishi vya Kiimenti yanayotokana na muungano wa irabu.

Hii ni baadhi ya michakato ya kifonolojia ambayo huathiri muundo wa kivumishi cha Kiimenti.

Mabadiliko mengine ya kipitio kando na Sandhi ni ya kileksia ambapo katika Kiimenti kuna visawe vya vivumishi ambavyo havina uhusiano wowote wa kifonetiki/kifonolojia, kwa mfano katika Kiswahili kuna neno angavu- nururifu, hodari-mahiri, stadi na mengine. Huu waweza kuwa ualomofia au usinonimu.  Hali hii inabainika katika vivumishi vya Kiimenti kama hivi:

| **Vivumishi** | **Maana** |
|---|---|
| ũmwanake [omwanakɛ], ũmwĩthĩ [omweθe] | mchanga |
| ũmũnoru [omonoru],  ũmũnene [omonɛnɛ] | mkubwa |
| jamaingĩ [ɟamainge], nkabo [nkabɔ] | mengi |
| ũmwega [omwɛga], mũkarimu [mokarimu] | mkarimu |

Kutokana na mifano ya vivumishi iliyotolewa hapo juu, inabainika kuwa baadhi ya visawe vya vivumishi vinatokana na Kiimenti kikikopa kutoka  lugha nyingine kama Kiswahili.

### 2.3.3 Hitimisho

Sura ya pili imejikita kufafanua maana ya kivumishi kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Pia, imeangazia aina za vivumishi na miundo inayobainika katika vivumishi husika. Imepiga hatua na kuchunguza usarufi katika maneno mbalimbali ili kuelekeza usarufi katika vivumishi vya Kiimenti. Vilevile, imegusia mpangilio wa vivumishi katika tungo mbalimbali. Hii ni kutokana na hali kwamba vivumishi huzingatia mpangilio fulani vinapotumika katika sentensi bali havipangiliwi kiholelaholela. Hatimaye, ufafanuzi wa nadharia za SGUZ na ile ya FZA na jinsi zilivyotumika kuongoza utafiti huu umetolewa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii imeshughulikia mwongozo uliozingatiwa katika utafiti ili kukusanya data na kuichanganua. Masuala yaliyoshughulikiwa ni yafuatayo: Muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, utafiti awali, utegemeo, uthabiti, utafiti wa maktaba, ukusanyaji wa data nyanjani na uchanganuzi wake.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano, kwa hivyo ulizingatia muundo wa kimaelezo. Maelezo yalitumika katika uchanganuzi na uwasilishi wa data iliyopatikana maktabani na nyanjani. Kwa kutumia maelezo muundo wa kivumishi cha Kiimenti na usarufi uliobainika ulielezwa kwa kina. Pia, ruwaza ya usarufi huo ilielezwa. Vilevile, maelezo yalitumika katika uchanganuzi wa data kutumia nadharia zilizotumika katika utafiti huu. Maelezo zaidi yalitumika kueleza ruwaza na sheria zinazozingatiwa wakati mkururo wa vivumishi unapopatikana katika sentensi. Hatua nyingine ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data ilihusu utumiaji wa majedwali. Matumizi ya rakamu hayakuhusishwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika wadi ya Abothũgũchi ya Magharibi, kaunti ndogo ya Meru ya Kati katika kaunti ya Meru ambapo wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti wanaishi. Mtafiti ni mzaliwa wa eneo hili na analifahamu vizuri. Hali ya mtafiti kufanya utafiti katika eneo analolifahamu humpunguzia shida za kisaikolojia (Mugenda na

Mugenda, 1999). Aidha, kujikita katika eneo husika kuliwezesha kupatikana kwa matokeo yaliyokubalika kwa sababu wakazi wengi wa eneo hili ni wazawa wa lahaja ya Kiimenti na wenye umilisi wa lugha husika. Mazingira ya eneo la utafiti yalikuwa ya mashambani na ilikuwa muhimu kukusanya data katika maeneo hayo kuliko ya mijini ambayo huwa na wakazi wengi wageni ambao licha ya kuwasiliana wakitumia Kiimenti hawakifahamu vizuri. Kwa hivyo, kukusanya data katika eneo hilo kuliwezesha kupatikana kwa matokeo yenye uthabiti na utegemeo. Kaskazini eneo hili linapakana na kaunti ndogo za Imenti Kaskazini na Bũũri ambalo ni eneo lenye athari za wageni wanaopatikana mjini Meru na viunga vyake. Upande wa Kusini eneo la utafiti linapakana na kaunti ndogo ya Imenti Kusini ambalo lina wahamiaji wengi kwa sababu ya shughuli za kilimo na za kibiashara. Upande wa Magharibi eneo la utafiti linapakana na msitu wa Mlima Kenya. Hivyo, halijapata athari zozote kilugha kutoka sehemu hiyo. Upande wa mashariki linapakana na wadi ya Abothũgũchi ya kati ambayo imeathiriwa na wageni hasa kwa sababu ya shughuli za kilimo na kibiashara baada ya kuimarika kwa miundo msingi kama ya barabara za lami. Utafiti huu ulizingatia wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti katika wadi ya Abothũgũchi ya Magharibi ambayo haijaathiriwa sana na lugha ngeni ikilinganishwa na maeneo hayo mengine.

### 3.4 Kundi Lengwa

Utafiti huu uliwalenga wasailiwa ambao ni wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti. Ilikuwa muhimu kuzingatia kipengele hiki kwa sababu walikuwa na umilisi wa lahaja ya Kiimenti na waliweza kutumia vivumishi mbalimbali katika tungo za Kiimenti kwenye mazungumzo yao. Walengwa wa utafiti walipatikana katika miktadha ya mikutano ya

chifu, shule, kanisa. Kigezo muhimu cha kuchagua watafitiwa kilikuwa uwezo wao wa kuzungumza Kiimenti bali si misingi ya jinsia, umri, ukoo, dini, rika, elimu na kadhalika.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulitumia sampuli makusudi ili kuibua data. Lugha ya Kimeru ina lahaja tisa lakini Kiimenti ndicho kilichaguliwa. Kulikuwa na manufaa ya mtafiti kuchunguza lahaja hii kwa sababu ni mzawa mzungumzaji wa Kiimenti na aliweza kutumia umilisi wake kuchuja data yake na kuzalisha nyingine alipokosa kupata kiwango cha data alichohitaji. Pia, lahaja ya Kiimenti ina maandishi machache. Wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti walikuwa watafitiwa kwenye utafiti huu kwa sababu wana umilisi wa lahaja husika. Aidha, hawana athari nyingi kutokana na lugha au lahaja nyingine za Kimeru. Kwa hivyo, sampuli ya utafiti huu ilikuwa na wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti ambao waliweza kutoa tungo zenye vivumishi ambavyo vilichanganuliwa. Kwa ujumla vivumishi 415 vilichanganuliwa katika utafiti huu. Aidha, sentensi 237 zilicahanganuliwa ili kuonyesha ruwaza mbalimbali za mpangilio wa vivumishi katika sentensi husika.

### 3.6 Vifaa vya Utafiti

Rununu ilitumika kunasia mazungumzo kutoka nyanjani. Rununu ilikuwa muhimu kwa sababu ilibebeka kwa urahisi na mtafiti aliweza kunasa mazungumzo yake pasipo kuzua taharuki kwa wasailiwa wake. Kwa upande mwingine, data iliyopatikana kuhusu vivumishi na mpangilio wake katika sentensi za lahaja ya Kiimenti ilinakiliwa kwenye daftari kwa kutumia kalamu.

### 3.7 Utafiti wa Awali

Kabla ya kwenda nyanjani kufanya utafiti kamili, mtafiti alifanya utafiti wa awali. Utafiti huu ulimsaidia kutathmini hali ya mambo kabla ya utafiti kamili. Kwa mfano, mtafiti alipata nafasi ya kujaribu ufaafu wa vifaa na mbinu za utafiti. Hii ilimsaidia mtafiti kutambua vifaa na mbinu zenye dosari. Utafiti wa awali ulimsaidia mtafiti kuchagua mbinu na vifaa bora vya kutumia kwenye utafiti huu. Aidha, utafiti wa awali ulimwelekeza mtafiti kuelewa maeneo ya kufanyia pendekezo lake marekebisho ili aweze kupata data yenye welekevu wakati wa utafiti kamili. Katika utafiti awali mtafiti alirekodi mazungumzo katika miktadha ya mikutano kwa kutumia kinasa sauti cha rununu yake. Mbinu nyingine ilikuwa kurekodi sentensi zenye vivumishi mbalimbali kwenye daftari kwa kutumia kalamu. Miktadha ya mikutano iliyofanyiwa utafiti wa awali ni pamoja na kanisa la Gĩkune la A.I.P.C.A. na mkutano mmoja wa walimu na wazazi katika shule ya msingi ya Katheri. Miktadha hii ya mikutano ilipatikana katika eneo lililoteuliwa kufanyiwa utafiti. Vilevile, mtafiti alisoma Bibilia ya Kimeru, kamusi ya Kimeru na vitabu vya Kimeru ambavyo husomwa na wanafunzi wa shule za msingi.

Baada ya utafiti awali, mtafiti alinakili vivumishi kwenye majedwali yaliyodhihirisha aina mbalimbali za vivumishi huku akiondoa uradidi. Kila jedwali lilikuwa na aina moja ya vivumishi ambavyo vilifanyiwa unukuzi na kuchanganuliwa ili kudhihirisha usarufi. Hatua nyingine ilikuwa kuandika sentensi zenye mpangilio sawa wa vivumishi pamoja. Kisha alizifanyia unukuzi na kuzitafsiri. Hatimaye aliandika ruwaza mbalimbali za mpangilio wa vivumishi katika sentensi hizo. Kila ruwaza ilikuwa na sentensi zake tofauti na nyingine. Miktadha ya mikutano ambayo ilifanyiwa utafiti wa awali haikufanyiwa utafiti kamili.

## 3.8 Utegemeo

Utegemeo ni hali ambapo kifaa cha utafiti kinapojaribiwa mara nyingi au kinapotumika kukusanya data matokeo hayabadiliki au data inayopatikana ni ileile (Mugenda na Mugenda, wataje). Ili kuhakikisha utegemeo katika utafiti huu, utafiti wa awali ulifanyiwa wasailiwa walio sawa na waliotumika katika utafiti kamili. Ni vizuri kufahamu kuwa utafiti kamili haukuwalenga wasailiwa waliohusishwa katika utafiti wa awali. Hali hii ilimsaidia mtafiti kutathmini utegemeo wa vifaa vyake katika utafiti huu. Mtafiti aligundua kuwa vilikuwa na utegemeo na hivyo akavitumia. Iwapo angegundua kuwa vilikuwa na dosari na havingefanya kazi vizuri angevibadilisha kwa vingine au kuviimarisha.

## 3.9 Uthabiti

Uthabiti ni hali ya kuwa na matokeo yenye uhakika na maana. Kwa maelezo mengine ni hali ya matokeo yaliyochanganuliwa kuwakilisha kwa usahihi suala ambalo linachunguzwa katika utafiti (Mugenda na Mugenda, wataje; Wanjohi, 2014). Kwa mujibu wa Borg na Gall (1983) uthabiti wa kifaa cha utafiti unaweza kuimarishwa baada ya kujaribiwa na kisha mtafiti akatoa uamuzi wake. Hivyo, katika utafiti huu, utafiti awali ulitumika kujaribia vifaa na mbinu zilizotumika katika hatua ya kufanya utafiti kamili. Hatimaye, mtafiti alijadili matokeo ya utafiti wake wa awali na wasimamizi wake ili kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti kamili yalikuwa na uthabiti uliofaa. Baada ya hayo ilimbidi mtafiti kuzingatia nasaha yao ili kupata data iliyokubalika.

## 3.10 Utafiti wa Maktabani

Utafiti ulifanywa maktabani katika vyuo vya Nairobi, Moi, Kenyatta na Egerton. Hii ni kwa sababu vyuo hivyo vina idara za Kiswahili na Isimu ambazo zimekuwepo kwa muda

mrefu na zimehifadhi tasnifu za wasomi zilizofaa utafiti huu. Aidha, makala, majarida na kazi zingine zilizoangazia vivumishi na nadharia za SGUZ na FZA zilisomwa katika maktaba hizo. Kazi nyingine zilizofaa utafiti huu zilirejelewa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Chuka. Hii ni kwa sababu chuo hiki kina tasnifu za kiisimu na majarida yaliyofaa utafiti huu. Aidha, mtafiti alitembelea maktaba ya Wizara ya Elimu iliyoko Jogoo House jijini Nairobi ambapo alisoma tasnifu za utafiti zilizohifadhiwa za utafiti uliowahi kufanywa katika vyuo vikuu vya umma na vya kibinafsi hapa nchini Kenya ambazo zilifaidi utafiti huu. Aidha, mtafiti alisoma kazi za Kimeru hasa vitabu vya hadithi vya lahaja ya Kiimenti katika maktaba ya umma ya Mikumbune na ile Meru ili kuzalisha data zaidi hasa pale alihisi hakupata data ya kutosha. Maktaba hizi huhifadhi vitabu vya hadthi za Kiimenti ambazo zilifaa utafiti huu.

### 3.11 Ukusanyaji wa Data Nyanjani

Utafiti huu ulifanyika katika wadi ya Abothũgũci ya Magharibi, kaunti ndogo ya Meru ya Kati katika kaunti ya Meru ambapo wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti wanaishi. Katika eneo hilo wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kiimenti walipatikana. Hatua moja ilihusu mtafiti kuteua kimakusudi makanisa mawili ambapo mahubiri huongozwa kwa lahaja ya Kiimenti. Makanisa hayo ni yale ya Gĩthoene E.A.P.C. na lile la Kikatoliki la Kathiranga. Kwa kutumia simu tamba mtafiti alinasa mahubiri katika makanisa hayo na kunakili vivumishi na jinsi vilivyotumika katika sentensi mbalimbali.

Kabla ya mtafiti kuhudhuria mahubiri kwenye makanisa hayo, aliwatembelea wahubiri husika ili kuwaomba kibali cha kufanya utafiti huko. Vilevile, aliwaeleza kuwa umuhimu wa utafiti wake ulikuwa kukuza na kuendeleza lahaja ya Kiimenti kiisimu. Ilikuwa muhimu kuzingatia hali hii kwa sababu kunasa mahubiri kanisani ni suala tata na huweza

kuzua sintofahamu. Hii ni kwa sababu kulikuwa na uwezekano wa hadhira yake kuhisi kuwa kunasa mahubiri huweza kuwa na nia mbaya. Aidha, mtafiti alihudhuria mahubiri katika makanisa hayo akiwa mgeni lakini wahubiri na viongozi wake wakifahamu kusudi lake kuu. Licha ya kunasa mahubiri kwa simu, mtafiti alitumia kalamu na daftari kunakili vivumishi na jinsi vilivyotumika katika sentensi za Kiimenti.

Aidha, mtafiti alikusanya data kutoka kwa miktadha ya mikutano ya walimu na wazazi katika shule za msingi za Mũri na Mũthangene. Mtafiti alitumia kinasa sauti cha simu yake kunasa mazungumzo ya watafitiwa wake. Aidha, alitumia kalamu na karatasi kunakili kwenye daftari lake vivumishi vya Kiimenti na jinsi vilivyotumika katika sentensi za lahaja husika.

Ili kuongeza kanzi ya data yake, mtafiti alihudhuria mikutano miwili ya chifu. Mkutano mmoja alihudhuria katika kata ya Gĩthongo na mwingine kata ya Katheri. Kabla ya kuhudhuria mikutano hiyo, mtafiti aliwasiliana na machifu husika ili kujitambulisha na kupata kibali cha kukusanya data kwenye mikutano. Katika mikutano hiyo, mtafiti alitumia kinasa sauti cha rununu yake kunasa mazungumzo. Ilikuwa muhimu kwa mtafiti kutumia muktadha wa mkutano kama huo kwa sababu wanaouhudhuria ni watu wazima wenye umilisi unaofaa wa lahaja ya Kiimenti na huweza kuitumia lugha bila athari zozote.Ilikuwa muhimu kwa mtafiti kukusanya data yake katika mazingira ya mikutano iliyoangaziwa ili kuhakikisha kuwa utafiti wake uliendeshwa kwa misingi ya kisayansi.

Hatimaye, mtafiti akiwa mzawa wa lahaja ya Kiimenti ana uwezo wa kuzua data ya kutumika katika utafiti huu. Kwa hivyo, mtafiti aliweza kuzalisha data hiyo mwenyewe. Hii ni kwa sababu ana umilisi wa lahaja ya Kiimenti. Kauli hii ni kweli kwa mujibu wa Salesio (mtaje) akiwarejelea wasomi kama Chomsky (1965) na Radford (1981). Yeye

anasema kuwa mzungumzaji mzawa wa lugha fulani anaweza kuzalisha data ya kutumika na kuchanganuliwa katika utafiti wa kiisimu. Maoni haya yalimjasirisha mtafiti kuzua data ya utafiti huu.

Hatimaye mtafiti alifanikisha utafiti wake nyanjani baada ya kuidhinishwa na taasisi mbalimbali. Kwa hivyo, alitafuta kibali kutoka kwa Halmashauri ya Sayansi na Teknolojia na Uvumbuzi,

Mkuu wa kaunti ya Meru, Mkuu wa elimu katika kaunti ya Meru na Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

### 3.12 Uchanganuzi wa Data

Jumla ya vivumishi 415 viliyopatikana katika utafiti huu vilichanganuliwa kwa kuzingatia hatua hizi:

i) Kuorodhesha vivumishi vya lahaja ya Kiimenti kwa kutumia kalamu kwenye daftari.

ii) Kwa kutumia majedwali yaliyoonyesha aina za vivumishi; mpangilio mahsusi ulifanywa wa kutambua aina mbalimbali za vivumishi vya Kiimenti huku uradidi ukiondolewa.

iii) Kufanyia vivumishi vilivyopatikana unukuzi wa kifonetiki.

iv) Vivumishi vyote vilipitiwa na kutafsiriwa kwa Kiswahili ili kueleweka na wasomi ambao hawana umilisi wa lugha ya Kiimenti.

v) Kila aina ya kivumishi ilichanganuliwa kimofemiki na mofimu za kategoria mbalimbali kunakiliwa kwenye jedwali.

vi) Vivumishi vya Kiimenti ambavyo haviambishwi mofu zozote vilinakiliwa kwenye jedwali tofauti. Baada ya kuchanganua muundo wa vivumishi vya Kiimenti mofimu

mbalimbali zenye usarufi zilipatikana. Hali hii ilipelekea kupatikana kwa ruwaza ya mofimu zinazounda vivumishi vya lahaja ya Kiimenti katika utafiti huu.

vii) Idadi maalumu ya vivumishi vya Kiimenti ilizingatiwa ili kujiepusha na urudiaji mwingi wakati wa kuchanganuliwa kwa data kwa maelezo.

viii) Kutoa maelezo ya kiisimu kwa kila aina ya kivumishi cha Kiimenti.

ix) Maelezo yalitolewa kuhusu miundo ya vivumishi vya Kiimenti ili kudhihirisha usarufi wake. Kuhusiana na hali hii, mtafiti alijihimu kutoa maelezo ya kila muundo wa vivumishi vya Kiimenti na kuthibitisha mofimu zinazounda vivumishi hivyo kuzingatia ruwaza mahsusi.

x) Hatua nyingine muhimu katika uchanganuzi wa data ilihusu kuorodhesha sentensi ambazo zilitumia vivumishi mbalimbali kwa mujibu wa ruwaza ya vivumishi katika kila sentensi. Sentensi za ruwaza moja ziliorodheshwa pamoja na kufanyiwa unukuzi wa kifonetiki na kutafsiriwa kwa Kiswahili. Kwa mfano sentensi zifuatazo ziliorodheshwa pamoja. Hii ni kwa sababu zinaunda ruwaza ambapo kivumishi cha pekee kinatangulia kivumishi cha sifa.

I (a) *Muntu* ***ũngĩ ũmũraja*** *agũkinya.*

(b) [muntu **oŋge omoraɟa** agokiɲa]

(c) Mtu **mwingine mrefu** amefika.

2 (a) *Iuku* ***rĩngĩ*** rĩrĩerũ *rĩkũretwa.*

(b) [iuku **reŋge rereɛro** rekorɛtwa]

(c) Kitabu **kingine kipya** kimeletwa.

3 (a) ***ĩ****rinda* ***rĩngĩ rĩrĩerũ*** *r****ĩ****kũgũrwa.*

(b) [erinda **reŋge rereɛro** rekogorwa]

(c) Rinda **lingine refu** limenunuliwa.

xi) Hatimaye mtafiti alichanganua ruwaza mbalimbali na kuandika sheria za kila ruwaza.

xii) Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa kama ripoti ya utafiti huu.

## 3.13 Hitimisho

Sura ya tatu imeangazia mbinu za utafiti zilizozingatiwa katika utafiti huu ili kukusanya data na kuichanganua. Masuala yaliyoshughulikiwa ni pamoja na: Mpango wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, utafiti awali, utegemeo, uthabiti, utafiti wa maktaba, ukusanyaji wa data nyanjani na uchanganuzi wake.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia fonolojia na mofolojia ya Kiimenti. Kwa hivyo, sura imejikita katika kueleza masuala yafuatayo ya kifonolojia yanayohusu Kiimenti kama fonimu, silabi, wakaa katika silabi na michakato ya kifonolojia inayoathiri muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Pia sura hii imeeleza masuala ya kimofolojia katika Kiimenti kama dhana za mofu, mofimu, alomofu na ngeli za kimofolojia za lahaja husika. Aidha, michakato ya kimofolojia kama uradidi, mnyambuliko sarufi na geuzi imeelezwa na jinsi inavyochangia muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Hatimaye, mpangilio wa kivumishi cha Kiimenti katika sentensi mbalimbali umeelezwa na ruwaza zinazobainika katika mipangilio hiyo kuwekwa wazi.

## 4.2 Fonimu za Kiimenti

Fonimu ni kipande sauti ambacho kikipachikwa katika neno hubadili maana yake (TUKI, 1990).

Kwa hivyo, fonimu ni kipashio kidogo katika lugha chenye kubainisha maana (Habwe na Karanja, wataje). Ili kuweza kubainisha fonimu mbalimbali katika lugha yoyote, mbinu ya jozi mlinganuo finyu hutumika. Jozi ya mlinganuo finyu ni maneno mawili ambayo tofauti yake inatokana na fonimu moja (TUKI, 1990). Fonimu huweza kutambuliwa katika jozi mlinganuo finyu ikiwa maneno kwenye jozi yana idadi sawa ya fonimu. Vilevile, fonimu zote katika maneno hayo ni sawa isipokuwa moja na yana mpangilio sawa wa fonimu (Mgullu, 1999). Dhana ya jozi mlinganuo finyu ni kuwa maneno katika jozi hulingana sana hivi kwamba tofauti yao ni finyu au ndogo sana. Hali ya kutambua

fonimu katika lahaja ya Kiimenti huweza kudhihirika kupitia jozi ya maneno ifuatayo. Haya ni **gĩtĩ** [gete] (kiti) na **gĩkĩ** [geke] (hiki). Maneno haya yana idadi sawa ya fonimu na yanafanana katika fonimu zake isipokuwa moja. Aidha, yana mpangilio sawa wa fonimu. Kwa hivyo, katika jozi hiyo ni rahisi kugundua kuwa sauti /**t**/ na /**k**/ ni fonimu tofauti ambapo moja ikibadilishwa na nyingine katika mazingira zinamotokea maana ya neno hubadilika.

### 4.2.1 Fonimu za Irabu

Irabu ni sauti ambazo katika kutamkwa kwake hewa huwa haizuiliwi au haibanwi kwenye mkondohewa unaotoka mapafuni kupitia chemba ya kinywa na chemba ya pua na kwenda nje (Kihore na Wenzie, wataje). Lahaja ya Kiimenti ina irabu saba (Rukenya, mtaje). Hali hii inaelekea kuafikiana na Guthrie (1948) kuwa lugha nyingi za Kibantu huweza kuwa na irabu tano au sita.

Ili kueleza sifa bainifu za irabu sifa kuu tatu huzingatiwa. Sifa ya kwanza inahusu mahali ambapo irabu fulani inatamkiwa. Kulingana na sifa hii irabu huweza kutamkiwa mbele ya ulimi, kati ya ulimi au nyuma ya ulimi. Sifa ya pili inahusu mwinuko wa ulimi ambao unaweza kuwa juu wakati wa kutamka irabu /i/ na /u/, nusu chini wakati wa kutamka na chini wakati wa kutamka irabu. Sifa ya mwisho inahusu mkao wa midomo ambao hutandazwa au kuviringwa. Irabu zinazotamkwa mdomo ukiwa umeviringwa ni kama irabu /ɔ / na /u/ (Mgullu, 1999). Baadhi ya lahaja za Kibantu huwa na irabu saba (Mbaabu, mtaje). Hali hii inajitokeza katika lahaja ya Kiimenti ambapo kati ya irabu za mbele /i/ na /ɛ/ kuna irabu /ĩ/. Vilevile, kati ya irabu /ɔ / na /u/ kuna irabu /ũ/. Kwa kutumia jedwali lifuatalo tunaweza kuonyesha mahali ambapo irabu saba za lahaja ya Kiimenti hutamkiwa.

**Jedwali la 1: Utamkaji wa Irabu za Kiimenti**

| **Mahali pa Ulimi** | | **Sehemu ya Kutamkia** | |
|---|---|---|---|
| | **Mbele** | **Kati** | **Nyuma** |
| Juu | i | | u |
| Kati juu | ĩ | | ũ |
| Kati chini | e | | ɔ |
| Chini | | a | |

Irabu saba za Kiimenti zinazotamkiwa katika sehemu mbalimbali hubainisha unukuzi unaotofautiana. Unukuzi huu husaidia kutofautisha fonimu mbalimbali za lahaja husika. Jedwali lifuatalo linaonyesha irabu hizo na unukuzi wake. Aidha, matumizi yazo yamebainika katika maneno mbalimbali ya Kiimenti.

**Jedwali la 2: Irabu za Kiimenti na Unukuzi Wake**

| Fonimu | Tahajia | Neno | Maana |
|---|---|---|---|
| a | a | [anto] | watu |
| e | ɛ | [bɔnθɛ] | wote |
| ĩ | e | [erea] | ile |
| o | ɔ | [ɔmɛ] | nje |
| u | u | [munda] | shamba |
| i | i | [irĩa] | zile |
| ũ | o | [orea] | yule |

### 4.2.2 Wakaa katika Irabu

Wakaa ni muda unaotumika kutamka sauti au silabi (Massamba, 2004). Alama ya nukta pacha (:) huwekwa baada ya foni ili kuonyesha wakaa mrefu. Wakaa mrefu hutokea pale irabu moja inatokea kwa mfululizo (Mgullu, 1999). Kwa mfano nomino **baaba** (baba) ikinukuliwa itakuwa [βa:βa] na hivyo kuonyesha wakaa mrefu. Kwa mujibu wa Kindole (2020) dhana za irabu ndefu na irabu iliyorefushwa huwa na fahiwa tofauti katika fonolojia. Akimrejelea Wells (1985) anasema irabu ndefu hutumika kueleza irabu mbili ambazo hufanana huku zikifuatana na zinapotamkwa husikika kama irabu zilizo tofauti ya hizo mbili. Anazidi kueleza kuwa irabu zilizorefushwa ni zinazotumika kufidia urefu baada ya mchakato wa kifonolojia kama kuungana kwa irabu au kudondoshwa kwake. Kulingana na maelezo yake basi si rahisi kupata irabu mbili katika Kiimenti ambazo zinafanana huku zikifuatana na zinaweza kuzalisha irabu nyingine tofauti na hizo kama katika Kiingereza.

### 4.2.3 Fonimu za Nusu Irabu

Lahaja ya Kiimenti hudhihirisha nusu irabu mbili ambazo ni /j/ (y) na /w/. Sifa bainifu za nusu irabu hizi ni kama:

| (j) | (w) |
|---|---|
| +nusu irabu | +nusu irabu |
| +midomo kk laini | +kk gumu |
| -unazali | -unazali |
| +ughuna | +ughuna |

Konsonanti za nusu irabu zinapotamkwa hutamkika kwa urahisi kuliko konsonanti zingine. Hii ni kwa sababu zinapotamkwa hewa haizuiliwi katika ala mbalimbali za kutamkia. Kwa mfano, katika kutamka kivumishi **wetũ** [wɛto] (wetu) fonimu /w/ hutamkwa kwa urahisi na hughuna inapotamkwa. Vilevile, wakati wa kutamka fonimu /j/ katika neno kama **yawe** [jawɛ] (yake) inatamkwa kwa urahisi katika kaakaa gumu na hughuna. Hivyo sifa ya ughuna ni sifa bia inayopatikana wakati wa kutamka irabu zote saba katika lahaja ya Kiimenti.

### 4.2.4 Fonimu za Konsonanti za Kiimenti

Fonimu za konsonanti katika lahaja ya Kiimenti huweza kuainishwa kwa kutumia sifa za ukonsonanti, namna ya kuzitamka, mahali pa kuzitamkia, mkao wa glota na unazali. Wakati wa kutamka fonimu hizi hewa hubanwa au huzuiliwa katika ala mbalimbali za kutamkia. Ni vizuri kuelewa kuwa lahaja ya Kiimenti huweza kudhihirisha muundo wa silabi mwambatano. Muundo huu huweza kuwa wa fonimu za nazali na fonimu zingine. Kulingana na Mgullu (1999) ni vigumu kueleza wakati ambapo fonimu ya nazali ikifuatwa na konsonanti huunda fonimu moja na wakati ambapo zinakosa kuungana.

Mifano inayoweza kueleza hali hii ni kupitia fonimu /m/ na /n/ katika maneno **ndetũ** [ndɛto] (upande wetu) na **mbere** [mbɛrɛ] **(**mbele) katika lahaja ya Kiimenti. Maneno haya huweza kufikiriwa kuwa na fonimu nne au tano kama inavyodhihirishwa hapa chini.

Mbere

| | |
|---|---|
| /mb/+/e/+/r/+/e/ | /m/+/b/+/e/+/r/+/e/ |
| 1 2 3 4 | 1 2 3 4 5 |

ndetũ

| | |
|---|---|
| /nd/+/e/+/t/+/u/ | /n/+/d/+/e/+/t/+/u/ |
| 1 2 3 4 | 1 2 3 4 5 |

Kwa mujibu wa Mgullu (1999), ili kuweza kugundua ikiwa nazali na konsonanti zimeungana kuunda fonimu moja, kigezo cha kuzitamka kitiliwe uzito kuliko kuziandika. Hii itaweza kubainisha ikiwa /**mb**/ na /**nd**/ ni fonimu moja moja au ni zaidi. Kuzingatia kigezo cha kutamka sauti hizi katika mifano ya maneno tuliyotoa, inabainika wazi hizi ni fonimu zilizoundwa kwa mwambatano wa nazali na konsonanti. Kwa hivyo, kila mojawapo ni fonimu. Mwihaki (1997); Mugambi (2007); Mwaliwa (2000); Kanake (mtaje) wanaafiki kauli hii. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa lahaja ya Kiimenti huwasilisha konsonanti mwambatano kwa maneno fulani ambapo sauti ya kwanza hutamkiwa pale kitamkwa cha pili hutamkiwa. Mchakato huu hujulikana kama usilimisho pamwe wa nazali. Konsonanti /b/ hutamkwa kwa hewa kuzuiwa na kisha kuachiliwa kwa mpasuo. Hii inafanya nazali iliyoitangulia /m/ kutamkwa kwa jinsi hivyo. Vilevile, konsonanti /d/ hutamkiwa kwenye ufizi na hivyo kufanya nazali /n/ kutamkiwa hapo. Kwa ujumla basi inadhihirika kuwa konsonanti inaathiri nazali inayoitangulia. Hii ndiyo sababu Kihore na Wenzake (wataje) wakaita mfanyiko huu wa konsonanti kuathiri nazali.

Mawazo karibu sawa na haya ni ya Jumwa (mtaje), alipotafitia mnyambuliko wa vitenzi vya Kigiryama. Alisema kuwa katika lugha hiyo kitenzi kama **kwija** (kuiba); sauti /kw/ ni fonimu moja. Muundo wa ndani wa kitenzi hiki ni **kuija** (kuiba). Kwa maoni yake fonimu hii imeundwa kutokana na usigano wa vokali /u/ katika kiambishi awali. Anaendelea kueleza kuwa fonimu /u/ inayeyushwa na kuwa /w/. Kwa hivyo, anatambua usigano wa vokali na uyeyushaji wake kama dhana zinazoeleza kitu kimoja.

Vilevile, katika lahaja ya Kiimenti silabi mwambatano huundwa kwa kudondosha irabu. Mfano wa kitenzi **inkũrĩma** [inkorema] (ninalima) unaweza kutumika kueleza hali hii. Kitenzi hiki kikichanganuliwa kimofemiki kitakuwa /**i-ni-kũrĩma**/. Kwa mujibu wa Salesio (mtaje) irabu /i/ hudondoshwa ikitanguliwa na nazali na kufuatwa na konsonanti ya kipasuo /k/. Mchakato huu hufanyika ili kurahisha matamshi. Kwa hivyo, tunapata kitenzi **inkũrĩma** (ninalima) badala ya **/inikũrĩma**/, irabu /i/ ikidondoshwa.

Hata hivyo, wasomi wengine kama Ashton (mtaje), Polome (1967), Mohammed (mtaje) hawatambui silabi mwambatano kama fonimu. Kwa sababu hii hawazijadili pamoja na fonimu nyingine. Kwa hivyo, katika kazi zao wamepuuza fonimu hizi /mb/, /mv/, nd/, /nj/, /nj/na /nz/. Mohammed (mtaje) anadai kuwa kuwepo kwa fonimu kama hizi ni suala tata kwa wasomi na wanaisimu wa Kiswahili. Kuna uwezekano kuwa sababu hii imewafanya kukwepa fonimu hizi kama fonimu za Kiswahili.

Mukuthuria (2004) anaeleza kuwa kuwepo kwa baadhi ya silabi mwambatano katika lugha huweza kupatikana kutokana na mchakato wa kifonolojia wa usilimisho wa sauti pamwe za kipua, ambao ni mfano wa usilimisho nyuma. Mchakato huu huweza kutumika kueleza hali ya sauti kama /mp/, /mb/, /nt/, /nc/, /nth/ katika lahaja ya Kiimenti. Wakati wa kutamka sauti hizi sauti zinaathiriana hivi kwamba sauti ya kwanza (nazali)

inatamkiwa pahali pa konsonanti inayoandamana nayo. Kwa maoni yetu hali hii inafanya tuseme kuwa hizi pia ni fonimu. Kwa mfano, kutokana na mfanyiko tuliotaja sauti kama /m/ na /b/ huweza kuunda /mb/. Mfanyiko wa usilimisho nyuma hufanya kitamkwa /m/ kuacha pahali pake pa kutamkiwa na kutamkiwa katika pahali pa /b/. Hali hii inafanya sauti /m/ kuchukua sifa za pale /b/ inatamkiwa na kuhamisha sifa yake ya unazali kwa /b/. Kwa hivyo, sauti inayotamkwa ni moja na hivyo kusisitiza hiyo ni fonimu moja. Jedwali la 3 linaonyesha konsonanti mbalimbali za Kiimenti na unukuzi wake.

**Jedwali la 3: Konsonanti za Kiimenti**

| Fonimu | unukuzi | Maneno ya Kiimenti | Unukuzi | Maana Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| b | [β] | bangĩ | [βaŋge] | wengine |
| c | [c] | cionthe | [ciɔnθɛ] | zote |
| g | [ ɡ] | gĩkĩthongi | [ɡekeθɔŋgi] | kizuri |
| j | [ɟ] | jamathũku | [jamaθoku] | mabaya |
| k | [k] | kĩngĩ | [keŋge] | kingine |
| m | [m] | muntũ | [munto] | mtu |
| mb | [mb] | mbakĩ | [mbake] | tumbako |
| n | [n] | nũũ | [no:] | nani |
| p | [p] | pampu | [pampu] | pampu |
| ng’ | [ŋ] | ng’ombe | [ŋɔmbɛ] | ng’ombe |
| ng | [ng] | ngari | [ŋgarĩ] | gari |
| ny | [ɲ] | nyoni | [ɲɔni] | nyuni |
| nk | [nk] | nkamĩĩra | [nkame:ra] | ngamia |
| nd | [nd] | ndene | [ndɛnɛ] | ndani |
| nc | [nc] | ncandi | [ncandi] | ndizichanga |
| nch | [nch] | ncheege | [nchɛ:gɛ] | nungu |
| nt | [nt] | ntũũra | [nto:ra] | kijiji |
| nth | [nθ] | nthitangi | [nθitaŋgi] | ainaya jembe |
| r | [r] | rũgendo | [rogɛndɔ] | safari |
| t | [t] | tara | [tara] | hesabu |
| s | [s] | sabuni | [sabuni] | sabuni |
| th | [θ] | thitanga | [θitaŋga] | shitaki |
| nj | [nɟ] | njaũ | [nɟao] | ndama |
| mp | [mp] | mpandi | [mpandi] | panzi |

### 4.3 Umuhimu wa Fonimu katika Lugha

Fonimu huwa na majukumu mengi katika lugha yoyote ile. Kwa mfano, katika lahaja ya Kiimenti fonimu hutumika kuunda vipashio vikubwa mbalimbali kama silabi, mofu na hata maneno yanayoungana ili kuunda sentensi. Fonimu /ũ/, /m/, /ũ/, /r/, /a/, /j/, /a/ huungana ili kuunda kivumishi **ũmũraja** [omoraɟa] (mrefu). Kivumishi hiki kinaweza kuchanganuliwa ili kupata silabi ambazo zimekiunda. Tukifanya hivyo kitakuwa hivi **$ũ$mũ$ra$ja$** na hivyo kudhihirisha silabi nne. Hii inaonyesha kuwa fonimu zinaweza kuungana ili kuunda silabi kama za konsonanti ikitangulia irabu. Aidha, fonimu zinaweza kuungana na kuunda mofu zinazowakilisha mofimu mbalimbali. Kwa jinsi hii kivumishi **ũmũraja**/u-mũ-raja/ (mrefu) huchanganuliwa kimofemiki na kudhihirisha mofimu mbalimbali. Mofu {**ũ-**} huwakilisha nafsi/idadi (umoja) na ngeli ya sintaksia. Mofu {-**mũ**-} huainisha ngeli ya kwanza ya mofolojia, idadi (umoja) na kiambishi awali cha nomino katika ngeli ya kwanza ya mofolojia. Hatimaye, mofu {-**raja**} huwakilisha mzizi wa kivumishi ambao ni kiini cha ujumbe. Kivumishi **ũmũraja** (mrefu) ni mfano wa neno lenye maana ya mrefu ambalo limeundwa kwa kutumia fonimu mbalimbali. Hili ni dhihirisho kuwa fonimu hutumika kuunda hata maneno yenye maana katika lugha. Fonimu pia hutofautisha maana ya maneno mbalimbali. Mifano ifuatayo ya jozi za mlinganuo finyu katika jedwali la 4 hudhihirisha hali hii.

**Jedwali la 4: Jozi za Mlinganuo Finyu**

| **Kivumishi** | | **Maana** |
|---|---|---|
| **i**rĩa | [irea] | zile |
| **ĩ**rĩa | [erea] | ile |
| **i**ngĩ | [iŋge] | zingine |
| **ĩ**ngĩ | [enge] | nyingine |
| **i**ji | [iɟi] | hizi |
| **ĩ**jĩ | [eje] | hii |

Dhima nyingine ya fonimu ni kubadilisha maana ya neno. Kwa mfano kitenzi cha Kiimenti **ita** kina maana ya 'toa'. Hata hivyo, fonimu /i/ ikibadilishwa na /ĩ/ ili kuunda kitenzi **ĩta** maana hubadilika na kuwa na maana ya 'enda'. Aidha, **Meru** [mɛru] ni nomino ya pahali katika Kiimenti. Fonimu /u/ ya mwisho ikibadilishwa na /ũ/ inakuwa **Merũ** ambalo ni jina la mtu.

Kwa kubadilisha mpangilio wa fonimu katika maneno kuna uwezekano wa kutumia mofimu zizo hizo kuunda maneno mapya. Kwa mfano, kitenzi **ita** [ita] (toa) kina fonimu zinazoweza kuunda nomino mpya ambayo ni 'tai' (tai). Hili ni neno la kategoria tofauti.

### 4.4 Miundo ya Silabi za Kiimenti

TUKI (1990) inaeleza silabi kama kipashio cha utamkaji ambacho kwa kawaida ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho huruhusu sauti kutamkwa kama fungu moja na ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo

kuliko neno (Massamba na Wenzie, wataje). Maelezo mengine ni kuwa silabi ni sehemu ya neno ambayo hutamkika na kusikika ikiwa tofauti na nyingine katika neno. Sifa za silabi hutofautiana kutoka lugha hadi nyingine (Habwe na Karanja, wataje). Vilevile, silabi huweza kuelezwa kama sehemu ya neno ambayo huweza kutamkwa kwa pamoja kama fungu la sauti. Hivyo maneno katika lugha hutamkwa yakizingatia mpangilio wa silabi (Kihore na Wenzie, wataje). Ufafanuzi uliotolewa na watalaamu tuliorejelea kwa kiasi unaafiki maelezo ya silabi. Hata hivyo, maelezo ya TUKI (1999) na Massamba na Wenzie (wataje) kuwa silabi ni kubwa kuliko fonimu yana dosari.

Kwa maoni yetu si kila wakati ambapo silabi huwa kubwa kuliko fonimu. Kuna wakati ambapo zote mbili zina hadhi sawa au zinalingana. Tunaweza kudhihirisha hali hii kwa kutumia fonimu za irabu kutoka lahaja ya Kiimenti, Kwa mfano, vivumishi viashiria vifuatavyo vya Kiimenti **au** [au] (hapo) na **uu** [ũu] (huyo) vinaweza kuchanganuliwa hivi $a$u$ na $u$ũ$, hivyo tunapata silabi mbalimbali za irabu. Kwa kutumia mbinu ya jozi mlinganuo finyu tunaweza kupata fonimu /a/ na /u/. Vilevile, vitenzi vya Kiswahili ‘oa’ na ‘ua’ vikichanganuliwa kama tulivyofanyia viashiria vya Kiimenti itadhihirika kuwa /o/ na /u/ ni fonimu tofauti. Aidha, hizi ni silabi za irabu mbalimbali katika vitenzi hivyo. Kwa hivyo, kulingana na mifano tuliyotoa ni dhahiri kuwa si kila wakati fonimu inakuwa kubwa kuliko silabi. Katika lahaja ya Kiimenti miundo ifuatayo ya silabi huweza kudhihirika:

### 4.4.1 Irabu Pekee (I)

Lahaja ya Kiimenti huweza kuwa na muudo wa irabu moja katika neno **area** [arɛa] (pale) ambalo likichanganuliwa litakuwa **$a$re$a$.** Irabu **$a$** ya mwanzo na **$a$** ya mwisho katika neno hilo ni mfano wa muundo wa irabu moja katika neno husika. Hali

inayojitokeza hapa ni kuwa muundo wa irabu moja pekee huweza kutokea mwanzo na mwisho wa neno. Hata hivyo, muundo wa irabu moja pekee huweza hata kutokea katikati ya neno kama katika neno **biakũrĩa** [βiakorea] (chakula) ambalo likichanganuliwa litakuwa **$bi$a$kũ$rĩ$a$.** Hapa inaonekana irabu **$a$** ikitokea katikati ya neno **biakũrĩa** (chakula). Hii ina maana kuwa muundo wa irabu moja pekee huweza kutokea katika mazingira yote ya neno.

### 4.4.2 Nusu Irabu (½ I) na Irabu (I)

Vivumishi vya Kiimenti kama **yao** [jaɔ] (yao) na **wenu** [wɛnu] (wenu) vikichanganuliwa vitakuwa **$ya$o$** na **$we$nu$.** Hii inaonyesha kuwa irabu **$ya$** na **$we$** katika maneno hayo huzingatia muundo wa nusu irabu ikifuatwa na irabu. Muundo huu wa irabu unaonekana kutokea katika mwanzo wa maneno. Aidha, unaweza kupatikana katika mwisho wa vivumishi kama **yawe** [jawɛ] (yake) na **wawe** [wawɛ] (wake).

### 4.4.3. Konsonanti (K) na Irabu (I)

Muundo mwingine wa irabu unaodhihirika ni wa konsonanti na irabu. Muundo huu hudhihirika kama hivi katika neno **kĩĩĩj** [keːɟe] (mvulana mkubwa). Neno hilo likichanganuliwa litakuwa **$kĩ$ĩ$jĩ$.** Silabi **$kĩ$** na **$jĩ$** ni mifano ya irabu zinazozingatia muundo wa konsonanti na irabu. Muundo wa konsonanti na irabu huweza kutokea katika maeneo mbalimbali ya neno. Mfano tuliotoa unaonyesha muundo huo ukitokea mwanzo na mwisho wa neno. Katika kivumishi **gĩkĩthongi** [gekeθɔŋgi] (kizuri) silabi **$kĩ$** inapatikana ikiwa kati ya neno hilo linapochanganuliwa kama hivi **$gĩ$kĩ$tho$ngi$.** Silabi **$kĩ$** huweza kutokea ikiwa ya mwisho katika neno gĩkĩ (hiki). Linapochanganuliwa linakuwa **$gĩ$kĩ$.** Hii ni kuonyesha kuwa aina moja ya silabi yenye muundo wa konsonanti na irabu huweza kutokea mwanzo, katikati na mwisho wa neno

kama ilivyodhihirishwa na silabi **$kĩ$** katika maneno **gĩkĩthongi, gĩkĩ na kĩĩjĩ.** Silabi zenye muundo wa konsonanti na irabu hupendelewa sana katika uundaji wa maneno katika lugha za Kibantu (Mbaabu, mtaje). Muundo huo hutumika kwa wingi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingi za ulimwengu (Mgullu, mtaje).

### 4.4.4 Konsonanti (K), Konsonanti (K) na Irabu (I)

Kila lugha huwa na kanuni inazofuata katika kuzipanga sauti za irabu na konsonanti. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili sawa na lugha za Kibantu hutumia mwambatano wa konsonanti na irabu ili kuunda maneno (Mbaabu, 1999). Muundo kama huu hubainika katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, kuna muundo wa konsonanti, konsonanti na irabu katika lahaja ya Kiimenti unaodhihirika katika mazingira yote ya neno. Kwa mfano, neno **chetani** [ʧɛtani] (shetani) likichanganuliwa litakuwa **$che$ta$ni$** [ʧɛtani] ambapo silabi **$che$** ni ya mwanzo kwenye neno hilo yenye muundo wa konsonanti, konsonanti na irabu. Muundo kama huo unadhihirika kati ya neno katika neno **nkenkeia** [nkɛnkɛia] (aina ya magugu ya shambani) linalochanganuliwa hivi **$nke$nke$i$a$** na kupata silabi **$nke$** ikiwa ya kati katika neno hilo. Muundo sawa na huo unadhihirika mwishoni mwa neno **antũ** [anto] (watu) ambalo likichanganuliwa linakuwa **$a$ntũ$.** Kwa hivyo, silabi **$ntũ$** ni ya mwisho katika neno **antũ.** Katika lahaja ya Kiimenti, si konsonanti zote ambazo zinaweza kutumika mwanzoni mwa silabi kuunda silabi za konsonanti, konsonanti na irabu yoyote. Zile ambazo zina uwezo wa kushirikishwa katika sehemu hiyo ni za aina mbili. Hizi ni konsonanti za nazali na vipasuo. Hali hii inadhihirika katika mifano ya silabi hizi kama **$mbi$** na $**ntũ$** katika maneno **mbica** [mbica] (picha) na **ntukũ** [ntuko] (siku) na maneno mengine yenye kudhihirisha hali hiyo. Kulingana na mifano hii konsonanti za mwanzo katika silabi hizi ni /m/ na /n/ ambazo ni nazali.

### 4.4.5 Konsonanti (K) Nusu Irabu (½I) na Irabu (I)

Muundo huu hudhihirika mwanzo na mwisho wa maneno kama **ĩmwe** [emwɛ] (moja) na **mwene** [mwɛnɛ] (mwenyewe). Maneno hayo yanapochanganuliwa kama hivi **$ĩ$mwe$** na **$mwe$ne$** tunapata silabi **$mwe$** ikiwa ya mwanzo na mwisho kwenye maneno hayo. Mifano mingine ya maneno yenye muundo sawa wa silabi tulioangazia ni kama **twana** [twana] (watoto), **bagwĩta** [βagweta] (wameenda), **bakwĩja** [βakweɟa] (wamekuja), **bwĩje** [βweɟɛ] (mje), **nyama** [ɲama] (nyama), **nyoni** [ɲɔni] (nyuni) na kadhalika. Maneno haya yakichanganuliwa tutapata silabi hizi: **$twa$na$**, **$ba$gwĩ$ta$**, **$ba$kw$ĩja$**, **$bwĩ$je$**, **$nya$ma$** na **$nyo$ni$**. Kulingana na mifano tuliyotoa inaonekana muundo wa konsonanti, nusu irabu na irabu huundwa na sauti za vituo zikifuatwa na nusu irabu /w/ na kisha irabu yoyote. Sauti hizi za vituo zinazopatikanana mwanzoni mwa silabi hizi ni /b/, /k/, /g/ na /t/ kama inavyodhihirika kwenye mifano tuliyoangazia kushadidia dai letu.

### 4.4.6 Konsonanti (K), Konsonanti (K), Nusu Irabu (½ I) na Irabu (I)

Muundo huu huweza kupatikana katika maneno kama **nkwĩja** [nkweɟa] (nimekuja) na **nkware** [nkwarɛ] (kware). Maneno hayo yakichanganuliwa yatakuwa hivi **$nkwĩ$ja$** na **$nkwa$re$**. Kwa hivyo, silabi zinazozingatia muundo wa konsonanti, konsonanti, nusu irabu na irabu ni **$nkwi$** na **$nkwa$** ambazo zote ni silabi awali katika maneno hayo.

Tukirejelea miundo ya silabi za lahaja ya Kiimenti ni wazi kuwa kuna silabi za muundo wa irabu pekee; nusu irabu na irabu; konsonanti na irabu; konsonanti, konsonanti, irabu; konsonanti, nusu irabu na irabu; na konsonanti, konsonanti, nusu irabu na irabu.

Kwa mujibu wa mifano ya miundo mbalimbali ya silabi za lahaja ya Kiimenti, ni wazi kuwa lahaja hiyo inapendelea silabi huru au wazi kuliko funge. Silabi huru ni ile ambayo

huishia na irabu ilhali funge huishia kwa konsonanti. Maoni ya Kihore na Wenzie (wataje) ni kuwa lugha za Kibantu hupendelea mfumo wa silabi huru. Aidha, imedhihirika kuwa silabi huweza kuwakilishwa na sauti moja, mbili, tatu, na hata nne katika lahaja ya Kiimenti.

**4.5 Dhana ya Mofu**

Mofu ni kipashio kidogo sana cha neno ambacho hakiwezi kukatwa kwa vipande vidogo zaidi na kuwasilisha maana. Maana inayowakilishwa na mofu ndiyo hutambulikana kama mofimu. Tukirejelea sifa za mofu kulingana na Mgullu (1999) tunaweza kusema kuwa mofu ni sehemu ndogo sana ya neno yenye maana ambayo hudhihirika kifonolojia na kimofolojia. Ikiwa basi mofimu ni maana iliyosetiriwa na mofu ndiyo mofimu; ni muhimu kuchanganua neno kwa misingi ya mofu zake ndipo tupate mofimu. Katika lahaja ya Kiimenti umbo la kivumishi cha sifa **jamathongi** [ɟamaθɔŋgi]; huweza kuchanganuliwa na kuwa **/ja-ma-thongi/** na kudhihirisha mofu tatu. Mofu hizi tatu huweza kuchanganuliwa na kuelezwa maana zilizosetiriwa na hivyo kurejelea dhana ya mofimu ambapo utendakazi wake kisarufi utabainika. Hivyo, umbo la kivumishi /**jamathongi/** huweza kuwasilisha mofimu mbalimbali zenye usarufi kama hivi.

**{-ja-} –** mofimu ya kipatanishi cha ngeli ya 6/16 ya mofolojia (wingi)

- mofimu ya idadi ya umoja

- mofimu inayowakilisha nomino katika ngeli ya 6/16 (MA) (wingi)

**{-ma-}** -mofimu ya idadi ya wingi

-kiwakilishi cha ngeli

**{-thongi-}-** mzizi wa kitenzi unaowasilisha maana ya kileksia

Kwa mujibu wa mfano wa umbo la kivumishi cha Kiimenti /**jamathongi**/ imebainika kuwa mofu ni tatu ilhali mofimu ni tano. Kwa hivyo, mofu ni sehemu halisi ya neno ambayo huweza kuandikwa na kutamkwa na wazungumzaji wa lugha yoyote ile. Hii ina maana kuwa maneno ya lahaja ya Kiimenti na lugha zote ulimwenguni huwasilisha maana. Maana hiyo huwasilishwa na mofu za maumbo ya maneno.

### 4.5.1 Mofu, Alomofu na Mofimu katika Lahaja ya Kiimenti

Dhana za mofu, alomofu na mofimu hukaribiana na zinahusiana (Mgullu, 1988). Vilevile, hutumika sana katika uchambuzi wa kiisimu hasa katika ngazi ya mofolojia. Hata hivyo hukanganya watumiaji wake (Mgullu, 1999). Kwa hivyo ni muhimu kuelewa dhana hizi vizuri kwa sababu ni muhimu katika uchanganuzi wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Hii ni kwa sababu zisipoeleweka vizuri zinaweza kutatiza uelewaji wa usarufi katika vivumishi vya Kiimenti. Tayari tumeeleza kuwa mofu ni kipashio kidogo sana katika neno kinachowasilisha maana. Maana inayowasilishwa na mofu nayo ni mofimu. Uhusiano kati ya mofu na mofimu ni ule wa kiashiria na kiashiriwa au umbo na yaliyomo (Habwe na Karanja, wataje). Kwa hivyo, mofu huwa kiashiria na mofimu kiashiriwa. Maana ya mofimu imekabiliwa na mabadiliko hasa baada ya kuasisiwa kwa Sarufi Zalishi. Kabla ya kuasisiwa kwa Sarufi Zalishi dhana ya mofimu ilikuwa kama tulivyojadili maana ya mofu. Lakini baada ya kuasisiwa Sarufi Zalishi ndipo mofimu ikaelezwa kama maana inayosetiriwa katika umbo la mofu. Hartman (1972) akinukuliwa na Mgullu (1999) anaeleza mofimu kama kipashio dhahania cha umbo fulani ambacho huwakilishwa na mofu. Hii ina maana kuwa huwezi kuona, kuandika au kutamka mofimu. Mofimu ikiondolewa  katika neno, basi maana ya neno huathirika. Mofimu huweza kubeba maana ya kisarufi au ya kileksia. Maana ya kisarufi hutokana na

utendakazi wa mofimu mbalimbali katika neno baada ya kulichanganua kimofemiki. Kwa mfano kivumishi cha sifa cha Kiimenti **ũmũkũrũ** [omokoro] (aliyezeeka) kikichanganuliwa tunapata mofimu zifuatazo {**u-**}, {**-mũ -**} na {**-kũrũ}**. Uamilifu wa mofimu hizi ni kama ifuatavyo:

**{**ũ **-}** mofimu ya kuwakilisha nafsi

mofimu ya idadi (umoja)

kipatanishi cha ngeli ya 1 ya mofolojia (MU/MW) (umoja)

**{-mũ -}** mofimu ya kuwakilisha ngeli ya 1 ya mofolojia (MU/MW) (umoja)

Mofimu ya idadi (umoja)

Mofimu inayowakilisha nomino katika ngeli ya (MU/MW) (umoja)

**{-kũrũ}** mofimu ya mzizi wa kivumishi na hubeba maana ya msingi (kileksia)

### 4.5.2 Mofimu katika Lahaja ya Kiimenti

Mofimu ni kipashio kidogo sana cha kisarufi chenye maana ama ya kisarufi au ya kileksia (TUKI, 2004). Vivumishi **gĩkĩnene**[gekenɛnɛ] (kikubwa), **bibithũku** [βiβiθoku] (vibaya) na **ũmũnene** [omonɛnɛ](mkubwa) katika lahaja ya Kiimenti huweza kuchanganuliwa kimofemiki na kupata mofimu zifuatazo:

**gĩkĩnene** [gekenɛnɛ] (kikubwa) /gĩ-kĩ-nene/

{gĩ -}- kipatanishi cha ngeli ya 7 GĨ/KĨ (umoja)

-mofimu ya idadi (umoja)

{- ki -} – kiambishi cha ngeli ya 7 GĨ/KĨ (umoja)

- Mofimu ya idadi (umoja)
- Mofimu inayowakilisha nomino katika ngeli ya 7 GĨ/KĨ (umoja)

{-nene}- mzizi wa kivumishi cha sifa.

**bibithũku** [βiβiθoku] (vibaya) /bi-bi-thuku/

{bi-}-kipatanishi cha ngeli ya 8 I/BI (wingi)

-mofimu ya idadi (wingi)

{-bi-}-kiambishi cha ngeli ya 8 I/BI (wingi)

- Mofimu inayowakilisha nomino katika ngeli ya 8 I/BI (wingi)
- Mofimu ya idadi (wingi)

{-thũku}-mzizi wa kivumishi cha sifa

**ũmũnene** [omonɛnɛ](mkubwa) **/ũ -mũ -nene/**

{ũ-}-kipatanishi cha ngeli ya 1 MU/MŨ /MW (umoja)

-mofimu ya idadi (umoja)

{-mũ-} – kiambishi cha ngeli ya 1 MU/MŨ /MW (umoja)

- Mofimu inayowakilisha nomino katika ngeli ya 1 MU/ MŨ /MW (umoja).
- Mofimu ya idadi (umoja)

-nene- mzizi wa kivumishi cha sifa.

Mifano ya vivumishi vilivyochanganuliwa kimofemiki tuliyotoa inaonyesha kuwa mizizi {-**nene**} na {-**thũku**} imeambishwa viambishi awali au viambishi kabla ya mzizi. Viambishi hivyo vinatekeleza kazi mbalimbali za kisarufi. Kwa mfano katika kivumishi **bibithũku** [βiβiθoku] (vibaya) kuna mzizi –**thũku** ulioambishwa viambishi awali **{ũ -}** na **{-mũ -}**. Mofu **{ũ -}** katika kivumishi hicho huwakilisha mofimu ya kipatanishi cha ngeli na idadi ya wingi. Kipatanishi cha ngeli ni umbo ambalo huwekwa mwanzoni mwa kitenzi kulingana na nomino inayoelezwa habari zake katika kitenzi (Mgullu, 1999; Mohammed, mtaje). Maelezo zaidi ya Mohammed (mtaje) ni kuwa kipatanishi huwakilisha ngeli ya nomino, nomino yenyewe na huwa na kazi mbalimbali za kisarufi.

Kwa kiasi maelezo haya yana upungufu fulani kwa sababu hatuelezwi kipatanishi huwakilisha ngeli gani. Kwa maoni yetu kipatanishi huwakilisha ngeli za sintaksia. Hii ni kwa sababu ngeli za kisintaksia zimeundwa kwa kutumia vipatanishi. Aidha, kazi mbalimbali za kisarufi hazikubainishwa. Lakini kwa maoni yetu kazi hizi ni kama idadi na kadhalika. Hata hivyo, tunakubaliana naye kuwa kipatanishi huweza kuwakilisha nomino.

Mofu **{-bi-}** nayo inawakilisha mofimu ya kiambishi ngeli. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa maumbo mbalimbali ya kivumishi cha lahaja ya Kiimenti huwasilisha mofu zenye usarufi. Mpaka hapa ni wazi kuwa dhana za mofu na mofimu zimebainika kwa uwazi.

Kwa upande mwingine alomofu ni dhana ya kueleza sura mbalimbali za mofimu moja (Munguti, 1989; Habwe na Karanja, wataje). Hii ni kwa sababu kila mofu huwakilisha mofimu moja lakini kuna uwezekano wa mofu zaidi ya moja kuwakilisha mofimu moja. Hali hiyo ndiyo hujulikana kama ualomofu na mofu zinazohusika huitwa alomofu (Habwe na Karanja, wataje). Kwa mfano, katika ngeli ya 7 G**Ĩ**/K**Ĩ** (umoja), mofu {**gĩ} na** {**k**ĩ} hutumika kuwakilisha mofimu moja ambayo ni kiambishi ngeli katika ngeli hiyo. Kwa hivyo, majina katika ngeli hiyo huweza kuwa ama na kiambishi {**gĩ}** au {**kĩ}** mwanzoni au kama viambishi awali. Mfano wa majina hayo ni kama:

kĩbanga [keβanga] (panga), **k**ĩthii [keθi:] (kinu), **k**ĩbiriti [keβiriti] (kiberiti), **k**ĩrombero [kerɔmbɛrɔ] (kanisa). **g**ĩtĩ [gete] (kiti), **g**ĩntu [gento] (kitu), **g**ĩkombe [gekɔmbɛ] (kikombe), **g**ĩciko [gecikɔ] (kijiko) na **g**ĩkabu [gekaβu] (kikapu).

Itaeleweka zaidi kuwa mofu {**g**ĩ} **na** {**k**ĩ} ni alomofu za mofimu moja kwa kutumia baadhi ya majina tuliyotoa hapo juu kwenye sentensi. Kwa mfano:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i. | Gĩkombe **g**ĩkĩthũku **g**ĩkũgũrwa | Ikombe bibithũku bikũgũrwa |
| | [Gekɔmbɛ gekeθoku gekogorwa] | [Ikɔmbɛ βiβiθoku βik**o**g**o**rwa] |
| | Kikombe kibaya kimenunuliwa. | Vikombe vibaya vimenunuliwa. |
| ii. | Gĩkabu **g**ĩkũrũ **k**ĩgũtambũka | Ikabũ bibikũrũ bigũtambũka |
| | [Gekabo gekoro kegotamboka] | [Ikabo βiβikoro βigotamboka] |
| | Kikapu kizee kimeharibika. | Vikapu vizee vimeharibika. |
| iii | Kĩbanga **g**ĩkiega **g**ĩkũgũrwa | Ibanga bibiega bikũgũrwa |
| | [Keβaŋga gekeɛga gekogorwa] | [Iβaŋga βiβiɛga βikogorwa] |
| | Panga nzuri imenunuliwa. | Mapanga mazuri yamenunuliwa. |
| iv. | **Kĩt**hii **k**ĩngĩ **k**ĩgwakwa | Ithii bingĩ bigwakwa |
| | [Keθi: keŋge kegwakwa] | [Iθi: βiŋge βigwakwa] |
| | Kinu kingine kimejengwa | Vinu vingine vimejengwa. |

Kwa hivyo, kutokana na mifano ya sentensi hii, mofu {gĩ} na {kĩ} ni alomofu za mofimu ya ngeli katika ngeli ya 7 Kĩ/Gĩ. Hii ni kwa sababu majina hayo yana mzizi awali ambao ni {gĩ} au {kĩ} katika umoja. Katika hali ya wingi majina haya yanaambishwa mofu i, ya wingi. Vilevile, majina katika ngeli husika huwakilishwa na kipatanishi {kĩ} au {gĩ}. Hii ni sababu nyingine ya kudai kuwa mofu hizi ni alomofu za mofimu moja.

Vilevile, idadi (umoja) katika ngeli ya Gĩ /Kĩ huweza kuonyeshwa kutumia viambishi (mofu) {**g**ĩ} na {**k**ĩ}**.** Hii basi inasisitiza kuwa hizi ni alomofu kwa sababu ni mofu mbili ambazo zinawakilisha dhana moja au mofimu moja ya idadi katika ngeli husika.

Mfano mwingine kuhusu alomofu unapatikana katika ngeli ya 5 (Ĩ/I/RI). Katika ngeli hii mofu /ĩ/, /i/ na /ri/ ni alomofu za mofimu ya umoja. Hii ina maana kuwa mofu hizo mbili

huweza kutumika kama kiambishi awali cha nomino katika majina ya ngeli hiyo (umoja). Mifano ya majina yafuatayo ambayo ni ya ngeli hii hushadidia hali hii: **iga** [iga] (jiwe), **ĩgo** [egɔ] (jino), **ĩrinya** [eriɲa] (shimo), **iuku** [iuku] (kitabu), **ĩrandu** [erandu] (deni), **ĩjai** [eɟai] (yai), **ĩrigu** [erigu] (ndizi), **riko** [rikɔ] (jiko), **ritho** [riθɔ] (jicho), **riĩtwa** [rietwa] (jina).

Vilevile, mifano mingine ya alomofu hupatikana katika ngeli ya 17 na 18 (KA/GA – TW/TŨ) ambapo majina katika ngeli hiyo huambishwa mofu /ka/ au /ga/ katika umoja, na mofu /tw/ au /tũ / katika wingi. Kwa mfano, **kamuntũ** [kamunto] – **tũmuntũ** [tomunto], **gakabũ** [gakabo] – **tũkabũ** [tokabo] na **kaana** [ka:na] – **twaana** [twa:na]. Kulingana na mifano hii umoja wa majina ya ngeli huweza kuwakilishwa kutumia mofu /ka/ au /ga/. Wingi huwakilishwa kutukia mofu /tw/ au /tũ /. Kwa hivyo ni wazi kuwa mofu **/ka/, /ga/, /tw/ na /tũ /** ni alomofu za mofimu za ngeli, idadi na hata nomino. Mifano tuliyotoa ni michache kuhusu alomofu kwenye lahaja ya Kiimenti. Kuna mingine mingi lakini hii inatosha kuweka wazi suala hili lenye utata kwa wasomaji wengi. Hata kama alomofu hutokea katika maneno, hazitokei kiholela. Hali hii inasisitizwa na Mgullu (1999) anaposema kuwa kila alomofu ina mahali pa kutokea, yaani zimegawana mahali pa kutokea. Hii ina maana kuwa zina mgawanyo wa kiutoano.

### 4.5.3 Aina za Mofu katika Lahaja ya Kiimenti

Mofu huainishwa kwa kutumia vigezo viwili. Vigezo hivi ni mofolojia ya mofu na maana zinazoziwakilisha. Kwa kutumia kigezo cha maana zinazowakilishwa na mofu aina tatu za mofu hupatikana. Hizi ni mofu huru, funge na tata. Kwa kutumia kigezo cha mofolojia au maumbo ya mofu yenyewe, mofu kapa na changamano huainishwa. Kwa kuzingatia vigezo viwili vilivyodokezwa aina tano za mofu hubainishwa. Hizi ni mofu huru, funge,

tata, kapa na changamano (Mgullu, 1999). Lahaja ya Kiimenti huweza kudhihirisha aina hizi za mofu katika matumizi yake.

#### 4.5.3.1 Mofu Huru katika Lahaja ya Kiimenti

Mofu huru hubeba mofimu zilizokamilika na hujisimamia kimaana. Mofu huru huweza kuwa neno kamili linalojisimamia kimaana na halihitaji mofimu zingine ili kukamilisha maana. Huwezi kutoa kipande chochote katika mofu huru bila kuathiri maana yake. Mofimu huru huweza kuwa mizizi ya maneno inayobeba maana ya kileksia (Habwe na Karanja, wataje). Mifano ya mofimu huru katika lahaja ya Kiimenti ni kama **maami** [ma:mi] (mama), **baaba** [βa:βa] (baba), **kurũ** [kuro] (mbwa). **guci** [guci] (paka), **ng'ombe** [ŋɔmbɛ] (ng'ombe). Mofu hizi zikikatwakatwa hadi vipande vidogovidogo zitapoteza maana asilia. Kwa mfano, mofu huru {**guci**}[guci] na {**kurũ**} [kuro] zikitengwa katika silabi zake zitakuwa /**gu-ci**/ na /**ku-ru**/ na zitapoteza maana asilia kabisa. Kwa hivyo, lahaja ya Kiimenti ina mofu huru hata kama baadhi yazo ni za kukopwa.

#### 4.5.3.2 Mofu Funge katika Lahaja ya Kiimenti

Mofu funge ni zile ambazo hazikai kwa neno peke yake na kukamilisha maana ya neno bali lazima zitegemee mofu zingine ndipo kukamilisha maana ya neno. Mofu funge haiwezi kutumika peke yake kama neno lenye maana kamili bali hutumiwa kama kiambishi kinachoambatana na kiambishi au viambishi vingine ili kukamilisha maana ya neno (Habwe na Karanja, wataje). Mofu funge huitwa pia mofu tegemezi kwa sababu ya hali ya kukosa kukaa peke yake kama neno kamili bila kutotegemea mofu zingine. Mofu funge mara nyingi huwakilisha maana ya kisarufi (Mgullu, 1999). Kwa mfano kivumishi

cha lahaja ya Kiimenti kama **ĩmĩkũrũ** [emekoro] (iliyozeeka) kikichanganuliwa kimofemiki mofu zenye usarufi zinazowakilisha mofimu zifuatazo hupatikana:

ĩmĩkuru [emekoro] /**ĩ-mĩ-kũrũ**/ (iliyozeeka)

{**ĩ** -} - mofu inayowakilisha mofimu ya umoja

- mofu inayowakilisha mofimu ya kipatanishi

**{-mĩ-}**- mofu inayowakilisha kiambishingeli katika ngeli ya 4 MĨ (umoja)

- mofu inayowakilisha mofimu ya nomino katika ngeli ya 4 MĨ (umoja)

- mofimu ya idadi (umoja)

**{-kũrũ}**- mzizi wa kivumishi unaobeba maana ya kileksia

Kutokana na mfano huo mofu funge ni **{ĩ-}** na **{-mĩ-}** kwa sababu kila mojawapo haiwezi kukamilisha maana ya neno pasipo kutegemea nyingine. Vilevile, mofimu hizo huwakilisha maana ya kisarufi kuliko ile ya kileksia. Hata zinajulikana kama viambishi awali kwa sababu zimeambishwa kwa mzizi **{-kũrũ}.**

**4.5.3.3 Mofu Tata katika Lahaja ya Kiimenti**

Mofu tata ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja (Mgullu, 1999). Kwa mfano sentensi ifuatayo ya lahaja ya Kiimenti inadhihirisha mofu tata.

**Mũrĩthi akũringĩra ĩthe thimũ**.

[Moreθi akoriŋgera ethɛ θimo]

Murithi amepigia babake simu.

Sentensi hii ina utata kwa sababu ina maana zaidi ya moja. Utata wake unasababishwa na kitenzi **akũringĩra** bali si wa kisarufi. Kitenzi kina mofu tano ambazo ni:

{a}+{kũ}+{ring}+{ĩr}+{a}

Katika kitenzi hicho mofu yenye utata ni ya nne (tukihesabu kutoka kushoto hadi kulia) au mofu ya pili kutoka mwisho. Mofu yenyewe ni {**ĩr**} ambayo inaonyesha hali ya kutendea. Utata wenyewe unatokana na hali hiyo ya kutendea. Hii ni kwa sababu tafsiri nyingi huweza kufanyiwa sentensi hiyo. Baadhi ya tafsiri hizi ni kama:

i). Mũrĩthi alipiga simu kwa babake ili awasiliane naye.

ii). Mũrĩthi alipiga simu kwa niaba ya babake. Hii ina maana kuwa babake alipaswa kupiga simu pahali fulani lakini Murithi akafanya kitendo hicho kwa niaba ya babake.

iii). Mũrĩthi alipokuwa akipita karibu na ilipokuwa simu ya babake aliigonga au aliipiga.

iv). Babake Mũrĩthi hana uwezo au weledi wa kupiga simu. Kwa hivyo, ili kuwasiliana kwa simu alimtegemea Mũrĩthi.

Mpaka hapa ni wazi kuwa sentensi yetu imepata maana nne kutokana na mofu tata {-ĩr-} ya kutendea. Mofu tata licha ya kutokea katika lugha, ifahamike kuwa ni mofu funge. Hii ina maana haiwezi kukamilisha maana pasipo kutegemea mofu zingine katika neno.

#### 4.5.3.4 Mofu Mseto katika Lahaja ya Kiimenti

Mofu mseto ni ile ambayo ina uamilifu zaidi ya mmoja katika neno. Mofu hii hubainika katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, kivumishi **inthũku** [inθoku] /i-n-thũku/(mbaya) kinaweza kuchanganuliwa na kuonyesha mofu mseto. Kinaweza kuchanganuliwa hivi:

**inthũku** [inθoku] /i-n-thũku/(mbaya)

{i-} kiwakilishi cha ngeli ya sintaksia

Kipatanishi cha ngeli ya 10

Kiwakilishi cha idadi (umoja)

{-n-} kiwakilishi cha ngeli ya mofolojia ya 10 (N)

Kiwakilishi awali cha nomino katika ngeli ya 10 (N)

Kiwakilishi cha idadi

{-thũku} mzizi wa kivumishi

Kutokana na mfano wa kitenzi **inthũku** [inθoku] /i-n-thũku/(mbaya) imebainika kuwa mofu {i-} na {-n-} zina utendakazi zaidi ya mmoja. Hizo ni mofu mseto katika kivumishi husika.

#### 4.5.3.5 Mofu Kapa katika Lahaja ya Kiimenti

Mofu kapa ni kipashio cha kiisimu ambacho ni cha kidhahania kinachotumika katika uchanganuzi na hakidhihiriki (TUKI, 2004). Mofu kapa hazina umbo, hazitamkwi, hazionekani wala kuandikwa lakini huwasilisha maana (Mgullu, 1999). Ili kueleza dhana ya mofu kapa vizuri nomino katika ngeli za 9/10 ambazo huwakilishwa na herufi N/N katika umoja na wingi huweza kutumika. Majina yafuatayo huweza kupatikana katika ngeli hizo.

**Jedwali la 5: Mofu Kapa**

| Umoja | | wingi | |
|---|---|---|---|
| **nyon**i (nyuni) | [ɲɔni] | **ø - nyoni** (nyuni) | [ɲɔni] |
| **ndege** (ndege) | [ndɛgɛ] | **ø - ndege** (ndege) | [ndɛgɛ] |
| **ngarĩ** (gari) | [ŋgare] | **ø - ngarĩ** (gari) | [ŋgare] |
| **ngitũjũ** (sungura) | [ŋgitojo] | **ø - ngitũjũ** (sungura) | [ŋgitojo] |
| **ng'ombe** (ng'ombe) | [ŋɔmbɛ] | **ø - ng'ombe** (ng'ombe) | [ŋɔmbɛ] |

Majina katika hali ya umoja na wingi hayabadiliki kama ilivyo katika baadhi ya ngeli zingine katika lahaja ya Kiimenti. Hata hivyo, wingi wa majina hayo upo na huwakilishwa na mofu kapa. Mofu kapa huweza kudhihirika katika ngeli hiyo kwa kutunga sentensi kutumia majina hayo. Hii ni kwa sababu hata kama majina hayabadiliki sentensi huweza kuainishwa kama iko katika wingi au umoja. Kwa mfano:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| i) **Ngari ĩkũgũrwa.** | **Ngari ikũgũrwa.** |
| [ŋgare ekogorwa] | [ŋgare ikogorwa] |
| Gari limenunuliwa. | Magari yamenunuliwa. |
| **ii) Nyoni ĩkumatuka.** | **Nyoni ikũmatũka.** |
| [ɲɔni ekomatoka] | [ɲɔni ikomatoka] |
| Ndege ametoroka. | Ndege wametoroka. |
| **iii) Ng'ombe ĩgukua.** | **Ng'ombe igũkua.** |
| [ŋɔmbɛ egokua] | [ŋɔmbɛ igokua] |
| Ng'ombe amekufa. | Ng'ombe wamekufa. |

Kwa hivyo, wingi wa majina katika ngeli ya 10 (N) huweza kubainishwa kwa kutumia mofu kapa ambayo huwasilishwa kwa kutumia alama hii **(ø).** Hii ni kwa sababu tumethibitisha kuwa majina katika ngeli hiyo huweza kuwasilisha wingi licha ya kukosa umbo la kuandikwa au la kutamkwa. Umbo hilo dhahania linalosaidia katika uchanganuzi wa kiisimu ndilo linajulikana kama mofu kapa.

### 4.6 Dhana ya Mzizi katika lahaja ya Kiimenti

Curr (mtaje) anasema kuwa mzizi ni sehemu ya neno ambayo hubaki baada ya kuondoa viambishi vyote vinavyopatikana katika neno. Anatoa mfano wa neno la Kiingereza

“unfriendliness” ambapo ukiondoa kiambishi awali *un-* na viambishi tamati “-ly” na “–ness” unabaki na “friend” kama mzizi. Kuna ukuruba mwingi kati ya mzizi katika lugha za Kibantu kama Kiswahili na lahaja ya Kiimenti. Ni vizuri kufahamu kuwa dhana za mzizi na shina hutatiza wasomi wengi. Haja yetu si kujihusisha katika kuainisha mzizi na shina katika maneno ya lugha. Tunatoa rai wasomi waweke wazi istilahi hizi ili kuepuka maelezo yanayohitilafiana. Maelezo mengine ni kuwa mzizi ni sehemu ya neno ambayo huwa haibadiliki (TUKI, 1999). Vilevile mzizi ni sehemu ya neno ambayo ni kiini cha maana na haiwezi kuchanganuliwa zaidi bila kupoteza utambulisho wake (TUKI, 2004). Hii ina maana kuwa mzizi ukivunjwavunjwa hadi sehemu ndogondogo utakosa uamilifu wa kuwa kiini cha maana ya neno. Kwa mfano mizizi ya vivumishi vya Kiimenti huweza kudhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 6: Mizizi ya Vivumishi vya Kiimenti**

| **Kivumishi** | **Viambishi Awali** | **Mzizi** |
|---|---|---|
| biao [βiaɔ] (vyao) | bi- | -ao |
| bibirũ [βiβiro] (vyeusi) | bi-bi- | -irũ |
| ũmũnoru [omonɔru] (mnono) | ũ -mũ - | -noru |
| inthũku [inθoku] (mbaya) | i-n- | -thũku |
| jũmwega [ɟomwɛga] (mzuri) | jũ-mw- | -ega |
| intune  [intunɛ] (nyekundu) | i-n- | -tune |
| bangĩ [βaŋge]  (wengine) | ba- | -ngĩ |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali lililo hapo juu linaonyesha sehemu ya mzizi katika baadhi ya vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Aidha, inabainika kuwa kuna mizizi ya vivumishi vya Kiimenti inayoanzia kwa konsonanti na mingine irabu. Kwa ujumla mizizi ya vivumishi vya Kiimenti huishia kwa irabu. Ifahamike kuwa sehemu ya mzizi wa kivumishi haibadiliki licha ya kuongeza viambishi awali. Kinachobadilika ni viambishi vinavyopatikana kwenye mzizi kutegemea ngeli ya jina linalovumishwa.

Kuna mizizi ya aina mbili ambayo ni mizizi huru na tegemezi. Mizizi huru ni ile ambayo inaweza kujisimamia kimaana pasipo kuongezewa viambishi vyovyote. Mizizi tegemezi nayo ni ile ambayo huongezewa viambishi ili iweze kukamilisha maana. Ikiwa peke yake haiwezi kutoa maana kamili, sharti iongezewe viambishi mbalimbali (Mgullu, 1999).

Wakati mwingine si rahisi kubaini mzizi ni wa kategoria gani ya maneno. Hii ni kwa sababu itabidi mzizi huo uambishwe ili uweze kuelewa kategoria ya neno linalobainishwa katika mzizi wowote ule.

### 4.6.1 Mizizi Huru katika Lahaja ya Kiimenti

Kategoria mbalimbali za maneno ya Kiimenti hudhihirisha mizizi huru. Kwa mfano nomino kama **baaba**[βa:βa] (baba), **kũrũ** [koro] (mbwa), **mbũri** [mbori] (mbuzi) na **ngũrwe** [ngorwɛ] (nguruwe) ni mizizi huru. Mifano ya vivumishi ambavyo ni mizizi huru ni kama **maritati** [maritati] (maridadi), **atari** [atari] (hatari) na kadhalika. Mizizi huru ya vielezi ni kama **mono** [mɔnɔ] (mno), **cana** [cana] (sana), **cawa** [cawa] (sawa) na vielezi vingine.

### 4.6.2 Mizizi Tegemezi katika Lahaja ya Kiimenti

Mizizi tegemezi ni ile ambayo hutegemea viambishi awali au viambishi tamati ili kukamilisha maana. Mizizi mingi ya vivumishi vya Kiimenti huongezwa viambishi awali

ili kukamilisha maana. Kwa mfano, mzizi -irũ [-iro] huweza kuongezwa viambishi awali kama {jũ-}na {-mw- } ili kuunda vivumishi **jũmwirũ** [jomwiro] (mweusi) na **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi). Kwa hivyo, **-irũ** [-iro] ni mfano wa mzizi tegemezi. Jedwali la 6 hapo juu linaonyesha mizizi tegemezi mingine.

### 4.6.3 Miundo ya Mizizi ya Vivumishi vya Kiimenti

Hali nyingine ya kuchunguza miundo ya vivumishi vya Kiimenti ni kubainisha jinsi fonimu za irabu na vokali zilivyopangiliwa katika mizizi mbalimbali ya vivumishi husika. Vivumishi vya Kiimenti kabla ya kuishia na irabu huwa na mpangilio mahsusi wa sauti za irabu, nusu irabu na konsonanti. Kwetu ilikuwa muhimu kutalii miundo hii ili kupata uelewa wa miundo mbalimbali ya vivumishi vya Kiimenti na hasa kupata ufahamu wa mizizi inayoambishwa na uamilifu kisarufi katika vivumishi hivyo.

i) Muundo wa irabu pekee katika mzizi **-a** katika vivumishi vya –a unganifu kama **wa /**w-a/ [wa] (wa), **bia** /bi-a/ [βia] (vya), **ja** /j-a/ [ɟa] (ya) na **rĩa** /rĩ-a/ [rea] (la) au mzizi **–u** [u] wa kuonyesha vivumishi viashiria vya mbali kidogo kama **au** /a-u/ [au] (hapo), **ũu** /ũ -u/ [ou] (huyo) na **kĩu** /ki-u/ [keu] (hicho).

ii) Muundo wa konsonanti peke yake kama mzizi **-j**- unaotumika katika kuunda vivumishi viashiria vya karibu. Mifano ni kama **ũju** /ũ-j-ũ / [oɟo] (huyu), **iji** /i-j-i/ [iɟi] (hizi) na **jũjũ** /jũ-j-ũ / [ɟoɟo] (huu).

iii) Muundo wa irabu na irabu kama mzizi–**ao** (-ao) [ao] katika vivumishi kama **yao** /y-ao/ [jaɔ] (yao), **biao** /bi-ao/ [βiaɔ] (vyao), **wao** /w-ao/ [waɔ] (wao) na **rĩao** /rĩ -ao/ [reao] (lao).

iii) Konsonanti na irabu kama mzizi -na (nne) katika kivumishi bina /bi-na/ [βina] (vinne)

iv). Muundo wa irabu, konsonanti na irabu kwenye mizizi –**enu** (-enu) katika kivumishi **wenu** /w-enu/ (wenu), mzizi -**etũ** [-ɛto] (-etu) katika kivumishi **wetũ** /w-etũ / [wɛto] (wetu), mzizi -**irũ** [-iro] (eusi) katika kivumishi **ũmwirũ** /ũ-mw-irũ/ [omwiro] na mzizi -erũ [-ɛro] (-eupe) katika kivumishi **jũmwerũ** /jũ-mw-erũ [ɟomwɛro] mweupe.

v). Muundo wa konsonanti, konsonanti na irabu katika mzizi –**ngĩ** [-ŋge] (-ingine) unaopatikana katika vivumishi kama **ũngi** /o-ngĩ / (mwingine), **bangĩ** /ba-ngĩ / [βaŋge] (wengine) na **jangĩ** [ɟaŋge] /ja-ngĩ / (mengine).

vi). Muundo wa konsonanti, konsonanti, nusu irabu na irabu kama mzizi –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe) katika vivumishi **wengwa** /we-ngwa/ [wɛŋgwa] (mwenyewe), **kĩongwa** /kĩ-o-ngwa/ [kiɔŋgwa] (chenyewe), **rĩongwa** /rĩ-o-ngwa/ [reɔŋgwa] (lenyewe) na **bongwa** /bo-ngwa/ [βɔŋgwa] (wenyewe).

vii). Muundo wa konsonanti, irabu na irabu katika mizizi –**kai** (-chache) na -**kuĩ** [-kue] (-fupi) unayopatikana katika vivumishi **bakai** /ba-kai/ [βakai] (wachache), **bikai** /bi-kai/ [βikai] (vichache), ũmũkũĩ /ũ-mũ-kuĩ/ [omokue] (mfupi) na jamakuĩ /ja-ma-kuĩ/ [ɟamakue] (mafupi).

viii). Muundo wa konsonanti, nusu irabu na irabu katika mzizi –**mwe** [-mwɛ] (moja) unaopatikana katika vivumishi **ũmwe** /ũ-mwe/ [omwɛ] mmoja, **kĩmwe** /kĩ-mwe/ [kemwɛ] (kimoja) na **jũmwe** /jũ-mwe/ [ɟomwɛ] (mmoja).

ix) Muundo wa konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti na irabu katika mizizi –**thũku** [-θoku] (-baya), -**thatũ** [-θato] (-tatu) -**thano** [-θanɔ] (-tano) na -**theru** [-θɛru] (-safi) inayopatikana katika vivumishi **ũmũthũku** /ũ -mũ-thũku/[omothoku] (mbaya), **ithatũ** /i-thatũ / [iθato] (tatu), **ithano** /i-thano/ [iθanɔ] (tano) na **gĩkĩtheru** /gĩ -kĩ-theru/ [gekeθɛru] (kilicho safi).

x) Muundo wa konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, konsonanti na irabu katika mzizi–**thongi** [-θɔŋgi] (-zuri) unaopatikana katika vivumishi **ũmũthongi** / ũ-mũ-thongi/ [omoθɔŋgi] (mzuri) **jamathongi** /ja-ma-thongi/ [ɟamaθɔŋgi] (mazuri) na **gĩkĩthongi** /gĩ-kĩ-thongi/ [gekeθɔŋgi].

xi). Muundo wa konsonanti, irabu, konsonanti na irabu katika mizizi kama –**nene** [-nɛnɛ] (kubwa), **-noru** [-nɔnɔ] (nono), **-kũrũ** [-koro] (zeeka), na -**kũmi** [-komi] (kumi). Vivumishi vyenye muundo wa mizizi hiyo ni kama **mũnene** /mũ-nene/ [monɛnɛ] (mkubwa), **ũmũnoru** /ũ-mũ-noru/ [omonoru] (aliye mnono), **inkũrũ** /i-n-kũrũ / [inkoro] (zilizozeeka) na **ĩkũmi** /ĩ -kumi/ [ekomi] (kumi).

xii) Muundo wa konsonanti, konsonanti, irabu na irabu katika mzizi **–thao** [-θaɔ] (-vivu). Kivumishi cha jina **mũthao** /mu-thao/ [moθaɔ] (mvivu) huonyesha mzizi wenye muundo huo.

xiii) Muundo wa mzizi wenye konsonanti, irabu, konsonanti, nusu irabu, irabu, konsonanti, konsonanti na irabu katika kivumishi **mũgwanja** /mũgwanja/ [mogwanɟa] (saba)

xiv). Muundo wa mzizi wenye irabu, konsonanti, nusu irabu na irabu katika mzizi **–akwa** (-angu). Mzizi huu hupatikana katika vivumishi kama **biakwa** /bi-akwa/ [βiakwa] (vyangu), **wakwa** /w-akwa/ [wakwa] (wangu) na **rĩakwa** /rĩ-akwa/ [reakwa] (langu).

xvi). Muundo wa mzizi wenye konsonanti, konsonanti, konsonanti na irabu kama –**nthe** [-nθɛ] (-ote). Vivumishi vyenye mzizi huo ni kama **bonthe** /bo-nthe/ [βɔnθɛ] (wote) na **bionthe** /bi-o-nthe/ [βiɔnθɛ] (vyote).

xvii). Muundo wa mzizi wenye konsonanti, irabu, konsonanti, konsonanti na irabu katika kivumishi **jamagundu** /ja-ma-gundu/ [ɟamagundu] (yaliyoiva).

xviii). Muundo wa mzizi wenye konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu, konsonanti na irabu katika kivumishi **bang'anona** /ba-ng'anona/ [βaŋanɔna] (idadi wastani).

xiv) Muundo wa mzizi wenye konsonanti, irabu, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu katika kivumishi **ũ**m**ũ**rajaraja /ũ -mũ -rajaraja/ [omoraɟaraɟa] (mrefu zaidi).

**4.7 Uamilifu wa Viambishi katika Kivumishi cha Kiimenti**

Kivumishi cha lahaja ya Kiimenti hubeba viambishi vyenye uamilifu wa kisarufi. Hata hivyo, hakibebi viambishi vingi vyenye uamilifu kisarufi kama kitenzi katika lahaja hiyo. Inaaminika kuwa kitenzi cha lahaja ya Kiimenti hubeba viambishi vyenye usarufi kuliko kategoria nyingine za maneno ya Kiimenti kama vile vivumishi, vielezi, viwakilishi na nomino. Aina nyingine za maneno kama; vihusishi na viunganishi huenda yasiambishwe katika lahaja ya Kiimenti. Viambishi vinapotokea katika vivumishi huwa na uamilifu wa kisarufi. Viambishi hivi hutokea kama viambishi awali na vichache vikiwa viambishi tamati kwenye mzizi wa kivumishi. Lahaja ya Kiimenti kama zilivyo lugha za Kibantu ni lugha ambishi. Kwa hivyo, viambishi huweza kudhihirika katika kivumishi cha lahaja ya Kiimenti na hivyo kupanua maana yake.

Kwa mfano, kivumishi cha Kiimenti kikiongezewa kiambishi au viambishi awali kwenye mzizi hupanuka kimaana lakini havibadili kategoria ya maneno. Mzizi wa kivumishi cha sifa kama **{-raja}** [-refu] huweza kutumika kuunda vivumishi mbalimbali. Hivi ni kama **ũmũraja** [omoraɟa], (mrefu), **baraja/babaraja** [βaraɟa/βaβaraɟa] (warefu), **gĩkĩraja** [gekeraɟa] (kirefu), biraja/**bibiraja** [βiraɟa/βiβiraɟa] (virefu), **jũmũraja** [ɟomoraɟa] (mrefu), **ĩmĩraja** [emeraɟa] (mirefu) na **ĩndaja** [endaɟa] (ndefu) kuonyesha umoja wa kitu

katika ngeli ya 9 (N) na **indaja** [indaɟa] [ndefu] kuonyesha wingi wa vitu katika ngeli ya 10 (N). Matumizi ya /i/ na /ĩ/ katika indaja (ndefu) na **ĩndaja** (ndefu) yanaonyesha mfano mzuri wa jozi mlingano finyu katika lahaja ya Kiimenti. Hali ambapo mzizi wa neno huongezwa viambishi mbalimbali na neno halibadilishi kategoria yake hujulikana kama mnyambuliko sarufi. Mifano zaidi ya jinsi mchakato wa mnyambuliko sarufi hubainika katika vivumishi vya Kiimenti inapatikana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 7: Mnyambuliko Sarufi (Vivumishi kutokana na Vivumishi)**

| **Kivumishi** | **Maana** | **Kivumishi** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| -nene | kuwa -kubwa | gĩkĩnene[gekenɛnɛ] | kikubwa |
| -nene | kuwa -kubwa | ũmũnene [omonɛnɛ] | mkubwa |
| -nene | kuwa -kubwa | bibinene [βiβinɛnɛ] | vikubwa |
| -nene | kuwa -kubwa | babanene [βaβanɛnɛ] | wakubwa |
| -nene | kuwa -kubwa | jamanene [ɟamanɛnɛ] | makubwa |
| -nene | kuwa -kubwa | jũmũnene [ɟomonɛnɛ] | mkubwa |
| -thongi | (pendeza) | ũmũthongi [omoθɔŋgi] | anayependeza |
| -thongi | (pendeza) | jamathongi[ɟamaθɔŋgi] | yanayopendeza |
| -thongi | (pendeza) | jũmũthongi[ɟomoθɔŋgi] | unaopendeza |
| -thongi | (pendeza) | babathongi[βaβaθɔŋgi] | wanaopendeza |
| -thongi | (pendeza) | gĩkĩthongi[gekeθɔŋgi] | kinachopendeza |
| -thũku | (-baya) | bibithũku [βiβiθoku] | vibaya |
| -thũku | (-baya) | inthũku [inθoku] | mbaya |
| -thũku | (-baya) | jamathũku [ɟamaθoku] | mabaya |
| -thũku | (-baya) | babathũku [βaβaθoku] | wabaya |
| -thũku | (-baya) | ĩmĩthũku [emeθoku] | mibaya |
| -thũku | (-baya) | gĩkĩthũku[gekeθoku] | kibaya |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Licha ya mzizi wa kivumishi cha Kiimenti kuambishwa mwanzoni hakijabadilika bali kimebaki kuwa kivumishi. Hali hii ni wazi kwani mizizi -**nene** [-nɛnɛ] (-kubwa), **-thongi [-**θɔŋgi] (-pendeza) na **-thũku** [-θoku] (-baya) imetumika kuunda vivumishi vingine. Kwa hivyo, kategoria ya maneno yanayoundwa inabaki kuwa vivumishi kama inavyodhihirika katika jedwali la 7 hapo juu.

Ni vizuri kufahamu kuwa kitenzi cha Kiimenti huweza kunyambuliwa na kuunda kivumishi cha lahaja hiyo. Hali hii inawezekana kwa kuondoa kiishio cha kitenzi na kuongeza kiambishi tamati kwenye mzizi wa kivumishi. Kwa mfano, mzizi wa kitenzi -**thũka** huweza kuunda vivumishi kama**:** jama**thũku,** bibi**thũku,** ĩmĩ**thũku** na ũmũ**thũku**. Hali inayotokea ni kuwa wakati wa kuunda vivumishi, mizizi ya vitenzi huambishwa mwanzoni na mwishoni. Kwa mfano, mzizi -**thũk-** unaotokana na kitenzi **thũka** umeambishwa viambishi {**ja}, {ma}, {bi}, {ĩ}, {mĩ}, {ũ}** na **{mũ}**. Huu ni mfano wa mnyambuliko geuzi unaohusu kivumishi cha lahaja ya Kiimenti ambapo kitenzi kimenyambuliwa na kubadili kategoria yake na kuwa kivumishi. Jedwali lifuatalo linadhihirisha hali hii zaidi.

**Jedwali la 8: Mnyambuliko geuzi (Vivumishi kutokana na Vitenzi)**

| Kitenzi | Maana | Kategoria Mpya (Kivumishi) | |
|---|---|---|---|
| kũra | kua | gĩkũrũ [gekoro] | (kizee) |
| nunka | kunuka | jũmũnunku [ɟomonunku] | (unaonuka) |
| nora | nona | ũmũnoru [omonɔru] | (aliye mnono) |
| thũka | kuwa baya | gĩkĩthũku [gekeθoku] | (kibaya) |
| ng'enta | kali | ũmũng'entu[omoŋɛntu] | (aliye mkali) |
| thera | safi | ũmũtheru [omoθɛru] | (aliye safi) |
| gunda | fanya bivu | jamagundu [ɟamagundu] | (yaliyoiva) |
| ceng'a | kuwa konde | ũmũceng'u [omocɛŋu] | (aliye konda) |
| ũma | kuwa gumu | injũmo [injomɔ] | (zilizo gumu) |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali la 8 hapo juu imebainika kuwa kitenzi cha Kiimenti kinaweza kutumika kuunda kivumishi cha lahaja husika. Mchakato wa uundaji wa kivumishi cha Kiimenti unahusu mzizi wa kitenzi kuambishwa mwanzoni na kisha udondoshaji wa kiishio katika kitenzi kutokea. Udondoshaji unapotokea mwishoni mwa mzizi wa kitenzi irabu kama /u/ na /ɛ/ huchopekwa baada ya mzizi wa kitenzi.

Mfano mwingine wa mnyambuliko geuzi katika lahaja ya Kiimenti unahusu uambishaji wa vivumishi mwishoni na kuunda vitenzi. Hali hii inawasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 9: Mnyambuliko geuzi (Vitenzi kutokana na Vivumishi)**

| **Kivumishi** | **Maana** | **Kategoria Mpya (kitenzi)** |
|---|---|---|
| -nene | nenea [nɛnɛa] | kua |
| -irũ | irũa [iroa] | fanya eusi |
| -erũ | erũa [ɛroa] | fanya eupe |
| -kuĩ | kuĩa [kuea] | fanya fupi |
| -tune | tunea [tunɛa] | fanya ekundu |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Katika jedwali la 9 vivumishi vimetumika kuunda vitenzi vya lahaja ya Kiimenti. Ili kufanikisha uundaji huo irabu /a/ imechopekwa mwishoni mwa mzizi wa kivumishi na hivyo kuunda kategoria mpya ya maneno.

Vilevile, kuna uwezekano wa viambishi kutumika katika mchakato wa mnyambuliko geuzi ambapo nomino za Kiimenti huundwa kutokana na mizizi ya vivumishi vya lahaja husika. Jedwali la 10 linaonyesha mifano ya nomino zilizoundwa kutokana na mizizi ya vivumishi husika.

**Jedwali la 10: Mnyambuliko geuzi (Nomino kutokana na Vivumishi)**

| Kivumishi | Maana | Kategoria Mpya (nomino) |
|---|---|---|
| -thũku | ũthũku [oθoku] | ubaya |
| -nene | ũnene [onɛnɛ] | ukubwa |
| -irũ | wirũ [wiro] | weusi |
| -ega | wega [wɛga] | uzuri |
| -erũ | werũ [wɛro] | weupe |
| -ceke | ũceke [ocɛkɛ] | wembamba |
| -kuĩ | ũkuĩ [okue] | ufupi |
| -tune | ũtune [otunɛ] | wekundu |
| -nini | ũnini [onini] | udogo |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Mifano ya nomino za Kiimenti katika jedwali la 10 zilizoundwa kutokana na mizizi ya vivumishi vya lahaja husika huonyesha kuwa nyingi ni za dhahania. Nomino hizo zimeundwa kwa mzizi wa kivumishi kuambishwa mwanzoni. Baadhi ya viambishi vinapotangulia mzizi wa kivumishi ili kuunda nomino ni kama {ũ-} na {w-}.

Aidha, inawezekana vivumishi vya lahaja ya Kiimenti kufanyiwa mnyambuliko geuzi na vielezi vya lahaja hiyo kuundwa. Hali hii inawezekana kwa kuongezea mizizi ya vivumishi viambishi awali mbalimbali. Mfano wa hali hii unaweza kuwasilishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 11: Mnyambuliko Geuzi (Vielezi kutokana na Vivumishi)**

| Kivumishi | Maana | Viambishi Awali | Kategoria Mpya (Kielezi) |
|---|---|---|---|
| -thuku | -baya | bũ | bũthũkũ [βoθoku] |
| -nene | -nene | bũ | bũnene [βonɛnɛ] |
| -bui | -baya | bũ | bũbũi [βoβoi] |
| -ritu | -jinga | kĩ | kĩũritu [keoritu] |
| -kũrũ | -zee | gĩ | gĩkũrũ [kekoro] |
| -thongi | pendeza | bũ | bũthongi [βoθɔŋgi] |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Ni vizuri kufahamu kuwa vielezi vilivyoundwa katika jedwali la 11 havitofautiani kimuundo na vivumishi katika lahaja ya Kiimenti. Hata hivyo, katika muktadha wa matumizi ndipo unaweza kueleza kategoria ya neno lililotumika. Kwa mfano, **bũthũku** [βoθoku] (baya/vibaya) huweza kutumika kama kivumishi na kielezi. Hali hii inabainika katika mifano ya sentensi zifuatazo:

**Mũrĩmi akũrĩma bũthũku.**

[Moremi akorema βoθoku]

Mkulima amelima vibaya.

Sentensi iliyo hapo juu inaonyesha matumizi ya **bũthũku** [βoθoku] kama kielezi**.**

Kielezi hicho kinaeleza jinsi mkulima alivyolima.

**Ũntũ bũthũku bũkugwa mũcemanione.**

[Onto βoθoku βokugwa mocεmaniɔnε]

Jambo baya limesemwa mkutanoni.

Sentensi iliyo hapo juu inaonyesha matumizi ya **bũthũku** [βoθoku] kama kivumishi**.** Kivumishi hicho kinavumisha jambo ambalo lilisemwa kwenye mkutano.

Mpaka hapa ni wazi kuwa viambishi vya lahaja wa Kiimenti vina nafasi muhimu katika kutekeleza mnyambuliko sarufi na geuzi. Akizungumzia mnyambuliko wa maneno kwa ujumla Stump (1988) amejaribu kutofautisha mnyambuliko sarufi na geuzi. Anasisitisa kuwa katika mnyambuliko sarufi neno linalopatikana halibadilishi kategoria. Lakini katika mnyambuliko geuzi neno linaloundwa huwa ni la kategoria tofauti. Aidha, anasema kuwa mchakato wa mnyambuliko sarufi huwa na uzalishaji mwingi kuliko mynambuliko geuzi. Hii ina maana kuwa maneno mengi huweza kupatikana kutokana na mnyambuliko sarufi kuliko mnyambuliko geuzi. Hatimaye, neno linaloundwa kutokana na myambuliko sarufi haliwezi kuorodheshwa kwenye kamusi kama leksimu. Lakini katika mnymbuliko geuzi linaweza kuorodheshwa kwenye kamusi kama leksimu.

Vivumishi vinaweza kuunda virai nomino. Dhana inayodhihirika hapa ni kuwa vivumishi vilivyoundwa kutokana na mnyambuliko geuzi wa vitenzi vina uamilifu kama vivumishi vyovyote vya lugha zingine. Hii ndiyo sababu ya kutumia vivumishi vilivyoundwa kutokana na vitenzi ili kusisitiza kuwa ni vivumishi kulingana na jukumu linalotekelezwa la kufafanua majina. Inadhihirika kama inavyodaiwa kuwa kivumishi huja baada ya nomino inayovumishwa. Jedwali la 12 linaonyesha jinsi vivumishi vilivyoundwa kutokana na vitenzi vya Kiimenti hutumika kuunda virai nomino katika lahaja husika.

**Jedwali la 12: Matumizi ya Vivumishi katika Virai Nomino**

| KV | Sentensi | | Maana | |
|---|---|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| gĩkũrũ | kĩratũ gikũrũ | iratũ bibikũrũ | kiatu kizee | viatu vizee |
| ũmũnoru | muntũ ũmũnoru | antũ babanoru | mtu mnene | watu wanene |
| gĩkĩthũku | gĩtĩ gĩkĩthũku | itĩ bibithũku | kiti kibaya | viti vibaya |
| ũmũng'entu | muntũ ũmũng'entu | antũ babang'entũ | mtu mkali | watu wakali |
| ũmũtheru | mwarĩ ũmũtheru | aarĩ babatherũ | msichana safi | wasichana safi |
| jamagundu | ĩrigũ rĩrĩgundu | marigũ jamagundu | ndizi mbivu | ndizi mbivu |
| ũmũceng'u | muntũ ũmuceng'u | antũ babaceng'u | mtu mwembamba | watu wembamba |
| ũmũritu | muntũ ũmũritu | antũ babaritu | mtu mjinga | watu wajinga |
| injũmo | rũkũ rũrũmo | nkũũ injũmo | ukuni mgumu | kuni ngumu |
| inthatu | kũrũ inthatu | kũrũ inthatu | mbwa tasa | mbwa tasa |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Aidha, jedwali linaonyesha kuwa vivumishi huchukua viambishi awali ambavyo ni vipatanishi vya nomino inayovumishwa kulingana na ngeli. Kwa mfano, katika ngeli za 7 na 8 (GĨ /KĨ-I/BI) viambishi vya upatanisho ni{gĩ }na{kĩ }katika umoja na {i} katika wingi. Hivyo, nomino **kĩratũ** [kerato] (kiatu) na **iratũ** [irato] (viatu) katika umoja na wingi huvumishwa na vivumishi **gĩkũrũ** [gekoro] (kizee) na **bibikũrũ** [βiβikoro] (vizee). Mofu {gĩ} na {bi} husimamia wingi wa nomino katika vivumishi husika. Ni muhimu kuelewa kuwa kivumishi **bibikũrũ** (vizee) huweza kuandikwa kama **bikũrũ** [βikoro}

(vizee) na hivyo mofu {bi} kuachwa na kuwakilishwa na mofu kapa. Umbo kapa hapa huwakilisha mofimu ya idadi (umoja), jina na ngeli ya jina husika katika umoja. Yafaa ieleweke kuwa katika ngeli ya 7 (GĨ/KĨ) kuna alomofu mbili ambazo ni {gĩ} na {kĩ} katika umoja. Kwa hivyo, kuna uwezekano wa kupata majina katika ngeli hiyo yakitumia kiambishi awali {gĩ} au {kĩ}. Kwa mfano majina yafuatayo huweza kupatikana katika ngeli hiyo: **gĩtĩ** [gete] (kiti), **gĩkabũ** [gekaβo] (kikapu), **gĩkombe** [gekɔmbɛ] (kikombe), **kĩbanga** [keβaŋga] (panga), **kĩtheti** [keɵɛti] (kikapu), **kĩu** [keu] (tumbo), **kĩboko** [keβɔkɔ] (kiboko) na **kĩnii** [keni:] (ufizi).

Vielezi katika Virai Vitenzi

| | | |
|---|---|---|
| buthũku | akũrima buthũku | amelima vibaya |
| bũnene | akuga bũnene | amesema makubwa. |
| bũbũĩ | akwaria bũbũĩ | amezungumza vibaya |
| kiũritu | akũthoma kĩũritu | amesoma kijinga |
| kiũkũrũ | akwaria kiũkũrũ | amezungumza kizee |
| bũthongi | akũrima buthongi | amelima vizuri |

## 4.8 Aina ya Vivumishi vya Kiimenti

### 4.8.1 Vivumishi vya Sifa

Vivumishi vya sifa ni vivumishi ambavyo hutaja tabia au namna vitu vilivyo au vinavyoonekana (Kihore na Wenzie, wataje). Kwa kifupi vivumishi hivi hueleza jinsi mtu, mnyama, kitu au hali fulani ilivyo na inavyoonekana. Vivumishi hivi hueleza sifa ya nomino inayovumishwa. Hii ndiyo sababu vinaitwa vivumishi vya sifa. Lahaja ya Kiimenti huwa na vivumishi vya sifa vinavyozingatia miundo mbalimbali kimofolojia. Kwa mfano:

i) Vivumishi vinavyochukua mianzo ya konsonanti kama –**nene** [-nɛnɛ] (-nene), -**nini** [-nini] (-dogo), **-thũku** [-θoku] (-baya), **-kuĩ** [-kue] (-fupi), -**kũra** [kora] (-zee), **-thongi** [-θɔngi] (-pendeza), **-ceng'u** [-cɛŋu] (-konda), **-gundu** [-gundu] (-bivu), -**noru** (-nono) [-nɔru], **-tune** [-tunɛ] (-ekundu), **-ceke** [-cɛkɛ] (-embamba), **-thĩ** [-θe] (-bichi), **-ng'anu** [-ŋanu] (-tosha) na mizizi mingine. Vivumishi ambavyo huundwa kutokana na mizizi hiyo ni kama **binene** [βinɛnɛ] (vikubwa), **jũmũnini** [ɟomonini] (mdogo), **gĩkĩthũku** [gekeθoku] (kibaya), **ũmũkui** [omokui] (mfupi), **gikithongi** [gekeθɔngi] (kinachopendeza), **ũmũceng'u** [omocɛŋu] (aliyekonda), **rĩrĩgundu** [reregundu] (lililoiva), **ũmũnoru** [omonɔru] (mnono), **ĩntune** [entunɛ] (nyeupe), **gĩkĩceke** [gekecɛkɛ] chembamba), **ũmwĩthĩ** [omweθe] (mbichi) na **ũmũng'anu** [omoŋanu] (anayetosha).

ii) Vivumishi vinavyochukua mianzo ya irabu kama –**irũ** [-iro] (-eusi), **-erũ** [-ɛru] (-eupe), **ega** [-ɛga] (-zuri), **-oru** [-oru] (-oza). Baadhi ya vivumishi vinavyoundwa kutokana na mzizi hii ni kama **injirũ** [inɟiro] (nyeusi), **injerũ** [inɟɛro] (nyeupe), **gĩkĩega** [gekeɛga] (kizuri) na **bibioru** [βiβiɔru] (vilivyooza).

### 4.8.2 Vivumishi vya Idadi

Vivumishi vya idadi ni vile huonyesha jumla au hesabu ya vitu na huweza kugawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza huonyesha idadi kwa ujumla ilhali la pili huonyesha idadi kwa hesabu (Kihore na Wenzie, wataje). Muainisho sawa na huu ni ule wa Mgullu, (1999) ambaye anaeleza aina mbili za vivumishi vya idadi ambavyo anaviita idadi dhahiri na isiyo dhahiri. Vivumishi vya idadi dhahiri anasema kuwa kuna vile ambavyo huchukua viambishi awali vya nomino na visivyochukua viambishi hivyo. Vinavyochukua viambishi awali vya nomino katika Kiswahili ni namba 1-5 ilhali 6 -10 haziambishwi viambishi vya nomino. Hata hivyo, anaendelea kusema kuna uwezekano

namba 8 kuambishwa viambishi vya nomino. Anaendelea kufafanua idadi isiyo dhahiri kama vivumishi ambavyo hutaja kiasi kwa ujumla bila tarakimu au idadi mahsusi. Mifano ya mizizi ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri ni kama –chache, -o-ote, -ingine, kidogo na kiasi.

#### 4.8.2.1 Vivumishi vya idadi halisi

Hivi ni vivumishi ambavyo hutaja idadi kamili ya nomino. Mifano ya vivumishi hivi ni tarakimu mbalimbali kama **baĩrĩ** [baere] (wawili), **bathatũ** [βaθato](watatu)**, bana** [βana] (wanne)**, batano** [βatano] (watano)**, batantatũ** [βatantato] (sita)**, mũgwanja** [mogwanja] (saba)**, banana** [βanana] (wanane), **kenda** [kɛnda] (tisa au kenda), **ĩkumi** [ekumi] (kumi), **ĩgana [egana]** (mia moja), **ngiri ĩmwe** [ngiri emwɛ] (elfu moja)**, ngiri ithatũ** [ngiri iθato] (laki tatu), **ngiri inya** [ŋgiri iɲa] (laki nne) na **miriũni** [mirioni] (milioni). Ni vizuri kufahamu kuwa mzizi –**mwe** [-mwɛ] (-moja) hutumika kuonyesha idadi halisi katika hali ya wingi. Ukitumika kuvumisha nomino katika hali ya umoja maana inayojitokeza ni tofauti na idadi halisi kama ilivyoelezwa katika sehemu ya idadi ya jumla katika tasnifu hii. Kwa hivyo tunaweza kupata vivumishi vya idadi halisi vinavyoundwa kutoka na mzizi –**mwe** (-moja) katika umoja kama: **ũmwe** [omwɛ] (mmoja), **jũmwe** [ɟomwɛ] (mmoja), **rĩmwe** [remwɛ] (moja), **kĩmwe** [kemwɛ] (kimoja), **imwe** (moja) [imwɛ] na mifano mingine.

#### 4.8.2.2 Vivumishi vya idadi jumla

Lahaja ya Kiimenti huwa na vivumishi vya idadi jumla ambavyo huweza kuwasilisha dhana mbalimbali. Dhana hizi huwasilishwa kupitia mizizi ifuatayo:

Mzizi **-ingĩ** [-iŋge] (-ingi)

Hutumiwa kuvumisha nomino katika wingi kama mũtuu **jũmwingi** [motu: ɟomwiŋgi] (unga mwingi), **antũ babaingĩ** [anto βaβaiŋge] (watu wengi) **mĩtĩ ĩmingĩ** [miti emiŋge] (miti mingi). Mifano mingine ya vivumishi katika hali ya wingi ni kama **jamaĩngĩ** [ɟamaeŋge] (mengi), **bibingĩ** [βiβiŋge] (vingi), **tũtwingĩ** [totwiŋge] (vingi). Mzizi **–ingĩ** huambishwa viambishi awali ambavyo ni vipatanishi vya nomino na viambishi ngeli katika ngeli mbalimbali.

ii) Mzizi –**kai** [-kai] (-chache)

Mzizi huu huweza kutumiwa pamoja na majina kuwasilisha dhana ya uchache wa nomino zinazovumishwa. Kwa mfano, **antũ bakai** [anto βakai] (watu wachache), **mũtuu jũmũkai** [motu: ɟomokai] (kiasi kidogo cha unga).

**iii) Mzizi –mwe [-**mwɛ] (baadhi ya /sehemu ya)

Mzizi –mwe (baadhi ya/sehemu ya) hutumika kuonyesha sehemu fulani ya nomino katika wingi. Kwa hivyo unaweza kuvumisha majina katika hali ya wingi pekee. Dhana inayowasilishwa na mzizi huu ni ile ya baadhi ya au sehemu ya kitu fulani bila kuwa na uhakika wa idadi ya nomino zinazohusika. Kwa hivyo, mzizi huu hutumika kuvumisha majina katika ngeli ambazo huonyesha wingi pekee.

Sentensi ifuatayo inaweza kutumika kueleza dhana inayowasilishwa na mzizi **–mwe [-**mwɛ] (baadhi ya) katika ngeli ya 2 kuashiria wingi.

**Antu *bamwe* bati na nthoni.**

[Antu βamwɛ βati na nθɔni]

**Baadhi** ya watu hawana soni.

Mifano zaidi ya kuonyesha jinsi mzizi –**mwe** (baadhi ya/sehemu ya) hutumika kuonyesha idadi katika ngeli mbalimbali ni kama **ĩmwe** [emwɛ] (ngeli ya 3, 10 na 12), **jamwe** [ɟamwɛ] (ngeli ya 6 na 16), **bimwe** [βimwɛ] (ngeli ya 8), **bũmwe** [βomwɛ] (ngeli ya14), **tũmwe** [tomwɛ] (ngeli ya 18) na **kũmwe** [komwɛ] (ngeli ya 20).

**iv) Mzizi –thũmba** [-thũmba] (-ngi)

Mzizi **–thũmba** [-thũmba] (-ngi) hutumika kuonyesha dhana mbalimbali za idadi ya jumla katika wingi. Kutokana na mzizi huwo tunaweza kupata vivumishi vya idadi ya jumla kama **kathũmba** [kaθomβa] (kuonyesha wingi) na **kĩthũmba** [keθumβa] (kuonyesha wingi zaidi). Kutokana na vivumishi hivi tunaweza kuwa na virai nomino vinavyoonyesha dhana hizo.

| **Virai Nomino** | **Maana** |
|---|---|
| **antũ kathũmba** [anto kaθomβa] | watu wengi |
| **antũ kĩthũmba** [anto keθomβa] | watu wengi zaidi |
| **mĩtĩ kathũmba** [mete kaθomβa] | miti mingi |
| **mĩtĩ  kĩthũmba** [mete keθomβa] | miti mingi zaidi |
| **nguũ kathũmba** [ŋguo kaθomβa] | nguo nyingi |
| **nguũ  kĩthũmba** [ŋguo keθomβa] | nguo nyingi zaidi |

Kutokana na mifano ya vivumishi katika virai nomino hapo juu, ni wazi kuwa mzizi –**thumba** (-ngi) huambishwa mofu **{ka-}** au **{kĩ}** peke yake kuonyesha dhana mbalimbali za idadi. Uambishaji huo hautofautiani kutoka ngeli moja hadi nyingine. Hii ina maana kuwa vyote hutumika katika ngeli moja kuonyesha idadi isiyo kamili. Kwa mfano, majina kama **antũ, mĩtĩ** na **nguũ** ni ya ngeli za 2, 3 na 10 na yote hutumia viambishi **{ka-}** na **{kĩ-}** kuonyesha dhana mbalimbali za idadi.

### 4.8.3 Vivumishi Viulizi

Vivumishi viulizi ni vile huuliza maswali kuhusiana na nomino inayoandamana navyo (Kihore na Wenzie, mtaje). Katika lahaja ya Kiimenti mizizi ifuatayo hutumika kama vivumishi viulizi:

#### 4.8.3.1 Mzizi wa kiulizi -ng'ana (kiasi /-ngapi)

Mzizi **–ng'ana [-**ŋana] (-ngapi) unapotumika kuvumisha nomino mbalimbali hutoa dhana mbili. Unapotumika kuvumisha majina katika umoja huwa na dhana ya kiasi cha urefu au ukubwa wa nomino inayoangaziwa. Kwa mfano, katika sentensi:

**Ũrĩenda mũtĩ jũng'ana?**

[Orenda mote ɟoŋana]

(Unataka mti kiasi gani?)

Sentensi hiyo iko katika umoja na dhana ya mzizi **–ng'ana** ni kuonyesha urefu, ukubwa au hata wembamba wa mti unaotakikana au saizi yake. Mifano zaidi katika umoja ni kama **ũng'ana** [oŋana] katika ngeli ya 1, **jũng'ana** [ɟoŋana] katika ngeli ya 3, **kĩng'ana** [keŋana] katika ngeli ya 5, **ing'ana** [iŋana] katika ngeli ya 9, **rũng'ana** [roŋana] katika ngeli ya 11, **bũng'ana** [βoŋana] katika ngeli ya 13 na 15, **tũng'ana** [toŋana] katika ngeli ya 18 na kadhalika.

Mzizi huo unapotumika kuvumisha nomino katika hali ya wingi huashiria kiasi cha idadi cha nomino inayovumishwa au zinazovumishwa. Kwa mfano, katika sentensi:

**Ni mauku jang'ana ũkwenda?**

[Ni mauku ɟaŋana okwɛnda?]

(Unataka vitabu vingapi?)

Sentensi iliyo hapo juu inaashiria idadi ya jumla ya vitabu vinavyohitajika. Idadi kamili huweza kupatikana kupitia jibu la swali. Mzizi **–ng'ana** [-ŋana] hutanguliwa na viambishi awali vya upatanishi wa nomino katika ngeli mbalimbali. Kwa hivyo, matumizi yake hubadilika kutoka ngeli moja hadi nyingine kutegemea vipatanishi vya nomino katika ngeli hizo: kama **ing'ana [i**ŋana] **(**-ngapi) katika ngeli ya 3, **jang'ana** [ɟaŋana] (mangapi) katika ngeli ya 6 na 16, **bing'ana** [βiŋana] (vingapi) katika ngeli ya 8, **ing'ana** [iŋana] (ngapi) katika ngeli ya 10 na 12, **bũng'ana** [βoŋana] (kiasi gani) katika ngeli ya ngeli ya 14, **tũng'ana** [toŋana] (vingapi) ngeli ya 18 na **kũng'ana [k**oŋana] (kungapi) katika ngeli ya 20.

#### 4.8.3.2 Mzizi wa Kiulizi –rĩku (-ipi)

Mifano ya vivumishi vinavyoundwa kutokana na mzizi **–rĩku** (ipi) katika umoja na wingi ni kama, **ũrĩkũ** [oreku] (yupi), **jarĩkũ** [ɟareko] (yapi), **irĩkũ** [ireko] (ipi), **kĩrĩkũ** [kereko] (kipi), **birĩkũ** [βireko] (vipi), **irĩku** [ireko] (zipi) na kadhalika.

#### 4.8.3.3 Mzizi wa Kiulizi –au? (kina nani?)

Mzizi huu unapotumika humtambulisha mumiliki wa kitu au hali fulani. Tunaweza kukariri hali hii kwa kutumia sentensi zifuatazo:

**1) Ni ngari *yau* yathũka?**

[Ni ŋgari jau jaθoka?]

Ni gari la nani limeharibika?

2) **Ni into *biaũ* ũkwenda?**

[Ni into βiao okwɛnda?]

Ni vitu vya nani unataka?

3) **Ni mwana *waũ* ũkwenda?**

[Ni mwana wao okwɛnda?]

Ni mtoto wa nani unataka?

Sentensi hizi kwa kutumia vivumishi viulizi **yaũ** [jao] (nani), **biaũ** [βiao] (nani) na **waũ** [wao] (nani) huwa na nia ya kuwatambulisha watu fulani ambao wanamiliki vitu fulani. Kwa mfano, sentensi ya kwanza kwa kutumia **yaũ** [jao] (nani) ina nia ya kumtambulisha mwenye gari. Sentsnsi ya pili inatumia **biau** [βiao] ((nani) kwa nia ya kumtambulisha mumiliki wa vitu vinavyotakikana. Nayo ya tatu inatumia **waũ** [wao] (nani) kwa nia ya kutambulisha mwenye mtoto.

### 4.8.4 Vivumishi Vimilikishi

Katika lugha ya Kiswahili vivumishi vimilikishi huchukua viambishi awali ambavyo huwa tofauti na vile vya nomino inayovumishwa. Kwa mfano,” mti wangu”, “gari langu” na “nyumba yangu”. (Habwe & Karanja, wataje). Hata hivyo, hii ni kauli ya kijumla sana kwa sababu kuna vimilikishi ambavyo huchukua viambishi vya nomino kama katika virai nomino hivi:‘watoto wengi’, ‘watu wachache’, ‘viatu vyangu’ na kadhalika. Katika lahaja ya Kiimenti vimiliksh huchukua viambishi ambavyo ni vipatanishi vya ngeli ambapo nomino hupatikana. Vivumishi vimilikishi hueleza jinsi nomino inavyomilikiwa (Mgullu, 1999).

Katika lahaja ya Kiimenti mizizi ya vivumishi vimilikishi ni sita, ambapo kila nafsi huwa na mizizi miwili kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 13: Nafsi na Vivumishi Vimilikishi vya Kiimenti**

| | Kiimenti | | Kiswahili | |
|---|---|---|---|---|
| Nafsi | umoja | wingi | umoja | wingi |
| 1 | -akwa | -etũ | -angu | -etu |
| 2 | -aku | -enu | -ako | -enu |
| 3 | -awe | -ao | -ake | -ao |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

#### 4.8.4.1 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya Kwanza

Kama inavyodhihirika katika jedwali la 13 mizizi ya vivumishi vimilikishi vya nafsi ya kwanza katika lahaja ya Kiimenti ni miwili, ambayo ni **{-akwa}** {-angu} na **{-etũ}** {-etu} katika umoja na wingi. Mifano ya vivumishi hivi ni kama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **wakwa** [wakwa] (wangu) | **wetũ** [wɛto] (wetu) |
| **bakwa [**βakwa] (wangu) | **betũ** [βɛto] (wetu) |
| **jwakwa**[ɟwakwa] (wangu) | **jwetũ** [ɟwɛto] (wetu) |
| **yakwa** [jakwa] (yangu) | **yetũ** [jɛto] (yetu) |
| **rĩakwa**[reakwa] (langu) | **rĩetũ** [reɛto] (letu) |
| **jakwa**[jakwa] (yangu) | **jetũ** [ɟɛto] (yetu) |
| **gĩakwa**[geakwa] (changu) | **gĩetũ** [geɛtu] (chetu) |

**biakwa** [βiakwa] (vyangu) **bietũ** [βiɛto] (vyetu)

#### 4.8.4.2 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya pili

Mizizi ya vivumishi vimilikishi vya nafsi ya pili katika lahaja ya Kiimenti ni **{-aku}** {-enu} na {**-ako}** {-enu} katika umoja na wingi. Mifano ya vivumishi hivi ni kama ifuatayo:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| **waku** [waku] (wako) | **wenu** [wɛnu] (wenu) |
| **baku** [βaku] (wako) | **benu** [βɛnu] (wenu) |
| **jwaku** [ɟwaku] (wako) | **jwenu** [ɟwɛnu] (wenu) |
| **yaku** [jaku](yako) | **yenu** [jɛnu] (yenu) |
| **rĩaku** [reaku] (lako) | **rĩenu** [reɛnu] (lenu) |
| **jaku** [ɟaku] (yako) | **jenu** [ɟɛnu] (yenu) |
| **gĩaku** [geaku] (chako) | **kĩenu** [keɛnu] (vyenu) |
| **biaku** [βiaku] (vyako) | **bienu** [βiɛnu] (vyenu) |

#### 4.8.4.3 Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi ya Tatu

Vimilikishi vya nafsi ya tatu huwakilishwa na mzizi **{-awe}** {-ake} na **{-ao}** {-ao}katika umoja na wingi katika lahaja ya Kiimenti. Mifano ya vivumishi hivi ni kama ifuatayo:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| **wawe** [wawɛ] (wake) | **wao** [waɔ] (wao) |
| **bawe** [βawɛ] (wake) | **bao**[βaɔ] (wao) |
| **jwawe** [ɟwawɛ] (wake) | **jwao** [ɟwaɔ] (wao) |
| **yawe** [jawɛ] (yake) | **yao** [jaɔ] (yao) |
| **rĩawe** [reawɛ] (lake) | **rĩao** [reaɔ] (lao) |
| **jawe** [ɟawɛ] (yake) | **jao** [ɟaɔ] (yetu) |

**kĩawe** [keawɛ] (chake) **kĩao** [keaɔ] (vyau)

**biawe** [βiawɛ] (vyake) **biao** [βiaɔ] (yao)

### 4.8.5 Vivumishi vya Pekee

Vivumishi vya pekee katika lahaja ya Kiimenti huundwa kutokana na mizizi **–ngĩ** [-ŋge] (-ingine), **ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe), **-nka** [-nka] (pekee) na **–nthe** [-nθɛ] (-ote). Vivumishi hivi vinaitwa vivumishi vya pekee kwa sababu licha ya kuwa vivumishi vya majina, kila kivumishi kina matumizi mengine ya kipekee. Yaani huwasilisha dhana ya kipekee ambayo ni tofauti na kivumishi kingine cha pekee. Vilevile, upekee katika vivumishi hivi unatokana na hali ya jinsi vinavyoundwa. Isipokuwa vivumishi vya pekee vilivyoundwa kutokana na mzizi **–ngĩ** [-ŋge] (-ingine) ambavyo huzingatia ruwaza maalum, hivyo vingine huweza kuzingatia mpangilio maalum au kukosa kuuzingatia. Vivumishi vingi vya lahaja ya Kiimenti huundwa kipatanishi kinapoambishwa mzizi wa kivumishi. Katika baadhi ya vivumishi vya pekee tulivyoangazia mzizi unaambishwa viungo vilivyo tofauti na vipatanishi. Kwa hivyo, hudhihirisha muundo wenye upekee na usiozingatia mpangilio wa kutabirika. Hali hii itaeleweka zaidi baada ya kuangazia kila aina ya kivumishi kwa kina.

#### 4.8.5.1 Mzizi –ngĩ [-nge] (-ingine)

Katika lahaja ya Kiimenti mzizi **–ngĩ** [-ŋge] huwakilisha kivumishi cha pekee chenye dhana ya zaidi ya. Kwa mfano, **Muntũ ũngĩ akeja** [munto oŋge akɛɟa] (Mtu mwingine atakuja) huonyesha kuwa kuna watu fulani pahali lakini kuna mwingine ambaye atakuja. Yaani kuna nyongeza ya idadi iliyoko ambayo inatarajiwa kwa kufika kwa mtu mwingine.

#### 4.8.5.2 Mzizi –ene [-ɛnɛ] (-enye)

Mzizi huu hutoa dhana ya kumiliki kitu au hali fulani. Mzizi **–ene [-**ɛnɛ] (-enye) huonyesha muundo wa kipekee katika ngeli mbalimbali kama vivumishi vingine vya pekee. Mifano ya vivumishi hivi ni kama **mwene** [mwɛne] (mwenyewe), **ene** [ɛnɛ] (wenyewe), **jwene** [ɟwɛnɛ] (wa wenyewe), **yene** [jɛnɛ] (ya wenyewe), **rĩene** [reɛnɛ] (la wenyewe, **jene [**ɟɛnɛ] (ya wenyewe), **kĩene** [keɛnɛ] (cha wenyewe), **biene** [βiɛnɛ] (vya wenyewe) na **kwene** [kwɛnɛ] (kwa wenyewe).

#### 4.8.5.3 Mzizi –ngwa [-ŋgwa] (-enyewe)

Kivumishi **–ngwa** (-enyewe) hutumika kwa nia ya kusisitiza au kutilia mkazo nomino ambayo inavumishwa. Vivumishi kama **jungwa** [ɟuŋgwa] (wenyewe)**, na kungwa** [kuŋgwa] (kwenyewe) vinaundwa kwa vipatanishi vya nomino kuambishwa kwenye mzizi kama viambishi awali.

#### 4.8.5.4 Mzizi –nthe [-nθɛ] (-ote)

Mzizi **–nthe** (-ote) unapotumika kuvumisha nomino hutoa dhana ya kuhusika kwake kwa ujumla bila kubaki. Kwa mfano, tunaweza kusema, **Antũ bonthe bagwĩta.** [Anto βɔnθɛ βagweta] (Watu wote wameenda). Sentensi hii inatoa dhana ya kuwa ni watu wote ambao wameenda bila kubaki hata mmoja. Katika uundaji wa vivumishi vyenye mzizi **–nthe** [-nθɛ] (-ote), viambishi hutangulia mzizi husika. Vinapoundwa havizingatii mpangilio maalum, isipokuwa vichache kati ya vyote vinavyoundwa. Hivi ni kama **junthe** [ɟunθɛ] (wote)**, runthe** [runθɛ] (wote)**, bunthe** [βunθɛ] (wote) na **kunthe** [kunθɛ] (kwote).

#### 4.8.5.5 Mzizi -nka [-nka] (bila kuhusisha mtu/kitu/hali fulani)

Mzizi -**nka** hutumika katika Kiimenti kuonyesha dhana ya kutohusisha mtu. kitu au hali fulani. Kutokana na mzizi huo vivumishi kama **bonka** [βɔnka] (wao bila kuhusisha

wengine), **wenka** [wɛnka] (yeye bila kuhusisha mwingine) na **gĩonka** [geɔnka] (kitu fulani bila kuhusisha kingine). Ni vizuri kufahamu kuwa katika matumizi, vivumishi hivi huonyesha dhana ya upekee. Hata hivyo, isisahaulike kuwa katika muundo vinazingatia ule wa vivumishi vingine vya pekee. Vivumishi vyenye dhana ya upekee havipatikani katika lugha ya Kiswahili. Mizizi ya vivumishi vya pekee katika Kiswahili ni takriban mitano. Katika lahaja ya Kiimenti ni sita. Hii ina maana kuwa lugha za Kibantu huweza kutofautiana kimuundo katika masuala fulani.

### 4.8.6 Vivumishi Viradidi

#### 4.8.6.1 Viradidi Visisitizi

Mzizi **–ngwa** [-ŋgwa] umeelezwa tayari kama kivumishi cha pekee katika lahaja ya Kiimenti chenye dhana ya kusisitiza. Kwa mfano mzizi **–ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe) ukiambishwa mofu {**we}** unaunda kivumishi cha kusisitiza **wengwa** [wɛŋgwa] (mwenyewe). Hata hivyo, mofu {**we-}** ikiambishwa kama kiambishi awali kwenye kivumishi hicho, kivumishi cha kusisitiza **wewengwa** [wɛwɛngwa] (kusisitiza mwenyewe) kinapatikana. Kivumishi **wewengwa** [wɛwɛŋgwa] (kusisitiza mwenyewe zaidi) kimeundwa kupitia mchakato wa uradidi. Mchakato huu umeelezwa zaidi katika sehemu ya uradidi kwenye tasnifu hii. Mifano ifuatayo inabainisha jinsi vivumishi huweza kuunda vivumishi viradidi ambavyo hutoa dhana ya kusisitiza zaidi.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi cha baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| bongwa [βɔgŋwa] | > | bobongwa [βɔβɔŋgwa] (kusisitiza wenyewe zaidi) |
| jungwa [[ɟuŋgwa] | > | jujungwa [ɟuɟuŋgwa] (kusisitiza wenyewe zaidi) |
| yongwa [jɔŋgwa] | > | yoyongwa [jɔjɔŋgwa] (kusisitiza yenyewe zaidi) |
| rĩongwa [reɔŋgwa] | > | rĩorĩongwa [reɔreɔŋgwa] (kusisitiza lenyewe zaidi) |

jongwa [[ɟɔŋgwa] > jojongwa [[ɟɔɟɔŋgwa] (kusisitiza yenyewe zaidi)

kĩongwa [keɔŋgwa] > kĩokĩongwa [keɔkeɔŋgwa] (kusisitiza chenyewe zaidi)

#### 4.8.6.2 Viradidi Vilinganishi

Utafiti wetu ulidhihirisha kuwa lahaja ya Kiimenti huwa na vivumishi vya kulinganisha. Dhana kuu ya vivumishi hivi ni kulinganisha nomino mbili au zaidi kwa nia ya kuonyesha moja ni tofauti kidogo na nyingine au zingine. Kutokana na kivumishi **jũmũraja** [ɟomoraja] (mrefu) tunaweza kufanyia mzizi uradidi na kuunda kivumishi **jũmũrajaraja** [ɟomorajaraja] (mrefu zaidi). Dhana ya kulinganisha inayowasilishwa katika kivumishi hiki huweza kueleweka zaidi kwa kuchunguza sentensi ifuatayo.

**Murimi arienda muti jũmũrajaraja**.

[Murimi ariɛnda mute ɟomorajaraja]

(Mkulima anapenda mti mrefu zaidi).

Kivumishi **jũmũrajaraja** [ɟomorajaraja] (mrefu zaidi) kinaonyesha tayari kuna mti mrefu, lakini mkulima anataka ule mrefu zaidi kuliko ule uliyoko. Kwa hali hiyo, kuna hali ya kulinganisha kati ya miti iliyoko na ule mkulima anahitaji ambao ni mrefu zaidi. Mifano zaidi ya vivumishi vilinganishi vilivyoundwa kupitia urudufu imetolewa hapa nchini.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| ũmũkuĩ [omokue] | > | ũmũkuakuĩ [omokuakue**]** (mfupi zaidi) |
| jũmũraja [ɟomoraja] | > | jũmũrajaraja [ɟomorajaraja] (mrefu zaidi) |
| inthũku [inɵoku] | > | inthũkathũku [inθokaθoku] (mbaya zaidi) |
| bibiega[βiβiɛga] | > | bibiegaega [βiβiɛgaɛga] (vizuri zaidi) |
| gĩkirũ [gekiro] | > | gĩkirairũ [gekirairo] (cheusi zaidi) |

gĩkĩthũku [gekeɵoku] > geketh̃ukathũku [gekeθokaθoku] (kibaya zaidi)

#### 4.9.7 Vivumishi Vionyeshi

##### 4.9.7.1 Vivumishi Vionyeshi vya Karibu

Vivumishi vya karibu hutumika kuvumisha nomino ambayo iko karibu sana na mzungumzaji. Mifano ya vivumishi hivyo ni kama **ũjũ** [oɟo] (huyu), **iji** [iɟi] (hizi), **gĩkĩ** [geke] (hiki), **gũkũ** [goko] (huku), **baba** [βaβa] (hawa), **baa** [ba:] (hawa), **bibi** [βiβi] (hivi), **jaja** [ɟaɟa] (haya) na **jaa** [ɟa:] (haya).

##### 4.9.7.2 Vivumishi Vionyeshi vya Mbali kidogo

Mzizi wa kivumishi cha kuonyesha kuwa nomino inayovumishwa haiko mbali sana ni –u (h-). Mifano ya vivumishi vionyeshi vya mbali kidogo ni kama **ũu** [ou] (huyo), **biu** [βiu] (hivyo), **jau** [ɟau] (hayo), **kĩu** [keu] (hicho), **bau** [βau] (hao), **iu** [iu] (hizo) na **rĩu** [reu] (hilo).

##### 4.9.7.3 Vivumishi Vionyeshi vya mbali zaidi

Mzizi **–rĩa** [-rea] (-ile) hutumika katika lahaja ya Kiimenti kuvumisha nomino ambayo iko mbali sana. Nomino zinazovumishwa zinakuwa mbali na mzungumzaji hivi kwamba hawezi kuzishika kwa sababu ziko mbali naye. Badhi ya vivumishi vionyeshi vya mbali zaidi ni kama **ũrĩa** [orea] (yule), **barĩa** [βarea] (wale), **jũrĩa** [ɟorea] (ule), **irĩa** [irea] (ile), **kĩrĩa** [kerea] (kile), **birĩa** [βirea] (vile), **kũrĩa** [korea] (kule) na **jarĩa** [ɟarea] (yale).

#### 4.10 Vivumishi vya A - unganifu

Dhana kuu inayowasilishwa na vivumishi vya a – unganifu vinapovumisha nomino mbalimbali, ni ile ya kumilikiwa kwa mtu, kitu au hali fulani. Wakati wa kuvumisha nomino mbalimbali a – unganifu huweza kuunganisha aina mbalimbali za maneno. Kwa mfano:

### 4.10.1 Nomino, a –unganifu na nomino

A – unganifu huunganisha nomino mbili ambapo nomino ya kwanza au ya pili huonyesha umilikaji. Kwa mfano, tukisema **mwekũrũ wa rũritho** [mwɛkoro wa roriθɔ] (mwanamke wa wivu) inaonyesha kuwa mwanamke fulani ana wivu. Hapa nomino ya kwanza ndiyo inaonyesha hali ya umilikaji. Hata hivyo, katika mfano **ngarĩ ya baaba** [ŋgare ya βa:βa] (gari la baba) inaonyesha nomino ya pili (**baaba**) ndiyo inamiliki ile ya kwanza. Mifano mingine kama hii ni **iratũ bia mwana** [irato βia mwana] (viatu vya mtoto), **mbũri ya jũũjũ** [mbori ja ɟo:ɟo] (mbuzi wa nyanya), **nyomba ya mũthaka** [ɲɔmba ja moθaka] (nyumba ya mvulana) na **iuku rĩa mũritwa** [iuku rea moritwa] (kitabu cha mwanafunzi).

### 4.10.2 Nomino, a –unganifu na kitenzi

Vilevile, a –unganifu hutumika kuunganisha nomino na kitenzi kwa nia ya kufafanua nomino zaidi. Kwa mfano, tukisema **muntũ wa kũrĩma** [munto wa korema] (mtu wa kulima) tunaonyesha kuwa mtu tunayerejelea ana sifa ya kulima inayopatikana kwenye kitenzi. Mifano mingine kama hii ni, **mwarimũ wa kũritana** [mwarimo wa koritana] (mwalimu wa kufundisha), **ng'ombe ya kũrĩma** [ɲɔmba ya korema] (ng'ombe wa kulima), **mwekũrũ wa kũruga** [mwɛkoro wa koruga] (mwanamke wa kupika) na **kĩbanga kĩa gũtema** [keβaŋga kea gotɛma] (upanga wa kukata).

### 4.10.3 Nomino, a –unganifu na kielezi

A – unganifu huunganisha pia nomino na kielezi katika mfano kama huu, **ntukũ ya rũũjũ** [ntuko ya ro:ɟo] (siku ya kesho). Katika mfano huo, siku ni nomino na kesho ni kielezi.

### 4.11 Vivumishi vya Majina

Vivumishi vya majina ni majina (nomino) ambayo hufafanua mengine na hivyo kujulikana kama vivumishi vya majina. Hali hii hupatikana katika lahaja ya Kiimenti. Majina kama **muntũ** [munto] (mtu), **mwarimũ** [mwarimo] (mwalimu), **mũrũme** [moromɛ] (mwanamume) na **mũthao** [moθaɔ] (mvivu) yanaweza kuvumisha majina na kukawa na mifano kama hii: **muntũ mũka** [munto moka] (mtu mwanamke), **mũka mwarimũ** [moka mwarimo] (mwanamke mwalimu) **muntũ mũrũme** [munto moromɛ] (mtu mwanamume) na **mũka mũthao** na [moka moθaɔ] **(**mwanamke mvivu).

### 4.12 Vivumishi vya Mkopo

Vivumishi hivi vimeingia katika lahaja ya Kiimenti katika harakati za mawasiliano na wazungumzaji wa Kiimenti. Vivumishi vya mkopo vya Kiimenti vimetokana na lugha ya Kiswahili. Mifano ya vivumishi vya mkopo ni kama vile vya sifa kama **cawa** [cawa] (sawa) na **atarĩ** (hatari) [hatari]. Vingine ni vivumishi visisitizi kama **cawacawa** [cawacawa] (sawasawa). Pia kuna nomino za mkopo ambazo hutumika kama vivumishi katika Kiimenti. Mifano ni kama **kanga** [kanga] katika **athikarĩ kanga** [aθikare kanga] (askari kanga). Hatimaye, vivumishi vya idadi ambavyo vimekopwa hupatikana katika Kiimenti. Mifano ni kama **ijĩrĩ** [iɟere] (mbili), **ithatũ** [iθato] (tatu), **inya** [iɲa] (nne), **ithano** [iθanɔ] ((tano), **kenda** [kɛnda] (kenda/tisa), **ĩkũmi** [ekomi] (kumi), **ĩkũmi na ũmwe** [ekomi na omwɛ] (kumi na mmoja), **ĩkũmi na baĩrĩ** [ekomi na βaere] (kumi na wawili).

### 4.13 Sifa za Vivumishi vya Kiimenti

Vivumishi vya Kiimenti vinapotokea katika sentensi ndivyo hutanguliwa na nomino ambayo inavumishwa. Kwa mfano katika sentensi hii: *Mũkũrũ umũthũku akwĩja.*

[mokoro omoθoko akweja] (mzee mbaya amekuja), kivumishi **umũthũkũ** [omoθoko] (mbaya) kinatanguliwa na nomino **mũkũrũ** [mokoro] (mzee). Hata hivyo, katika lugha ya Kiingereza kivumishi hutangulia nomino (Philipo na Kuyenga, wataje).

Sifa nyingine ya vivumishi ni kuwa vinaweza kufuatana ili kuvumisha nomino moja. Kauli hii inatiliwa mkazo na Philipo na Kuyenga (wataje). Hii ina maana kuwa kuna uwezekano wa kupata mkururo wa vivumishi vya Kiimenti vikifafanua nomino moja. Mifano ya vivumishi hivyo inapatikana katika sehemu ya ruwaza za vivumishi katika tasnifu hii.

Aidha, sifa nyingine ni kuwa katika vivumishi vya Kiimenti viambishi awali vya ngeli, nomino au vipatanishi vyake hudhihirika katika vivumishi hivyo ili kukamilisha muundo wake. Kwa hivyo, nomino ina mchango mkubwa sana katika muundo wa vivumishi hivyo. Hii ni kwa sababu ndiyo huchangia viambishi awali katika ngeli za mofolojia na sintaksia ambazo ni muhimu katika muundo wa vivumishi ili kuhakikisha kuna upatanishi katika nomino, kivumishi na kategoria zingine za maneno katika sentensi. Ni vizuri kufahamu kuwa si vivumishi vyote vya Kiimenti ambavyo huchukua viambishi ngeli viwili kama viambishi awali. Vingine huchukua kipatanishi pekee kama kiambishi awali. Hali hii imeangaziwa zaidi katika sehemu ya muundo wa vivumishi katika tasnifu hii. Jinsi nomino hudhibiti viambishi awali vya vivumishi huweza kubainika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 14: Jinsi Nomino Hudhibiti Viambishi Awali vya Vivumishi**

| Ngeli | Nomino | kipatanishi | kivumishi |
|---|---|---|---|
| 1. MU/MW/MŨ | muntũ (mtu) | **ũ -** | **ũ**mũraja/ũ -mũ-raja/ (mrefu) |
| 2. A | antũ (watu) | **ba-** | **baba**raja/ba-ba-raja/ (warefu) |
| 3. MŨ | mutĩ (mti) | **jũ -** | **jũ**mũraja/jũ -mũ -raja/ (mrefu) |
| 4. Ĩ | mĩtĩ (miti) | **ĩ -** | **ĩ**mĩraja/ĩ -mĩ-raja/ (mirefu) |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Katika jedwali la 14 mifano imetolewa ya nomino katika ngeli mbalimbali za kimofolojia. Aidha, vipatanishi vya nomino hizo na vivumishi vinavyozivumisha umetolewa. Kwa mfano, katika ngeli ya 1 (MU/MW/MŨ) nomino **muntũ** [munto] (mtu) ina kipatanishi {**ũ-**} ambacho kinapatikana kama kiambishi awali katika kivumishi **ũ**mũraja/ũ -mũ-raja/ (mrefu) kikiwakilisha nomino husika. Hali hii ndio inaonyesha jinsi nomino mbalimbali huathiri muundo wa vivumishi vya Kiimenti.

**4.14 Uamilifu wa Vivumishi vya Lahaja ya Kiimenti**

i) Vivumishi huwasilisha maana. Kwa mfano mizizi huru huwasilisha maana kamili na tegemezi huambishwa ili kuwasilisha maana. Mfano wa mizizi huru ni kama **kenda** [kɛnda] (tisa) **mũgwana** [mogwanɟa] (saba), **mwanyamwanya** [mwaɲamwaɲa] (tofautitofauti), **tafautitafauti** [tɔfautitɔfauti] (tofautitofauti) na **cawacawa** [cawacawa] (sawasawa). Hii ni mizizi huru ambayo ni sawa na leksia inayowasilisha maana kamili.

Mizizi hii ikitenganishwa maana inayowasilishwa itaathirika. Vilevile, mizizi tegemezi ya vivumishi vya Kiimenti ikiambishwa mofu mbalimbali huweza kuwasilisha maana katika lahaja hii. Kwa mfano, mizizi kama **–ega** [-ɛga] (-zuri), **-thukũ** [-θoku] (-baya) na **–thatũ** [-θato] (tatu) inaweza kuambishwa mwanzoni na kuunda vivumishi vyenye maana kama **ũmwega** [omwɛga] /u-mw-ega/ (mzuri), **babathũku** [βaβaθoku] /ba-ba-thuku (wabaya) na **ithatũ** [iθato] /**i-thatu**/ (tatu)**.** Maana mbalimbali huibuliwa na aina mbalimbali za vivumishi vya Kiimenti vinapotumika. Kwa mfano maana ya hali ya uhusiano au umilikaji hubainika vivumishi vya kumiliki na vile vya a-unganifu vinapotumika. Kwa hivyo, vivumishi vimilikishi vinavyoundwa kutokana na mizizi kama **–akwa** [-akwa] (-angu), **-etũ** [-ɛto] (-etu), **-aku** [-aku] (-ako), **-enu** [-ɛnu] (-enu) huonyesha umilikaji wa nomino ambayo inatangulia vivumishi hivi. Vilevile, mofu {a} hutumika pamoja na vipatanishi vya nomino kutoa dhana ya umilikaji katika ngeli mbalimbali.

ii) Hufafanua nomino kwa nia ya kueleza sifa zake au idadi yake. Kwa mfano, **antũ bathatũ** [anto βaθatu] (watu watatu) na **ngari inyingĩ** [ŋgari iɲinge] (magari mengi); **antũ bathatu** [anto βaθatu] (watatu) na **inyingĩ** [iɲinge] (nyingi) ni vivumishi vya idadi ambavyo vinaeleza idadi ya nomino zilizotajwa. Aidha, vivumishi **ũmũnene** [omonɛnɛ] (mkubwa) na **ũmũraja** [omoraɟa] (mrefu) katika virai vivumishi **muntũ ũmũnene** [muntu omonɛnɛ] na **muntũ ũmũraja** [munto omoraɟa] (mtu mrefu) huonyesha sifa ya ukubwa na urefu wa mtu anayerejelewa katika nomino. Hata nomino hutumika kama vivumishi kufafanua nomino nyingine. Kwa mfano, **mũka mwarimũ** [moka mwarimo] (mwanamke mwalimu), **muntũ mũrogi** [munto morɔgi] (mtu mrogi/mchawi) na **mũkũrũ mũrĩmi** [mokoro moremi] (mzee mkulima). Nomino **mwarimũ [mwarimo]**

(mwalimu), **mũrogi [**morɔgi] (mrogi/mchawi) na **mũrimi** [moremi] (mkulima) zina utendakazi wa kuvumisha nomino zingine. Kwa hivyo, zina uamilifu wa vivumishi katika muktadha huo.

Licha ya vivumishi kueleza sifa za nomino, hupiga hatua hata kulinganisha sifa hizo. Kwa mfano, **ũmũkũrakũrũ** [omokorakoro] (mzee zaidi), **ũmwegaega** [omwɛgaɛga] (mzuri zaidi), **inthũkathũku** [inθokaθoku] (mbaya zaidi) na **injegaega** [inɟɛgaɟɛga] (nzuri zaidi) hutumika kulinganisha hali ya **ũkũrũ** [okoro] (uzee), **wega** [wɛga] (uzuri), na **ũthũku** [oθoku] (ubaya). Hali ya vivumishi kuwa na sifa ya kulinganisha inaangaziwa zaidi na Dixon na Aikhenvald (2005). Katika lugha ya Kiingereza vivumishi huongezwa mofu <-*er*> na <-*est*> ili kuonyesha ulinganisho. Hivyo, kutokana na kivumishi *big* tunaweza kuunda vivumishi *bigger* na *biggest* (Philipo na Kuyenga, wataje)

iii) Vivumishi hutumika kama vijenzi vya virai vivumishi katika lahaja ya Kiimenti. Kuna miundo mbalimbali ya virai vivumishi katika lahaja hiyo. Miundo mbalimbali ya virai vivumishi vilivyoundwa ni kama:

a) Kirai kivumishi cha kivumishi kimoja kama **ũmũraja** [omoraɟa] (mrefu), **ũmũkũru** [omokoro] (mzee), **ũmũkuĩ** [omokue] (mfupi).

b) Kirai kivumishi chenye muundo wa kivumishi na kielezi. Kwa mfano, **ũmũkũru cana** [omokoro cana] (mzee sana) na **ũmũkuĩ mono** [omokue mɔnɔ] (mfupi sana).

c) Kirai kivumishi chenye mkururo wa vivumishi viwili. Kwa mfano **baĩrĩ babega [**βaere βaβɛga] (wawili wazuri).

d) Kirai kivumishi chenye mfuatano wa kivumishi, kivumishi na kielezi. Kwa mfano, **bathatũ babathũku mono** [βaθato βaβaθoku mɔnɔ] (watatu wabaya mno).

iv) Hubeba mofu zenye usarufi kama umoja, wingi, ngeli za sintaksia, ngeli za mofolojia, udogo, ukubwa na kadhalika. Baadhi ya usarufi huu unaweza kueleweka kwa kuchunguza vivumishi katika sentensi hizi.

**Mũti jũmũnene jũgũtemwa.** [mote ɟomonɛnɛ ɟogomtɛmwa] (Mti mkubwa umekatwa). - umoja

**Mĩtĩ ĩmĩnene ĩgũtemwa**. [mete emenɛnɛ egotɛmwa] (Miti mikubwa imekatwa) - wingi.

Vivumishi katika sentensi hizi ni **jũmũnene** [ɟomonɛnɛ] (mkubwa) na **ĩmĩnene** [emenɛnɛ] (mikubwa). Vivumishi hivi vikichanganuliwa vitadhihirisha mofimu mbalimbali. Kwa mfano,

**jũmũnene** [ɟomonɛnɛ] **/jũ-mũ-nene/** (mkubwa)

**{jũ }** mofu ya idadi (umoja)

Kipatanishi cha nomino

Kiwakilishi cha ngeli ya sintaksia ya 3 (JU) katika umoja

**{mũ}** Kiambishi awali cha nomino inayovumishwa

Kiambishi cha ngeli ya kimofolojia ya 3 (MU) – umoja.

**ĩmĩnene**[emenɛnɛ]**/ĩ-mĩ-nene/** (mikubwa)

**{ĩ}** mofu ya idadi (umoja)

Kipatanishi cha nomino

Kiwakilishi cha ngeli ya sintaksia 4 (Ĩ) (wingi)

**{mĩ}** Kiambishi awali cha nomino inayovumishwa

Kiambishi cha ngeli ya kimofolojia ya 3(MĨ) – wingi.

Aidha, udogo na ukubwa huweza kueleweka kwa kuangazia sentensi zifuatazo:

**Kamũtĩ kamwe kagũtemwa** [kamote kamwɛ kagotɛmwa]. (Kijiti kimoja kimekatwa.)

**Kimũtĩ kĩmwe kĩgũtemwa**. [kemote kemwɛ kegotɛmwa] (Jiti moja limekatwa.}

Mifano hii inaonyesha kuwa vivumishi ni **kamwe** [kamwɛ**]** (udogo) na **kĩmwe** [kemwɛ**]** (ukubwa) ambavyo vikichanganuliwa vinakuwa **kamwe** /ka-mwe/ (kamoja) na **kĩmwe**/kĩ-mwe/. Katika vivumishi hivi mofu {ka} ni ya udogo na mofu {kĩ} ni ya ukubwa. Hata hivyo, mofu hizi zina usarufi mwingine kama wa idadi na ngeli.

v) Kivumishi huchangia usarufi katika sentensi. Kinaweza kukosekana katika sentensi na ikawa sahihi huku ikawasilisha maana kamili. Hata hivyo, sentensi kama, **Mwana ũmwega mono akwĩja.** [mwana omwɛga mɔnɔ akweja] (Mtoto mzuri sana amekuja) itakosa usarufi ikiwa kivumishi **ũmwega** [omwɛga] (mzuri) kitaondolewa. Kwa hivyo, kivumishi na aina nyingine za maneno ni kijenzi muhimu cha sentensi (Mbaabu, mtaje).

vi) Vivumishi huwa na uamilifu wa kusisitiza zaidi katika tungo mbalimbali. Kwa mfano **ũrĩaũrĩa** [oreaorea] (yuleyule), **bobongwa/bongwabongwa** [βɔβɔŋgwa/βɔŋgwaβɔŋgwa] (wenyewewenyewe**),** **wewengwa/wengwawengwa** [wɛwɛngwa/wɛngwawɛngwa] (mwenyewemwenyewe). Aidha, vivumishi viwili vikitumika pamoja katika sentensi, kile cha pili husisitiza kile cha kwanza. Hali kama hii inabainika katika vivumishi vya Kiimenti.

vi) Hutumika kama kijenzi cha virai nomino. Virai nomino vina miundo mbalimbali. Hata hivyo, kunawezekana kuwa na muundo wa nomino na kivumishi. Kwa mfano, **ngũgĩ inthongi** [ngoge inθɔŋgi] (kazi nzuri).

vii) Vivumishi vya Kiimenti huweza kutumika kama msingi wa mnyambuliko sarufi. Hii ina maana kuwa vivumishi vya Kiimenti hunyambuliwa na kuunda maneno ya kategoria hiyo. Kwa mfano, mizizi –**thũku [-**θoku] na **–ega** [-ɛga] ikiambishwa mwanzoni huunda vivumishi vingine. Kwa mfano,

| **{-thukũ} (-baya)** | **{-ega} (-zuri)** |
|---|---|
| ũmũthũku [omoθoku] /ũ -mũ-thũ ku/ (mbaya) | ũmwega[umwɛga]/u-mw-ega/ (mzuri) |
| gĩkĩthũku [gekeθoku] /gĩ-kĩ -thũku/ (kibaya) | gĩkĩega [gekeɛga] /gĩ-kĩ-ega/ (kizuri) |
| bibithũku [βiβiθoku] /bi-bi-thuku/ (vibaya) | bibiega [βiβiɛga]/bi-bi-ega/ (vizuri) |
| babathũku [βaβaθoku] /ba-ba-thuku/ (wabaya) | babega [βaβɛga]/ba-be-ega/(wazuri) |

viii) Vivumishi vya Kiimenti huweza kutumika kufanikisha mnyambuliko geuzi. Hii inaashiria kuwa vinaweza kutumika kuunda kategoria nyingine za maneno kama nomino dhahania.

| **Mzizi wa Kivumishi** | **Nomino Dhanania Inayoundwa** |
|---|---|
| **-thũku** (-baya) [-θoku] | **ũthũku** [oθoku] (ubaya) |
| **-ega** [-ɛga] (-zuri) | **wega** [wɛga] (uzuri) |
| **-nene** [-nɛnɛ] (-kubwa) | **ũnene** [onɛnɛ] (ukubwa) |

ix) Vivumishi hushirikiana na maneno mengine katika sentensi ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Hii ina maana kuwa sawa na maneno kama ya vitenzi, vivumishi hudhibitiwa na nomino kwa viambishi vya nomino kuambishwa mzizi wa kivumishi ili kuhakikisha kuna upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kwa mfano: *Ngari ĩnthongi ĩkũgũrwa narua*. *[ngarĩ ĩnθɔngi ekogorwa narua*] (Gari zuri limenunuliwa leo). Kivumishi **ĩnthongi** [inθɔŋgi] (nzuri) kinaambishwa kipatanishi cha nomino ili kuleta upatanishi unaofaa katika sentensi hiyo.

x) Vivumishi hufanya kazi ya kijalizo katika sentensi (Habwe na Karanja, wataje). Kwa mfano, **muntũ ũrĩa i mwarimũ**. [munto orea i mwarimo] (Mtu yule ni mwalimu). **Mwarimũ** [mwarimo] (mwalimu) ni kivumishi kinachofanya kazi ya kijalizo.

## 4.15 Ngeli za Mofolojia za Lahaja ya Kiimenti

Kwa mujibu wa Mukuthuria (2004) ngeli ni mpangilio wa maneno ya nomino katika makundi. Anaendelea kusema kuwa lugha za Kibantu zina mtindo wa kuainisha makundi ya nomino kwa kutumia ngeli. Kulingana na Kapinga (1983) ngeli ni makundi ya majina ambayo yana mabadiliko ya aina moja ya viambishi vya umoja na wingi. Anazidi kudai kuwa viambishi hivi huleta upatanisho wa kisarufi wa namna moja katika fungutenzi, vivumishi na kwa viwakilishi. Kwa maoni yake hali ya kuambisha nomino mbalimbali mwanzoni ni njia moja ya kuainisha ngeli. Mwanasarufi huyu anakiri kuwa idadi ya ngeli katika lugha za Kibantu na jinsi ya kuzihesabu huhitilafiana. Kundi la ngeli za kimofolojia ambalo lina nomino zenye viambishi awali vya umoja na wingi huonekana kukamilika zaidi kuliko makundi mengine ya ngeli (Mgullu, 1999). Utaratibu huu ndio ulizingatiwa katika kuainisha ngeli za Kimeru.

Suala la sarufi halikamiliki katika lugha za Kibantu bila kuangazia ngeli za lugha husika (Mukuria, 1987). Kwa hivyo, ni vizuri kuangazia ngeli za kimofolojia za Kiimenti kwa sababu utafiti huu ulihusu mofolojia kwa hali moja licha ya kuangalia hata kipengele cha sintaksia. Aidha, Wa Mberia (1993) anaeleza kuwa muundo wa kivumishi hutegemea ngeli. Kwa hivyo, ngeli za Kiimenti zilikuwa na umuhimu katika kuchanganua miundo mbalimbali ya vivumishi. Ngeli hizi zimeundwa kwa kutumia nomino mbalimbali. Nomino hufafanuliwa na vivumishi mbalimbali. Kwa hivyo ilifaa kuangalia ngeli za kimofolojia za Kiimenti na vipatanishi vya nomino katika ngeli hizo. Hii ni kwa sababu vipatanishi vya nomino vina utendakazi katika kuchunguza miundo mbalimbali ya vivumishi vya Kiimenti. Vilevile, viambishi vinavyotambulisha makundi ya ngeli vinachangia muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, katika ngeli ya MŨ/MW

na MĨ (ngeli ya 3 na 4), si rahisi kuzungumzia muundo wa vivumishi vya Kiimenti bila kurejelea vipatanishi vya nomino husika. Hii inapelekea hali ya kuweko kwa vipatanishi kwa kila ngeli ya kimofolojia ya Kiimenti. Kwa hivyo, nomino katika kundi moja la ngeli huweza kuwa na vipatanishi vya aina moja katika umoja au wingi. Kwa hivyo, ilikuwa muhimu kuchunguza ngeli za kimofolojia za Kiimenti.

Ngeli za nomino zilituelekeza kuchunguza vipatanishi vya nomino katika ngeli ambavyo vina uamilifu katika uundaji wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa hivyo, makundi haya ya maneno na vipatanishi ni muhimu. Hatuwezi kuwa na vipatanishi bila kuangazia nomino zinazounda makundi mbalimbali ya nomino yanayoitwa ngeli. Jedwali lifuatalo linatufaa zaidi kuelewa ngeli za kimofolojia za Kiimenti na vipatanishi vya nomino mbalimbali za lahaja hiyo katika kila ngeli. Jedwali hilo limeainisha ngeli ishirini na mbili za Kiimenti. Muainisho kama huu ndio hutumika wanasarufi wanapotumia kigezo cha kimofolojia kuainisha ngeli (Simiyu na Buregeya, 2010). Hii ina maana kuwa ngeli ya MU/MŨ/MW/ø na A hutazamwa kama ngeli ya kwanza na pili katika lahaja ya Kiimenti bali si ngeli moja. Nomino katika makundi haya huathiri vipatanishi vinavyopatikana katika maneno mengine kama vitenzi. Ili kuonyesha umuhimu wa ngeli katika muundo wa vivumishi viashiria vya Kiswahili, Mbaabu (mtaje) anasema kuwa vinategemea ngeli za nomino. Hali kama hiyo inabainika katika Kiimenti.

**Jedwali la 15: Ngeli Mbalimbali za Kiimenti**

| | Ngeli | Kipatanishi | Nomino | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MU/MW/MŨ | a [a] | mũkũrũ [mokoro] | mzee |
| 2 | A | ba [βa] | akũrũ [akoro] | wazee |
| 3 | MŨ/MW | jũ [ɟo] | mutĩ [mote] mwari [mwari] | mti, mlango |
| 4 | MĨ | ĩ [e] | mĩtĩ [mete], mĩari [meari] | Miti, milango |
| 5 | Ĩ/I/RĨ | rĩ [re] | ĩgo [egɔ] | jino |
| 6 | MA | ja [ɟa] | maigo [maĩgɔ] | meno |
| 7 | KĨ/GĨ | gĩ /kĩ [ge/ke] | kĩratũ [kerato], gĩtĩ [gete] | kiatu, kiti |
| 8 | I/bi | i/bi [i/βi] | iratũ [erato], itĩ [ite] | viatu, viti |
| 9 | N | ĩ [e] | nyomba [ɲɔmba] | nyumba |
| 10 | N | i [i] | nyomba [ɲɔmba] | nyumba |
| 11 | RŨ | rũ [ro] | rũthingo [ruθiŋgɔ] | ukuta |
| 12 | N | i [i] | nthingo[ nθiŋgɔ] | kuta |
| 13 | Ũ | bũ [βo] | ucinka [ocinka] | ujinga |
| 14 | Ũ | bũ [βo] | ucinka [ocinka] | ujinga |
| 15 | Ũ | bũ [βo] | ũntũ [onto] | jambo |
| 16 | MA | ja [ɟo] | mantũ [manto] | mambo |
| 17 | KA/GA | ga [ga] | kaana [ka:na] | kijitoto |
| 18 | TW/TŨ | tũ [to] | twaana, [twa:na] | vijitoto |
| 19 | KŨ | gũ [ko] | kurĩma [korema] | kulima |
| 20 | KŨ | gũ [ko] | kurĩma [korema] | kulima |
| 21 | A | a [a] | antũ [anto] | pahali |
| 22 | GŨ | gũ [go] | guntũ [gonto] | mahali |

Asili: Mukuthuria (2004) (Limelifanyia mabadiliko)

**1. MU-/ MŨ- /MW- 2. A-**

Ngeli hizi huwa na majina ambayo huanza kwa mofu MU/ MŨ /MW katika umoja na A katika wingi. Nomino katika ngeli hizi ambazo zina mizizi inayoanza kwa konsonanti huwekwa kiambishi awali MU au MŨ. Kiambishi awali MW nacho huambishwa mizizi

ya nomino inayoanza kwa irabu kama kiambishi awali. Baadhi ya majina yanayopatikana katika ngeli hizi ni:

i) majina ya binadamu

| **Umoja** | **Wingi** | **Maana (Umoja)** | **Maana (Wingi)** |
|---|---|---|---|
| muntũ [munto] | antũ [anto] | mtu | watu |
| mũritwa [moritwa] | aritwa [aritwa] | mwanafunzi | wanafunzi |
| mũgambi [mogambi] | agambi [agambi] | mtetezi | watetezi |
| mwarimũ [mwarimo] | arimũ [arimo] | mwalimu | walimu |
| mwamba [mwamba] | amba [amba] | mwizi | wezi |
| batĩrĩ [βatere] | abatĩrĩ [aβatere] | padri | padri |

Majina mengine yanayopatikana katika ngeli hizi ni ya makabila mbalimbali kama:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mũmerũ [momɛro] | wamerũ [wamɛro] |
| Mũjaruũ [moɟaruo] | wajaruũ [waɟaruo] |
| Mũkĩkũyũ [mokekojo] | wakekoyo [wakikuju] |
| Mũchuka [moʧuka] | wachuka[waʧuka] |
| Mũembu [moɛmbu] | waembu [waɛmbu] |
| Mũĩgoji [moegɔɟi] | waĩgoji [waegɔɟi] |

**3.MU- 4.MĨ -**

Majina katika ngeli hizi huambishwa kiambishi **mu** kwenye mzizi katika umoja na **mi** katika wingi. Baadhi ya majina katika ngeli hii ni yale ya:

i) sehemu za mwili wa binadamu na wanyama kama:

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| mũthumo [moθumɔ] | (mguu) | mĩthumo[meθumɔ] (miguu) |
| mũtwe [motwɛ] | (kichwa) | mĩtwe [metwɛ] (vichwa) |
| mũkou [mokɔu] | (kitovu) | mĩkou [mekɔu] (vitovu) |
| mũtundu [motundu] | (nywele) | mĩtundu [metundu] (nywele) |
| mũnyiritha [moɲiriθa] | (mgwisho) | mĩnyiritha[meɲiriθa] (migwisho) |
| mũkĩa [mokia] | (mkia) | mĩkia [mekia] (mikia) |
| mũgongo [mogɔŋgɔ] (mgongo) | | mĩgongo [megɔŋgɔ] (migongo) |

ii) majina ya miti na mimea

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mũtĩ [mote] (mti) | mĩtĩ [mete] (miti) |
| mũpera [mopɛra] (mpera) | mĩpera [mepɛra] (mipera) |
| mũtunda [motunda] (mtunda) | mĩtunda [metunda] (mitunda) |

Majina ya miti ambayo hayajatafsiriwa kutoka Kiimenti hadi Kiswahili hayana majina ya Kiswahili.

iii) majina ya vifaa/vitu mbalimbali

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mũcibi [mociβi] (mshipii) | mĩcibi [meciβi] (mishipi) |
| mũgate [mogatɛ] (mkate) | mĩgate[megatɛ] (mikate) |
| mũkebe [mokɛβɛ] (mkebe) | mĩkebe [mekɛβɛ] (mikebe) |

**5. I/Ĩ- /RI-                    6. MA-**

Nomino katika makundi haya huambishwa viambishi **ĩ, i** na **ri** kwenye mzizi katika umoja, na kiambishi **ma** katika mzizi katika hali ya wingi. Baadhi ya majina katika ngeli hizi ni:

i) majina ya vifaa/vitu mbalimbali

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| riko [rikɔ] (jiko) | mariko [marikɔ] (meko) |
| ĩthandũkũ [eθandoko] (sanduku) | mathandũkũ [maθandoko] (masanduku) |
| ĩtangi [etaŋgi] (jiko) | matangi [mataŋgi] (matangi) |
| iuku [iuku] (kitabu) | mauku [mauku] (vitabu) |
| iga [iga] (jiwe) | maiga [maiga] (mawe) |

ii) sehemu za mwili

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| ĩgo [egɔ] (jino) | maĩgo [maegɔ] (meno) |
| ritho [riθɔ] (jicho) | metho [mɛθɔ] (macho) |
| ĩtina [etina] (kalio) | matina [matina] (makalio) |

iii) majina ya mkopo

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| cukuru [cukuru] | macukuru [macukuru] (mashule) |
| cibitari [ciβitari] | macibitari[maciβitari] (mahospitali) |

**7. KĨ-/GĨ-`     8. I- /BI-**

Majina katika ngeli hizi huanza kwa viambishi **kĩ** au **gĩ** katika hali ya umoja, na katika wingi huanza kwa viambishi **i** au **bi**. Baadhi ya majina katika ngeli hizi ni:

i) majina ya sehemu za mwili

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| kĩbara [keβara] (kifua) | ibara [iβara] (vifua) |
| kĩu [keu] (tumbo) | iu [iu] (matumbo) |

ii) majina ya vitu/ vifaa

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| kĩratũ [kerato] (kiatu) | iratũ [irato] (viatu) |
| kĩbanga [keβaŋga] (panga) | ibanga [iβaŋga] (mapanga) |
| kĩbati [keβati] (bati) | ibati [iβati] (mabati) |
| gĩkombe [gekɔmbɛ] (kikombe) | ikombe [ikɔmbɛ] (vikombe) |
| gĩkabũ [gekaβo] (kikapu) | ikabũ [ikaβo] (vikapu) |
| gĩtĩ [gete] (kiti) | itĩ [ite] (viti) |
| kĩoro [keɔrɔ] (choo) | bioro [βiɔrɔ] (vyoo) |
| kĩoni [keɔni] (kioo) | bioni [βiɔni] (vioo) |

iii) majina ya ukubwa

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| kĩana [keana] (toto) | biana [βiana] (matoto) |
| kĩmuntũ [kemunto] (jitu) | imuntũ [imunto] (majitu) |
| kĩmwarĩ [kemware] (jisichana) | imwarĩ [imware] (majisichana) |
| kĩmwĩjĩ [kemweɟe] (jivulana) | imwĩjĩ [imweɟe] (majivulana) |
| kĩmũkũrũ [kemokoro] (jizee) | imũkũrũ [imokoro] (majizee) |
| kĩng'ombe [keŋɔmbɛ] (gombe) | ing'ombe[iŋɔmbɛ] (magombe) |

**9. N-     10. N-**

Nomino katika makundi haya hazina tofauti katika umoja au wingi na huanza kwa **N** katika umoja na wingi au viambishi vingine. Baadhi ya nomino katika ngeli hizi ni:

i) majina ya wanyama wa nyumbani na msituni

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mbũri [mbori] (mbuzi) | mbũri [mbori] (mbuzi) |
| mbogo [mbɔgɔ] (mbogo) | mbogo [mbɔgɔ] (mbogo) |
| kũrũ [koro] (mbwa) | kũrũ [koro] (mbwa) |
| ng'ombe [ŋɔmbɛ] (ng'ombe) | ng'ombe [ŋɔmbɛ] (ng'ombe) |
| ng'ondu [ŋɔndu] (kondoo) | ng'ondu [ŋɔndu] (kondoo) |
| ngũkũ [ŋgoko] (kuku) | ngũkũ [ŋgoko] (kuku) |

ii) nomino za vifaa/vitu mbalimbali

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| ndege [ndɛgɛ] (ndege) | ndege [ndɛgɛ] (ndege) |
| ngarĩ [ŋgare] (gari) | ngarĩ [ŋgare] (gari) |
| nthitangi [nθitaŋgi] (jembe) | nthitangi [nθitaŋgi] (jembe) |
| nyondo [ɲɔndɔ] (nyundo) | nyondo [ɲɔndɔ] (nyundo) |

iii) sehemu za mwili

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| nyonto [ɲɔntɔ] (ziwa) | nyonto [ɲɔntɔ] (maziwa) |
| nkoro [nkɔrɔ] (moyo) | nkoro [nkɔrɔ] (nyoyo) |
| nkingo [nkiŋgɔ] (shingo) | nkingo [nkiŋgɔ] (shingo) |
| njara [nɟara] (mkono) | njara [nɟara] (mikono) |

**11. RŨ - 12 N-**

Nomino katika makundi haya huanza kwa kiambishi **rũ**- katika umoja, na **n-** katika hali ya wingi. Nomino zinazopatikana katika makundi haya ni za vitu ambavyo havina uhai kama:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| rũritho [roriθɔ] (wivu) | ndũritho [ndoriθɔ] (wivu) |
| rũciara [rociara] (kizazi) | nciara [nciara] (vizazi) |
| rũgendo [rogɛndɔ] (safari) | ngendo [ngɛndɔ] (safari) |
| rũgutũ [roguto] (uvumi) | ngũtũ [ngoto] (uvumi) |
| rũthingo [ruθiŋgɔ] (kiambaza) | nthingo [nθiŋgɔ] (viambaza) |
| rũbito [ruβitɔ] (ufito) | mbito [mβitɔ] (fito) |
| rwego [rwɛgɔ] (ua) | ndwego [ndwɛgɔ] (nyua) |

**13.Ũ - 14. Ũ -**

Nomino katika makundi haya hazibadiliki katika hali ya wingi. Nyingi ya nomino katika makundi haya ni zile za dhahania.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| ũchinka[otʃinka] (ujinga) | ũchinka[otʃinka] (ujinga) |
| ũjanja[oɟanɟa] (ujanja) | ũjanja[oɟanɟa] (ujanja) |
| ũtũrũtũ [otoroto] (usumbufu) | ũtũrũtũ [otoroto] (usumbufu) |
| ũgambi [ogamβi] (utetezi) | ũgambi [ogamβi] (utetezi) |
| ũkiri [okiri] (unyamavu) | ũkiri [okiri] (unyamavu) |
| wamba [wamβa] (wizi) | wamba [wamβa] (wizi) |
| ũkĩa [okea] (umaskini) | ũkĩa [okea] (umaskini) |

**15 Ũ - 16.MA-**

Nomino zinazopatikana katika makundi haya huanza kwa **u-** katika hali ya umoja na **ma**- katika hali ya wingi.

| **Umoja** | | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|---|
| ũtheru | [oθɛru] | (usafi) | motheru [mɔθɛru] | (usafi) |
| ũntũ | [onto] | (jambo) | mantũ [manto] | (mambo) |
| ũkĩa | [okea] | (umaskini) | mokĩa [mɔkea] | (umaskini) |
| ũritu | [oritu] | (ujinga) | moritu [mɔritu] | (ujinga) |

**17. KA-/GA- 18, TW-/TŨ-**

Makundi haya ya nomino hushirikisha nomino ambazo huanza kwa viambishi **ka/ga** katika umoja, na **tw/tũ** katika wingi. Nomino katika ngeli hizi ni kama:

i)Nomino za hali ya udogo au kudunisha

| **Umoja** | | | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| kaĩjĩ | [kaeje] | (kivulana) | tũĩjĩ [tueje] (vivulana) |
| kaana | [ka:na] | (kitoto) | twaana [twa:na] (vitoto) |
| kaara | [ka:ra] | (kijidole) | twaara [twa:ra] (vijidole) |
| kagarĩ | [kagare] | (kijigari) | tũgarĩ [togare] (vijigari) |
| kang'ombe | [kaŋɔmbɛ] | (kijigombe) | tũng'ombe[tuŋɔmbɛ] (vijigombe) |
| kaboka | [kaβɔka] | (kijiboga) | tũboka [toβɔka] (vijiboga) |

**19. KŨ - 20. KŨ -**

Majina katika makundi haya hayana wingi na huambishwa **ku** katika mianzo yake. Nomino katika makundi haya hutumika pia kama vitenzi. Hii ndiyo sifa muhimu ya

majina katika ngeli hizi. Ili kubainisha ikiwa neno ni kitenzi au nomino lazima liwe kwenye muktadha wa sentensi. Baadhi ya nomino katika ngeli hizi ni kama:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| kũrima [korima] (kulima) | kũrima [korima] (kulima) |
| kũruga [koruga] (kupika) | kũruga [koruga] (kupika) |
| kũrara [korara] (kulala) | kũrara [korara] (kulala) |
| kũthoma [koθɔma] (kusoma) | kũthoma [koθɔma] (kusoma) |
| kwina [kwina] (kuimba) | kwina [kwina] (kuimba) |
| kũtharima [koθarima] (kubariki) | kũtharima [koθarima] (kubariki) |
| kũthũra [koθora] (kukasirika) | kũthũra [koθora] (kukasirika) |
| kũgambia [kogamβia] (kuchumbia) | kũgambia [kogamβia] (kuchumbia) |
| kũthogia [koθɔgia] (kusaka) | kũthogia[koθɔgia] (kusaka) |

**21. A- 22.GŨ -**

Haya ni makundi ya nomino za mahali zinazochukua upatanisho wa kisarufi wa mofu **a-** katika umoja na **ga**-/**ka**- katika wingi. Mofu hizi huwa na uamilifu wa viwakilishi vya nomino katika vitenzi vinavyoashiria mahali.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| antũ [anto] (mahali) | gũntũ [gonto] (mahali) |

### 4.16 Muundo ya Vivumishi vya Kiimenti

#### 4.16.1 Muundo wa Mzizi Pekee

Baadhi ya vivumishi vya Kiimenti huzingatia mipangilio ifuatayo:

i) V ⟶ Mz

Muundo huu unaonyesha kuwa vivumishi fulani vya Kiimenti vina mofolojia ya mzizi wa kivumishi pekee. Vivumishi hivi havibebi mofu au viashiria vya mofimu. Vivumishi vya namna hii hujitokeza kama mizizi inayojisimamia au mofimu huru. Katika hali hii kivumishi hubeba maana iliyokamilika, yaani maana ya kileksia. Muundo wa vivumishi hivi unaweza kuwakilishwa kama (V= Leksia (L). Vivumishi vya namna hii hueleweka bila kuongezea mofu yoyote. Mfano wa vivumishi hivi ni kama vile vya mkopo kutoka lugha nyingine hadi kwa Kiimenti. Hivi ni vivumishi kama **tofauti/tafauti** (tofauti), **atari** (hatari), **maarumu** (maalum) na **cawacawa** (sawasawa). Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2011) etimolojia ya vivumishi hivi vitatu ni Kiarabu. Muundo wa vivumishi hivi vya mkopo ni kuwa mofu kapa huambishwa mwanzoni mwa kivumishi ikiwakilisha ngeli ya mofolojia au nomino inayovumishwa.

| **Muundo wa Ndani** | **Muundo wa Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| cawacawa/ø-cawacawa/ | cawacawa [cawacawa] | sawasawa |
| atarĩ /ø -atarĩ / | atarĩ [atare] | hatari |
| tafauti /ø-tafauti/ | tofauti [tafauti ] | tofauti |
| maarumu/ø-maarumu/ | maarumu [ma:rumu] | maalumu |
| maritati/ø-maritati/ | maritati [maritati] | maridadi |

### 4.16.2 Muundo wa Viambishi Awali na Mzizi

ii) V ⟶ VA+Mz

Muundo huu huwakilisha vivumishi vinavyoundwa kwa mizizi yavyo kuambishwa viambishi awali. Vivumishi vingi katika lahaja ya Kiimenti huundwa kwa kuzingatia mchakato huu kuliko ile mingine. Viambishi awali vinavyotangulia mzizi huweza kuwa vianishi vya umoja, wingi na hata ngeli. Tunaweza kusema kuwa vivumishi hivi huundwa

kwa kutumia mofimu tegemezi. Baadhi ya vivumishi vya sifa, idadi, pekee, vionyeshi, a – unganifu, viulizi na vimilikishi katika lahaja ya Kiimenti huzingatia mofolojia ya mzizi kutanguliwa na viambishi awali vyenye uamilifu tofauti. Ni vizuri kufahamu kuwa kuna mizizi ya vivumishi ambayo itaambishwa mwanzoni mara moja na mingine mara mbili.

#### 4.16.2.1 Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip+Mz)

Vivumishi vya idadi kamili na vya jumla huambishwa mwanzoni mwa mizizi yake vinapoundwa. Kwa namna moja kuna vile ambavyo kipatanishi huambishwa kwenye mzizi wa kivumishi na kuunda kivumishi. Mfano wa kivumishi **baĩrĩ** [βaere] (wawili) kimeundwa kwa mzizi **-ĩrĩ** [-ere] (-ili) kuambishwa kipatanishi /ba/ cha ngeli ya 2 (BA). Kwa hivyo muundo wa kipatanishi kutangulia mzizi ndio unaozingatiwa katika muundo wa vivumishi husika. Jedwali lifuatalo linaonyesha jinsi vivumishi mbalimbali vya idadi vinaundwa katika lahaja ya Kiimenti.

**Jedwali la 16: Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 MW/MU/MŨ | ũ - | -mwe | ũ + mwe | ũmwe [omwɛ] | mmoja |
| 2 A | ba- | -thatũ | ba + thatũ | bathatũ [βaθato] | watatu |
| 2 A | ba- | -kai | ba +kai | bakai [βakai] | wachache |
| 4 MI | i- | -ng'anona | i + ng'anona | ing'anona [iŋanɔna] | wastani |
| 6 MA | ja- | -ng'anona | ja + ng'anona | jang'anona [ɟaŋanɔna] | kiasi |
| 8 I/BI | bi- | -ng'ana | bi + ng'ana | bing'ana [βiŋana] | vingapi |
| 10 N | i- | -ng'ana | i + ng'ana | ing'ana[iŋana] | ngapi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali la 16 vivumishi vya idadi vya Kiimenti vimeundwa huku mizizi ya vivumishi husika ikiambishwa mwanzoni. Mwanzoni mizizi ya vivumishi imeambishwa vipatanishi vya ngeli za kimofolojia kama {ũ-} katika ngeli ya 1 (MW/MU/MŨ) na kuunda kivumishi **ũmwe** [omwɛ] (mmoja), {ba-} katika ngeli ya 2 (A) na kuunda kivumishi **bakai** [βakai] (wachache), (i-) katika ngeli ya 3 ili kuunda kivumishi **ing'anona** [iŋanɔna (kiasi wastani) na kadhalika.

#### 4.16.2.2 Muundo wa Vivumishi vya Idadi vya Kiimenti (Kip+Kip+Mz)

Muundo mwingine wa vivumishi vya idadi unahusu hali ya mzizi wa kivumishi husika kuambishwa vipatanishi viwili vya aina moja kama viambishi awali. Hali hii haipatikani katika ngeli zote kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 17: Muundo wa Vivumishi vya Idadi (Kip+Kip+Mz)**

| Ngeli | Kip | Kip | Mz | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | ba- | ba- | -kai | babakai [βaβakai] | wachache |
| 5 | rĩ - | ri- | -ingĩ | riringĩ [reriŋge] | linaloonyesha wingi |
| 8 | bi- | bi- | -ega | bibiega[βiβiɛga] | vizuri |
| 11 | rũ- | rũ- | -irũ | rũrwirũ [rorwiro] | iliyo nyeusi |
| 13 | bũ | bũ - | -ingĩ | bũbwingĩ [βoβwiŋge] | iliyo nyingi |
| 14 | bũ- | bũ- | -ingĩ | bũbwingĩ [βoβwiŋge] | iliyo nyingi |
| 15 | bũ- | bũ- | -ingĩ | bũbwingĩ [ βoβwiŋge] | iliyo nyingi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Licha ya kuwa vivumishi fulani katika Kiimenti hasa vile vya sifa na idadi huundwa kutumia vipatanishi tangulizi viwili, konsonanti ya kile cha pili huweza kudondoshwa (Mutahi, 1977; Wa Mberia, 1981). Aidha, michakato kama ya kifonolojia huweza kutokea katika muundo wa vivumishi vya idadi vya Kiimenti. Kutokana na jedwali la 17 uyeyushaji umetokea katika kuunda kivumishi **bũbwingi** [βoβwinge] (iliyo nyingi). Katika hali hii irabu /ũ/ inayopatikana katika kipatanishi cha pili inayeyushwa na kuwa /w/.

#### 4.16.2.3 Muundo wa Vivumishi vya Pekee Katika Kiimenti.

Pia, vivumishi mbalimbali vya pekee huundwa kutumia mofu ya kipatanishi ikiambishwa katika mzizi wa kivumishi kama kiambishi awali. Kwa hivyo, muundo wa vivumishi

vinavyopatikana ni wa kuambishwa mofu moja mwanzoni mwa mzizi ambayo ina uamilifu wake. Jedwali lifuatalo linashadidia muundo huu.

**Jedwali la 18: Muundo wa Vivumishi vya Pekee vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 MW/MU/MŨ | ũ - | -nka | ũ + nka | wenka [wɛnka] | pekee |
| 2 A | ba- | -ngĩ | ba + ngĩ | bangĩ [βaŋge] | wengine |
| 3 MU | ju- | -ngwa | ju + ngwa | jungwa[ɟuŋgwa] | wenyewe |
| 3 MŨ | jũ- | -ene | jũ + ene | jwene [ɟwɛnɛ] | wenye |
| 4 MĨ | ĩ - | -nthe | ĩ + nthe | yonthe [jɔnθɛ] | yote |
| 19 KU | ku- | -nthe | ku + nthe | kunthe [kunθɛ] | kwote |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

#### 4.16.2.4 Muundo wa Vivumishi Vionyeshi Katika Kiimenti

Vivumishi vionyeshi ni vya aina tatu. Hata hivyo, vionyeshi vya mbali kidogo na vile vya mbali ndivyo huzingatia mofolojia ya mzizi wa kivumishi kuambishwa mwanzoni. Vivumishi vionyeshi vya mbali kidogo na mbali hubainishwa kwa kutumia mizizi miwili. Vile vya mbali kidogo huonyeshwa kwa kutumia mzizi **u-** (h-) ilhali vile vya mbali husimamiwa na mzizi **-ria** (-le). Jinsi namna zote mbili za vivumishi zinavyoundwa inaweza kubainika katika jedwali la 18 na 19.

**Jedwali la 19: Muundo wa Vivumishi vya Mbali Kidogo vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 KĨ/GĨ | kĩ- | -u | kĩ + u | kĩu [keu] | hicho |
| 8 I/BI | bi- | -u | bi + u | biu [βiu] | hivyo |
| 9 N | ĩ - | -u | ĩ + u | ĩu [eu] | hiyo |
| 11 RŨ | rũ- | -u | rũ + u | rũu [rou] | huo |
| 16 MA | ja- | -u | ja + u | jau [ɟau] | hayo |
| 17 KA/GA | ka- | -u | ka + u | kau [kau] | hicho |
| 18 TW/TŨ | tũ - | -u | tũ + u | tũu [tou] | hivyo |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali la 19 inabainika wazi kuwa vivumishi vionyeshi vya mbali kidogo huzingatia muundo wa mzizi kuambishwa kipatanishi mwanzoni. Mifano ya vivumishi vinavyoundwa ni kama **kĩu** [keu] (hicho) katika ngeli ya 7 (KĨ/GĨ), **biu** [βiu] (hivyo) katika ngeli ya 8 (I/BI) na **ĩu** [eu] (hiyo) katika ngeli ya 9 (N). Ni vizuri kufahamu kuwa mzizi wa vivumishi vya mbali kidogo unabaki kuwa {-u}. Kwa hivyo, haubadiliki katika ngeli mbalimbali.

Aidha, vivumishi vya mbali katika Kiimenti huzingatia mofolojia ya mzizi kuambishwa mwanzoni kama inavyodhihirika katika jedwali la 20 hapo chini. Mofolojia kama hii ndiyo imebainika katika muundo wa vivumishi vionyeshi vya mbali kidogo katika jedwali la 19.

**Jedwali la 20: Muundo wa Vivumishi vya Mbali vya Kiimenti (Kip + Mz)oro**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.MW/MW/ MŨ | ũ - | -rĩa | ũ + rĩa | ũrĩa | [orea] | yule |
| 2. A | ba- | -rĩa | ba + rĩa | barĩa | [βarea] | wale |
| 3. MŨ | jũ- | -rĩa | jũ + rĩa | jũrĩa | [ɟorea] | ule |
| 4 MĨ | ĩ - | -rĩa | ĩ + rĩa | ĩrĩa | [erea] | ile |
| 5 I/RĨ | rĩ - | -rĩa | rĩ + ria | rĩrĩa | [rerea] | lile |
| 6 MA | ja- | -rĩa | ja + rĩa | jarĩa | [ɟarea] | yale |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 20 linaonyesha mifano ya vivumishi vionyeshi vya mbali kama **ũrĩa** [orea] (yule) katika ngeli ya 1 (MW/MW/MŨ, **barĩa** [βarea] (wale) katika ngeli ya 2 (A), **jũrĩa** [ɟorea] (ule) katika ngeli ya 3 (MŨ), **ĩrĩa** [erea] (ile) katika ngeli ya 4 (MĨ) na mifano mingine kama hiyo. Imebainika wazi kuwa mzizi wa vivumishi vya mbali kutokana na mifano ya vivumishi hivyo katika jedwali ni **-rĩa** (-le). Mzizi huu huongezewa viambishi awali vya ngeli za sintakia (vipatanishi) ili kuunda vivumishi vionyeshi vya mbali. Viambishi hivi ni kama {ũ-} katika ngeli ya 1 (MW/MW/ MŨ), {ba-} katika ngeli ya 2 (A) na vingine katika ngeli mbalimbali.

**4.16.2.5 Muundo wa Vivumishi vya A – Unganifu vya Kiimenti**

Aidha, vivumishi vya a – unganifu huzingatia muundo wa mzizi wa kivumishi kuambishwa mwanzoni. Kwa hivyo vinazingatia muundo wa kipatanishi kutangulia

mzizi katika ngeli mbalimbali. Muundo wa vivumishi vya A – unganifu unaonyeshwa katika jedwali la 21.

**Jedwali la 21: Muundo wa Vivumishi vya A – Unganifu vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| **Ngeli** | **Kip** | **Mz** | **Kip + Mz** | **Kivumishi** | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 KĨ/GĨ | kĩ- | -a | kĩ + a | kĩa | [kea] | cha |
| 8 I/BI | bi- | -a | bi + a | bia | [βia] | vya |
| 9 N | ĩ - | -a | ĩ + a | ya | [ja] | ya |
| 12 N | chi- | -a | chi + a | chia | [ʧia] | za |
| 19 KŨ | kũ- | -a | kũ + a | kwa | [kwa] | kwa |
| 21 A | a- | -a | a + a | a | [a] | pa |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 21 linonyesha jinsi vipatanishi katika ngeli mbalimbali hutumika kuunda vivumishi vya a – unganifu. Vipatanishi ndivyo hupatikana mwanzoni mwa vivumishi vya a – unganifu kama viambishi awali. Kwa hivyo, muundo wa vivumishi hivi hubadilika kutoka ngeli moja hadi nyingine kutegemea viambishi vya ngeli za sintaksia vya kila ngeli. Hata hivyo, mzizi wa vivumishi vya a – unganifu unabaki {-a}.

#### 4.16.2.6 Muundo wa Vivumishi Viulizi vya Kiimenti

Vilevile, vivumishi viulizi katika Kiimenti huundwa wakati mofu ya kipatanishi huambishwa mzizi wa kivumishi kama kiambishi awali. Mifano ya vivumishi viulizi vinavyopatikana katika mchakato huu inabainika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 22: Muundo wa Vivumishi Viulizi vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 MU/MW/MŨ | ũ - | -rĩkũ | ũ + rĩkũ | ũrĩkũ | [oreko] | yupi |
| 2 A | ba- | -rĩkũ | ba + rĩkũ | barĩkũ | [βareko] | wepi |
| 4 M Ĩ | ĩ - | -rĩkũ | ĩ + rĩkũ | ĩrĩkũ | [ereko] | ipi |
| 6 MA | ja- | -rĩkũ | ja + rĩkũ | jarĩkũ | [ɟareko] | yapi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 22 linaonyesha jinsi mzizi huambishwa vipatanishi katika ngeli mbalimbali ili kuunda vivumishi viulizi vya Kiimenti. Kwa mfano, mzizi wa kivumishi kiulizi **-rĩkũ** (-pi) hutanguliwa na kipatanishi katika ngeli mbalimbali na kuunda vivumishi kama **ũrĩkũ** [oreko] (yupi), **barĩkũ** [βareko] wepi, **ĩrĩkũ** [ereko] ipi na **jarĩkũ** [ɟareko] yapi.

#### 4.16.2.7 Muundo wa Vivumishi Vimilikishi vya Kiimenti

Vimilikishi katika nafsi zote (umoja na wingi) huambishwa mwanzoni vinapoundwa. Kipatanishi cha ngeli ndicho huambishwa mwanzoni mwa kila kimilikishi kinapoundwa. Kipatanishi kinachotangulia mzizi huwa na utendekakazi wake katika Kiimenti. Jedwali lifuatalo linaweza kuangazia muundo wa vivumishi hivi zaidi.

**Jedwali la 23: Muundo wa Vimilikishi vya Kiimenti (Kip + Mz)**

| Ngeli | Kip | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 MU/MW/ MŨ | ũ - | -akwa | ũ + akwa | wakwa | [wakwa] | wangu |
| 3 MŨ | jũ- | -etũ | jũ + etũ | jwetũ | [ɟwɛto] | wetu |
| 4 MĨ | ĩ - | -enu | ĩ + enu | yenu | [jɛnu] | yenu |
| 5 I/RĨ | rĩ- | -aku | rĩ + aku | rĩaku | [reaku] | lako |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Inabainika wazi kutokana na jedwali la 23 kuwa kipatanishi kinapoambishwa katika mwanzo wa mzizi wa kivumishi kimilikishi, vivumishi vya aina hiyo vinaundwa. Mifano ya vimilikishi hivyo ni kama **wakwa** [wakwa] (wangu) katika ngeli ya 1 (MU/MW/ MŨ), **jwetũ** [ɟwɛto] (wetu) katika ngeli ya 3 (MŨ), **yenu** [jɛnu] (yenu) katika ngeli ya 4 (MĨ) na **rĩaku** [reaku] (lako) katika ngeli ya 5 (I/RĨ). Mchakato wa uyeyushaji unabainika katika uundaji wa vimilikishi **jwetũ** [ɟwɛto] wetu na **wakwa** [wakwa] (wangu). Hata hivyo, mifano mingine ya vimilikishi katika jedwali haidhihirishi uyeyushaji.

#### 4.16.2.8 Muundo wa Vivumishi vya Majina vya Kiimenti

Muundo wa vivumishi vya majina katika lahaja ya Kiimenti huzingatia mzizi wa nomino kuambishwa mwanzoni. Kwa hivyo, kiambishi awali katika vivumishi vya majina ni kiambishi cha ngeli za mofolojia. Huu pia ndio muundo unaozingatiwa katika uundaji wa nomino katika Kiimenti. Hivyo, ni vizuri kufahamu kuwa vivumishi vya majina, ni majina katika Kiimenti na yana muundo wa majina mengine katika lahaja hiyo. Jedwali

lifuatalo linaonyesha muundo wa majina ambayo yanaweza kuwa na uamilifu kama vivumishi.

**Jedwali la 24: Muundo wa Vivumishi vya Majina vya Kiimenti (KiN + Mz)**

| Ngeli | KiN | Mz | Kip + Mz | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 MU/MW/MŨ | mũ -/mw- | -ka | mũ + ka | mũka [moka] | mwanamke |
| 1 MU/MU/ MŨ | mũ -/mw- | -arimũ | mũ + arimũ | mwarimũ[mwarimo] | mwalimu |
| 1 MU/MU/ MŨ | mũ -/mw- | -rume | mũ + rume | mũrũme [moromɛ] | mwanamume |
| 9 N | n- | -tũrũtũ | n + tũrũtũ | ntũrũtũ [ntoroto] | msumbufu |
| 9 N | n- | -ka | n + ka | nka [nka] | kike |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na vivumishi vya majina kwenye jedwali la 24 virai nomino vingi vinaweza kuundwa. Katika virai nomino vifuatavyo, nomino ya pili inatumika kuvumisha nomino ya kwanza. Hivi ni kama **muntũ mũka** [munto moka] (mtu mwanamke), **mũka mwarimũ** [moka mwarimo] (mwanamke mwalimu), **mbũri nka** [mbori nka] (mbuzi jike), **mũkũrũ mũthao** [mokoro moθaɔ] (mzee mvivu), **mbũri ntũrũtũ** [mbori ntoroto] (mbuzi msumbufu) na **mwana mwamba** [mwana mwamba] (mtoto mwizi). Nomino ya pili inayotumika kama kivumishi ina muundo wa kiambishi awali cha ngeli ya mofolojia na mzizi wa nomino. Jedwali la 24 linaonyesha muundo wa nomino ya pili inayotumika kama kivumishi cha jina.

#### 4.16.2.9 Muundo wa Vivumishi vya Sifa vya Kiimenti

Vivumishi vya sifa katika Kiimenti huzingatia miundo miwili. Muundo wa kwanza unahusu mzizi wa kivumishi kuambishwa mofu ya kipatanishi ikifuatwa na ile ya kiambishi ngeli na kisha mzizi wa kivumishi. Muundo mwingine unahusu vipatanishi viwili vya aina moja kuambishwa mwanzoni mwa mzizi wa kivumishi na kuunda vivumishi vya sifa vya Kiimenti.

#### 4.16.2.9.1 Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip + KiN + Mz)

Muundo huu unahusu uambishaji wa kipatanishi kikifuatwa na kiambishi cha ngeli ya kimofolojia na kisha mzizi. Vivumishi vya sifa huzingatia ruwaza maalumu. Kwa jinsi hii mzizi wa kivumishi cha sifa huambishwa viambishi awali. Hivyo, kimofolojia vivumishi hivi huzingatia ruwaza maalumu. Ruwaza inayozingatiwa kupangilia mofu za vivumishi hivi ni kama, {Kip}+{KiN}+Mzizi. Kwa mfano, kivumishi cha sifa cha Kiimenti, **jũmũthũku** [ɟomoθuku] (mbaya) kimeundwa hivi **jũ+mũ+thũku** (mbaya). Katika mfano huu viambishi awali ni {**jũ**} na {**mũ**}. Kiambishi {**jũ**} ni kipatanishi cha nomino katika ngeli ya tatu ya sintaksia **{jũ}** ilhali {**mũ**} ni kiambishi kinachowakilisha ngeli ya tatu ya mofolojia (MŨ). Viambishi hivi ndivyo huambishwa mzizi {**–thũku**} (-baya) ili kuunda kivumishi **jũmũthũku/**jũ-mũ-thũku (mbaya). Kwa kuwa ngeli ni nyingi basi kuna vipatanishi vingi na viambishi ngeli vingi tofauti. Hivyo, mzizi {**–thũku**} (-baya) huambishwa vipatanishi na viambishi ngeli tofauti kulingana na ngeli ya nomino husika. Mzizi wa kivumishi hubeba maana ya kileksia ya kivumishi husika. Ni vizuri kufahamu kuwa vivumishi vingi vya sifa vyenye asili ya Kibantu tulivyokumbana navyo katika utafiti wetu ni mizizi tegemezi. Hatukupata vivumishi ambavyo ni mizizi huru. Jedwali lifuatalo linaonyesha mofolojia ya vivumishi vya sifa katika ngeli mbalimbali

kwa kutumia mzizi {–**thũku**} (-baya) kuonyesha hali hii tukizingatia muundo wa Kip + KiN + Mz.

**Jedwali la 25: Muundo wa Vivumishi vya Sifa vya Kiimenti (Kip+KiN + Mz)**

| | NGELI | Kip | Kip + KiN + Mzizi | Kivumishi -thuku (-baya) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MU/MW/MŨ | a | ũ +mũ+thũku | ũmũthũku (mbaya) |
| 2 | A | ba | - | - |
| 3 | MŨ | jũ | jũ +mũ +thũku | jũmũthũku (mbaya) |
| 4 | MĨ | ĩ | ĩ+mĩ +thũku | ĩmithũku (mibaya) |
| 5 | I/RI | rĩ | - | - |
| 6 | MA | ja | ja+ma+thũku | jamathũku (mabaya) |
| 7 | KĨ /GĨ | gĩ | gĩ +kĩ +thũku | gĩkĩthũku (kibaya) |
| 8 | I/ BI | bi | - | - |
| 9 | N | ĩ | ĩ +n+thũku | ĩnthũku (mbaya) |
| 10 | N | i | i+n+thũku | inthũku (mbaya) |
| 11 | RŨ | rũ | - | - |
| 12 | N | ĩ | ĩ +n+thũku | ĩnthũku (mbaya) |
| 13 | Ũ | bũ | - | - |
| 14 | Ũ | bũ | - | - |
| 15 | Ũ | bũ | - | - |
| 16 | MA | ja | ja+ma+thũku | jamathũku (mabaya) |
| 17 | KA/GA | ga | ga+ka+thũ ku | gakathũku (kilicho kibaya) |
| 19 | KŨ | gu | gũ +kũ+thũku | gũkũthũku (pabaya) |
| 20 | KŨ | gu | gũ +kũ+thũku | gũkũthũku (pabaya) |
| 22 | GŨ | gu | gũ +kũ+thũku | gũkũthũku (pabaya) |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali hapo juu inabainika kuwa muundo wa Kip + KiN + Mz haupatikani katika ngeli zote. Muundo kama huo unabainka katika ngeli ya 1 (MU/MW/MŨ), 3 (MŨ), 4 (MĨ), 6 (MA), 7 (KĨ/GĨ), 9 (N), 10 (N), 12 (N), 16 (MA), 17 (KA/GA), 19 (KŨ), 20 (KŨ) na 22 (GŨ).

#### 4.16.2.9.2 Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip+ Kip+Mz)

Kuna vivumishi vya Kiimenti ambavyo huundwa kwa mzizi wa kivumishi kutanguliwa na vipatanishi viwili. Baadhi ya vivumishi vinavyozingatia muundo huo ni kama vile vya sifa. Katika jedwali lilopo hapo juu ni wazi kuwa hakuna vivumishi vyenye muundo wa Kip + KiN + Mz vilivyoonyeshwa katika ngeli ya 2 (A), 5 (I/RI), 8 (I), 11 (RŨ), 13 (Ũ), 14 (Ũ), 15 (Ũ) na 18 (TW/TŨ). Vivumishi vya sifa katika ngeli hizo huchukua muundo wa mzizi kutanguliwa na vipatanishi viwili. Kwa kutumia mzizi **–thũku** (-baya) tunaweza kuonyesha muundo huo katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 26: Muundo wa Vivumishi vya Sifa (Kip + Kip + Mz)**

| | NGELI | Kip | Kip | Mzizi | Kip+Kip+Mzizi | Kivumishi –thũku(-baya) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | A | ba | a | -thũku | ba+ba+thũku | babathũku (wabaya) |
| 5 | I/RI | rĩ | i/rĩ | -thũku | rĩ+rĩ +thũku | rĩrĩthũku (lililo baya) |
| 8 | I | bi | i | -thũku | bi+bi+thũku | bibithũku (vibaya) |
| 11 | RŨ | rũ | rũ | -thũku | rũ+rũ+thũku | rũrũthũku (ulio mbaya) |
| 13 | Ũ | bũ | ũ | -thũku | bũ+bũ+thũku | bũbũthũku (mbaya) |
| 14 | Ũ | bũ | ũ | -thũku | bũ+bũ+thũku | bũbũthũku (mbaya) |
| 15 | Ũ | bũ | ũ | -thũku | bũ+bũ+thũku | bũbũthũku(mbaya) |
| 18 | TW/TŨ | tũ | tw/tũ | -thũku | tũ+tũ+thũku | tũtũthũku (vibaya) |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 26 linaonyesha muundo wa vivumishi mbalimbali vya sifa vikitumia mzizi –**thũku** (baya). Vivumishi vingi vya sifa vimeundwa vinapoambishwa vipatanishi viwili mwanzoni. Hivi ni kama **babathũku** (wabaya) katika ngeli ya 2 (A), **rĩrĩthũku** (lililo baya) katika ngeli ya 5 (I/RI), **bibithũku** (vibaya) katika ngeli ya 8 (I) na **rũrũthũku** (ulio mbaya) katika ngeli ya 18. Mpaka hapa tumefika inafaa ieleweke kuwa vivumishi kama vile vya sifa huweza kubainisha miundo minne kama ifuatavyo:

*a)* Kip + KiN + Mz ⟶ ũmũraja/ũ -mũ-raja/ (mrefu), jamairũ /ja-ma-irũ / (meusi)

*b)* KiN + Mz ⟶ maritati/ø-maritati/ (maridadi), cawa/ø-cawa/ (sawa)

*c)* Kip + Kip + Mz ⟶ babakuĩ /ba-ba-kuĩ/ (wafupi), babairu/ba-ba-irũ (weusi)

*d)* Kip + Mz ⟶ bakuĩ /ba-kuĩ / (wafupi), bairũ /ba-irũ (weusi)

### 4.16.3 Muundo wa Viashiria vya Karibu (VA+Mz+VT)

Vivumishi ambavyo ni viashiria vya karibu ndivyo huundwa kuzingatia mofolojia ya mzizi kuambishwa mwanzoni na mwishoni. Pia, vivumishi hivi ni mofimu tegemezi. Kimofolojia kuna mizizi mingi inayoambishwa mwanzoni na tamati ili kuunda vivumishi vya karibu. Mizizi ya vivumishi hivi ni kama: -j-, -b-, -r-, -k-, na –t-. Kwa mfano, mzizi kama –j- huweza kuambishwa kiambishi awali {**ũ-}** na kiambishi tamati {**-ũ}** na kuunda kivumishi kionyeshi **ũjũ** [oɟo](huyu). Mzizi huu umeambishwa kiambishi awali ambacho ni kipatanishi cha nomino katika ngeli ya 1 ambayo ni MU/MŨ /MW na kiambishi tamati ambacho ni irabu inayopatikana kwenye kipatanishi. Vivumishi vionyeshi vya karibu ndivyo vivumishi ambavyo vina viambishi tamati katika lahaja ya Kiimenti. Vingine vina muundo wa viambishi awali na kisha mzizi. Kwa hivyo, muundo unaozingatiwa ni wa {Kip} + {Mzizi} + {I - Kip). Hali hii inabainika zaidi katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 27: Muundo wa Vivumishi Vionyeshi vya Karibu (Kip + Mz + I- (KiP)**

| | NGELI | Kip | Mz | Irabu (Kip) | Kip+Mzi+ I (Kip) | Vionyeshi vya Karibu | Vivumishi konsonanti inapodondoshwa | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MU/MŨ /MW | **u** | -j- | u | ũ +j+ũ | ũjũ | ũũ | huyu |
| 2 | A | **ba** | -b- | a | ba+b+a | baba | baa | hawa |
| 3 | MŨ | **jũ** | -j- | ũ | jũ+j+ũ | jũjũ | jũũ | huu |
| 4 | MĨ | ĩ | -j- | ĩ | ĩ +j+ĩ | ĩjĩ | ĩĩ | hizi |
| 5 | I/RĨ | **rĩ** | -r- | ĩ | rĩ+r+ĩ | rĩrĩ | rĩĩ | hili |
| 6 | MA | **ja** | -j- | a | ja+j+a | jaja | jaa | haya |
| 7 | KĨ/GĨ | **gĩ** | -k- | ĩ | gĩ+k+ĩ | gĩkĩ | kĩĩ | hiki |
| 8 | I/ BI | **bi** | -b- | i | bi+b+i | bibi | bii | hivi |
| 9 | N | Ĩ | -j- | ĩ | ĩ +j+ĩ | ĩjĩ | ĩĩ | hizi |
| 10 | N | **i** | -j- | i | i+j+i | iji | ii | Hii |
| 11 | RŨ | **rũ** | -r- | ũ | rũ+r+ũ | rũrũ | rũũ | huu |
| 12 | N | **i** | -j- | i | i+j+i | iji | ii | hizi |
| 13 | Ũ | **bũ** | -b- | ũ | bũ+b+ũ | bũbũ | bũũ | huu |
| 14 | Ũ | **bũ** | -b- | ũ | bũ+b+ũ | bũbũ | bũũ | huu |
| 15 | Ũ | **bũ** | -b- | ũ | bũ+b+ũ | bũbũ | bũũ | huu |
| 16 | MA | **ja** | -j- | a | ja+j+a | jaja | jaa | haya |
| 17 | KA/GA | **ga** | -k- | a | ga+k+a | gaka | kaa | hiki |
| 18 | TW/TŨ | **tũ** | -t- | ũ | tũ+t+ũ | tũtũ | tũũ | hivi |
| 19 | KŨ | **gũ** | -k- | ũ | gũ+k+ũ | gũkũ | kũũ | huku |
| 20 | KŨ | **gũ** | -k- | ũ | gũ+k+ũ | gũkũ | kũũ | huku |
| 21 | A | **a** | -j- | a | a+j+a | aja | aa | hapa |
| 22 | GŨ | **gũ** | -k- | ũ | gũ+k+ũ | gũkũ | kũũ | huku |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kama inavyobainika katika jedwali lililopo hapo juu kuna uwezekano wa konsonanti inayopatikana kwenye kivumishi kiashiria cha karibu kudondoshwa. Kwa hivyo,

kivumishi kama **ũjũ** [oɟo] (huyu) katika ngeli ya 1 kinadondosha konsonanti na kubaki kuwa **ũũ** [o:] (huyu) na kudumisha uamilifu wake. Udondoshaji wa konsonanti katika vivumishi hivi na vingine umeangaziwa katika sehemu ya michakato ya kifonolojia katika tasnifu hii. Konsonanti /j/ inayoondolewa inatokea baina ya irabu mbili. Udondoshaji kama huu unabainika katika konsonanti zingine zinazoangaziwa katika jedwali. Hata hivyo katika ngeli ya 7 (KĨ/GĨ) tungetarajia kupata kivumishi **gĩĩ** [ge:] (hiki) baada ya konsonanti kudondoshwa. Badala yake tunapata kivumishi **kĩĩ** [ke:] (hiki). Hali hii inaweza kuelezwa hivi, mofu {kĩ} na {gĩ} ni alomofu za mofimu moja ya kipatanishi. Kwa hivyo, mofu {kĩ} inaweza kutumika katika kuunda kivumishi **kĩkĩ** [keke] (hiki) ndiposa konsonanti inayopatikana baina ya irabu mbili inadondoshwa na tunabaki na **kĩĩ** [ke:] (hiki). Maelezo kama haya yanaweka wazi sababu ya kuwa na **kaa** [ka:] (kuonyesha udogo) badala ya **gaa** [ga:] katika ngeli ya 17. Aidha, ndiyo sababu tunapata **kũũ** [ko:] badala ya **gũgũ** [gogo] (huku) katika ngeli ya 22 (GU).

### 4.17 Usarufi Unaobainika katika Vivumishi vya Kiimenti

Kivumishi cha lahaja ya Kiimenti hubeba viambishi vyenye usarufi. Hata hivyo, hakibebi viambishi vingi vyenye uamilifu wa kisarufi kama kitenzi katika lahaja hiyo. Inaaminika kuwa kitenzi cha lahaja ya Kiimenti hubeba viambishi vingi vyenye usarufi kuliko kategoria nyingine za maneno ya Kiimenti kama vile vivumishi, vielezi, viwakilishi na nomino. Viambishi vinapotokea katika vivumishi huwa na usarufi fulani. Lahaja ya Kiimenti kama zilivyo lugha za Kibantu ni lugha ambishi. Kwa hivyo, mizizi ya vivumishi huwekwa viambishi ambavyo hupanua maana yake. Kwa jinsi hii kivumishi cha Kiimenti huweza kuainisha kazi nyingi za kisarufi. Hizi ni kipatanishi, ngeli ya sintaksia, nomino, ngeli ya mofolojia, idadi (umoja na wingi), ukubwa na udogo, mofu

jenzi, mofu kapa, mzizi wa kivumishi na irabu ya kipatanishi. Kivumishi kama **ũmũnoru** [omonɔru] (mnene) ni mfano wa kivumishi ambacho huwekwa viambishi awali viwili vyenye usarufi wake. Kinaweza kupatikana katika kirai nomino kama **muntũ ũmũnoru** [munto omonɔru] (mtu mnene). Kinaweza kuchanganuliwa kimofemiki hivi **ũ-mũ-noru** (mnene) na kudhihirisha mofimu mbalimbali. Mofu **{ũ-}** ya awali huweza kuainisha mofimu ya kipatanishi cha nomino, ngeli ya 2 (U) ya sintaksia na idadi. Mofu **{-Mũ-}** huwakilisha mofimu ya ngeli ya 1 (MU) ya mofolojia, nomino na idadi (umoja). Mofimu ya kuwakilisha mzizi ni **{-noru}** ambayo hubeba maana ya kivumishi. **Ũmunoru** **[**omonɔru] (mnene) ni mfano wa kivumishi ambacho kina mzizi unaowekwa viambishi awali vyenye usarufi. Kwa ujumla mofimu sita zimeainishwa katika kivumishi hicho. Hata hivyo, mofimu ya idadi imedhihirika katika mofu **{ũ}** na **{mũ}.** Kivumishi **ũmũnoru** (mnene) kinaweza kuchanganuliwa hivi:

**ũmũnoru** [omonɔru] /u-mu-noru/(mnene)

{ũ-} kipatanishi cha nomino/umoja/ngeli ya sintaksia ya 2 (U)

{-mũ-} mofu ya ngeli ya 1 (MU) (umoja) /nomino

{-noru} mzizi wa kivumishi

Kivumishi **ũmũnoru** [omonɔru] (mnene) huweza kuunda kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wannene) katika hali ya wingi. Kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) kikichanganuliwa kimofemiki kitadhihirisha usarufi kama unaopatikana katika kivumishi **ũmũnoru** [umunɔru] (mnono) lakini katika hali ya wingi kama hivi.

**babanoru [**βaβanɔru]/ba-ba-noru/(wanene)

{ba-} kipatanishi cha nomino/wingi/ngeli ya sintaksia ya 2.

{-ba-} kipatanishi cha nomino/wingi/ngeli ya sintaksia ya 2 (U)

{-noru} mzizi wa kivumishi

Katika lahaja ya Kiimenti kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) huweza kutumika kama **banoru** [βanɔru](wanene) kwa kudondosha mofu **{ba-}** ya kwanza. Kikichanganuliwa kitakuwa na mofu mbili ambazo ni **{ba}** na **{-noru}.** Usarufi katika mofu **{ba-}** ya kwanza na ya pili katika kivumishi **babanoru** (wanene) ni wa aina moja au unakaririwa. Kwa hivyo, hakuna haja ya mofu mbili za **{ba}** katika kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) kwa sababu zinawakilisha usarufi mmoja. Kauli hii ya kudondoshwa kwa mofu moja katika kivumishi kama hicho inaelezwa zaidi na Wa Mberia (1993) alipochunguza kivumishi cha Kitharaka. Anadai kuwa baadhi ya vivumishi kama vya sifa kama **babanoru** [βaβanɔru] (wanene); si lazima kuwa na mofu mbili ambazo zinafanana kiumbo zikiambishwa kama viambishi awali kwenye mzizi wa kivumishi. Anasema kuwa viambishi vyote viwili huweza kutumika au kimoja kudondoshwa. Anasisitiza kuwa katika kivumishi kama **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) mofu **{ba-}** ya kwanza siyo ya lazima. Kwa hivyo, inaweza kudondoshwa na usarufi wa kivumishi kutoathirika. Mwanalugha huyu hakueleza sababu za kutotumika kwa mofu **{ba}** mara mbili katika kivumishi kama **babanoru** [βaβanɔru] (wanene). Hata hivyo, kwa maoni yetu tumeeleza ni kwa sababu wa mofu hizo kuwakilisha usarufi mmoja. Kwa hivyo, **banoru** [βanɔru] (wanene) itakuwa na mofimu zifuatazo:

**banoru** [βanɔru] /ba-noru/ (wanene)

{ba-}   kipatanishi cha nomino/wingi/ngeli ya sintaksia ya 2 (U).

{-noru} mzizi wa kivumishi

Katika matumizi kwenye lahaja ya Kiimenti **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) na **banoru** [βanɔru] (wanene) huweza kutumika na kuwasilisha maana moja. Pia, huweza kutumika

kuvumisha nomino moja pasipo maana kuathirika kama **antũ babanoru** [anto βaβanɔru] (watu wanono) na **antũ banoru** [anto βanɔru] (watu wanene). Kwa kutumia **antũ babanoru** (watu wanene) au **antũ banoru** (watu wanene) maana inayojitokeza ni moja. Kwa hivyo, kivumishi kimoja kinaweza kutumika badala ya kingine. Hata kama vivumishi hivi viwili havitofautiani kimaana vinaweza kutofautiana kwa mambo fulani kama inavyobainika kutokana na mifano tuliyotoa. Kwanza, kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) kina mofu tatu ilhali **banoru** [βanɔru] (wanene) kina mofu mbili. Pili, kivumishi **babanoru** [βaβanɔru] (wanene) kina usarufi mwingi kuliko **banoru** [βanɔru] (wanene). Tatu, mchakato wa udondoshaji umeathiri kivumishi **banoru** [βanɔru] (wanene) lakini haukuathiri **babanoru** [βaβanɔru] (wanene).

Mifano mingine ya vivumishi ambavyo huweza kukabiliwa na udondoshaji wa mofu awali moja ili kupunguza uradidi wazo ni kama: **babakai** [βaβakai] (wachache), **babaingĩ** [βaβaiŋge] (wengi), **rũrũthũku** [roroθoku] (iliyo mbaya), **rũrũraja** [rororaɟa] (iliyo ndefu) na **bibithũku** [βiβiθoku] (vibaya). Ni vizuri kufahamu kuwa si wakati wote ambapo kivumishi cha Kiimenti kitadondosha mofu ambayo inarudiwarudiwa kama kiambishi awali. Kuna vivumishi vingine ambavyo havitaidondosha hiyo. Kwa hivyo, si hiari kwavyo kukosa kuitumia kama ilivyodokezwa na Wa Mberia (1993). Vivumishi vingine huihifadhi ili kukamilisha maana. Kwa mfano, kivumishi **bũbwingĩ** [βoβwiŋge] (wingi wa hali/kitu) katika kirai nomino **ũchinka bũbwingĩ** [uʧinka βoβwiŋge] ( ujinga mwingi) kina muundo wa ndani ambao ni **bũbũingi** [βoβoinge] (mwingi)/bũ-bũ-ingĩ. Muundo wake wa nje ni **bũbwingĩ** [βoβwiŋge] (mwingi) na hutumika katika maandishi na mazungumzo ya Kiimenti kikiwa hivyo. Ili kuunda **bũbwingĩ** [βoβwiŋge] (mwingi) irabu /ũ/ ya kiambishi kinachotangulia mzizi wa kivumishi inayeyushwa na kuwa /w/.

Mfano wa kivumishi ambao huwekwa kiambishi awali kimoja ni kama **ũmwe** (mmoja) katika kirai nomino **mwarimũ ũmwe** [mwarimo omwɛ] (mwalimu mmoja). Kinapochanganuliwa kimofemiki kitakuwa hivi **ũ-mwe** (mmoja). Mofu **{ũ-}** huwakilisha ngeli ya 1 (U) ya sintaksia, kipatanishi na idadi (umoja). Mofu **{-mwe}** huwakilisha mofimu ya mzizi wa kivumishi. Kwa hivyo, kivumishi **ũmwe** (mmoja) kimeainisha kazi nne za kisarufi ambazo hudhihirika hivi:

**ũmwe** [umwɛ] **/ũ-mwe/ (mmoja)**

{ũ-} mofimu ya ngeli ya sintaksia ya 1 (U) – (umoja)

kipatanishi cha nomino (umoja)

{-mwe} mzizi wa kivumishi

Mofimu ambazo zinapatikana katika kivumishi cha idadi dhahiri kama **ũmwe** [ũmwɛ] (mmoja) zinadhihirika katika vivumishi vya a-unganifu vya Kiimenti. Matumizi ya a - unganifu yanaweza kuonyeshwa katika virai nomino hivi: *Ngari* ***ya*** *mwarimũ* [ŋgari ja mwarimo] (Gari la mwalimu), *iratũ* ***bia*** *mũritwa* [irato βia moritwa] (viatu vya mwanafunzi) na *mũtĩ* ***jwa*** *nthitangi* [mote ɟwa nθitangi] (mpini wa jembe). Katika virai nomino hivyo, vivumishi vya a - unganifu ni kama **ya** [ja] (la), **bia** [βia] vya) na **jwa** [ɟwa] (wa). Kivumishi a - unganifu ni mfano wa kivumishi chenye mzizi wa sauti moja ambayo ni irabu /a/ inayoambishwa vipatanishi vya nomino katika ngeli mbalimbali. Kwa mfano, kivumishi **ya** [ja] (la) /y-a/ huchanganuliwa kimofemiki na kuonyesha mofimu zifuatazo:

**ya** [ja] **/y-a/(ya)**

{y-} mofimu ya ngeli ya 9 sintaksia ya (N) (umoja)

kipatanishi cha nomino (umoja)

{-a}		mzizi wa kivumishi

Kivumishi **jũjũ** [ɟoɟo](huu) katika kirai nomino kama **mũtĩ jũjũ** [mute ɟoɟo] (mti huu) ni mfano wa kivumishi ambacho mzizi huambishwa kiambishi awali na tamati. Kikichanganuliwa kimofemiki kitakuwa **jũ -j-ũ** (huu) na kudhihirisha mofu **{jũ-}, {-j-}** na **{-ũ}.** Mofu ya awali ni **{jũ-}** huwakilisha ngeli 3 (JŨ) ya sintaksia, kipatanishi na idadi (umoja). Mofu {**-j-}** ni mzizi ambao huambishwa mofu awali na tamati. Hatimaye {-i} ni irabu inayopatikana katika kipatanishi. Hali hii inaweza kubainishwa hivi:

**jũjũ** [ɟoɟo]/jũ-j-ũ / (huu)

{jũ -}	kipatanishi cha nomino/umoja

	kipatanishi cha ngeli 3 (JŨ) ya sintaksia/umoja

{-j-}	mzizi wa kitenzi

{-ũ}	irabu ya kipatanishi

Kivumishi **jũjũ** [ɟoɟo](huu) huweza kukabiliwa na mchakato wa udondoshaji wa konsonanti /j/ inayopatikana baina ya irabu /ũ / mbili na kubaki kuwa **jũũ** [ɟo:] (huu). Maana ya kivumishi hicho haibadiliki hata baada ya udondoshaji. Kikichanganuliwa kimofemiki kitadhihirisha mofimu zifuatazo.

**jũũ** [ɟo:]/jũ -ũ / (huu)

{jũ -}	kipatanishi cha nomino/umoja

	kianishi cha ngeli 3 ya sintaksia (Jũ) /umoja

{- ũ}	irabu ya kipatanishi

Kama ilivyobainika kivumishi **jũjũ** [ɟoɟo] (huu) kina mofu nyingi na usarufi mwingi kuliko jũũ [ɟo:] (huu) ambacho kimepatikana baada ya udondoshaji wa konsonanti.

Mifano zaidi ya vivumishi kama hivi ambavyo vimedondosha konsonanti na huainisha muundo na usarufi kama tulioangazia inaweza kupatikana katika tasnifu hii.

Lahaja ya Kiimenti huwa na nomino ambazo huweza kuvumisha nomino zingine. Mfano wa nomino hii ni kama **mũnene** [monɛnɛ] (mkubwa) katika kirai nomino **mwarimũ mũnene** [mwarimu monɛnɛ] (mwalimu mkubwa/hedimasta). Katika muktadha huu nomino **mũnene** [monɛnɛ] (mkubwa) ina uamilifu wa kivumishi ikifafanua nomino **mwarimũ** [mwarimo] (mwalimu). Ikichanganuliwa kimofemiki itakuwa na mofu mbili ambazo ni **{mũ-}** na **{-nene}.** Mofu **{mũ-}** huwakilisha mofimu ya ngeli ya 1 mofolojia ya (MU/MŨ MW)/ (umoja) na mzizi wa kivumishi ambao ni **{-nene}.** Kwa hivyo, mofimu tatu zimejitokeza katika nomino hiyo. **Mũnene** [monɛnɛ] (mkubwa) ni mfano wa kivumishi ambacho huwekwa kiambishi awali cha ngeli pekee bila kuhusisha kipatanishi kama vivumishi vingi vya Kiimenti.

Mofu kapa huweza kutumika katika kuainisha mofimu katika kivumishi cha Kiimenti. Mofu hii huweza kutumika katika uchanganuzi wa kisarufi hasa pale hakuna maumbo dhahiri katika kivumishi husika. Mfano wa vivumishi ambapo mofu kapa hutumika kuainisha usarufi ni katika vivumishi vya mkopo. Hivi ni vile ambavyo lahaja ya Kiimenti imekopa kutoka lugha nyingine. Mfano wa vivumishi hivi ni kama **atarĩ** [atare] (hatari) katika kirai nomino **muntũ atarĩ [**munto atare] (hatari). **Atarĩ** [atare] (hatari) ni kivumishi cha mkopo kinachofafanua nomino **muntũ** (mtu). Kivumishi hiki huweza kuchanganuliwa hivi ili kubainisha mofimu zake. **Atarĩ** [atare] (hatari) /ø-atari/. Hapa mofu kapa **{ø}** huwakilisha mofimu ya ngeli ya mofolojia na idadi (umoja). Mofu **{-atarĩ}** huwakilisha mofimu ya mzizi wa kivumishi. Hali hii inaweza kuwasilishwa hivi hapa chini. Aidha, kuna mifano zaidi ya kuweka wazi mawazo haya kwa kutumia mifano ya

vivumishi vifuatayvo kama, **kenda** [kɛnda] (kenda, tisa), **tafauti/tofauti** [tafauti/tɔfauti] (tofauti) na **maritati** [maritati] (maridadi) ambayo imechanganuliwa hapa chini. Etimolojia ya vivumishi vyote vilivyochanganuliwa hapa chini ni lugha ya Kiarabu (BAKITA, 2015). Vivumishi husika vilikopwa na lugha ya Kiswahili halafu lahaja ya Kiimenti ikavikopa kutoka kwa Kiswahili.

**atarĩ** [atare]/ø-atarĩ/ (hatari)

{ø} mofu kapa inayowakilisha mofimu ya ngeli ya mofolojia.

kiainishi cha idadi (umoja).

{-atarĩ} mzizi wa kivumishi mkopo

**maritati** [maritati] (maridadi)/ø-maridadi/

{ø} mofu kapa inayowakilisha mofimu ya ngeli ya mofolojia.

Kiainishi cha idadi (umoja).

{-maridadi} mzizi wa kivumishi mkopo

**kenda** [kɛnda] /ø-kenda/ (kenda, tisa)

{ø} mofu kapa inayowakilisha mofimu ya ngeli ya mofolojia.

Kiwakilishi cha idadi (umoja).

{-kenda} mzizi wa kivumishi mkopo

mofu inayowakilisha idadi (umoja).

Ni vizuri kufahamu kuwa vivumishi vya mkopo tulivyochanganua hapo juu havitabadilisha umbo vikivumisha nomino za Kiimenti katika umoja au wingi katika ngeli mbalimbali. Hata hivyo, kivumishi cha idadi **kenda** [kɛnda] (tisa, kenda) huweza kutumika kuvumisha nomino katika wingi pekee kama: **antũ kenda** [anto kɛnda] (watu

tisa), **itĩ kenda** [ite kɛnda] (viti tisa), **ngarĩ kenda** [ŋgare kɛnda] (magari tisa) na **mĩkebe kenda** [mekɛβɛ kɛnda] (mikebe tisa).

Mofu jenzi huweza kujitokeza katika vivumishi vya Kiimenti. Hii ni mofu ambayo haina usarufi lakini husaidia uchanganuzi wa maneno. Baadhi ya vivumishi vilivyoainisha mofu hii ni vile vya pekee vinavyoundwa kutokana na mizizi kama –**nthe** [-nθɛ] (-ote) na –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe). Vivumishi hivi ni kama **rĩonthe** [reɔnθɛ] (lote), **bionthe** [βiɔnθɛ] (vyote), **kĩonthe** [keɔnθɛ] (chote), **chionthe** [ʧiɔnθɛ] (zote), **rĩongwa** [reɔŋgwa] (lenyewe), **biongwa** [βiɔŋgwa] (vyenyewe), **kĩongwa** [keɔŋgwa] (chenyewe) na **chiongwa** [ʧiɔŋgwa] (zenyewe). Kwa mfano, kivumishi **rĩonthe** [reɔnθɛ] (lote) katika kirai nomino **ĩrinda rĩonthe** [erinda reɔnθɛ] (linda lote); kikichanganulia kimofemiki hudhihirisha mofu tatu ambazo ni **{rĩ}, {o}**na **{-nthe}.** Mofu **{rĩ}** huwakilisha mofimu za kipatanishi, ngeli ya 5 ya sintaksia (**RĨ**) katika umoja. Mofu **{o}** ni mofu jenzi ambayo husaidia uchanganuzi wa kivumishi hicho na haiwakilishi usarufi wowote. **{-nthe}** ni mzizi wa kivumishi ambao huwakilisha maana ya kileksia. Uchanganuzi kimofemiki wa kivumishi **rĩonthe** [reɔnθɛ] (lote) unaweza kudhihirishwa hapa chini ili kuweka hali hiyo wazi zaidi.

**rĩonthe** [reɔnθɛ] /rĩ-o-nthe (lote)

| | |
|---|---|
| {rĩ-} | kipatanishi cha nomino (umoja) |
| | Mofimu ya ngeli ya 5 ya sintaksia (RĨ) /umoja |
| {-o-} | mofu jenzi |
| {-nthe} | mzizi wa kivumishi |

Vivumishi vya Kiimenti huwa na mofu mseto. Hii ni mofu ambayo ina zaidi ya kazi moja ya kisarufi. Tumeona kutokana na mifano ya vivumishi **ũmũnoru** [omonɔru] (mnono),

**ũmwe** [umwɛ] (mmoja), **jũjũ** (huu) na **mũnene** [monɛnɛ] (mkubwa) viambishi awali huwa na zaidi ya kazi moja ya kisarufi.

Aidha, imebainika kuwa kivumishi cha Kiimenti kikichanganuliwa kimofemiki kitadhihirisha mofimu ya ngeli ya mofolojia na sintaksia katika kivumishi kimoja. Mfano kama huu ulipatikana tulipochanganua **ũmũnoru** [omonɔru] (mnono). Hata hivyo, kivumishi kama **jũjũ** [ɟuɟu](huu) kinadhihirisha tu mofimu ya ngeli ya sintaksia. Kwa hali nyingine kivumishi **mũnene** [munɛnɛ] (mkubwa) kinaainisha mofimu ya ngeli ya mofolojia pekee pamoja na mzizi. Kwa hivyo, kuna vivumishi vya Kiimenti ambavyo huainisha ngeli za Kiimenti za mofolojia na sintaksia pamoja. Vingine huainisha ngeli ya sintaksia pekee. Aidha, usarufi hutofautiana katika vivumishi mbalimbali. Kwa mfano, tumedhihirisha kuwa kivumishi **ũmũnoru** [omonɔru] (mnono) huainisha kazi sita za kisarufi ilhali katika kivumishi **ũmwe** [omwɛ] (mmoja) huonyesha mofimu nne, **jũjũ** [ɟoɟo] (huu) tano na **mũnene** [monɛnɛ] (mkubwa) tatu. Kwa hivyo, jinsi kivumishi kilivyo na viambishi vingi ndivyo kinaweza kuwa na kazi nyingi za kisarufi.

Suala la alomofu hujitokeza katika lahaja ya Kiimenti. Kwa hivyo, viambishi awali vya nomino mbalimbali huweza kudhihirisha alomofu mbalimbali. Hali hii hudhihirika hata katika ngeli mbalimbali. Kwa mfano, ngeli ya 1 huainishwa na alomofu /mu/mũ na /mw/ katika umoja. Aidha, ngeli ya 7 na 8 umoja huanishwa kwa kutumia alomofu /kĩ/ na /gĩ/ ilhali wingi huainishwa kutumia alomofu / i/ na /bi/. Inafaa ieleweke kuwa viambishi vya ngeli na nomino huathiri muundo wa kivumishi cha Kiimenti. Hata hivyo, ualomofu wa viambishi vya ngeli na nomino hauonekani katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa hivyo, nomino **kĩbanga** [keβaŋga] (panga) na **gĩtĩ** [gete] (kiti) huweza kuvumishwa na kivumishi **gĩkĩthongi** [gekeθɔŋgi] (kizuri) na kuwa na kirai nomino kama **kĩbanga gĩkĩthongi**

[kiβaŋga gekeθɔŋgi] (panga zuri) na **gĩtĩ gĩkĩthongi** [giti gekeθɔŋgi] (kiti kizuri). Kivumishi **gĩkĩthongi** [gekeθɔŋgi] (kizuri) hakionyeshi ualomofu licha ya hali hiyo kujitokeza katika ngeli ya KĨ /GĨ – I/BI (umoja).

### 4.18 Ruwaza ya Mofimu katika Vivumishi vya Kiimenti

Usarufi unaoainishwa katika vivumishi vya Kiimenti huzingatia ruwaza maalumu. Kila mofimu ina nafasi yake katika kivumishi husika. Kwa mfano, imebainika kuwa nafasi ya kwanza hukaliwa na mofimu ya kipatanishi kimoja au viwili. Kiambishi ngeli (KiN) au mofu jenzi (Mj) hufuata kipatanishi na mzizi (Mz) wa kivumishi huchukua nafasi ya tatu. Ni vizuri kufahamu kuwa kipatanishi ni kiambishi cha ngeli za sintaksia na kiambishi ngeli ni kiainishi cha ngeli za mofolojia. Hii ina maana kuwa kivumishi kikiwa na muundo wa kiambishi cha ngeli ya sintaksia na ile ya mofolojia, basi mofimu ya ngeli ya sintaksia hutangulia ile ya mofolojia. Hata hivyo, vivumishi kama vya majina havina vipatanishi. Kwa hivyo, kiambishi ngeli hutangulia mzizi wa kivumishi. Katika nafasi ya nne kunapatikana irabu ya kipatanishi (I-Kip). Kwa ujumla, ruwaza zifuatazo za mofimu hubainika katika vivumishi vya Kiimenti.

i. Ruwaza ya mofimu mbili za kipatanishi na kisha mzizi wa kivumishi (Kip + Kip + Mz) katika vivumishi kama **bibithũku** [βiβiθoku] /bi-bi-thũku (vibaya), **bibiega** [βiβiɛga] ]/bi-bi-ega (vizuri), **babakũrũ** [βaβakoro]/ba-ba-kũrũ/ (waliozeeka), **babakai** [βaβakai] /ba-ba-kai/ (wachache) na **bibiraja** [βiβiraɟa] /bi-bi-raja (virefu). Kivumishi **bibithũku** [βiβiθoku] (vibaya) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kudhihirisha ruwaza ya Kip + Kip + Mz.

**bibithũku** [βiβiθoku] /bi-bi-thũku/ (vibaya)

{bi-} mofimu ya ngeli ya sintaksia ya 8 (I/BI)

kipatanishi cha ngeli ya sintaksia ya 8 (I/BI)

idadi (wingi)

{bi-} mofimu ya ngeli ya sintaksia ya 8 (I/BI)

kipatanishi cha ngeli ya sintaksia ya 8 (I/BI)

idadi (umoja)

{-thũku} mzizi wa kivumishi

ii. Ruwaza ya mofimu ya kipatanishi, kiambishi ngeli na mzizi wa kivumishi (Kip + KiN + Mz) hupatikana katika vivumishi kama **ũmũraja** [omoraɟa] /ũ-mũ-raja/ (mrefu), **ũmũthũku** [omoθoku] / ũ-mũ-thũku/ (mbaya), **kĩgĩkũrũ** [kegekoro] /kĩ-gĩ-kũrũ (kizee), **jũmũthongi** [ɟomoθɔ ŋgi] /jũ-mũ-thongi/ (unaopendeza) na **inkai** [inkai] /i-n-kai/ (chache). Kivumishi ũmũraja [omoraɟa] /ũ -mũ -raja/ (mrefu) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kudhihirisha ruwaza ya Kip + KiN + Mz.

**ũmũraja** [omoraɟa] /ũ -mũ -raja/ (mrefu)

{ũ -} mofimu ya ngeli ya sintaksia ya 1 (U)

kipatanishi cha ngeli ya sintaksia ya 1 (U)

idadi (umoja)

{-mũ -} mofimu ya ngeli ya mofolojia ya 1 (MU/MŨ/MW)

Kiambishi awali cha majina ya ngeli ya mofolojia ya 1 (MU/MŨ/MW)

idadi (umoja)

{-raja} mzizi wa kivumishi

iii. Ruwaza ya mofimu ya kipatanishi na mzizi wa kivumishi (Kip + Mz) katika vivumishi **ũmwe [**omwɛ] /ũ-mwe/ (mmoja), **bakai [**βakai] /ba-kai (wachache), **batano** [βatanɔ] /ba-tano/ (watano), **ũrĩa** [orea] /ũ -rĩa/ (yule) na **batantatũ [**βatantato] /ba-tantatũ/ (sita).

Kivumishi **bakai** [βakai] /ba-kai/ (wachache) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kudhihirisha ruwaza ya Kip + Mz.

**bakai [**βakai] /ba-kai/ (wachache)

| | |
|---|---|
| {ba-} | mofimu ya ngeli ya sintaksia ya 2 (A) |
| | kipatanishi cha ngeli ya sintaksia ya 2 (A) |
| | Idadi (wingi) |
| {-kai} | mzizi wa kivumishi |

iv. Ruwaza ya mofimu ya ngeli na mzizi wa kivumishi (KiN + Mz). Ruwaza kama hii hubainika katika majina ambayo hutumika kuvumisha nomino mbalimbali. Kwa mfano, **ntũrũtũ** [ntoroto] /n-tũrũtũ/ (msumbufu), **mũthao** [moθaɔ] /mu-thao/ (mvivu), **mwamba** [mwamβa] /mw-amba/ (mwizi) na **nka** [aka] /n-ka/ (jike). Kivumishi **mũthao** [moθaɔ] /mu-thao/ (mvivu) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kubainisha ruwaza ya KiN + Mz.

**mũthao** [muθaɔ] /mu-thao/ (mvivu)

| | |
|---|---|
| {mũ -} | mofimu ya ngeli ya 1 ya mofolojia (MU/ MŨ /MW) |
| | kiambishi awali cha nomino inayovumishwa katika ngeli (MU/ MŨ /MW) |
| | idadi (umoja) |
| {-thao} | mzizi wa kivumishi |

Mofu kapa (ø) hutumika kuainisha mofimu ya ngeli katika vivumishi vya kukopa kama **atarĩ** [atare] /ø-atarĩ/ (hatari), **cawacawa** [cawacawa] /ø-cawacawa/ (sawasawa) na **maritati**/ [maritati] /ø-maritati/ (maridadi) ambavyo vimeingia katika Kiimenti. Kivumishi **atarĩ** [atare] (hatari) kinaweza kuunda kirai nomino kama **muntũ atarĩ**

[munto atare] (mtu hatari). Katika hali hii kivumishi **atarĩ** [atare] (hatari) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kubainisha ruwaza ya KiN+ Mz.

**atarĩ** [atare] /ø-atari/ (hatari)

{ø-} mofimu ya ngeli ya 1 ya mofolojia (MU/ MŨ/MW)

kiambishi awali cha nomino inayovumishwa katika ngeli (MU/ MŨ /MW)

idadi (umoja)

{-atarĩ } mzizi wa kivumishi

v. Ruwaza ya mofimu ya kipatanishi, mzizi wa kivumishi na irabu ya kipatanishi (Kip + Mz + I – Kip). Mfano wa vivumishi vyenye ruwaza hii ya mofimu ni kama **ũjũ** /ũ-j-ũ / (huyu), **iji**/i-j-i (hizi), **aja** [aɟa] /a-j-a/ (hapa) na **jũjũ [**ɟoɟo] /jũ -j- ũ/ (huu). Kivumishi **jũjũ [**ɟoɟo] /jũ-j-ũ / (huu) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kuonyesha ruwaza ya Kip + Mz + I - (Kip) kama ifuatavyo.

**jũjũ [**ɟoɟo] /jũ -j- ũ/ (huu)

{jũ -} kipatanishi cha nomino/umoja

kianishi cha ngeli ya sintaksia ya 3 (JU)

mofimu ya idadi (umoja)

{-j-} mzizi wa kitenzi

{-ũ} irabu ya kipatanishi

vi. Ruwaza ya kipatanishi, mofu jenzi na mzizi (Kip + Mj + Mz) inabainika katika vivumishi kama **bionka** [βiɔnka] /bi-o-nka (vilivyo pekee), **kĩongwa** [keɔŋgwa] /ki-o-ngwa/ (chenyewe), **rĩonthe** [reɔnθɛ] /ri-o-nthe (lote), **bionthe** [βiɔnθɛ] /bi-o-nthe/ (vyote) na **chionthe** [ʧiɔnθɛ]/ chi-o-nthe/ (zote). Kivumishi kama **rĩonthe** [reɔnθɛ] /ri-o-nthe (lote) kikichanganuliwa kimofemiki kinaweza kuonyesha ruwaza ya Kip + Mj + Mz.

**rĩonthe** [reɔnθɛ] /ri-o-nthe (lote)

{rĩ -} kipatanishi cha nomino

Kianishi cha ngeli ya sintaksia ya 5 (Ĩ/RĨ)

Mofimu ya idadi (umoja)

{-o-} mofu jenzi

{-nthe} mzizi wa kitenzi

Ruwaza sita zinazobainika zinaweza kuwakilishwa kutumia alama zifuatazo.

i.Kip + Kip + Mz

ii. Kip + KiN + Mz

iii.Kip + Mz

iv.KiN +Mz

v. Kip + Mz + I – Kip

vi. Kip + Mj + Mz

Jedwali la 28 linaweza kutumika kutoa muhtasari wa ruwaza za mpangilio wa mofimu katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti.

**Jedwali la 28: Muhtasari wa Ruwaza za Mofimu katika Vivumishi vya Kiimenti**

| Viambishi Awali | | | | Mzizi | Viambishi Tamati |
|---|---|---|---|---|---|
| Kip | Kip | KiN | Mj | | I - Kip |
| bi- | -bi- | - | - | -thukũ | - |
| bi- | -bi | - | - | -ega | - |
| - | ũ - | -mũ - | - | -raja | - |
| - | kĩ- | -gĩ- | - | -kũrũ | - |
| - | ba- | - | - | -kai | - |
| - | ba- | - | - | -tano | - |
| - | ũ- | - | - | -ria | - |
| - | - | mũ - | - | -thao | - |
| - | - | n- | - | -tũrũtũ | - |
| - | - | ø- | - | -atari | - |
| - | - | ø- | - | -maritati | - |
| - | ũ- | - | - | -j- | -ũ |
| - | i- | - | - | -j- | -i |
| - | a- | - | - | -j- | -a |
| - | jũ- | - | - | -j- | -ũ |
| - | bi- | - | -o- | -nka | - |
| - | kĩ- | - | -o- | -ngwa | - |

Asili: Data ya  Nyanjani (2022)

## 4.19 Hitimisho

Kwa kifupi sura hii imejikita katika vivumishi mbalimbali vya Kiimenti vilivyobainika katika uchunguzi uliofanyika. Uainishaji wa vivumishi husika huku muundo mahsusi wa kila aina ya kivumishi ukielezwa. Pia, utendakazi wa mofimu katika vivumishi mbalimbali na ruwaza za mofimu husika umeelezwa.

# SURA YA TANO

## MICHAKATO YA KIFONOLOJIA, MOFOLOJIA NA RUWAZA ZA VIVUMISHI KATIKA TUNGO ZA KIIMENTI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii imeangazia michakato ya kifonolojia ambayo huathiri fonimu za konsonanti na irabu katika muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Hata hivyo, michakato ya kifonolojia haitoshi kueleza muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa hivyo, mchakato wa uradidi umeangaziwa ili kukamilsha kueleza muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Hii ni kutokana na hali kwamba uradidi huchangia muundo wa vivumishi vya lahaja hiyo.

### 5.2 Michakato ya Kifonolojia inayoathiri Vivumishi vya Kiimenti

Muundo wa kivumishi cha Kiimenti hauwezi kukamilika bila ya kuangazia baadhi ya michakato ya kifonolojia inayoathiri kategoria hii ya maneno. Kwa mujibu wa Kihore na Wenzie (wataje) mifanyiko ya kifonolojia ni mabadiliko yanayotokea wakati sauti mbalimbali zinapokabiliana katika neno au maneno. Kwa maoni yao, mabadiliko hayo hayatokei kiholela bali huongozwa na kanuni fulani za kifonolojia. Kanuni hizi ni udondoshaji, uyeyushaji, muungano wa sauti, nazali kuathiri konsonanti, konsonanti kuathiri nazali na tangamano la irabu. Wanaendelea kusema kuwa hata kama kanuni hizi hufanya kazi katika mazingira mengi, kuna vighairi vyake. Yaani kuna maneno yanayoenda kinyume cha kanuni hizi. Wanakiri kuwa hii ni kawaida kwa lugha za ulimwengu. Suala la mabadiliko ya kifonolojia limeangaziwa pia na Habwe na Karanja (wataje). Wameainisha michakato inayoathiri konsonanti kama udhoofikaji, uimarikaji, udondoshaji, uchopekaji na ukaakaishaji wake. Wanaendelea kujadili michakato inayoathiri vokali kama uwiano wake, kuungana au kufupishwa kwa vokali,

kudondoshwa na uyeyushaji. Kwa upande mwingine Mgullu (1999) amejadili mikondo saba ya kifonolojia. Hii ni pamoja na uimarikaji wa fonimu, kudhoofika kwake, ukaakaishaji, usilimisho pamwe na nazali, mvutano wa irabu, tangamano la irabu na udondoshaji wake.

Nia ya kuangazia michakato hii ni kwa sababu ilisaidia kutoa mwangaza kuhusu michakato ya kifonolojia inayopatikana katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Kwa hivyo, michakato iliyojadiliwa ni ile iliyopatikana katika muundo wa vivumishi vya lahaja ya Kiimenti. Hii ni uimarikaji wa fonimu, udondoshaji wa irabu, uyeyushaji wa vokali na muungano wa vokali au sauti.

### 5.2.1 Uyeyushaji

Mchakato wa uyeyushaji hutokea wakati wa kuunda baadhi ya vivumishi vya sifa. Kwa mujibu wa Mwaliwa (mtaje), uyeyushaji hutokea panapotokea mkururo wa irabu na kunatokea haja ya kuuvunja ili kupata muundo wa silabi unaopendelewa, na hivyo kurahisisha matamshi. Muundo wa silabi za KVV unazua utata katika kutamka. Kwa hivyo, kunatokea uyeyushaji ambao utakuwa na muundo KYV, ambao ni rahisi kutamka. Maneno kama **jũmwirũ** [ɟomwiro] (mweusi)**, ũmwerũ [**omwɛro] (mpya)**, jũmwega [**ɟomwɛru] (mzuri) na **ũmwega [**omwɛga] (mzuri) ni vivumishi vya sifa vya Kiimenti ambavyo vinadhihirisha mchakato wa uyeyushaji vinapoundwa. Kihore na Wenzie (wataje) wanasema kuwa uyeyushaji ni mchakato unaotokea katika lugha zote za Kibantu. Kwa hivyo, hali hiyo inajitokeza kwa Kiimenti, kikiwa mojawapo ya lahaja za Kimeru ambayo ni lugha ya Kibantu. Ili kuweza kuelewa kanuni ya uyeyushaji katika vivumishi hivi, ni vizuri kuainisha umbo la nje na la ndani. Mifano hii inadhihirisha

mfuatano wa irabu katika muundo wa ndani wa vivumishi. Mifano hii inaweza kudhihirisha hali hii.

| Umbo la ndani | Umbo la nje | Maana |
|---|---|---|
| jũ +mũ +irũ | [ɟomwiro] | mweusi |
| ũ + mũ + ĩthĩ | [omweθe] | mbichi |
| ũ +mũ + irũ | [omwiro] | mweusi |
| bũ + bũ + irũ | [βoβwiro] | ulio mweusi |
| jũ +mũ+ingĩ | [ɟomwiŋge] | mwingi |
| rũ + rũ + irũ | [rorwiro] | nyeusi |
| tũ +tũ+ingĩ | [totwiŋge] | vilivyo vingi |
| bũ +bũ +ingĩ | [βoβwiŋge] | ulio mwingi |
| gũ+kũ+ingĩ | [gokwiŋge] | kwingi |
| gũ + kũ + irũ | [gokwiro] | kweusi |

Kutokana na mifano hii, irabu **o** ikifuatwa na na /**i**/ kwenye mzizi wa kivumishi hubadilika na kuwa /**w**/. Hivyo, /o /+/i/ / → w.

Sheria inayohusika katika mabadiliko haya ni:

/ũ / → /w/ / _ I au

/ũ / → /w/ / -V (isiyo / ũ /)

Matumizi ya sheria zinazotumia ishara kama hapo juu ni muhimu kwa sababu husaidia kupatikana kwa iktisadi katika lugha. Aidha, husaidia kuepuka utata ambao unaweza kuhusishwa na maelezo mengi. Watumiaji wa lugha hufahamu sheria hizi na huzihifadhi katika bongo zao (Habwe na Karanja, wataje).

Katika hali nyingine irabu /o/ hubadilika na kuwa /w/ ikitangulia irabu /ɛ/ ya mzizi wa kivumishi. Mifano ifuatayo inashadidia hali hii.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| jũ +mũ +ega | [ɟomwɛga] | mzuri |
| ũ +mũ +ega | [omwɛga] | mzuri |
| ũ +mũ+erũ | [omwɛro] | mweupe |
| jũ +enu | [ɟwɛnu] | wenu |
| bũ +etũ | [βwɛto] | wetu |
| jũ +enu | [ɟwɛnu] | wenu |
| gũ + etũ | [gweto] | kwetu |
| kũ+enu | [kwɛnu] | kwenu |
| jũ +etũ | [ɟwɛto] | jwenu |

Hivyo, /o /+/ɛ/ → /w/. Sheria inayohusika katika mabadiliko haya ni:

/o/ → /w/ / -V)

Hii inamaanisha kuwa vokali /o / hubadilika na kuwa nusu irabu /w/ ikiwa itatokea katika mazingira ya kutangulia vokali /ɛ/.

Aidha, irabu /o/ hubadilika na kuwa /w/ ikitokea katika mazingira ya kutangulia irabu /a/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| **Umbo la ndani** | **Umbo la nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| jũ + akwa | [ɟwakwa] | wangu |
| jũ+awe | [ɟwawɛ] | wake |
| jũ +ao | [ɟwaɔ] | wao |

| | | |
|---|---|---|
| rũ +ao | [rwaɔ] | ulio wao |
| bũ +awe | [βwawɛ] | ulio wake |
| kũ + awe | [kwawɛ] | kwake |
| kũ + ao | [kwaɔ] | kwao |
| jũ +aku | [ɟwaku] | wako |
| gũ + akwa | [gwakwa] | kwangu |

Kutokana na mifano iliyopo hapo juu /o/+/a/ → /w/. Sheria inayohusika katika mabadiliko haya ni: /o/ → /w/ / -V)

Hii inamaanisha kuwa vokali /o/ hubadilika na kuwa nusu irabu /w/ ikiwa itatokea katika mazingira ambapo haikutangulia vokali /ũ/ yenyewe.

Sheria inayohusika katika mabadiliko haya ni:

/o/ → /w/ / _ I au

/o/ → /w/ / -V (isiyo o)

Hii inamaanisha kuwa vokali /o/ hubadilika na kuwa nusu irabu /w/ ikiwa itatokea katika mazingira ambapo haikutangulia vokali /o/ yenyewe.

Katika hali nyingine irabu /o/ huyeyushwa na kuwa /w/ ikipatikana katika mazingira ya kutangulia irabu /ɔ/ katika mizizi ya kivumishi. Hata hivyo, si vivumishi vingi vya Kiimenti ambavyo huonyesha mchakato huu. Baadhi ya mifano hii ni kama ifuatayo.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ũ+ mũ + oru | [omwɔru] | aliyeoza |
| jũ + mũ + oro | [ɟomwɔrɔ] | ulio laini |
| ũ + mũ + oro | [omwɔrɔ] | aliye laini |

| | | |
|---|---|---|
| jũ + mũ + oru | [ɟomwɔru] | uliooza |
| tũ + tũ + oru | [totwɔru] | enye uozo |
| tũ + tũ+ oro | [totwɔrɔ] | enye ulaini |

Pia, irabu /**i/** kwenye kipatanishi huyeyushwa na kuwa irabu /**y/** ikifuatwa na irabu /**a/** katika mzizi wa kivumishi**.** Vivumishi vimilikishi katika nafsi zote tatu (umoja na wingi) huonyesha mchakato wa uyeyushaji. Kwa hivyo, /i/+/a/ ⟶ /j/. Hali hii inaweza kupatikana katika mifano ya vivumishi vya kumiliki vya lahaja ya Kiimenti vifuatayo.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** |
|---|---|
| i+awe | [jawɛ] |
| i+ao | [jaɔ] |
| i+aku | [jaku] |
| i+akwa | [jakwa] |

Inawezekana pia irabu /**i/** kwenye kipatanishi kuyeyushwa na kuwa irabu /**y/** ikifuatwa na irabu /ɛ/ katika mzizi wa kivumishi**.** Vivumishi vimilikishi katika nafsi zote tatu (umoja na wingi) huonyesha mchakato wa uyeyushaji. Kwa hivyo, / i/+/ɛ/ ⟶ /j/.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** |
|---|---|
| i+enu | [jɛnu] |
| i+etũ | [jɛto] |

Sheria zinazohusika katika mabadiliko haya ni:

/i/ ⟶ /j/ / —— V (iliyo /a/)

/i/ ⟶ /j/ / ——V (iliyo /ɛ/)

/Au /i/ ⟶ /j/ / — I

Mchakato zaidi wa uyeyushaji unahusu irabu /a/ kuyeyushwa na kuwa nusu irabu /w/ ikitangulia nyenzake au irabu /ɛ/. Hali hizi zinabainika katika mifano ifuatayo.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| a+aku | [waku] | wako |
| a+akwa | [wakwa] | wangu |
| a+awe | [wawɛ] | wake |
| a+ao | [waɔ] | wao |
| a+etũ | [wɛto] | wetu |
| a+enu | [wɛnu] | wenu |

Mifano hii inadhihirisha kuwa /a/+/a/ → /w/ na /a /+/ ɛ/ → /w/. Sheria inayohusika katika mabadiliko haya ni:

/a/ → /w/ / — V (iliyo /a/, /ɛ/)

Hii inamaanisha kuwa vokali /a/ hubadilika na kuwa nusu irabu /w/ ikiwa itatokea katika mazingira ambapo itatangulia vokali /a/ na yenyewe.

**5.2.2 Uimarikaji wa Fonimu**

Vilevile, vivumishi vya sifa vinapoundwa mchakato wa uimarikaji wa fonimu hutokea, na unahusu kuimarika kwa konsonanti na si irabu. Mchakato huu unapatikana wakati wa kuunda kivumishi **indaja** [indaɟa] (ndefu). Kivumishi hiki kinaundwa kwa kutumia mofu hizi: i + **n** + r**aja** → **indaja**. Kinapoundwa kimadende /r/ kinabadilika na kuwa kizuiwa ghuna /d/. Kwa hivyo kinaimarika. Hii ndiyo sababu kivumishi kinachopatikana kinakuwa **indaja** badala ya **inraja**. Mfanyiko unaopatikana unaitwa uimarikaji wa fonimu kwa sababu kitamkwa /r/ kiko ngazi ya 14 na kitamkwa /d/ ngazi

ya 4. Ngazi inayorejelewa hapa ni mpangilio wa vitamkwa kulingana na nguvu inayohitajika kuvitamka. Kwa hivyo, jinsi kitamkwa kilivyo ngazi ya juu ndivyo kinahitaji nguvu nyingi kukitamka. Vitamkwa vimepangwa kutoka vinavyohitaji nguvu sana kutamka hadi vinavyohitaji nguvu kidogo (Mgullu, 1999). Mchakato huu wa uimarikajai hutokea ili kurahisisha matamshi (Munguti, mtaje).

Uimarikaji wa kimadende /r/ na kuwa kizuiwa ghuna /d/ unaweza kuelezwa na sheria hii:

[r] ⟶ [d] / /n/ -

**5.2.3 Usilimisho Nyuma**

Usilimisho nyuma ni hali ambapo kitamkwa kilicho mbele huathiri chenziwe kilicho nyuma ili vyote pamoja viweze kuafikiana katika utamkaji (Mukuthuria, 1997). Ufafanuzi zaidi kuhusu usilimisho nyuma umetolewa na Kihore na Wenzie (wataje). Wanasema kuwa mchakato wa usilimisho nyuma ni kanuni ya konsonanti kuathiri nazali. Wanaendelea kusema kuwa katika lugha za Kibantu nazali huathiriwa na konsonanti inayoifuata. Katika hali hii nazali huathiriwa na konsonanti inayoiandama na kulazimika kutamkiwa mahali pa konsonanti. Hii ndiyo sababu Kihore na Wenzie (wataje) wanasema nazali imeathiriwa na konsonanti. Curr (mtaje) anaeleza kuwa katika usilimisho tulioangazia, sauti ya nazali hutamkiwa mahali pa sauti ya kipasuo, kikwamizwa au kizuiwa kwamizwa ambayo inaifuata. Mchakato wa usilimisho anaueleza kama wa kifonetiki unaohusiana na sheria za kifonetiki zilizoelezwa katika nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Mfano tuliotoa hapo juu wa kuimarika kwa fonimu unaweza kufaa hapa. Kivumishi cha sifa **indaja** [indaɟa] (ndefu) kimetokana na uimarikaji wa fonimu /r/ ndipo tukapata fonimu /d/. Hivyo, tukapata **indaja** [indaɟa] (ndefu) badala ya **inraja.** Kivumishi **indaja** [indaɟa] (ndefu) kinaweza pia kudhihirisha hali ya usilimisho nyuma. Hii ni kwa

sababu nazali /n/ hutamkiwa mahali pa kutamkia konsonanti /d/ katika mazingira ya kivumishi **indaja** [indaɟa] (**ndefu**). Maelezo haya yanaafiki kauli tuliyoangazia ya Mukuthuria (1997) hapo juu. Sheria hii inaweza kutumika kueleza mabadiliko hayo.

N → [n] / __ d

Mifano ifuatayo inashadidia usilimisho nyuma katika vivumishi vya Kiimenti.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ĩ + n + ĩthi | [emβeθi] | mbichi |

Mfano mwingine wa usilimisho nyuma unahusu kivumishi **ĩmbĩthĩ** [emβeθe] (mbichi) nazali /m/ inatamkiwa mahali pa konsonanti /b/. Sheria hii inaweza kutumika kuelezea hali hiyo:

N → [m] / __ b

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ĩ + n + jerũ | [enɟɛro] | nyeupe |
| ĩ + n + jirũ | [enɟiro] | nyeusi |
| ĩ + n + jega | [enɟɛga] | nzuri |

Aidha, katika vivumishi vingine vya sifa kama **ĩnjirũ [**enɟiro] (nyeusi), **injerũ [**enɟɛro] (nyeupe) na **ĩnjega [**enɟɛga] (nzuri) vilivyoonyeshwa hapo juu, nazali /n/ ya ufizi katika vivumishi hivyo hutamkiwa kwenye kaakaa gumu ambapo konsonamti /j/ hutamkiwa. Sheria ifuatayo inaeleza hali hiyo:

N → [n] / __ j

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ĩ + n + kũrũ | [enkoro] | iliyozeeka |

| | | |
|---|---|---|
| ĩ + n + kuĩ | [enkue] | fupi |

Pia, kivumishi **ĩnkũrũ** [enkoro] (zilizozeeka) na **ĩnkuĩ** [enkue] (fupi) vinabainisha usilimisho nyuma kwa sababu nazali /n/ ya ufizi inatamkiwa kwenye kaakaa laini ambapo konsonanti /k/ inatamkiwa. Sheria hii inaeleza hali hiyo.

N ⟶ [n] / — k

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ĩ + n + gundu | [engundu] | mbivu |

Vilevile, katika kivumishi **ĩngundu** (zilizoiva) nazali /n/ ndiyo inatangulia konsonanti /g/. Hivyo, kinapotamkwa nazali /n/ inatamkiwa nyuma kwenye kaakaa laini mahali ambapo sauti /g/ hutamkiwa.

### 5.2.4 Udondoshaji wa Irabu

Katika lugha ya Kiswahili, Kihore na Wenzie (wataje) wanasema kuwa udondoshaji hutokea pale kuna vokali mbili ambazo hufanana na hufuatana. Udondoshaji hutokea katika mazingira ambapo kuna uziada. Kauli hii inaungwa mkono na Hooper (mtaje); Mgullu (1999) na Mwaliwa (mtaje) wanaposema irabu hudondoshwa pale ambapo kuna irabu mbili zinazofanana huku zikifuatana. Mgullu (1999), anaendelea kudai kuwa udondoshaji wa irabu hutokea ili kurahisisha matamshi. Katika lahaja ya Kiimenti hali si tofauti. Hii ni kwa sababu udondoshaji wa irabu hutokea sana pale ambapo irabu mbili zinazofanana hufuatana. Udondoshaji huu ni muhimu kwa sababu hurahisisha matamshi katika lahaja ya Kiimenti. Kwa mfano, kivumishi cha idadi **bibingĩ [**βiβiŋge] (vingi) huweza kuwa na **bibiingĩ** [βiβi:ŋge] (vingi) kama umbo la ndani ambalo ni vigumu

kulitamka kwa sababu ya mfuatano wa irabu /**i/** mbili. Hali ya udondoshaji katika vivumishi vya Kiimenti huweza kubainika katika mifano ifuatayo:

| **Umbo la ndani** | **Umbo la nje** |
|---|---|
| βi+βi+ingĩ | [βiβiŋge] (vingi) |
| ĩ +mi+ingĩ | [emiŋge] (mingi) |
| gĩ+ki+irũ | [gekiro] (cheusi) |
| gĩ+ki+ingĩ | [gekiŋge] (kingi) |
| bi+bi+irũ | [βiβiro] (vyeusi) |

Sheria hii inaweza kutumiwa kuelezea hali hii:

V ⟶ **(Ø)** / — V. Mfano wa udondoshaji katika kivumishi **bibingĩ [**βiβinge] (vingi) chenye muundo wa ndani **bibiingi** (vingi) ukitumiwa, udondoshaji wa irabu /i/ unaweza kuelezwa hivi: [i] > **[Ø]** / — V

[ + voweli
- nyuma
-mviringo ] > [ **Ø ]** / —— #

Udondoshaji mwingine unahusu irabu /a/ inapokutana na nyenzake. Hali hii inadhihirika katika mifano ifuatayo.

| **Umbo la ndani** | **Umbo la nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ja+ao | [ɟaɔ] | yao |
| ba+ao | [βaɔ] | wao |
| ja+awe | [ɟawɛ] | yake |
| a+awe | [awɛ] | pake |

| | | |
|---|---|---|
| a +a | [a] | pa |
| a + ao | [aɔ] | pao |
| ba+ a | [βa] | wa |
| ja + a | [ɟa] | ya |

Udondoshaji wa irabu /a/ inapokabiliana na nyenzake katika mifano ya vivumishi vilivyo hapo juu unaweza kuelezwa kupitia sheria ifuatayo:

[a] > [**Ø**] / ___ V

$$\begin{bmatrix} \text{+ voweli} \\ \text{+ mbele} \\ \text{-mviringo} \end{bmatrix} > [\,\mathbf{Ø}\,] \;/\; ___ \;\#$$

**5.2.5 Udondoshaji na Uchopekaji wa Vokali**

Mabadiliko mbalimbali ya sauti hubainika mzizi wa kivumishi unaporadidiwa. Kwa mfano, sehemu ya mzizi hukaririwa lakini irabu /o/ ambayo ni ya juu kudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/. Hali hii inaweza kubainika katika mifano ya vivumishi vifuatavyo vilivyoundwa kutokana na mchakato wa uradidi.

| **Kivumishi** | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|
| ũmũthũku [omoθoku] (mbaya) | > ũmũthũkathũku [omoθokaθoku] (mbaya zaidi) |
| gĩkirũ gĩkirũ [gekiro] (cheusi) | > gĩkirairũ [gekirairo] (cheusi zaidi) |

Mabadiliko yanayotokea hapo juu wakati irabu /o/ inapodondoshwa na mahali pake kuchopekwa irabu /a/ yanaelezwa kupitia sheria hii:

[o] > [a] / ______ #__________

| | | | |
|---|---|---|---|
| +nyuma | > | +mbele | / ________#_________ |
| + nusu juu | | +chini | |
| +mviringo | | -mviringo | |

Aidha, sehemu ya mzizi wa kivumishi huweza kukaririwa na irabu ya juu /u/ kudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /a/. Hali hii inaweza kubainika katika mifano ya vivumishi vifuatavyo vilivyoundwa kutokana na mchakato wa uradidi:

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| ũmũnoru [omonɔru] (mnono) | > | ũmũnoranoru [omonɔranɔru] (mnono zaidi) |
| rĩrĩoru [rereɔru] (lililooza) | > | rĩrĩoraoru [rereɔraɔru] ( lililooza zaidi) |

Mabadiliko yanayotokea hapo juu wakati irabu /u/ inapodondoshwa na mahali pake kuchopekwa irabu /a/ yanaelezwa kupitia sheria hii:

[u] > [a] / ______ #__________

| | | | |
|---|---|---|---|
| +nyuma | > | +mbele | / ________#_________ |
| +juu | | +chini | |
| +mviringo | | -mviringo | |

Katika mfano mwingine sehemu ya mzizi hukaririwa lakini irabu /ĩ/ ambayo ni ya nusu juu kudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| ũmwĩthĩ [omweθe] (mbichi) | > | ũmwĩthaithĩ [omweθaeθe] (mbichi zaidi) |
| jũmwingĩ [ɟomwiŋge] (mwingi) | > | jũmwingaingĩ [jomwiŋgaiŋge] (mwingi zaidi) |

Sheria ifuatayo inaweza kueleza hali ya irabu /ĩ/ kudondoshwa na mahali pake kuchopekwa irabu /a/ hapo juu.

[ĩ] > [a] / ___# ____

$$\begin{bmatrix} +mbele \\ +nusu\ juu \\ -mviringo \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} +mbele \\ +chini \\ -mviringo \end{bmatrix} / _____\#_____$$

Katika mfano mwingine sehemu ya mzizi hukaririwa lakini irabu /ɔ/ ambayo ni ya nusu chini hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| ĩnjũmo [enɟomɔ] (ngumu) | > | ĩnjũmajũmo [enɟomaɟomɔ] (ngumu zaidi) |
| ĩnjoro [inɟɔrɔ] (nyororo) | > | ĩnjorajoro [inɟɔraɟɔrɔ] (nyororo zaidi) |

Mabadiliko ya irabu /ɔ/ kudondoshwa na mahali pake kuchopekwa irabu /a/ hapo juu yanaelezwa kupitia sheria ifuatayo:

[ɔ] > [a] / ___# ____

$$\begin{bmatrix} +nyuma \\ +nusu\ chini \\ +mviringo \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} +mbele \\ +chini \\ -mviringo \end{bmatrix} / _____\#_____$$

Mabadiliko ya sauti yanayoshuhudiwa katika sehemu ya mzizi wa kivumishi baada ya uradidi yanaweza kuelezwa. Kwa mujibu wa Gachugi (2007) irabu za juu /i/, /u/ na ya kati /ɛ/ hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /a/ ya chini kutumiwa katika uradidi ili kuunda maneno ya Kiembu. Hali hii inadhihirika pia katika lahaja ya Kiimenti.

Kiimenti ni lahaja ya Kimeru ambayo ni lugha ya Kibantu sawa na Kiembu. Kwa hivyo, michakato ya kifonolojia inayoaathiri vipengele mbalimbali vya lugha hizo huweza kushabihiana. Hii inaonyesha jinsi michakato ya kifonolojia hutagusana na uradidi katika uundaji wa vivumishi vya Kiimenti. Uradidi kama huu ambapo mabadiliko ya sauti yanajitokeza unatambulikana kama uradidi changamani (Rubino, 2005). Mabadiliko kama haya ya fonimu yanatufanya tufikie uamuzi kuwa uradidi ni mchakato ambao unahusisha hata fonolojia.

### 5.2.6 Mvutano wa Irabu

Kulingana na Mgullu (1999) irabu huvutana wakati irabu moja ni ya juu na nyingine ni ya chini. Katika hali hii irabu ya juu inavutwa chini kidogo ilhali ile ya chini inavutwa juu kidogo. Irabu inayotokea katika mchakato huu ni ya kati. Mfano kama huu hutokea katika lugha ya Kiswahili wakati irabu /i/ ya juu huvutwa chini na irabu /a/ ikavutwa juu. Matokeo ni irabu /ɛ / ambayo ni ya kati. Mfano unapatikana katika neno kama: ma+ino ⟶ [mɛnɔ]. Mchakato wa mvutano wa irabu huweza kurejelewa pia kama muungano wa irabu. Wa Mberia (1993) anaieleza hali hii kama udondoshaji wa irabu. Anasema irabu mbili zikikutana, moja hudondoshwa. Mfano anaotoa ni irabu /a /+/ɛ/ ⟶ /ɛ/ katika ka + enu [kɛnu] (kilicho chenu). Pia, ka + oru ⟶ [kɔru] (kilichooza). Maoni yake ni kuwa irabu ya chini ikikutana na ya juu, basi ya chini hudondoshwa. Huu unapaswa kuelezwa kama mvutano wa irabu na si udondoshaji wa irabu.

Wald (2014) anasema muungano wa sauti hutokea pale fonimu mbili tofauti huungana na kuunda fonimu nyingine tofauti na zile za awali. Mawazo sawa na haya ni yale ya TUKI (2004) wanaposema kuwa muungano wa sauti ni namna ya usilimisho ambapo kila

kitamkwa huathiri chenzake kilicho jirani yacho. Wanaendelea kukariri kuwa katika aina hii ya usilimisho vitamkwa vyote viwili huungana na kutoa kitamkwa kimoja ambacho ni tofauti na vitamkwa vyote viwili.

Habwe na Karanja wakimrejelea Bakari (1982) wanaeleza kuwa vokali za Kiswahili huungana ili kurahisisha matamshi. Vilevile, katika lahaja ya Kiimenti muungano wa sauti hufanyika ili kurahisisha matamshi. Kwa mfano, kivumishi kimilikishi **betũ** [βεto] (wetu) kimeundwa kwa kutumia mofu **ba+etũ**. Kwa hivyo, umbo la ndani lingekuwa **baetũ.** Ni vigumu kutamka **baetũ.** Hivyo irabu **/a/** katika kipatanishi na irabu **/ ε /** katika mzizi wa kivumishi huungana na kuunda sauti moja ambayo ni irabu **/ ε/** ili kurahisisha matamshi. Mchakato kama huu unadhihirika hata katika vivumishi vya Kigiryama ambapo Jumwa (2008) anadhihirisha hali hii kwa kutumia vivumishi hivi: **/ha/+/ehu/** ⟶ **/hehu**/ (petu) na **/wa/ +/enge/** ⟶ **/wenge**/(wenyewe).

Kwa mujibu wa Mwaliwa (mtaje) mvutano wa irabu katika lugha ya Kidawida hutokea pale irabu /a/ ya kiambishi hukutana na irabu /i/ au /ε / na irabu /ε/ inapatikana. Mfano mwingine ni pale irabu /a/ au /ɔ/ kwenye kiambishi hukutana na irabu /ɔ/ ya mzizi na ndipo irabu / ɔ/ hupatikana.

Katika uchunguzi huu muungano wa sauti ambao tulikumbana nao ulihusu vokali pekee. Kihore na Wenzie (wataje) wakiangazia suala hili katika lugha ya Kiswahili wanasema kuwa irabu /a/ na irabu za mbele ambazo ni /i/ na / ε/ zinapokutana huzaa irabu /ε/. Kwa hivyo, /a/ +/ε/ ⟶ /ε/ au /a/ +/i/ ⟶ /ε. Katika Kitharaka, Wa Mberia (1993) anasema katika muungano wa irabu, irabu mbili huungana na kuunda irabu nyingine tofauti. Lakini mfano ambao anatuonyesha haudhihirishi hali hii. Hii ni kwa sababu anatoa mfano wa /a/ + /ε/ ⟶ /ε / katika neno ma + εru ⟶ [mεru]

(yaliyoiva). Kwa mujibu wa Mwaliwa (mtaje) mvutano wa irabu katika lugha ya Kidawida hutokea pale irabu /a/ ya kiambishi hukutana na irabu /i/ au /ɛ / na irabu /ɛ/ inapatikana. Muungano kama huu unabainika wazi kupitia mifano ifuatayo ya vivumishi vimilikishi.

| **Umbo la ndani** | **Umbo la nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ba+etũ | [βɛto] | wetu |
| ja+etũ | [ɟɛto] | yetu |
| ga+etũ | [gɛto] | kilicho chetu |
| a+etũ | [ɛto] | petu |
| ba+enu | [βɛnu] | wenu |
| ja+enu | [ɟɛnu] | yenu |
| ka+enu | [kɛnu] | kilicho chenu |
| a+enu | [ɛnu] | penu |

Sheria: a ⟶ ɛ ___ [ɛ]

[a] > [ɛ] / ___# ____

$$\begin{bmatrix} \text{+mbele} \\ \text{+chini} \\ \text{-mviringo} \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} \text{+mbele} \\ \text{+kati juu} \\ \text{-mviringo} \end{bmatrix} / _____ \ \#_____$$

Mvutano mwingine wa irabu unahusu irabu /a/ kuungana na /u/ ili kuzaa irabu /ɔ /. Hivyo, /a/+/u/ ⟶ / ɔ/. Aidha, irabu /a/ na /ɔ/ huungana na kuzalisha irabu /ɔ/. Mifano ifuatayo inaweza kutumika kuonyesha hali hiyo.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ja + ma + ũthũ | [ɟamɔθo] | mepesi |
| ja + ma + oru | [ɟamɔru] | yaliyooza |
| ba + ba + ũjũru | [βaβɔjoru] | walio timamu |
| ja + ma + oro | [ɟamɔrɔ] | yaliyo laini |

Mchakato kama huu wa kuungana kwa irabu umeelezwa na Kasombo (2019) akitumia mifano ya Kiswahili kinachozungumzwa Lubumbashi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kwa hivyo, badala ya kutamka ‘utaona’ (u-ta-o-na), irabu /a/ na /o/ huungana na kuunda /o/ katika [utɔna].

Kwa mujibu wa Mwaliwa (mtaje) mvutano mwingine wa irabu hutokea pale irabu /a/ au /ɔ/ kwenye kiambishi hukutana na irabu /ɔ/ ya mzizi na ndipo irabu /ɔ/ hupatikana. Hali kama hii inadhihirika katika lahaja ya Kiimenti kuonyesha kuwa lugha za Kibantu hulingana katika masuala fulani ya michakato ya kifonolojia.

Sheria zifuatazo zinaeleza mabadiliko yanayotokea wakati irabu /a/ hukutana na irabu /o/ na /u/.

(i) [a] > [ o]

$$\begin{bmatrix} +\text{mbele} \\ +\text{chini} \\ -\text{mviringo} \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} +\text{nyuma} \\ +\text{kati juu} \\ +\text{mviringo} \end{bmatrix} \quad ______ \# ______$$

(ii) [a] > [ɔ]

| | |
|---|---|
| +mbele<br>+chini<br>-mviringo | +nyuma<br>+kati juu<br>+kati chini<br>+mviringo |

### 5.2.7 Uwiano wa Irabu

Kulingana na Wa Mberia (1993; 2015) uwiano wa irabu hutokea katika vivumishi vya sifa katika lugha za Kibantu kama Kitharaka. Hali hii ilibainika katika vivumishi vya Kiimenti. Kulingana naye vivumishi huweza kuwa na viambishi awali vya lazima na vivumishi vingine si lazima kuwa navyo. Hii hutegemea ngeli mbalimbali. Uwiano wa irabu tunaoelezea hapa unahusu hali ambapo irabu ya kwanza katika kivumishi inawiana na irabu ambayo inapatikana katika kiambishi ngeli kinachotangulia mzizi wa kivumishi. Kwa mfano, katika ngeli ya 1 (MW/MU/MŨ) tunaweza kuwa na kivumishi kama **ũmũraja** [omoraɟa] / ũ-mũ-raja/ (mrefu). Irabu **/ũ/** katika mofu **{-mũ}** kwenye kivumishi inafanana au inawiana na irabu /**ũ**-/ ambayo inaitangulia katika kivumishi hicho. Katika kivumishi **ĩmĩkuĩ** [emekue]/ĩ-mĩ-kuĩ / (mifupi) irabu /ĩ/ inawiana na irabu nyenzake katika mofu {-mĩ}. Huu ni mfano mwingine wa uwiano wa irabu. Hata hivyo, uwiano wa irabu katika vivumishi vya sifa unaozingatia mtindo huu haupatikani katika ngeli nyingi za lahaja ya Kiimenti. Mifano zaidi ya kudhihirisha uwiano wa irabu inahusiana na vivumishi vionyeshi vya karibu kama **ũjũ** [oɟo] (huyu), **iji** [iɟi] (hizi) na **aja** [aɟa] (hapa) ambapo irabu ya kipatanishi ndiyo inapatikana mwisho wa kivumishi. Katika vivumishi hivi irabu /ũ/, /i/ na /a/ ni irabu za vipatanishi na ni viambishi awali vya vivumishi husika.

Irabu hizi zinapatikana kama viambishi tamati katika vivumishi hivyo na hivyo kuonyesha hali nyingine ya uwiano wa irabu. Uwiano kama huu wa irabu katika vivumishi vionyeshi unakaririwa zaidi na Wa Mberia (1993; 2015) na Gacunku (mtaje).

Hali nyingine ya kuangalia uwiano wa irabu ni pale ambapo irabu inayopatikana kwenye kipatanishi inaradididiwa. Kwa mfano, katika kivumishi **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) rĩ-rĩ-raja katika ngeli ya 5 kunapatikana mofu **{rĩ}** na **{-rĩ-}** ambapo {rĩ-} ya kwanza ni uradidi wa ya pili. Irabu **/i/** inapatikana katika mofu zote. Kulingana na Wa Mberia (1993) hii ni aina nyingine ya uwiano wa irabu. Anaendelea kusema kuwa si lazima vivumishi kuwa na viambishi **{rĩ-}** viwili. Hivyo, kivumishi **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) huweza hata kuwa **rĩraja** [reraɟa] (refu) na kuwasilisha maana kamili. Mifano zaidi ya kuonyesha uwiano wa irabu ni vivumishi kama **jũjũ** [ɟoɟo] (huu), **rĩrĩ** [rere] (hili), **baba** [βaβa] (hawa), **bibi** [βiβi] (hivi). Katika kuunda vivumishi hivi kipatanishi cha ngeli ndicho kinarudiwa.

### 5.2.8 Udondoshaji wa Konsonanti

Konsonanti ambazo zinafanana zikitokea katika kivumishi cha Kiimenti, kuna uwezekano wa udondoshaji wa konsonanti kutokea. Kwa mfano katika kivumishi kama **bibithũku [**βiβiθoku] /bi-bi-thũku (vibaya) hudondosha konsonanti ya kiambishi cha pili na tukawa na kivumishi **biithũku [**βi:θoku] (vibaya) ambapo irabu /i/ inarefushwa na kuwa [bi:thuku] (Mutahi, mtaje; Wa Mberia, 1981). Kiambishi /bi/ na chenzake vina uamilifu sawa wa kuwakilisha ngeli ya sintaksia. Kwa hivyo, vinaonyesha uradidi ambao hauchangii maana zaidi hata kimoja kikidondoshwa. Hivyo, kuna uziada wa kisemantiki unaochangia kudondoshwa kwa konsonanti ya kiambishi cha pili. Konsonanti ya kiambishi cha pili inapodondoshwa inamaanisha kuwa mofimu hiyo imedondoshwa yote. Irabu ya kiambishi hicho huwa sehemu ya kiambishi cha kwanza na muundo wake

ukabadilika kutoka KV hadi KVV: Huu ni udondoshaji wa konsonanti kutokana na uziada wa kisemantiki. Huu ni mfano wa sheria ya MP (Wa Mberia, 1981). Sheria hiyo inaweza kuandikwa hivi.

K ⟶ **Ø** ________________

[uziada wa kisemantiki]

Udondoshaji mwingine wa konsonanti unatokea wakati konsonanti inapatikana baina ya irabu mbili. Hali hii inaelezwa zaidi na Gacunku (mtaje) anapodai kuwa konsonanti katika vivumishi vionyeshi vya karibu huweza kudondoshwa na tukapata vivumishi kama vinavyopatikana hapa chini.

| **Umbo Asili** | **Umbo Jipya** | **Maana** |
|---|---|---|
| baba | baa [βa:] | hawa |
| jũjũ | jũũ [ɟo:] | huu |
| iji | ii [i:] | hii |
| jaja | jaa [ɟa:] | haya |
| bibi | bii [β:] | hivi |

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu inabainika kuwa konsonanti ikitokea baina ya irabu mbili zinazofanana inadondoshwa. Hata hivyo, maana ya kivumishi haibadiliki. Sheria ifuatayo inaweza kutumika kueleza mchakato wa udondoshaji wa konsonanti katika vivumishi vilivyo hapo juu.

K ⟶ [**Ø**] / _______#________

Udondoshaji mwingine wa konsonanti unaopatikana katika vivumishi vya Kiimenti unahusu kudondoshwa kwa konsonanti inayopatikana baina ya irabu mbili ambazo

hazifanani. Kwa mfano kivumishi **ũrĩkũ**? [oreko] (yupi) huweza kuwa **ũĩkũ**? [oeko] (yupi) baada ya konsonanti /r/ kudondoshwa. Hata hivyo, muundo wake wa nje ni **wĩkũ**? [weko] (yupi) baada ya kupitia mchakato wa uyeyushaji. Uyeyushaji unatokea iwapo irabu /ũ/ inatokea katika mazingira ya kukutana na irabu /ĩ / ya mzizi wa kivumishi. Mfano katika kivumishi **ũĩkũ?** [oeko] irabu /ũ/ inapotangulia irabu /ĩ/ inayeyushwa na kuwa **wĩkũ**? (yupi) [weko] baada ya konsonanti /r/ kudondoshwa. Wakati mwingine badala ya uyeyushaji wa irabu kutokea, kuna uwezekano wa irabu kurefushwa ikiwa irabu ya kiambishi awali inafanana na ile ya mzizi wa kivumishi. Mfano huu unapatikana katika kivumishi **giĩkũ** [gi:ko] (vipi) baada ya konsonanti /r/ kudondoshwa. Hata hivyo, irabu mbili ambazo hazifanani zikikutana baada ya konsonanti /r/ kudondoshwa zinatokea jinsi zilivyo bila ya kurefushwa au kuyeyushwa. Mfano ni kivumishi **baĩkũ** [βaeko] (wepi). Mifano zaidi inayohusiana na mzizi –rikũ (-ipi) inaweza kubainika hapa chini ili kuonyesha udondoshaji wa konsonanti.

| **Umbo la Ndani** | **Umbo la Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| ba + rĩkũ | baĩku[βaiko] | wepi |
| ja + rĩkũ | jaĩkũ [ɟaeko] | yepi |
| bi + rĩkũ | biĩkũ [βieko] | upi |
| kĩ + rĩkũ | gĩĩkũ [gi:ko] | kipi |
| ju + rĩkũ | juiĩkũ [ɟwiko] | upi |
| bũ + rĩkũ | buĩkũ [βwiko] | upi |

Sheria inayotumika kueleza udondoshaji wa konsonanti /r/ katika vivumishi hapo juu ni ifuatayo.

[r] ——— [**Ø**] / _______#________

Udondoshaji mwingine wa konsonanti ni ule unaoelezwa kwa kutumia sheria inayoitwa "Ganda Law." Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (wataje) sheria hii inaweza kutumiwa kueleza kudondoshwa kwa konsonanti. Kulingana nao sheria hii ilitumika na Carl Meinhorf alipochunguza lugha za Kibantu. Mtaalamu huyu alitumia sheria hii kueleza baadhi ya mabadiliko ya kifonolojia aliyokumbana nayo katika lugha za Kiganda. Kulingana na "Ganda Law" konsonanti katika neno hudondoshwa ikiwa imetanguliwa na sauti ya kipua kisha kufuatwa na irabu halafu nazali nyingine.

Kwa hivyo udondoshaji wa konsonanti katika kivumishi cha sifa kama **ing'entu** [iŋɛntu] (kali) unaweza kuelezwa kutumia sheria ya "Ganda Law". Kivumishi hiki kimepatikana baada ya udondoshaji wa konsonanti kufanyika. Kabla ya udondoshaji, kivumishi hiki kingekuwa **ingentu** na hivyo kutamkwa kama [**ingɛntu**] badala ya [**iŋɛntu**]. Baada ya udondoshaji kinatamkwa kama [**iŋɛntu**]. Hii ni kwa sababu si rahisi kutamka sauti /n/ ya ufizi ikifuatwa na sauti /g/ ya kaakaa laini. Hii ni kwa sababu sauti /n/ ni ya mbele ilhali /g/ ni ya nyuma. Kwa hivyo, ili kurahisisha matamshi sauti /n/ inavutwa nyuma ili itamkiwe mahali pa sauti /g/. Hali hii inaifanya sauti /n/ kuwa sauti ya nazali ya nyuma [ŋ] na hivyo kivumishi kutamkwa kama [**iŋɛntu**]. Katika hali hii sauti /g/ inadondoshwa kwa sababu kuna uziada wake. Sheria inayoweza kutumiwa kuelezea hali hii ni:

K ⟶ [ø] / N – VN

Kwa mujibu wa mabadiliko tuliokumbana nayo katika udondoshaji wa konsonanti tunaweza kueleza sheria hii. Kwa ujumla, inadokeza kuwa konsonanti hudondoshwa ikiwa imetanguliwa na nasali na kufuatwa na irabu na hatimaye nasali nyingine. Hali hii inashadidiwa zaidi na Munguti (mtaje). Katika kivumishi **ing'entu** [**iŋɛntu]** konsonanti /g/ ndiyo hudondoshwa. Konsonanti hiyo inaafiki kauli za sheria ya "Ganda Law" za

udondoshaji. Hii ni kwa sababu konsonanti /g/ ya kipasuo inadondoshwa kwa kutanguliwa na nazali /n/ kisha ikafuatwa na irabu /ε/ na hatimaye nazali /n/. Vivumishi vingine ambavyo vimepitia mchakato wa udondoshaji wa konsonanti ni kama **jang'anona** [ɟaŋanɔna**]** (kiasi) na **ing'anu** [iŋanu] (zinazotosha).

Ni vizuri kufahamu kuwa si vivumishi vyote vyenye muundo uliobainishwa hapo juu hukumbwa na mabadiliko kama hayo. Hii ni kwa sababu kivumishi kama **ingundu** (zilizoiva) hakidhihirishi mabadiliko yanayoangaziwa na "Ganda Law."

### 5.2.9 Uchopekaji wa Konsonanti

Baadhi ya vivumishi vya Kiimenti huchopekwa konsonanti baina ya irabu mbili. Mfano mzuri ni katika kivumishi **ijĩrĩ [**iɟere] (mbili) ambapo konsonanti /ɟ/ imechopekwa baina ya irabu /i/ na /ɟ/. Muundo wa kivumishi hiki ungekuwa **iĩrĩ** /i-ĩrĩ [iere] (mbili) ambapo irabu /i/ ni kipatanishi katika ngeli ya 9 ya sintaksia kikitangulia mzizi **-ĩrĩ** (mbili) ili kuunda **iĩrĩ [**iere] (mbili) lakini badala ya hivyo kivumishi **ijĩrĩ** [iɟere] (mbili) kimeundwa baada ya uchopekaji wa konsonanti /ɟ/ katikati ya irabu mbili. Muundo wa vivumishi vilivyoundwa kutokana na mzizi **– ĩrĩ** [-ere] ukitanguliwa na kipatanishi katika kila ngeli unabainika hapa chini.

**Jedwali la 29: Uchopekaji wa Konsonanti**

| Ngeli | Kip | Mzizi | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 2 A | ba | ĩrĩ | baĩrĩ [βaere] | wawili |
| 4 MĨ | ĩ | ĩrĩ | ĩĩrĩ [e:ire] | miwili |
| 6 MA | ja | ĩrĩ | jaĩrĩ [ɟaere] | mawili |
| 8 I/BI | bi | ĩrĩ | biĩrĩ [βiere] | viwili |
| 10 N | i | ĩrĩ | ijĩrĩ [iɟere] | mbili |
| 18 TW/TŨ | tũ | ĩrĩ | twĩrĩ [twere] | iliyo mbili |
| 20 KŨ | kũ | ĩrĩ | kwĩrĩ [kwere] | kuwili |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na jedwali inaonekana wazi kuwa kivumishi **ijĩrĩ [**iɟere] (mbili) kimechopekwa konsonanti /j/ lakini hivyo vingine havijafikwa na hali hiyo. Sheria ifuatayo inaweza kutumika kuelezea uchopekaji huo.

[**Ø**] ______ [ɟ**]** / ______#________

**5.2.10 Ukaakaishaji**

Baadhi ya vivumishi vya Kiimenti hupitia mchakato wa ukaakaishaji vinapoundwa. Katika mchakato huu, sauti ambazo si za kaakaa hubadilika na kutamkiwa katika kaakaa. Kwa mujibu wa Wa Mberia (2002) mchakato wa ukaakaishaji hutokea wakati sauti /n/ hutokea katika mazingira ya kutangulia irabu katika mzizi wa nomino, kivumishi na kategoria nyingine za maneno. Maelezo sawa na haya ni ya Curr (mtaje) anapoeleza kuwa

ukaakaishaji hutokea sana wakati sauti ya ufizi hutangulia irabu ya mbele katika neno. Hali kama hii ya ukaakaishaji hutokea katika lahaja ya Kiimenti. Kwa mfano, kuna uwezekano wa sauti /n/ ya ufizi kubadilika na kuwa [ɲ] inayotamkiwa kwenye kaakaa gumu. Hali hii inajitokeza katika kivumishi **inyingĩ** [iɲinge] /i-ny-ingĩ / ambapo sauti /n/ inabadilika na kuwa [ɲ] na hivyo kutamkiwa kwenye kaakaa gumu. Mabadiliko haya yanaweza kuelezwa kupitia mchakato wa ukaakaishaji. Vivumishi vingine ambavyo vimepitia mchakato huo ni hivi vifuatavyo:

| **Muunda wa Ndani** | **Muundo wa Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| i +na | [iɲa] | nne |
| i+na+na | [iɲaɲa] | nane |

Ukaakaishaji unaodhihirika katika mifano iliyo hapo juu ambapo [n] hubadilika na kuwa [ɲ] unaweza kuelezwa kupitia sheria hii.

[n] > [ɲ] / _______#________

[+nas, ufizi] > [+nas, +kk gumu]

**5.2.11 Sheria ya Dahl**

Sheria ya Dahl inahusishwa na Edmund Dahl ambaye husemekana kuwa mwasisi wake alipochunguza lugha za Kibantu. Kulingana na sheria hii ikiwa kuna mfuatano wa konsonanti mbili ghuna, moja hupoteza ughuna wake. Aidha, konsonanti mbili zisoghuna zikifuatana, basi moja yazo hufanywa ghuna. Mfano unaotolewa unahusu neno la Kiingereza *coat* lililokopwa na kuingia katika Kiswahili kama koti. Hatimaye limeingia katika lugha ya Ciruuri likiwa *ligoti (li+goti)*. Katika hali hii konsonanti ya kwanza ambayo haikuwa ghuna imefanywa kuwa ghuna (TUKI). Mabadiliko kama hayo

yameelezwa zaidi na Makini (2015) alipotoa maoni kuwa kisinkronia sauti /k/ huweza kubadilika na kuwa /g/ alipochunguza hali hiyo katika nomino na vitenzi vya Ekegusii. Hali kama hii ilitabiriwa na Meinhof (1932) aliposema kuwa sauti /k/ huweza kuwa ghuna ikiwa itatangulia konsonanti sighuna katika mzizi wa neno. Kwa maoni yake sauti ya kiambishi awali na ile ya kwanza katika mzizi hupaswa kutofautiana.

Sheria ya Dahl imejadiliwa zaidi na wataalamu kama Katamba (1989) na Armstrong (1967). Watafiti kama Kanana (2011), Kaimenyi (2002), Bickmore (1998), Lombardi (1991), na Wa Mberia (1981) wamethibitisha kupatikana kwa sheria hiyo katika uchanganuzi wao wa lugha za Kibantu.

Armstrong (mtaje) ana maoni kuwa suala la sheria ya Dahl katika lugha za Kibantu ni la kihistoria. Kwa mfano, anasema kuwa kiambishi kinachotangulia mzizi kikiwa na konsonanti /g/, basi konsonanti ya kwanza kwenye mzizi sharti iwe sighuna. Anaendelea kudai kuwa kiambishi awali kikiwa na konsonanti /k/, basi konsonanti inayofuata kwenye mzizi itakuwa na ughuna.

Sheria ya Dahl hujitokeza katika vivumishi vya lahaja ya Kiimenti na inaweza kutumika kueleza usawazisho wa sifa ya ughuna katika vivumishi mbalimbali. Hii ni kwa sababu inasawazisha sifa ya ughuna katika konsonanti iliyo kwenye kiambishi awali na inayoanza mzizi wa kivumishi. Kwa mfano konsonanti ya kwanza katika mzizi wa kivumishi ikiwa na ughuna, basi ile ya kiambishi kinachotangulia mzizi haitakuwa na ughuna. Vivyo hivyo, konsonanti ya kwanza ya mzizi wa kivumishi cha Kiimenti ikiwa si ghuna, basi konsonanti ya kwanza katika mzizi wa kivumishi itakuwa na ughuna. Maelezo kama haya yametolewa na Salesio (mtaje) alipodhihirisha jinsi sheria ya Dahl hufanya kazi katika vitenzi vya Kichuka. Kwa mfano vivumishi ambavyo huwa na sauti

/g/, /b/, /r/ na nasali /m/ na /n/ katika kiambishi awali na konsonanti /k/ au /th/ zikianzia mzizi wa kiambishi huonyesha usawazisho wa ughuna kulingana na sheria ya Dahl. Hii ni kwa sababu sauti za viambishi zina ughuna (+mghuno) ilhali zile za mizizi wa vivumishi hazina ughuna (-mghuno). Mifano ya vivumishi hivyo ni kama ifuatavyo:

| Muundo wa Ndani | Muundo wa Nje | Maana |
|---|---|---|
| gĩakwa /ge-akwa/ | [geakwa] | changu |
| gĩaku /gĩ-aku/ | [geaku] | chako |
| bakuĩ /ba-kuĩ/ | [βakue] | wafupi |
| biaku/bi-aku/ | [βiaku] | vyako |
| biakwa/bi-akwa/ | [βiaku] | vyangu |
| ũmũthũku/ũ -mũ -thũ -ku/ | [omoθoku] | mbaya |
| bathatũ /ba-thatũ / | [βaθato] | watatu |
| rĩkuĩ /rĩ-kuĩ/ | [rekue] | fupi |
| inkai /i-n-kai/ | [inkai] | chache |

Ni vizuri kuelewa kuwa si vivumishi vilivyoorodheshwa hapo juu hudhihirisha usawazisho wa sifa ya ughuna, konsonanti ya kiambishi na ile ya mzizi zinapokutana kuunda vivumishi vya Kiimenti pekee bali kuna vingine. Hata hivyo, si kila wakati ambapo sheria hiyo hutawala muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, katika vivumishi vifuatavyo konsonanti ya kiambishi na ile ya mzizi wake, zote ni ghuna. Hii ni mifano ya vighairi vya sheria ya Dahl:

| Muundo wa Ndani | Muundo wa Nje | Maana |
|---|---|---|
| barĩa /ba-rĩa/ | [βarea] | wale |
| rĩraja /rĩ-raja/ | [reraɟa] | refu |

| | | |
|---|---|---|
| banene /ba-nene/ | [βanɛnɛ] | wakubwa |
| ũmũraja / ũ -mũ-raja/ | [omoraɟa] | mrefu |
| injerũ /i-n-jerũ / | [iɲɟɛro] | nyeupe |
| injirũ /i-n-jirũ / | [iɲɟiro] | nyeusi |

Hata kuna uwezekano wa konsonanti ya kiambishi na ile ya mzizi kufuatana lakini hazina ughuna. Hii ni hali nyingine ya kuonyesha jinsi vivumishi vya Kiimenti havidhibitiwi na kanuni ya Dahl kila wakati. Mfano wa vivumishi hivyo ni kama:

| **Muundo wa Ndani** | **Muundo wa Nje** | **Maana** |
|---|---|---|
| tũkui /tũ -kuĩ / | [tokue] | kuonyesha ufupi |
| tũkũrũ /tũ -kũrũ / | [tokoro] | kuonyesha uzee |
| tũkai /tũ -kai/ | [tokai] | kuonyesha uchache |

## 5.3 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Kiimenti

### 5.3.1 Dhana ya Uradidi

Muundo wa vivumishi vya Kiimenti hauwezi kukamilika bila kuangazia mchakato wa uradidi ambao unaathiri muundo wa vivumishi husika. Dhana ya uradidi imejadiliwa na wanasarufi mbalimbali huku wakitoa kauli zinazohitilafiana. Kwa mfano, Mbaabu (mtaje) ameeleza uradidi kama urudiaji wa mizani, mizizi na maneno kamili. Bussmann (1996) ameeleza uradidi kama mbinu ya kurudia silabi awali katika mzizi au shina la neno. Maelezo haya yana kasoro kwa sababu uradidi huhusisha zaidi ya silabi. Uradidi umeelezwa zaidi kama urudufishaji wa maneno (Mbaabu, mtaje; Mrikaria, 2004) au takriri (Kiango, 1995). Neno linaporudiwa lote basi hali hiyo ni uradidi/urudufu kamili ilhali sehemu zake zinaporudiwa huo ni uradidi/urudufu nusu. Maelezo zaidi yanajeleza uradidi kama mbinu ya uundaji wa maneno ambapo neno au sehemu ya neno hurudiwa

(Frawley, 2003; Lai, 2006; Massamba, 2004). Mchakato wa uundaji maneno kupitia uradidi hutokea sana katika mazungumzo ya watu ambao wako huru kutumia mbinu zozote ili kufanikisha mawasiliano yao (Mnenuka, 2010). Uradidi ni mchakato unaotumika katika uundaji wa maneno ya lugha nyingi (Inkellas na Zoll, 2005) na ni sifa muhimu ya lugha za Kibantu (Ashton, mtaje). Kwa mfano, ni mojawapo ya mbinu zinazotumika kuunda maneno katika lugha za Kibantu (Contini-Morava, 2007). Sehemu ambayo imeradidiwa inaweza kuwa kabla na baada ya mzizi au mzizi wenyewe (Muhirwe na Trosterud, 2008). Hata hivyo, maneno yanayoundwa kupitia mchakato huo hueleweka vizuri yanapotokea katika muktadha wa matumizi (Gichuru, 2010). Mchakato wa uradidi unahusisha vipengele vya fonolojia (Kula, 2004; Odden, 1996) na vile vya mofolojia (Kauffman, 2015; Tak, 2007) katika lugha ili kuufanikisha. Kauli hii inashadidiwa na Silvemann (1993). Alipochunguza lugha ya Kihehe alibaini kuwa mchakato wa uradidi hufanikishwa kwa kuhusisha vipengele vya fonolojia na mofolojia pamoja. Lugha nyingi za ulimwengu hubainisha uradidi katika kategoria za nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi (Lusekelo, 2009).

### 5.3.2 Aina za Uradidi Katika Vivumishi vya Lahaja ya Kiimenti

Aina kuu mbili za uradidi hupatikana katika vivumishi vya Kiimenti. Hizi ni uradidi kamili na uradidi nusu (Rubanza, 2018) au urudufu kamili na urudufu nusu. Lugha ikidhihirisha uradidi nusu katika maneno yake hubainisha hata uradidi kamili (Moravesik, 1978). Kauli hii ina mashiko katika lahaja ya Kiimenti. Hii ni kwa sababu kwa kutumia vivumishi vya lahaja husika tumedhihirisha jinsi uradidi nusu na kamili hujitokeza.

#### 5.3.2.1 Uradidi Kamili wa Vivumishi

Uradidi kamili ni pale ambapo kivumishi chote hurudiwa jinsi kilivyo. Hali hii inaweza kubainishwa katika mifano ifuatayo ya vivumishi ambapo kipatanishi kinafanyiwa uradidi kamili na kisha kufanyiwa uradidi kamili mwingine.

**Jedwali la 30: Uradidi Kamili wa Vivumishi vya Kiimenti**

| Ngeli | Vipatanishi | Uradidi Kamili | Uradidi Kamili Mwingine |
|---|---|---|---|
| 2 | ba | baba [βaβa] (hawa) | babababa [βaβaβaβa] (hawahawa) |
| 3 | ju | jũjũ [ɟoɟo] (huu) | jũjũjũjũ [ɟoɟoɟoɟo](huuhuu) |
| 5 | rĩ | rĩrĩ [rere] (hili) | rĩrĩrĩrĩ [rererere] (hilihili) |
| 6 | ja | jaja [ɟaɟa] (haya) | jajajaja [ɟaɟaɟaɟa] (hayahaya) |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kutokana na mifano iliyopo hapo juu ni dhahiri kuwa kipatanishi kimoja kinaweza kufanyiwa uradidi kamili zaidi ya mmoja. Hali hii inaweza kuelezwa kwa kutumia kipatanishi {**ba-}** katika ngeli ya 2 ili kuunda kivumishi **baba** [βaβa] (hawa) ambacho kinafanyiwa uradidi kamili zaidi na kuunda kivumishi **babababa** [βaβaβaβa] (hawahawa). Kuradidiwa kwa kipatanishi {**ba-**} kunahusiana na maelezo ya Mbaabu (mtaje) aliposema kuwa katika uradidi mizani huweza kurudiwa. Badala ya kutumia uradidi wa mizani, uradidi wa silabi unatumika (Alsamadani na Taibah, 2019; Biwott na Ong'onda wataje). Hii inaonyesha kuwa kipatanishi {**ba-**} kinarudiwa zaidi ya mara moja. Kauli hii inaungwa mkono zaidi na Marantax (1982) aliposema kuwa katika lugha

nyingi sehemu inayorudiwa hurudiwa mara moja, lakini kuna uwezekano wa kurudiwa zaidi ya mara moja katika lugha nyingine. Anatoa mfano wa kitenzi *mejir* kutoka lugha ya *Pingelapese* na kuonyesha jinsi sehemu moja huweza kurudiwa kwa zaidi ya mara moja.

| Kitenzi | | Uradidi | | Uradidi Zaidi |
|---|---|---|---|---|
| *mejir* (lala) | > | *mejmejr* (analala) | > | *mejmejmejr* (kuendelea kulala) |

Mifano iliyotolewa ya uradidi wa vipatanishi mbalimbali ili kuunda vivumishi viashiria hapo juu inaafiki mfano wa kitenzi *mejir* (lala) katika lugha ya *Pingelapese*. Aidha, uradidi kamili unaweza kufanyiwa kivumishi kiashiria ambapo viambishi vyote pamoja na mzizi hurudiwa. Kwa mfano, kivumishi **ũjũ** [oɟo] (huyu) huradidiwa na kuunda kivumishi **ũjũũjũ** [oɟoːɟo] (huyuhuyu) ambapo kiambishi awali, mzizi na kiambishi tamati hurudiwa. Uradidi kama huu huzua maana ya kusisitiza kwa kivumishi kinachoundwa. Kwa hivyo, uradidi wa neno unaweza kutumika kuunda maneno yenye maana tofauti (Kiango, mtaje). Ni vizuri kufahamu kuwa kivumishi **ũjũ** [oɟo] (huyu) kikiradidiwa huunda **ũjũũjũ** [oɟoːɟo] (huyuhuyu) na baada ya mchakato huo tofauti za kisemantiki huibuka. Uradidi wa kivumishi jinsi kilivyo hujulikana kama uradidi kamili wa neno (Muhirwe na Trosterud, wataje).

### 5.3.2.2 Uradidi Nusu wa Vivumishi

Uradidi nusu ni pale ambapo sehemu fulani za neno kama la kivumishi hurudiwa. Uradidi nusu hubainisha ruwaza mbalimbali (Rubino, mtaje) ambazo hupatikana katika vivumishi vya Kiimenti. Ruwaza moja inahusu kiambishi awali cha kivumishi kurudiwa katika mfano wa kivumishi **wewengwa** [wɛwɛŋgwa] (kusisitiza mwenyewe zaidi). Pia, kipatanishi na mofu jenzi {**-o-**} hurudiwa mara mbili katika kivumishi **kĩokĩongwa**

[keɔkeɔŋgwa] (kusisitiza chenyewe zaidi). Mifano ifuatayo ya vivumishi vya pekee vilivyoundwa kutokana na uradidi wa kiambishi awali au kiambishi awali na mofu jenzi inabadilisha maana ya kivumishi na kukipatia dhana ya kusisitiza zaidi.

| **Kivumishi** | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|
| bongwa [boŋgwa] (wenyewe) | >bobongwa [βɔβɔŋgwa](kusisitiza wenyewe zaidi) |
| kungwa [kuŋgwa] (kwenyewe) | > kukungwa [kukuŋgwa](kusisitiza chenyewe zaidi |
| biongwa [βiɔŋgwa] (vyenyewe) | >biobiongwa [βiɔβiɔŋgwa](kusisitiza vyenyewe zaidi) |
| rĩongwa [reɔŋgwa] (chenyewe) | >rĩorĩongwa [reɔreɔŋgwa](kusisitiza lenyewe zaidi) |

Hata hivyo, katika mifano inayofuata ya vivumishi vya sifa ambavyo vimeundwa kutokana na uradidi havibadilishi maana. Hivyo kivumishi ambacho hakina uradidi wa kiambishi awali na kilicho na uradidi huo huwasilisha maana moja. Hii inaonyesha dhana ya uradidi wa viambishi awali au vipatanishi hubadilisha maana ya kivumishi husika au kutoibadilisha. Kwa hivyo, si kila wakati ambapo uradidi wa vivumishi vya Kiimenti huzua tofauti za kisemantiki kwa vivumishi.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| bithũku [βiθoku] (vibaya) | > | bibithũku [βiβiθoku] (vibaya) |
| bathongi [βaθɔŋgi] (wazuri) | > | babathongi [βaβaθɔŋgi] (wazuri) |
| bũthũku [βoθoku] (mbaya) | > | bũbũthũku [βoβoθɔku] (mbaya) |
| bithongi [βiθɔŋgi] (maridadi) | > | bibithongi [βiβiθɔŋgi] (maridadi) |

Ruwaza ya pili inahusu mzizi kukaririwa jinsi ulivyo bila kuhusisha sehemu zingine za kivumishi kama viambishi vyake vya ngeli. Huu ni uradidi kamili wa mzizi (Muhirwe na Trosterud, wataje). Mifano hii inadhibitisha hali hiyo.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| ũmũraja [omoraɟa](mrefu) | > | ũmũrajaraja [omoraɟaraɟa] (mrefu zaidi) |
| gĩkĩraja [gekeraɟa](kirefu) | > | gĩkĩrajaraja [gekeraɟaraɟa] (kirefu zaidi) |
| bibiega [βiβiɛga] (vizuri) | > | bibiegaega [βiβiɛgaɛga] (vizuri zaidi) |
| injega [inɟɛga] (nzuri) | > | injegajega [inɟɛgaɟɛga] (nzuri zaidi) |
| ũmwega [omwɛga] (mzuri) | > | ũmwegaega[omwɛgaɛga] (mzuri zaidi) |

Kutokana na mifano ya vivumishi hapo juu inabainika kuwa vivumishi **ũmũrajaraja**, **gĩkĩrajaraja, bibiegaega, injegajega** na **ũmwegaega** vimeundwa kutoka kwa mizizi **{–raja}** [raɟa] (-refu) na {**-ega**} [ɛga] (-zuri) ambayo imeradidiwa jinsi ilivyo.

Ruwaza ya tatu inahusu mzizi wa kivumishi kurudiwa ukionyesha mabadiliko ya sauti. Mabadiliko mbalimbali ya sauti hubainika mzizi wa kivumishi unaporadidiwa. Kwa mfano, sehemu ya mzizi hukaririwa lakini irabu /u/ ambayo ni ya juu kudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|
| ũmũnoru [omonɔru] (mnono) | > ũmũnoranoru [omonɔranɔru] (mnono zaidi) |
| ũmũthũku[omoθoku] (mbaya) | > ũmũthũkathũku [omoθokaθoku] (mbaya zaidi) |

Aidha, sehemu ya mzizi hukaririwa lakini irabu /ũ/ ambayo ni ya nusu juu kudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
|---|---|---|
| gĩkĩrũ [gekero](cheusi) | > | gĩkĩraĩrũ [gekeraero] (cheusi zaidi) |
| ũmũkũrũ [omokoro] (mzee) | > | ũmũkũrakũrũ [omokorakoro] (mzee zaidi) |

Pia, mzizi wa kivumishi hurudiwa lakini irabu /ĩ/ ya nusu juu kudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /a/ ambayo ni ya chini.

| **Kivumishi** | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
| --- | --- |
| ũmwĩthĩ [omweθe] (mbichi) | >omwethaithe[omweθaeθe] (mbichi zaidi) |
| jũmwingĩ [ɟomwiŋge](mwingi) | >jũmwingaingĩ [ɟomwiŋgaiŋge] (mwingi zaidi) |
| ũmũthongi[umuθɔŋgi] (maridadi) | >ũmũthongathongi [omoθɔŋgaθɔŋgi](maridadi zaidi) |
| jũmũkuĩ [ɟumukue](mfupi) | >jũmũkuakuĩ [ɟomokuakue] (mfupi zaidi) |

Aidha, mzizi wa kivumishi huradidiwa lakini irabu /ɔ/ ya nusu chini kudondoshwa na pahali pake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
| --- | --- | --- |
| injũmo [inɟomɔ] (ngumu) | > | injũmajũmo[inɟomajomɔ] (ngumu zaidi) |
| injoro[inɟɔrɔ] (nyororo) | > | injorajoro [inɟɔrajɔrɔ] (nyororo zaidi) |
| rĩrĩoru [rereɔru] (lililooza) | > | rĩrĩoraoru [rereɔraɔru] (lililooza zaidi) |

Hatimaye, mzizi wa kivumishi huradidiwa lakini irabu /ɛ/ ya nusu chini kudondoshwa na pahali pake kuchukuliwa na irabu ya chini /a/.

| **Kivumishi** | **Kivumishi baada ya Uradidi** |
| --- | --- |
| intune [intunɛ] (nyeupe) | > intunatune[intunatunɛ] (nyeupe zaidi) |
| gĩkĩnene [gekenɛnɛ] (kikubwa) | >gĩkĩnenanene[gekenɛnanɛnɛ] (kikubwa zaidi) |
| ũmũcheke [omoʧɛkɛ] (mwembamba) | >ũmũchekacheke[omoʧɛkaʧɛkɛ] (mwembamba zaidi) |
| ũmũme[omomɛ] (mwerevu) | >ũmũmaũme[omomaomɛ] (mwerevu zaidi) |

Mabadiliko ya sauti yanayoshuhudiwa katika sehemu ya mzizi wa kivumishi baada ya uradidi yanaweza kuelezwa. Kwa mujibu wa Gachugi (mtaje) irabu za juu /i/, /u/ na ya kati /ε/ hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /a/ ya chini kutumiwa katika uradidi ili kuunda maneno ya Kiembu. Hali hii inabainika katika lahaja ya Kiimenti. Kiimenti ni lahaja ya Kimeru ambayo ni lugha ya Kibantu sawa na Kiembu. Kwa hivyo, michakato ya kifonolojia inayoaathiri vipengele mbalimbali vya lugha hizo huweza kushabihiana. Hii inaonyesha jinsi michakato ya kifonolojia hutagusana na uradidi katika uundaji wa vivumishi vya Kiimenti. Uradidi kama huu ambapo mabadiliko ya sauti yanajitokeza unatambulikana kama uradidi changamani (Rubino, mtaje). Mabadiliko kama haya ya fonimu yanatufanya tufikie uamuzi kuwa uradidi ni mchakato unaohusisha hata fonolojia.

Ni vizuri kufahamu kuwa licha ya vivumishi vya Kiimenti kufanyiwa uradidi kamili na nusu havibadilishi kategoria yake, vinabaki tu kuwa vivumishi. Mbinu ya uradidi ni zalishi katika uundaji wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, kipatanishi **{ba-}** katika ngeli ya 2 kikifanyiwa urudufu kamili kinaweza kuunda kivumishi **baba** (hawa) ambacho kinaweza kuunda kivumishi **babababa** [βaβaβaβa] (hawahawa). Aidha, kutokana na kivumishi **babaingĩ** [βaβainge] (wengi) kivumishi **babaingaingĩ [**βaβaiŋgaiŋge] (wengi zaidi) kinaweza kuundwa. Hapa kumefanyika uradidi nusu. Hii inaonyesha kuwa kwa ujumla uradidi nusu na kamili unabainika katika uzalishaji wa vivumishi zaidi vya Kiimenti. Inasemekana uradidi wa vitenzi huonyesha uzalishaji mwingi kuliko vivumishi katika lugha za Kibantu (Cook, 2013). Hata hivyo, lugha mbalimbali huonyesha viwango tofauti vya uzalishaji (Marantax, mtaje).

### 5.3.3 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Sifa

Vivumishi vya sifa katika Kiimenti huzingatia mofolojia ya kipatanishi kuambishwa kwenye mzizi wa kivumishi kama kiambishi awali. Aidha, vinaweza kuundwa kwa kipatanishi na kiambishi ngeli kuambishwa kwenye mzizi wa kivumishi kuzingatia mpangilio huo. Kwa kuzingatia muundo wa kwanza, mzizi wa kivumishi **{-raja}** huweza kuambishwa vipatanishi mbalimbali na kuunda vivumishi tofauti kulingana na ngeli. Ukiambishwa kipatanishi cha ngeli ya 2, kivumishi **baraja** [βaraɟa] (warefu) kinaundwa. Kipatanishi **{ba-}** kinaweza kuambishwa katika kivumishi **baraja** [βaraɟa] (warefu) na kivumishi **babaraja** [βaβaraɟa] (warefu) kikaundwa. Kwa hivyo, vivumishi vya sifa vinapoundwa hudhihirisha uradidi wa kiambishi awali katika baadhi ya ngeli. Kivumishi **baraja** [βaraɟa] au **babaraja** [βaβaraɟa] huwa na maana moja na kimojawapo kinaweza kutumika katika mazungumzo na maandishi ya Kiimenti. Kwa hivyo, uradidi kama huu na wa vivumishi vingine vya sifa vyenye muundo huu hauna athari zozote za kisemantiki. Vivumishi vingine vyenye muundo huu ni kama **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) katika ngeli ya 5, **bibiraja** [βiβiraɟa] (virefu) katika ngeli ya 8 na **rũrũraja** [rororaraɟa] (mrefu) katika ngeli ya 11. Kulingana na Wa Mberia (1993) kiambishi cha kwanza katika kivumishi **babaraja** [βaβaraɟa] (warefu) kinaweza kuwepo au kudondoshwa. Kwa hivyo, si cha lazima katika kivumishi hicho na vingine vya sifa ambavyo tumeorodhesha katika jedwali la 31. Vivumishi vinavyoundwa kutokana na mchakato wa uradidi hupatikana katika hali ya umoja na wingi. **Babaraja** [βaβaraɟa] (warefu) katika ngeli ya 2 huonyesha wingi ilhali **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) katika ngeli 5 hudhihirisha hali ya umoja. Uradidi unaopatikana katika vivumishi hivi ndiyo hujulikana kama uradidi nusu.

**Jedwali la 31: Vivumishi vya Sifa Vilivyoundwa na Uradidi**

| Ngeli | kipatanishi | kivumishi | maana |
|---|---|---|---|
| 2 A | ba | baraja [βaraɟa] /babaraja[βaβaraɟa] | warefu |
| 5 I/RĨ | rĩ | rĩraja [reraɟa]/rĩrĩraja[rereraɟa] | refu |
| 8 I/BI | bi | biraja [βiraɟa]/bibiraja[βiβiraɟa] | virefu |
| 11 RŨ | rũ | rũraja [roraɟa]/rũrũraja[rororaɟa] | mrefu |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Vivumishi vya Kiimenti vinapoundwa kupitia uradidi uwiano wa irabu hutokea. Uwiano unaotokea unahusu irabu inayopatikana katika kipatanishi, hivi kwamba irabu hiyo inawiana na ya kipatanishi kingine vinapotumika kama viambishi awali vya mzizi wa kivumishi. Kwa mfano, kivumishi **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) rĩ-rĩ-raja katika ngeli ya 5 kina mofu **{rĩ}** na **{-rĩ-},** ambapo **{rĩ-}** ya pili ni uradidi wa ile ya kwanza. Irabu **/ĩ/** inapatikana katika mofu zote. Kulingana na Gacunku (mtaje) huu ni uwiano wa irabu ambao unahusu irabu zinazofanana. Anaendelea kusema kuwa uwiano kama huo unatokana na hali ya uradidi wa mofimu. Uradidi kama huu anauainisha kama mchakato wa mofolojia kuliko fonolojia. Kwa maoni yake si lazima vivumishi kuwa na viambishi awali **{rĩ-}** viwili**.** Hivyo, kivumishi **rĩrĩraja** [rereraɟa] (refu) huweza hata kuwa **rĩraja** [reraɟa] (refu) na kukosa kuzua athari zozote za kisemantiki. Uradidi ambao umetokea hapa unahusu vipatanishi viwili vinavyofanana kuambishwa kama viambishi awali vya

mzizi **{-raja}.** Ni vizuri kufahamu kuwa vipatanishi viwili vinavyofanana haviambishwi kwenye mizizi wa vivumishi katika ngeli zote.

### 5.3.4 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi Viashiria

Uradidi zaidi katika uundaji wa vivumishi hubainika katika vivumishi viashiria vya karibu. Muundo wa vivumishi hivi pia hutawaliwa na vipatanishi vya nomino katika vivumishi. Uradidi kamili na nusu hupatikana katika muundo wa vivumishi viashiria. Muundo wa vivumishi viashiria mbalimbali hubainika katika jedwali la 32 hapo chini.

**Jedwali la 32: Vivumishi Viashiria Vilivyoundwa Kutokana na Uradidi**

| Ngeli | Kipatanishi | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 MU/MW/MŨ | ũ | ũjũ / ũũ [oɟo/o:] | huyu |
| 2 A | ba | baba/baa[βaβa/βa:] | hawa |
| 3 MŨ | jũ | jũjũ /jũũ [ɟuɟu/ɟu:] | huu |
| 4 MĨ | i | ĩjĩ /ĩĩ [eɟe/ ĩ:] | hii |
| 5 I/RĨ | rĩ | rĩrĩ /rĩĩ [rere/re:] | hili |
| 6 MA | ja | jaja/jaa [ɟaɟa/ɟa:] | haya |
| 8 I/BI | bi | bibi/bii [βiβ/βi:] | hivi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 32 linaonyesha kuwa kipatanishi kinaweza kurudiwa jinsi kilivyo (uradidi kamili) au irabu inayopatikana kwenye kipatanishi kurudiwa (uradidi nusu). Kwa mfano katika ngeli ya 3 kipatanishi {**jũ-**} huradidiwa ili kuunda kivumishi kiashiria **jũjũ** [ɟoɟo]

(huu) au kipatanishi na irabu yake kuradidiwa na vikaunda **jũũ** [ɟo:] (huu). Hivyo, basi kivumishi **jũũ** [ɟo:] (huu) kimeundwa kwa irabu ya kipatanishi kurudiwa. Hali ya irabu ya kipatanishi kurudiwa ili kuunda vivumishi viashiria ni mfano wa uwiano wa irabu. Ni muhimu kufahamu kuwa kivumishi **jũjũ** [ɟoɟo] (huu) na **jũũ** [ɟo:] (huu) havina tofauti za kisemantiki. Kwa hivyo, inawezekana kwa vivumishi viashiria kufanyiwa uradidi kamili na nusu na kuwasilisha maana sawa. Mifano zaidi ni vivumishi vingine vyenye mofolojia tuliyojadili hapo juu na huwasilisha maana sawa ni kama, **baba/baa** [βaβa/βa:] (hawa) katika ngeli ya 2, **rĩrĩ/rĩĩ [**rere/re:] (hili) katika ngeli ya 5, **jaja/jaa** [ɟaɟa/ɟaa] (haya) katika ngeli ya 6 na 8. Katika ngeli zingine vivumishi viashiria huzingatia uradidi wa irabu ya kipatanishi pekee. Mifano ya vivumishi hivi ni **ũjũ** [oɟo] (huyu) katika ngeli ya 1 na **iji** [iɟi] (hii) katika ngeli ya 4. Jedwali la 32 linaonyesha jinsi uradidi wa kipatanishi na ule wa irabu ya kipatanishi unavyofanikisha uundaji wa vivumishi viashiria katika ngeli mbalimbali za Kiimenti.

### 5.3.5 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Pekee

Mizizi mingi hutumika katika lahaja ya Kiimenti kuonyesha vivumishi vya pekee. Hii ni kama –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe), **-onthe** [-ɔnθɛ] (-ote), **-nka** [-nka] (bila kuhusisha mtu/kitu) na **–ene** [-ɛnɛ] (-enye). Mchakato wa uradidi hubainika kwa namna moja katika vivumishi vyote vya pekee. Kwa hivyo, tutatumia mzizi **–ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe) kudhihirisha uradidi katika vivumishi vya pekee. Jedwali la 33 linaweza kutumika kuonyesha mchango wa uradidi katika muundo wa vivumishi mbalimbali vya pekee.

**Jedwali la 33: Uradidi katika Uundaji wa Vivumishi vya Pekee**

| Ngeli | Kip | Kivumishi | Maana | Kivumishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 /MŨ/MW | ũ | wengwa | mwenyewe | wewengwa | kusisitiza mwenyewe zaidi |
| 2 A | ba | bongwa | wenyewe | bobongwa | kusisitiza wenyewe zaidi |
| 3 MŨ | jũ | jũngwa | wenyewe | jũjũngwa | kusisitiza wenyewe zaidi |
| 4 MĨ | ĩ | yongwa | yenyewe | yoyongwa | kusisitiza yenyewe zaidi |
| 5 I/RĨ | rĩ | rĩongwa | lenyewe | rĩorĩongwa | kusisitiza lenyewe zaidi |
| 6 MA | ja | jongwa | yenyewe | jojongwa | kusisitiza yenyewe zaidi |
| 7KI/GI | gĩ | kĩongwa | chenyewe | kĩokĩongwa | kusisitiza chenyewe zaidi |
| 8I/bi | bi | biongwa | vyenyewe | biobiongwa | kusisitiza vyenyewe zaidi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Jedwali la 33 linaonyesha mzizi –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe) jinsi ulivyotumika kuunda kivumishi **wengwa** [wɛŋgwa] (mwenyewe) katika ngeli ya 1, **bongwa** [βɔŋgwa] (wenyewe) katika ngeli ya 2, **jũngwa** [ɟoŋgwa] (wenyewe) katika ngeli ya 3, **yongwa** [jɔŋgwa] (yenyewe) katika ngeli ya 4, **rĩongwa** [reɔŋgwa] (lenyewe) ngeli ya 5, **jongwa** [ɟɔŋgwa] (yenyewe) katika ngeli ya 6, **kĩongwa** [keɔŋgwa] (chenyewe) ngeli ya 7 na **biongwa** [βiɔŋgwa] (vyenyewe) katika ngeli ya 8. Vivumishi hivi vinaweza kuunda vivumishi vinavyoonyesha uradidi. Mfano mmoja ni kivumishi **wewengwa** [wɛwɛŋgwa] (kusisitiza mwenyewe zaidi) katika ngeli ya 1 ambacho kinaonyesha uradidi wa kiambishi awali **{we-}** kwenye mzizi wa kivumishi. Vivumishi vingine vinaweza

kuundwa kutumia utaratibu huu katika ngeli mbalimbali kama **bobongwa** [βɔβɔŋgwa]**, jũjũngwa** [ɟoɟoŋgwa], **yoyongwa** [jɔjɔŋgwa], **rĩorĩongwa** [reɔreɔŋgwa]**, jojongwa** [ɟɔɟɔŋgwa]**, kĩokĩongwa** [keɔkeɔŋgwa]na **biobiongwa** [βiɔβiɔŋgwa]**.** Uradidi nusu uliofanyika hapa unahusu kipatanishi au kiambishi awali cha kivumishi cha pekee. Maana inayojitokeza baada ya uradidi huo ni ile ya kusisitiza zaidi nomino ya ngeli.

Inafaa ifahamike kuwa vivumishi vya pekee kama **wengwa** [wɛŋgwa] (mwenyewe) na vingine vyenye muundo huo hufanyiwa uradidi kamili na kuunda vivumishi kama **wengwawengwa** [wɛ ŋgwawɛŋgwa] (mwenyewemwenyewe), **yongwayongwa** [jɔŋgwajɔŋgwa] (yenyeweyenyewe), **rĩongwarĩongwa** [reɔŋgwareɔŋgwa] (lenyewelenyewe), **jongwajongwa** [ɟɔŋgwaɟɔŋgwa] (yenyeweyenyewe), **kĩongwakĩongwa** [keɔŋgwakeɔŋgwa] (chenyewechenyewe) na **biongwabiongwa** [βiɔŋgwaβiɔŋgwa] (vyenyewevyenyewe). Uradidi kamili ambao unajitokeza hapa unahusisha kivumishi chote ambapo sehemu ya viambishi na mzizi huradidiwa. Vivumishi vinavyoundwa baada ya uradidi huu vinadhihirisha jinsi mchakato huo hutumika kuunda maneno changamani (Marantax, mtaje). Vivumishi vinavyoundwa kupitia utaratibu huu katika ngeli zote hutoa dhana ya kusisitiza zaidi. Kwa hivyo, kimaana hakuna tofauti ya **bobongwa** [βɔβɔŋgwa] na **bongwabongwa** [βɔŋgwaβɔŋgwa] kwani vyote hutoa dhana ya kusisitiza zaidi. (Kanan, mtaje).

### 5.3.6 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya Idadi

Idadi isiyo kamili huonyeshwa kwa kutumia mizizi **–kai** [kai] (-chache) na **–ingĩ** [-inge] (ingi). Mizizi hii huambishwa kipatanishi kimoja au viwili ambavyo vinafanana ili kuunda vivumishi vya Kiimenti. Muundo wa vivumishi hivyo unadhihirika katika jedwali la 34 hapo chini.

**Jedwali la 34: Uundaji wa Vivumishi vya Idadi Kupitia Uradidi**

| Ngeli | kipatanishi | Kivumishi –ingĩ [-inge] (-ingi) | Maana |
|---|---|---|---|
| 2 A | ba | baingĩ /babaingĩ [βaiŋge/βaβaiŋge] | wengi |
| 2 A | ba | bakai/babakai [βakai /βaβakai] | waachache |
| 5 1/RI | ri | ringĩ/rĩringĩ [riŋge]/reriŋge] | kuonyesha wingi |
| 8 I/BI | bi | bingĩ /bibingĩ [βiŋge /βiβiŋge] | vingi |
| 11 RŨ | rũ | rwingĩ /rũrwingĩ [rwiŋge /rorwiŋge] | mengi |
| 13 Ũ | bũ | bwingĩ /bũbwingĩ [βwiŋge/βoβwiŋge] | mwingi |
| 14 Ũ | bũ | bwingĩ /bũbwingĩ [βwiŋge /βoβwiŋge] | mwingi |
| 15 Ũ | bũ | bwingĩ /bũbwingĩ [βwiŋge /βoβwiŋge] | mwingi |

Asili: Data ya Nyanjani (2022)

Kulingana na jedwali la 34 hapo juu kipatanishi cha ngeli ya 2 ni **{ba-}** ambacho huambishwa mizizi **–kai** [kai] (-chache) na **–ingi** [-inge] (-ingi) ili kuunda vivumishi vya idadi, **bakai/babakai** [βakai/βaβakai] (wachache) na **baingĩ /babaingĩ [**βaiŋge/βaβaiŋge] (wengi). Kivumishi **bakai** [βakai] na **babakai** [βaβakai] huwasilisha maana sawa. Aidha, kivumishi **baingĩ** [βaiŋge] na **babaingĩ** [βaβaiŋge] huwa na maana moja. Jambo lililotokea katika kuunda kivumishi **babakai [**βaβakai]na **babaingĩ** [βaβaiŋge] ni kuwa kipatanishi kimerudiwa kama kiambishi awali katika mizizi ya vivumishi. Hali hii ni kama ilivyoelezwa na Mbaabu (mtaje) kuwa mizani ya kwanza katika neno huweza kufanana na ile ya pili katika mchakato wa uradidi. Mifano mingine ya uradidi ni **bibingĩ**

**[**βiβiŋge] (vingi) katika ngeli 8, **rũrwingi** [rorwiŋge] (mengi) katika ngeli ya 11, **bũbwingĩ** [βoβwiŋge] (mwingi) katika ngeli ya 13, 14 na 15. Uradidi nusu ndio unahusika katika uundaji wa vivumishi hivi. Jedwali la 34 linaeleza hali hiyo.

### 5.3.7 Uradidi katika Muundo wa Vivumishi vya mkopo

Uradidi zaidi unahusu vivumishi vya mkopo vilivyoingia katika lahaja ya Kiimenti kama **cawa** [cawa] (sawa), **atarĩ** [atare] (hatari) na vingine vingi. Vivumishi kama hivi hufanyiwa urudufu kamili na kuunda vivumishi kama **cawacawa** [cawacawa] (sawasawa) na **atarĩtarĩ** [atareatare] (hatarihatari).

### 5.3.8 Dhima ya Uradidi katika Vivumishi vya Kiimenti

Uradidi una dhima kadhaa (Lodhi, 2004). Tunaweza kutumia vivumishi vya Kiimenti kudhihirisha baadhi ya dhima hizo. Ifahamike kuwa uradidi hufanya neno kupata maana mpya (Frawley, mtaje). Kwa mfano uradidi wa mizizi ya vivumishi hufanya kivumishi kubadilisha maana na kudokeza dhana ya ulinganishi. Dhana ya vivumishi vilinganishi (comparative adjectives) katika lugha ya Kiswahili ilidokezwa na mwanasarufi mapokeo aliyejulikana kama Broomfield (mtaje). Vivumishi vya sifa na vile vya idadi ndivyo hutoa dhana ya ulinganishi baada ya mizizi kurudiwa. Kwa mfano, kivumishi **ũmũraja** [omoraɟa] (mrefu) katika ngeli ya 1 huradidiwa mzizi na kuunda kivumishi **ũmũrajaraja** [omoraɟaraɟa] (mrefu zaidi). Kivumishi cha idadi **ĩmingĩ** [emiŋge] (mingi) katika ngeli ya 3 hurudiwa mzizi wake na kuunda kivumishi **ĩmingaingĩ** [emiŋgaiŋge] (mingi zaidi). Kwa hivyo, inawezekana uradidi kuathiri sehemu ya mzizi pekee bila kuhusisha sehemu zingine za neno (Alsamadani na Taibah, wataje). Inapofanyika hivyo maana ya neno kama kivumishi hubadilika (Kouwenberg na Darlene, 2003). Uradidi unapotokea, kivumishi **ũmũrajaraja** [omoraɟaraɟa] (mrefu zaidi) hakionyeshi mabadiliko ya sauti

kwenye mzizi kwa sababu unarudiwa jinsi ulivyo. Uradidi wa namna hii ambapo mzizi hurudiwa jinsi ulivyo bila mabadiliko yoyote ya sauti hujulikana kama uradidi sahili (Rubino, mtaje). Hata hivyo, kivumishi **gĩkĩthũku** [gekeθoku] (kibaya) na **ĩmingĩ [**emiŋge] (mingi) hurudiwa sehemu ya mzizi na kuunda **gĩkĩthukathũku** [gekeθokaθoku] (kibaya zaidi) na **ĩmingaingĩ [**emiŋgaiŋge] (mingi zaidi). Hapa sehemu ya mzizi inaonyesha mabadiliko ya sauti. Irabu ya nusu juu /u/ inadondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /a/ ambayo ni ya chini. Kulingana na Kanana (mtaje) irabu /a/ inafanya kivumishi kupata dhana ya ulinganishi, na hivyo irabu hiyo ina uamilifu wa ulinganishi katika vivumishi vya kiimenti. Mabadiliko kama hayo ya sauti yanafanyika ili kusawazisha matamshi au kuleta uwiano wa kifonolojia (Sharum na Wenzie, 2010).

Aidha uradidi hufanya baadhi ya maneno kuonyesha hali ya kutilia jambo mkazo (Ashton, mtaje; Mbaabu, mtaje; Nyagah, 2014). Kwa mfano, kivumishi **iji** [iɟi] (hizi) kinapofanyiwa urudufu kamili kinakuwa **ijiiji** [iɟi:ɟi] (hizihizi) kuonyesha hali ya kusisitiza au kutilia jambo fulani mkazo. Hali ya uradidi kuleta dhana ya kusisitiza imetiliwa mkazo na (Bussmann, mtaje; Biwott na Ong'onda wataje). Aidha, kivumishi kiashiria **ũjũ** [oɟo] (huyu) kinapofanyiwa urudufu kamili kinaunda kivumishi **ũjũũjũ [**oɟo:ɟo] (huyuhuyu) kuonyesha dhana ya kusisitiza. Hali zaidi ya kusisitiza inatolewa na vivumishi vya pekee kama **wengwa** [wɛŋgwa] (mwenyewe) ambacho baada ya uradidi vivumishi **wengwawengwa** [wɛŋgwawɛŋgwa] na **wewengwa** [wɛwɛŋgwa] huundwa vikiwa na maana ya kusisitiza mwenyewe zaidi.

Pia, uradidi hubadili umbo la kivumishi ambapo umbo jingine la mzizi huibuka. Kwa mfano, kutokana na kivumishi **ũmũraja** [omoraɟa]/ũ-mũ-raja/ (mrefu) kivumishi **ũmũrajaraja** [omoraɟaraɟa]/ũ-mũ-rajaraja/ (mrefu zaidi) kinaweza kuundwa. Kwa

hivyo, mzizi wa kivumishi unabadilika kutoka {**-raja**} hadi {**-rajaraja**}. Aidha, umbo **ũmũrajaraja** [omoraɟaraɟa] (mrefu zaidi) ni tofauti na **ũmũraja** [omoraɟa] (mrefu). Kwa hivyo, uradidi una uwezo wa kubadili hata umbo zima la kivumishi.

Pamoja na hayo, uradidi hutumika kuonyesha idadi katika vivumishi vya Kiimenti. Kwa mfano, **inya** [iɲa] (nne) ni kivumishi cha idadi kinachotumika kuunda kivumishi **inyanya** [iɲaɲa](nane) baada ya uradidi wa mzizi wa kivumishi. Komu (2008), Kanana (mtaje), Biwott na Ong'onda wataje) hutambua kuwa dhima moja ya uradidi ni kuonyesha wingi wa vitu fulani. Hatimaye, uradidi husaidia katika uundaji wa vivumishi vyenye maana sawa kama **baraja/babaraja** [βaraɟa/βaβaraɟa] (warefu), **rĩraja/rĩrĩraja** [reraɟa/rereraɟa] (refu), **biraja/bibiraja** [βiraɟa/βiβiraɟa] (virefu) pamoja na vivumishi vingine. Kwa hivyo, uradidi una nafasi ya kupanua msamiati wa lugha.

## 5.4 Uhusiano wa Fonetiki na Mofolojia katika Uchanganuzi wa Vivumishi vya Kiimenti

Ngazi za fonolojia na mofolojia huingiliana. Hii ni kwa sababu baadhi ya fonimu zilizo kwenye mipaka ya mofu huathiriana na kusababisha mabadiliko ya kifonetiki. Hii ndiyo sababu kuna michakato ya kimofonolojia katika lugha. Hii ina maana kuwa kuna mabadiliko ya sura ya mofu ambayo hutokana na kuathiriana kwa fonimu zilizo kwenye mipaka ya mofu zinazopakana (Mgullu, 1999). Kwa mfano, kivumishi cha Kiimenti **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi) kikichanganuliwa kimofemiki ili kudhihirisha umbo la ndani kitakuwa na mofu hizi /**ũ -mũ -irũ** / (mweusi). Katika kivumishi hiki fonimu /ũ/ ya kiambishi inaathiriana na fonimu /i/ ya mzizi na kuwa fonimu /w/. Haya ni mabadiliko ya kifonetiki kwa sababu fonimu /i/ na /ũ/ ni fonimu zenye sifa bainifu tofauti.

Mfano mwingine unaoweza kutumiwa kuonyesha jinsi fonimu huathiriana kenye mipaka ya mofu unahusu udondoshaji wa baadhi ya fonimu hasa pale kuna uziada. Kwa mfano, katika kivumishi cha idadi **ĩmingĩ [**emiŋge] (mingi) huweza kuwa na umbo hili la ndani / **ĩ-mi-ingĩ**/ (mingi). Kutokana na kuwepo kwa mfuatano wa fonimu /i/ moja yazo inadondoshwa na kivumishi kinachoundwa kinakuwa **ĩmingĩ** [emiŋge] (mingi). Fonimu inayodondoshwa ni ile inayopatikana kwenye kiambishi. Kwa hivyo, kuathiriana kwa fonimu kwenye mipaka ya mofu kunazua fonimu nyingine tofauti ambazo zinasababisha mabadiliko ya mofu. Mofu zinazozopatikana huweza kuwa na fonimu tofauti na zilizokuwepo kabla ya kuathiriana katika mipaka ya mofu. Ni vizuri kufahamu kuwa fonimu ni suala la kifonetiki na mofu ni suala la kimofolojia. Hata hivyo, si rahisi kuweka mpaka wazi kati ya taaluma ya fonetiki na mofolojia. Hii ni kwa sababu zinaingiliana.

Vilevile fonolojia na mofolojia huhusiana kwa hali nyingine. Hii ni kwa sababu fonolojia ya lahaja ya Kiimenti hujichagulia sauti zake kutoka kwa bohari la sauti. Sauti zinazochaguliwa ni kama /u/, /m/, /n/, /t/ na kadhalika. Sauti hizi huungana na kuunda silabi kama $mu$ na $ntu$. Silabi hizi zinapoundwa sauti haziungani kiholela bali huzingatia mfumo wa KV au KKV. Mifumo hii ndiyo hutumika katika lugha nyingi za Kibantu. Silabi hizi huungana baadaye na kuunda neno kama **muntũ** [munto] (mtu). Hali ya sauti kuungana na kuunda maneno huweza kuchunguzwa katika kima cha fonolojia. Maneno haya yanapoundwa kuna taaluma nyingine ya isimu ambayo huchunguza jinsi yalivyoundwa kwa kutumia mofimu mbalimbali zenye usarufi. Hii ni taaluma ya mofolojia. Katika mofolojia neno kama **muntũ** [munto] (mtu) huchanganuliwa kimofemiki na kuwa na mofimu hizi:

{mu} mofimu ya idadi (umoja)

Mofimu ya ngeli ya MŨ/MW/MU

Mofimu ya kiambishi awali cha nomino

{-ntũ } mzizi wa kitenzi unaobeba maana ya kileksia.

Kwa hivyo, mofolojia badala ya kuchanganua neno kwa misingi ya sauti/fonimu zake inazingatia mofimu zake. Neno mtu (**muntũ)** [munto] lina mofu mbili lakini mofimu ni nne. Kwa jinsi hiyo fonolojia inahusiana na mofolojia.

### 5.5 Ruwaza za Vivumishi Mbalimbali katika Tungo za Kiimenti

Ruwaza za vivumishi katika tungo hurejelea mipangilio ya vivumishi mbalimbali vinapofuatana katika sentensi kwenye lugha yoyote. Hali hii inabainika katika lahaja ya Kiimenti. Ruwaza hizi hujitokeza katika sentensi kwa kuzingatia sheria fulani. Kwa mujibu wa Barber na Wenzake (2003) ni vigumu kueleza sheria hizi lakini watumiaji wa lugha huzijua na huzizingatia. Katika lahaja ya Kiimenti imebainika kuwa vivumishi vya pekee, vivumishi vya kumiliki, vivumishi vya idadi, vivumishi viulizi, vivumishi vya sifa, vivumishi vya majina na vivumishi viashiria hutangulia vingine katika sentensi mbalimbali. Kwa hivyo, ruwaza husika zinaongozwa na vivumishi hivi vikitangulia vingine katika sentensi anuwai. Kutokana na hali hii ruwaza zinazohusu vivumishi hivi zimejadiliwa katika sehemu inayofuata.

#### 5.5.1 Ruwaza za Kivumishi cha Pekee na Kivumishi kingine

Kulingana na Coates (1977) ruwaza ya vivumishi viwili ndiyo hupatikana kwa wingi katika lugha ya Kiingereza. Hali hii si tofauti na ile inayodhihirika katika lahaja ya Kiimenti. Kwa mfano, kivumishi cha pekee huweza kutangulia kingine cha aina hiyo katika sentensi. Pia, hutangulia kingine kama vile cha a - unganifu, sifa, idadi, kiashiria,

kimilikishi, cha jina na kiulizi. Kinapotumika pamoja na kingine ndicho hukitangulia na kwa ujumla kuunda ruwaza nane. Kwa mfano, vivumishi viwili vya pekee huweza kufuatana na kuunda ruwaza moja. Hata hivyo, kivumishi **–ngĩ** [-ŋge] (- ingine) ndicho hutangulia –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe), –**nthe** [-nθɛ] (-ote) na na –**nka** [-nka] (bila kuhusisha). Hii ina maana **–ngi** [-ŋge] (-ingine) hufuata nomino inayovumishwa na kufuatwa na mojawapo wa kivumishi kingine cha pekee. Sentensi zifuatazo zinaonyesha mfuatano wa vivumishi vilivyoundwa kutokana na mizizi **–ngi** [-ŋge] (- ingine), –**ngwa** [-ŋgwa] (-enyewe), –**nthe** [-nθɛ] (-ote) na na –**nka** [-nka] (bila kuhusisha).

1 (i) *Njogu yakarĩirie kĩthima* ***kĩngĩ  yongwa***.

[nɟɔgu jakareriɛ keθima keŋge jɔŋgwa]

Ndovu alichunga kisima **kingine mwenyewe**.

(ii) *Arĩmi* ***bangĩ   bongwa*** *ba marigũ bagatethua I thirikari.*

[Aremi βaŋgi βɔŋgwa βa marigo βagatɛθua I θirikari]

Wakulima **wengine wenyewe** wa ndizi watasaidiwa na serikali.

(iii) *Antũ bangĩ*  ***bonthe*** *bakwĩja.*

[Anto βaŋge βɔnθɛ βakweɟa]

Watu **wengine wote** wamekuja.

(iv) *Njĩra* ***ingĩ  cionthe*** *ni I nthũku.*

[Nɟira iŋge ciɔnθɛ ni I nθoku]

Barabara **nyingine zote** ni mbaya.

(v) *I muntu* ***ũngĩ  wenka*** *weja.*

[ I munto oŋge wɛnka wɛɟa]

Ni mtu **mwingine pekee** amekuja.

(vi) *Mpenderia mpoka **ĩngĩ yonka.***

[Mpɛndɛria mpɔka eŋge jɔnka]

Niuzie mboga **nyingine pekee**.

Ruwaza nyingine inahusu kivumishi cha pekee kikitokea kabla ya kile cha a – unganifu.

Sentensi zifuatazo zinaweza kutumika kueleza ruwaza hii:

2) (i) *Nyama ya kũgũrũ* ***kunthe kwa*** *mbũri ikũrugwa.*

[ɲama ja kogoro kunθɛ kwa mβori ikorugwa]

Nyama ya mguu **wote wa** mbuzi imepikwa.

(ii) *Matĩ **jonthe ja** nyomba jagatewa kenda kwĩthĩrwa kwĩna ũtherũ.*

[mate ɟɔθnθɛ ɟa ɲɔmβa ɟagatɛwa kɛnda kweθerwa kwena oθɛru]

Takataka **yote ya** nyumba itatupwa ili kuwe na usafi.

(iii) *Aini **bongwa ba** ndwĩmbo bakeja gũtwinĩra.*

[aini βɔŋgwa βa ndwemβɔ βakɛɟa gotwinera]

Waimbaji **wenyewe wa** nyimbo watakuja kutuimbia

(iv) *Antũ **bongwa ba** kũrĩma bakwĩja.*

[anto βɔŋgwa βa korema βakweɟa]

Watu **wenyewe wa** kulima wamefika.

(v) *Ũntũ **bũngi bwa** Kangangi bwarĩ kwĩnja mĩnyororo.*

[onto βoŋge βwa Kaŋgaŋgi βware kwenɟa meɲɔrɔrɔ]

Jambo **jingine la** Kangangi lilikuwa kutengeneza barabara.

(vi) *Antũ **bangĩ ba** Kenya batijĩ kũthoma na kũandika.*

[anto βaŋge βa Kɛɲa βatiɟe koθɔma na koandika]

Watu **wengine wa** Kenya hawajui kusoma na kuandika.

Pia, kivumishi cha pekee hutangulia kivumishi cha sifa na kuunda ruwaza ya tatu ambayo inabainika katika sentensi zinazofuata:

(3 (i) *Nyomba* ***ĩngĩ ĩnene*** *ĩgakwa au.*

[ɲɔmβa eŋge enɛnɛ egakwa au]

Nyumba **nyingine kubwa** itajengwa hapo.

( ii) *Mwekũrũ* ***ũngi ũmũnoru*** *akwĩja kũgũra maembe.*

[mwɛkoro oŋge omonɔru akweja kogora maɛmbɛ]

Mwanamke **mwingine mnene** amekuja kununua maembe.

(iii) Into **bionthe bithongi** biarĩ bia Mũmerũ.

[into βiɔθɛ βiɔθŋgi βiare βia Momɛro]

Vitu **vyote vizuri** vilikuwa vya Mumeru.

(iv) Nkoraga nyomoo **cionthe inkũrũ.**

[nkoraga ɲɔmɔ: ciɔnθɛ inkoro]

Nitaua wanyama **wote wazee**.

(v) *Muntũ* ***ũngi ũmwega*** *akũgũra marigũ jakwa.*

[munto oŋge omwɛga akogora marigo ɟakwa]

Mtu **mwingine mzuri** amenunua ndizi zangu.

Aidha, kuna ruwaza inayoundwa kwa kutumia kivumishi cha pekee **-ngĩ** [-nge] (-ingine) kikitokea kabla ya kile cha idadi –**ingĩ** [-inge] (-ingi) na kuunda ruwaza inayodokezwa hapa chini:

(4) (i) *Mathĩna* ***jangĩ jamaingĩ*** *ijamũgwete.*

[maθena ɟaŋge ɟamaiŋge iɟamogwɛtɛ.

Taabu **zingine nyingi** zimemkumba.

(ii) *Muntũ **ũngi ũmwe** akwĩja.*

[munto oŋgi omwɛ akweɟa]

Mtu **mwingine mmoja** amekuja.

(iii) Kĩama **kĩngĩ kĩmwe** gĩkũthithua.

[keama keŋge kemwɛ gekuθiθua]

Chama **kingine kimoja** kimeundwa.

(iii) Antũ **bangĩ babaingĩ** bakeja.

[anto βaŋge βaβaiŋge βakɛɟa]

Watu **wengine wengi** watakuja.

Vilevile, kivumishi cha pekee huweza kutangulia kiashiria katika sentensi za Kiimenti. Ashton (mtaje) anaeleza kuwa mpangilio kama huu hutokea hata katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inaweza kuelezwa na dhana kuwa Kiimenti ni lugha ya Kibantu sawa na kilivyo Kiswahili, na hivyo huweza kuhusiana katika masuala fulani kimuundo. Ruwaza hiyo inadhihirika katika sentensi hizi:

(5) (i) *Into **bionthe birĩa** bikwendeka bikagũrwa.*

[intɔ βiɔnθɛ βirea βikwɛndɛka βikagorwa]

Vitu **vyote vile** vinahitajika vitanunuliwa.

(ii) *Antũ **bonthe barĩa** barĩ na thĩna bagatethua.*

[anto βɔnθɛ βarea βare na θena βagatɛθua]

Watu **wote wale** wana shida watasaidiwa.

(iii) *Mauku **jangĩ jarĩa** jaandĩki ijakwendua.*

[mauku ɟaŋge ɟarea ɟa:ndeki iɟakwɛndua]

Vitabu **vingine vile** vimeandikwa vinauzwa.

(iv) *Antũ bangĩ* ***barĩa*** *bagakinya bakaritanwa mantũ ja urĩmĩ.*

[anto βaŋge βarea βagakiɲa βakaritanwa manto ɟa ureme]

Watu **wengine wale** watafika watafundishwa mambo ya ukulima.

Pamoja na hayo, ikiwa kivumishi cha pekee na kimilikishi vitatumika pamoja vitaunda ruwaza nyingine. Hali hii inajitokeza katika sentensi hizi:

(6) (i) *Gikundi* ***kĩngĩ kĩao*** *kĩgwĩta buru.*

[gikundi keŋge keaɔ kegweta βuru]

Kikundi **kingine chao** kimeenda kabisa.

(ii) *Antũ* ***bangĩ bao*** *bakeja rũũjũ.*

[anto βaŋge βaɔ βakɛɟa ro:jo]

Watu **wengine wao** watakuja kesho.

(iii) *Ngarĩ* ***ĩngĩ yakwa*** *ĩgũkinya.*

[ɲgare eŋge jakwa egokiɲa]

Gari **lingine langu** limefika.

(iv) *Muntũ* ***ũngĩ wao*** *akwĩja aja.*

[munto oŋge wao akweɟa aɟa]

Mtu **mwingine wenu** amekuja hapa.

(v) *Kĩbanga* ***kĩngi gĩakwa*** *gĩkũra*.

[keβaŋga keŋge geakwa gekora]

Upanga **mwingine wangu** umepotea.

Zaidi ya hayo, kivumishi cha pekee na kile cha jina huunda ruwaza nyingine tofauti. Ruwaza hii inabainika katika sentensi inayofuata:

(7) *Antũ* ***bonthe Amerũ*** *bakathoma iuku rĩu.*

[anto βɔnθɛ Amɛro βakaθɔma iuku reu]

Watu **wote wameru** watasoma kitabu hicho.

Ifahamike kuwa kivumishi cha pekee hutangulia kivumishi kiulizi na kuibua ruwaza nyingine kama inavyojitokeza hatika sentensi zifuatazo:

(8) (i) *Ni muntũ* ***ũngĩ ũrĩkũ*** *weja?*

[Ni munto oŋge oreko wɛɟa?]

Ni mtu **mwingine yupi** amekuja?

ii) "*Ni nyoni* ***ĩngĩ ĩrĩku*** *itigi ĩgũrũ?" Nyoni irorania ciongwa.*

[ni ɲɔni eŋge ereko itigi egoro? ɲɔni irɔrania ciɔngwa].

"Ni ndege **wepi wengine** wamebaki juu?" Ndege waliulizana wenyewe.

(iii) "*Ni muntũ* ***ũngi ũrĩkũ*** *ũkwenda kũngũrĩra mpoka?" Mwekũrũ ũmwe aroria].*

[ni munto oŋge oreko okwɛnda koŋgorera mpɔka? mwɛkoro omwɛ arɔria].

"Ni mtu **yupi mwingine** anataka kuninunulia mboga?" Mama mmoja akauliza.

(iv) *I ngarĩ* ***ĩngĩ ĩrĩkũ*** *ĩtĩrakinya? Muntũ ũmwe aroria.*

[I ŋgare eŋge ereko eterakiɲa? munto omwɛ arɔria.]

Ni gari **ipi nyingine** haijafika?

Sheria moja inaweza kujumlisha ruwaza 1– 8 zinazoibuka kivumishi cha pekee kinapotumika na kingine katika sentensi moja. Maelezo yake ni kuwa kivumishi cha pekee huweza kutangulia kingine cha pekee, a – unganifu, sifa, idadi, jina, kiashiria, kimilikishi au kiulizi. Sheria hiyo tunaweza kuiandika hivi:

(9) *kivumishi cha pekee; kivumishi cha a – unganifu; kivumishi cha sifa; kivumishi cha idadi; kivumishi cha jina; kiashiria; kimilikishi; kiulizi.*

Inafaa ieleweke kuwa mkururo wa vivumishi zaidi ya viwili huweza kutokea katika sentensi moja. Vinapotokea katika sentensi vyote hutumika kufafanua nomino inayovitangulia. Mpangilio wake hudhibitiwa na hali za kisemantiki bali havifuatani kiholela (Dixon, 1982). Kuhusiana na hali hii, Nthenya (2009) akimrejelea Radford (2004), anakariri kuwa vivumishi viwili au vitatu hufuatana katika sentensi. Hali kama hii inadhihirika wakati kivumishi cha pekee hutangulia vivumishi vingine viwili. Ruwaza moja yenye vivumishi vitatu inahusu kivumishi cha pekee kikitangulia kiashiria na kivumishi cha sifa kikitokea katika nafasi ya tatu. Sentensi hizi inaonyesha hali hiyo:

(10) (i) *Mũũro **jũngĩ jũrĩa mũnene** jwĩtagwa Kathita.*

[mo:rɔ ɟoŋge ɟorea monɛnɛ ɟwetagwa Kaθita]

Mto **mwingine ule mkubwa** unaitwa Kathita.

(ii) *Kĩrĩma **kĩngĩ kĩrĩa kĩnene** kĩrĩ au.*

[kerema keŋge kerea kenɛnɛ kere au]

Mlima **mwingine ule mkubwa** uko hapo.

(iv) *Njogu **ĩngĩ ĩrĩa nene** irakinya nthĩ na inya.*

[nɟɔgu iŋge irea nɛnɛ irakiɲa nθe na iɲa]

Ndovu **wengine wale wkubwa** walikanyaga ardhi kwa nguvu.

(v) *Antũ **bangĩ barĩa beega** bagwĩta.*

[Anto βaŋge βaria βɛ:ga βagweta]

Watu **wengine wale wazuri** wameenda.

(vi) *Muntũ **ũngĩ ũria mũnene** akeja aja.*

[munto oŋge orea monɛnɛ akɛɟa aɟa]

Mtu **mwingine yule mkubwa** atakuja hapa.

(vii) *Mbũri* ***ingĩ irĩa noru*** *cikũthinjwa.*

[mbori iŋge irea nɔru cikoθinɟwa]

Mbuzi **wengine wale wanono** wamechinjwa.

Ruwaza nyingine inayohusu kivumishi cha pekee na vivumishi vingine ni pale kinatokea kabla ya kivumishi cha sifa na kivumishi kiashiria kuwa cha mwisho katika sentensi. Ruwaza hiyo inabainika katika sentensi hizi:

(11) (i) *Chibũ naraberĩre mantũ* ***jonthe jamerũ jarĩa*** *thirikari ikwenda.*

[ʧiβo naraβɛrerɛ manto ɟɔnθɛ ɟamɛro ɟarea θirikari ikwɛnda]

Chifu aliwaambia mambo **yote mapya yale** serikali inataka.

(ii) *Jau nĩ mantũ jangĩ jamega jarĩa nkũmenya.*

[ɟau ne manto ɟaŋge ɟamɛga ɟarea nkomɛɲa]

Haya ni **mambo mengine mazuri** yale najua.

Aidha, mfuatano wa vivumishi vya pekee, a -unganifu na kile cha idadi huunda ruwaza nyingine. Sentensi zifuatazo zinaweza kutumika kueleza hali hiyo:

(12) (i) *Mwekũrũ ũũ ena rũgono* ***rũngĩ rwa ithatũ.***

[mwɛkoro o: ɛna rogɔnɔ roŋge rwa iθato]

Mwanamke huyo ana hadithi **nyingine ya tatu**.

(ii) *Mwekũrũ ũũ ena mwana* ***ũngĩ wa batano***.

[mwɛkoro o: ɛna mwana oŋge wa βatanɔ]

Mwanamke huyu ana mtoto **mwingine wa tano**.

(iii) *Ngarĩ* ***ĩngĩ ya ithanthatũ*** *ĩgũkũrũka.*

[ŋgare eŋge ɉa iθanθato egokoroka]

Gari **jingine la sita** limepita.

(iv) *Muntũ **ũngi wa mũgwanja** akwĩja.*

[munto oŋge wa mogwanɟa akweɟa]

Mtu **mwingine wa saba** amekuja.

(vi) *Mũguongo ena mũka **ũngĩ wa bathatũ**.*

[moguɔŋgɔ ɛna moka oŋge wa βaθato]

Muguongo ana mke **mwingine wa tatu.**

Pia, kivumishi cha pekee hufuatwa na kivumishi cha idadi na kivumishi cha a - unganifu ili kuunda ruwaza ifuatayo:

(13) *Antũ **bangi babaingĩ ba** kũrĩma bakeja.*

[anto βaŋge βaβaiŋge βa korema βakɛɟa]

Watu **wengine wengi wa** kulima watakuja.

Ruwaza ya mwisho kuhusu kivumishi cha pekee ni pale kinapotangulia kingine cha pekee na cha a - unganifu kikichukua nafasi ya mwisho katika sentensi. Sentensi ifuatayo inaonyesha hali hii:

(14) *Munda **jungĩ junthe jwa** cukuru jũkũrĩmwa.*

[munda ɟuŋge ɟunθɛ ɟwa cukuru ɟokoremwa]

Shamba **lingine lote la** shule limelimwa.

Ruwaza tano zinazojitokeza katika 10 – 14 wakati kivumishi cha pekee huandamana na vingine viwili katika sentensi huweza kuelezwa kutumia sheria hizi nne:

(15) (a) *Kivumishi cha pekee; kiashiria; kivumishi cha sifa.*

(b) *Kivumishi cha pekee; kivumishi cha sifa; kivumishi kiashiria.*

(c) *Kivumishi cha pekee; a - unganifu; kivumishi cha idadi.*

(d) *Kivumishi cha pekee; Kivumishi cha pekee; kivumishi cha idadi; a - unganifu;*

### 5.5.2 Ruwaza za Kimilikishi na Kivumishi Kingine

Kimilikishi hutokea kabla ya vivumishi mbalimbali na kuunda ruwaza kadhaa. Ruwaza moja inahusisha kimilikishi na kivumishi cha a – unganifu kama inavyoonekana katika mfano wa sentensi zifuatazo:

(16) (i) *Kauntĩ* ***yetũ ya*** *Meru ni ĩnthongi mono.*

[kaunte jeto ja Mɛru ni enθɔɲgi mɔnɔ]

Kaunti **yetu ya** Meru ni nzuri sana.

(ii) Into **biakwa bia** kwendia bikũgũrwa bionthe.

[intɔ βiakwa βia kwɛndia βikogorwa βiɔnθɛ]

Bidhaa **zangu za** kuuza zimenunuliwa zote.

(iii) *Ngarĩ* ***yetũ ya*** *mĩrĩgo ĩkũthũka.*

[ŋgare jɛto ja meregɔ ekoθoka]

Gari **letu la** mizigo limeharibika.

(iv) *Ũthongi* ***bwetũ bwa*** *Meru ibũkũgwĩria antũ babaingĩ mono*.

[uθɔŋgi βwɛto βwa Mɛru iβokogweria anto βaβaiŋge mɔnɔ]

Uzuri **wetu wa** Meru unafurahisha watu wengi sana.

(v) *Ĩgita* ***rĩawe rĩa*** *mũthia rĩgũkinya nandĩ.*

[egita reawɛ rea moθia regokiɲa nande]

Wakati **wake wa** mwisho umefika sasa.

Ruwaza ya pili ni pale kimilikishi kinafuatwa na kivumishi kiashiria kama inavyodhihirika katika sentensi hizi:

(17) (i) *Mũbira* ***jwawe jũrĩa*** *jwaũrĩte jũkwonora.*

[moβira ɟwawɛ ɟorea ɟwaoretɛ ɟokwɔnɔra]

Mpira **wake ule** uliokuwa umepotea umepatikana.

(ii) *Iuku* ***rĩao rĩrĩa*** *rĩaurĩre rĩkwonora.*

[iuku reaɔ rerea reaurerɛ rekwɔnɔra]

Kitabu **chao kile** kilikuwa kimepotea kimepatikana.

(iii) *Mwekũrũ atigĩirwe na mũcore* ***wawe ũrĩa*** *wetagwa Chiomũchio.*

[mwɛkoro atigerwɛ na mocɔrɛ wawɛ orea wɛtagwa ʧiɔmoʧiɔ]

Mwanamke aliachwa na rafiki **yake yule** aliyekuwa akiitwa Chiomuchio.

(iv) *Twaana nĩ twa mũkũrũ* ***wawe ũrĩa*** *wakuĩre.*

[twa:na ne twa mokoro wawɛ orea wakuerɛ]

Watoto ni wa bwana **yake yule** aliyekufa.

(v) *Mwekũrũ ũrĩa arĩraga mono nĩũntũ bwa twana* ***twawe tũrĩa*** *twakuĩre.*

[mwɛkoro orea areraga mɔnɔ neonto βwa twa:na twawɛ torea twakuerɛ]

Mwanamke huyo hulia sana kwa sababu ya watoto **wake wale** walikufa.

(vi) *Ndĩenda ũmbĩre nteto* ***ciaku ĩrĩa*** *ciĩna gĩtũmi.*

[ndeɛnda omβerɛ ntɛtɔ ciaku erea ciena getomi]

Nataka uniambie mambo **yako yale** yana umuhimu.

Ruwaza ya tatu inahusisha kimilikishi kikitokea kikiwa cha kwanza na kivumishi cha idadi kikifuata. Hali kama hii hupatikana hata katika lugha ya Kiswahili (Ashton, mtaje; Mbaabu, mtaje; Mochiwa, mtaje).

(18) (i) *Atana* ***bawe bathatũ*** *bakwĩja.*

[atana βawɛ βaθato βakweɟa]

Wavulana **wake watatu** wamekuja.

(ii) *Jũkia nkeethi* ***ciakwa inyingi****.*

[ɟokia nkɛ:θi ciakwa iɲiŋge]

Nakutumia salamu **zangu nyingi**.

(iii) *Antũ* ***betũ babaingĩ*** *batĩna ngũgĩ cia kũrita.*

[anto βɛtu βaβaiŋge βatena ngoge cia korita]

Watu **wetu wengi** hawana kazi za kufanya.

(iv) *Kũgũrũ* ***kwawe kũmwe*** *ikwonji.*

[kogoro kwawɛ komwɛ ikwɔɲɟi]

Mguu **wake mmoja** umelemaa.

Ruwaza ya nne ni ile ya kimilikishi kikitokea kabla ya kivumishi cha pekee kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

(19) (i) *Mwana* ***wawe wengwa*** *akwĩja.*

[mwana wawɛ wɛŋgwa akweɟa]

Mtoto **wake mwenyewe** amekuja.

(ii) *Ng'ombe* ***yao yongwa*** *ĩkwonora.*

[ɲɔmβɛ jaɔ jɔŋgwa ekwɔnɔra]

Ng'ombe **wao mwenyewe** amepatikana.

(iv) *Mũgongo* ***jwao junthe*** *ijũkũmwenda*.

[mogɔŋgɔ ɟwaɔ ɟunθɛ iɟokomwɛnda]

Jamii **yao yote** inamhitaji.

(v) *Nworagĩre akũrũ* ***betũ bonthe***.

[nwɔragerɛ akoro βɛto βɔnθɛ]

Uliua wanaume **wetu wote**.

(vi) Mbeca **ciaku cionka** ĩtĩng'ana.

[mβɛca ciaku ciɔnka eteɲana]

Pesa **zako pekee** hazitatosha.

(vii) Mĩgambo **yao yonka** ĩgatethia mwana ũũ.

[megamβɔ jaɔ jɔnka egatɛθia mwana o:]

Ushauri **wao pekee** utasaidia mtoto huyu.

(viii) Athoni **bakwa bangĩ** bakeja nyuma.

[aθɔni βakwa βaŋge βakɛɟa ɲuma]

Wakwe **wangu wengine** watakuja baadaye.

Ruwaza ya tano inahusu kimilikishi kikifuatwa na kivumishi cha sifa. Mpangilio sawa na huu wa vivumishi unapatikana pia katika lugha ya Kiswahili (Mochiwa, mtaje). Sentensi zifuatazo zinaonyesha hali hiyo:

(20) (i) *Amerũ barĩ na mantũ* ***jao jamega*** *mono.*

[Amɛro βare na manto ɟaɔ ɟamɛga mɔnɔ]

Wameru wana mambo **yao mazuri** sana.

(ii) *Mũntwenu arĩ na mũkenye* ***wawe ũmwega***.

[montwɛnu are na mokɛɲɛ wawɛ omwɛga]

Mjomba wenu ana msichana **wake mzuri** sana.

(iii) *Jũũjũ atũraga na ana* ***bawe babega.***

[ɟo: ɟo atoraga na ana βawɛ βaβɛga]

Nyanya aliishi na watoto **wake wazuri.**

(iv) *Ĩjĩ nĩ nyomba* ***yetũ ĩnjerũ***.

[eɟi ne ɲɔmβa jɛto eɲɟɛro]

Hii ni nyumba **yetu mpya**.

(v) Igua rwĩmbo **rwetu rũrũthongi**.

[I gua rwemβɔ rwɛtu roroθɔŋgi]

Sikiliza wimbo **wetu mzuri.**

Ruwaza moja ambayo ni sheria ya jumla inaweza kutumika kueleza ruwaza mbalimbali zinazojiri kimilikishi kinapotangulia kivumishi kingine katika sentensi kama inavyojitokeza katika 16 – 20 hapo juu. Kulingana na sheria hii kimilikishi hutangulia kivumishi kingine kama cha a – unganifu, kiashiria, idadi, pekee au cha sifa katika sentensi. Sheria hiyo inaweza kuandikwa hivi:

(21) *Kimilikishi; kivumishi cha a – unganifu; kiashiria; kivumishi cha idadi; kivumishi cha pekee; kivumishi cha sifa.*

Katika hali nyingine kimilikishi huweza kutumika pamoja na vivumishi vingine viwili katika sentensi moja. Kinapotumika kunatokea ruwaza moja ambapo kimilikishi hutangulia kiashiria na kivumishi cha sifa. Hali hii inaweza kudhihirika kwa kuangalia mifano ya sentensi zifuatazo:

(22) (i) *Ĩrĩnda* ***rĩawe rĩrĩa rĩraja*** *rĩkwonora.*

[erenda reawɛ rerea reraɟa rekwɔnɔra]

Rinda **lake lile refu** limepatikana.

(ii) *Iuku* ***rĩawe rĩrĩa rĩrĩerũ*** *rĩgũtambũka.*

[iuku reawɛ rerea rereɛro regotamβoka]

Kitabu **chake kile kipya** kimeraruka.

(iii) *Ngũgĩ yawe* ***ĩrĩa nene*** *nĩ gwĩtaga na njĩra akĩ.*

[ŋgoge jawɛ erea nɛnɛ ne gwetaga na ɲɟera ake]

Kazi **yake ile muhimu** ni kurandaranda kwa barabara pekee.

(iv) *Kĩbanga* ***kĩawe kĩriĩa kĩnene*** *gĩkwiwa.*

[keβaŋga keawɛ kerea kenɛnɛ gekwiwa]

Upanga **wake ule mkubwa** umeibwa.

(v) *Rũũjĩ* ***rwetũ rũrĩa rũnene*** *ndene ya nthĩgũrũ yetũ rwĩtagwa Thagana*.

[ro:je rwɛto rorea ronɛnɛ ndɛne ya nθigoro jɛto rwetagwa θagana]

Mto **wetu ule mkubwa** kwenye nchi yetu unaitwa Thagana.

(vi) *Mũnthũ* ***wetũ ũria mũnene*** *ni nkũnkũni.*

[monθo wɛto oria monɛnɛ ni nkonkoni]

Adui **wetu yule mkubwa** ni kunguni.

(vii) *Ngũũ* ***yawe ĩrĩa njega*** *ĩgũtambũka.*

[ŋgo: jawɛ erea ɲɟɛga egotamboka]

Nguo **yake ile nzuri** imeraruka.

Sheria hii ndiyo inajitokeza kutokana na ruwaza tuliyorejelea hapo juu:

(23) *Kimilikishi; kiashiria; kivumishi cha sifa.*

### 5.5.3 Ruwaza za Kivumishi cha Idadi na Kivumishi Kingine

Kivumishi cha idadi huweza kutangulia kivumishi kingine na kuunda ruwaza saba. Kwa mfano ruwaza ya vivumishi viwili vya idadi pamoja inaweza kujitokeza katika sentensi hii:

(24) *Mantũ* ***jaĩrĩ jathatũ*** *jakorua mũcemanione.*

[manto ɟaere ɟaθato ɟakɔrua mocɛmaniɔnɛ]

Mambo **mawili matatu** yataulizwa mkutanoni.

Mfano wa pili unahusisha kivumishi cha idadi kikifuatwa na kivumishi cha sifa na kuunda ruwaza nyingine. Hali kama hii ndiyo inasisitizwa na Mochiwa (mtaje) akirejelea kivumishi cha lugha ya Kiswahili. Sentensi hizi ni mifano ya ruwaza inayorejelewa:

25 (i) *Baaba ena into* ***bibingĩ bibierũ****.*

[βa:βa ɛna intɔ βiβiŋge βiβiɛro]

Baba ana vitu **vingi vipya**.

(ii) *Mũromo jũkũnĩkaĩra maĩgo* ***jamaingĩ jamathongĩ.***

[morɔmɔ ɟokonekaera maegɔ ɟamaeŋge ɟamaθɔŋgi]

Mdomo hufunikia meno **mengi mazuri.**

(iii) *Ikundi* ***bina binene*** *bikeja kũriũnga kuuma Nairobi.*

[ikundi βina βinɛne βikɛɟa korioɲga ku:ma Nairɔβi]

Vikundi **vinne vikubwa** vitakuja kuzuru kutoka Nairobi.

(iv) *Ĩndĩ kũrĩ ũntũ* ***bũmwe bũbwega****.*

[ende kore onto βomwɛ βoβwɛga]

Lakini kuna jambo **moja zuri.**

Katika mfano wa tatu kivumishi cha idadi hutokea kabla ya kivumishi cha jina na kuunda ruwaza inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

(26) (i) *Mũrĩngĩti ijũkwendwa nĩ muntũ* ***ũmwe gĩtonga.***

[moreŋgeti iɟokwɛndwa ne munto omwɛ getoŋga]

Blanketi inauzwa na mtu **mmoja tajiri**.

(ii) *Antũ bathatũ arimi abarejire kũmũgwatia kũrima*.

[anto baθato areme aβareɟĩrɛ komogwatia korema]

Watu **watatu wakulima** walikuja kumsaidia kulima.

Mfano wa nne unahusu kivumishi cha idadi kikitangulia kile cha pekee. Sentensi hizi zinaonyesha hali hii:

(27) (i) *Ng'ombe* ***ithatũ cionthe*** *icio ikang'ana kĩathone kũu.*

[ŋɔmβɛ iθato ciɔnθɛ icio ikaŋana keaθɔnɛ keu]

Ng'ombe **watatu wote** ndio watatosha katika sherehe hiyo.

(ii) *Antũ* ***baĩrĩ bonka*** *batĩna irio.*

[anto βaere βɔnka βatena iriɔ]

Watu **wawili pekee** hawana chakula.

(iii) *Ngũkũ ĩna magũrũ* ***jaĩrĩ jonka.***

[ŋgoko ena magoro ɟaere ɟɔnka]

Kuku ana miguu **miwili pekee**.

(iv) *Kĩama* ***kĩmwe gĩonka*** *gĩtĩtɛthia nthĩgũrũ ĩjĩ.*

[keama kemwɛ giɔnka geteteθia nθegoro eɟe]

Chama **kimoja pekee** hakitasaidia nchi hii.

(iv) *Kwĩna njĩra* ***ĩmwe yonka*** *ya gwĩta kwao.*

[kwena ŋɟera emwɛ jonka ja gweta kwaɔ]

Kuna njia **moja pekee** ya kwenda kwao.

Katika mfano wa tano, kivumishi cha idadi huchukua nafasi ya kwanza ilhali kimilikishi hutokea kikiwa cha pili kama inavyobainika hapa chini:

(28) (i) *Gĩkundi **kĩmwe kĩao** gĩetĩre ũtũkũ.*

[Gekundi kemwɛ keaɔ geɛtirɛ otoko]

Kikundi **kimoja chao** kilisafiri usiku.

(ii) *Muntũ **ũmwe wao** akeja rũũjũ.*

[munto omwɛ waɔ akɛɟa ro:ɟo]

Mtu **mmoja wao** atakuja kesho.

(iii) *Aritwa **ĩkũmi bao** ibaratorokere cukuru.*

[aretwa ekumi βaɔ iβaratɔrɔkɛrɛ cukuru]

Wanafunzi **kumi wao** walitoroka shule.

(iv) *Muntũ **ũmwe wetũ** nĩaronere ngũgĩ Nairobi.*

[munto omwɛ wɛto nearɔnɛrɛ ŋgoge Nairɔβi]

Mtu **mmoja wetu** amepata kazi Nairobi.

Mfano wa sita unahusu kivumishi cha idadi kikitangulia kivumishi kiashiria. Sentensi zifuatazo zinashadidia hali hiyo:

(29) (i) *Kũrĩna antũ **babaingĩ barĩa** bakwenda ngũgĩ.*

[korena anto βaβaiŋge βarea βakwɛnda ŋgogi]

Kuna watu **wengi wale** wanataka kazi.

(ii) *Jaja nĩjo mantũ jarĩa tũthomete maukune **jamaingĩ jarĩa** jaandĩki.*

[ɟaɟa neɟɔ manto ɟarea toθɔmɛtɛ maukunɛ ɟamaiŋge ɟarea ɟa:ndeki]

Haya ndiyo tumesoma kutoka kwa vitabu **vingi vile** vimeandikwa.

(iii) *Nĩ kwarĩ na mantũ* ***jathatũ jarĩa*** *jathithagua mbere ya mũranũ jwa Amerũ.*

[ne kware na manto ɟaθato ɟarea ɟaθiθagua mβɛrɛ ja morano ɟwa Amɛro]

Kulikuwa na mambo **matatu yale** yalifanywa kabla ya arusi ya Wameru.

(iv) *Muntũ* ***ũmwe ũrĩa*** *ũkeja akonua akũrara.*

[muntu omwɛ orea okɛɟa akɔnua akorara]

Mtu **mmoja yule** atakuja ataonyeshwa pahali pa kulala.

(v) *Ngũkũ ĩrĩ na anthũ* ***babaingĩ barĩa*** *bajũkaia nkara ciayo.*

[ŋgoko ere na anθo βaβaiŋge βarea βaɟokaia nkara ciajɔ]

Kuku ana adui **wengi wale** huchukua mayai yake.

Ruwaza ya saba inahusu kivumishi cha idadi kikitangulia kivumishi cha a - unganifu. Hali hii inajitokeza katika sentensi hizi:

(30) (i) *Ĩbũra* ***rĩmwe rĩa*** *mũtĩ rĩkũma.*

[eβora remwɛ rea mote rekoma]

Jani **moja la** mti limekauka.

(ii) *Antũ* ***babaingĩ ba*** *nthukĩ ĩjĩ batĩ nthoni ĩnjega.*

[anto βaβaiŋge βa nθuke eje βate nθɔni enɟɛga]

Watu **wengi wa** rika hili hawana adabu nzuri.

(iii) *Antũ* ***babaingĩ ba*** *mwĩrĩga jwawe bakwĩja mũranũne jwawe.*

[anto βaβaiŋge βa mwerega jwawɛ βakweɟa moranone jwawɛ]

Watu **wengi wa** kutoka kwa ukoo wake wamefika kwenye arusi yake.

(iv) *Aini* ***babaingĩ ba*** *Merũ bakaina kĩrĩ mambura jau.*

[aini βaβaiŋge βa mɛro βakaina kere mambura ɟau]

Waimbaji **wengi wa** Meru wataimba kwenye sherehe hiyo.

(v) *Kwĩna nyomba* ***inya cia*** *mũcemanio.*

[kwena ɲɔmβa iɲa cia mocemaniɔ]

Kuna nyumba **nne za** mkutano.

Ruwaza hizo saba katika 24 – 30 zinaunda ruwaza moja ambayo ni sheria ya kuzieleza. Inaweza kuelezwa kuwa kivumishi cha idadi huweza kutangulia kingine cha idadi au kile cha sifa, jina, pekee, kimilikishi, kiashiria ama cha a – unganifu katika sentensi. Sheria inayopatikana ni hii inayofuata:

(31) *Kivumishi cha idadi; kivumishi cha sifa; kivumishi cha jina; kivumishi cha pekee; kivumishi kimilikishi; kivumishi kiashiria; kivumishi cha a – unganifu.*

Aidha, kuna uwezekano wa kivumishi cha idadi kutumika pamoja na vivumishi vingine katika sentensi moja na hivyo kuunda ruwaza za mkururo wa vivumishi vitatu. Hii inapelekea kubuniwa kwa ruwaza sita za mpangilio wa vivumishi katika sentensi mbalimbali. Kila ruwaza hapa huanza kwa kivumishi cha idadi. Ruwaza ya kwanza ni pale kivumishi cha idadi kinatokea kabla ya kimilikishi na kiashiria kama inavyoonekana hapa chini:

(32) (i) *Kũrĩna ngũgĩ* ***ĩmwe yawe ĩrĩa*** *ĩtĩbui.*

[korena ŋgoge emwɛ jawɛ erea eteβui]

Kuna kazi **moja yake ile** haifai.

(ii) *Ntiũmba gũkwĩra ni twana* ***tũng'ana twakwa tũrĩa*** *ntete kĩthakene.*

[Ntiomβa gokwira ni twana toɲana twakwa torea ntɛtɛ keθakɛnɛ]

Siwezi kukwambia ni watoto **wangapi wangu wale** nimetupa kichakani.

Katika ruwaza ya pili, kivumishi cha idadi hutangulia kiashiria na kivumishi cha sifa kama inavyoonekana katika sentensi hii:

(33) *Muntũ* ***ũmwe ũrĩa ũmwega*** *ni we.*

[munto omwɛ oria omwɛga ni wɛ]

Mtu **mmoja yule mzuri** ni yeye.

Tatu, kivumishi cha idadi hutangulia kivumishi cha sifa na kiashiria. Sentensi zifuatazo zinaonyesha hali hiyo:

(34) (i) *Mantũ* ***jamaingĩ jamerũ jarĩa*** *jakaguna mũrĩmi jakaritanwa.*

[manto ɟamaiŋge ɟamɛru ɟarea ɟakaguna moremi ɟakaritanwa]

Mambo **mengi mapya yale** yatanufaisha mkulima yatafundishwa.

(ii) *Kwarĩ  na mũnene* ***ũmwe ũmũkũrũ ũrĩa*** *warĩ  ũmwega.*

[kware na monɛnɛ omwɛ omokoro orea ware omwɛga]

Kulikuwa na kiongozi **mmoja mzee yule** alikuwa mzuri.

(iii) *Magũrũ ja rũko ja ngii nĩ ta ageni* ***baĩrĩ babaĩ barĩa*** *bakũrũkaga nyomba ĩmwe.*

[magoro ɟa rokɔ ɟa ŋgi: ne ta agɛni βaere βaβae βarea βakorokaga ɲɔmβa emwɛ]

Miguu chafu ya nzi  ni kama wageni **wawili wabaya wale** wanaoingia katika nyumba moja.

(iv) *Mĩĩtĩre* ***ĩmwe ĩmĩthũkũ ĩria*** *ĩrĩ na nthukĩ cia nandĩ  ĩtiganwe nayo.*

[me:terɛ emwɛ  emeθoko erea ere na nθuke cia nande etiganwɛ nayɔ]

Desturi **zingine mbaya zile** zina rika la kisasa zitupiliwe mbali.

v) *Ũntũ* ***bũngi bũbũnene bũrĩa*** *bũkarigaria antũ bũkonekana rua*.

[onto βoŋge βoβonɛnɛ βũrea βokarigaria anto βokɔnɛkana rua]

Jambo **jingine kubwa lile** litashangaza watu litaonekana hivi karibuni.

Nne, kivumishi cha idadi huja kabla ya kiashiria na kivumishi cha pekee. Kwa mfano:

(35) *Kũrĩ ũntũ **bũmwe bũrĩa bunka** bũtĩbui.*

[kore onto βomwɛ βorea βunka βuteβui]

Kuna jambo **moja lile pekee** halifai.

Tano, mkururo wa kivumishi cha idadi, sifa na a - unganifu huunda ruwaza nyingine ambayo inadhihirika katika sentensi ifuatayo:

(36) *Mũcemanione jũũ antũ bakaritanwa njĩra **inyingĩ injerũ cia** kũritaga ngũgĩ ciao.*

[mocɛmaniɔnɛ ɟo: anto βakaritanwa ŋɟera iɲiŋge inɟɛro cia koritaga ŋgogi ciaɔ]

Watu watafundishwa njia **nyingi mpya za** kufanya kazi zao kwenye mkutano huo.

Mfano wa sita ni safu ya kivumishi cha idadi, a - unganifu na kisha kiashiria. Kwa mfano;

(37) *Jũũ I mũcinka **jũmwe jwa ĩrĩa** iraũrĩte.*

[ɟo: I mocinka ɟomwɛ ɟwa erea iraoretɛ]

Hii ni bunduki **moja ya zile** zilizokuwa zimepotea.

Ruwaza zote sita katika 32 – 37 zinaweza kuelezwa kwa kutumia sheria tatu ambazo zinaeleza ruwaza za kivumishi cha idadi kinapotangulia vingine katika sentensi. Sheria zinazojitokeza ni kama hizi:

(38) (a) *Kivumishi cha idadi; kivumishi cha a – unganifu; kiashiria; kivumishi cha sifa.*

(b) *Kivumishi cha idadi; kivumishi cha sifa; kiashiria; kivumishi cha pekee; kivumishi cha a –unganifu.*

(c) *Kivumishi cha idadi; kimilikishi; kiashiria.*

**5.5.4 Ruwaza za Kiulizi na Kivumishi Kingine**

Kiulizi hutangulia vivumishi vingine na kuunda ruwaza mbili za mfuatano wa vivumishi viwili. Katika ruwaza moja kivumishi cha sifa hufuata kiulizi kama inavyoonekana katika sentensi hii:

(39) *Ni ũntũ* ***bũrikũ bũnene*** *bwonekanĩre?*

[ni onto βoriko βonɛnɛ βwɔnɛkanerɛ?]

Ni jambo **lipi kubwa** lililotokea?

Ruwaza nyingine inahusu kivumishi kiulizi na kivumishi cha pekee. Mfano wa sentensi ifuatayo unaonyesha hali hii:

(40) *Nandĩ arĩ na ngũũ* ***ing'ana cionthe?***

[nande are na ŋgo: iŋana ciɔnθɛ?

Sasa ana nguo **ngapi zote**?

Sheria moja ifuatayo inaweza kuundwa kutokana na ruwaza katika 39 – 40. Maelezo yake ni kuwa kivumishi kiulizi huweza kutangulia kivumishi cha sifa au cha pekee katika sentensi.

(41) *Kivumishi kiulizi; kivumishi cha sifa; kivumishi cha pekee.*

Ni vizuri kufahamu kuwa kivumishi kiulizi huweza kutangulia vivumishi vingine viwili katika sentensi na kuunda ruwaza zingine. Ruwaza moja inayobainika inahusu kivumishi

kiulizi kikitokea kabla ya kivumishi cha sifa na kiashiria kuwa cha mwisho kama inavyoonekana katika mfano huu wa sentensi:

(42) *Ni mantũ* ***jarikũ jamega jarĩa*** *athithĩrie?*

[ni manto ɟariko ɟamɛga ɟarea aθiθeriɛ?]

Ni mambo **yapi mazuri yale** alifanya?

Nyingine inahusu kivumishi kiulizi kikitangulia kivumishi cha pekee na kisha kivumishi cha sifa. Hali hii inabainika katika sentensi hizi:

(43) (i) *Ni ntũkũ* ***ĩrĩkũ ĩngĩ ĩnene*** *ũkũrikana?*

[ni ntoko ereko eŋge enɛnɛ okorikana?]

Ni siku **ipi nyingine muhimu** unakumbuka?

(ii) I muntũ **ũrikũ ũnge ũmũnene** wakinya?

[I munto oriko oŋge omonene wakiɲa?]

Ni mtu **yupi mwingine mkubwa** amefika?

Aidha, kuna ruwaza ya mkururo wa vivumishi vinne ambapo kivumishi kiulizi ndicho hutangulia vingine. Katika ruwaza hii kivumishi kiulizi huandamwa na kivumishi cha pekee, sifa na hatimaye kivumishi kiashiria. Mfano wa sentensi hii unathibitisha ruwaza hii:

(44) *I muntũ* ***ũrikũ ũngi ũmwega ũria*** *ũkũrikana?*

[I munto oriko oŋgi omwɛga orea okorikana?]

Ni mtu **yupi mwingine mzuri yule** unakumbuka?

Ruwaza tatu kuhusiana na kivumishi kiulizi katika 42,43 na 44 huweza kuelezwa kutumia sheria katika 45. Sheria hii ina maana kuwa kivumishi kiulizi hutangulia kivumishi cha

pekee na cha sifa au kivumishi cha sifa na kivumishi kiashiria ama vivumishi vya pekee; sifa na kiashiria:

(45) *Kivumishi kiulizi; kivumishi cha pekee; kivumishi cha sifa; kivumishi kiashiria*

### 5.5.5 Ruwaza za Kivumishi cha Sifa na Kivumishi Kingine

Kwa mujibu wa Wales (2014) na Mochiwa (mtaje) vivumishi vyovyote vya sifa huweza kufuatana. Hata hivyo, wanatahadharisha kuwa masuala ya maana inayojitokeza lazima yatiliwe maanani vinapofuatana. Kwa hivyo, wanapendekeza kuwa kivumishi kinachoonyesha saizi au kiwango cha jina kitangulie vingine kama vinavyoonyesha rangi ya jina. Hali hii ndiyo tunapata katika sentensi ifuatayo:

46 *Muntũ* ***ũmũraja ũmwirũ*** *akwĩja.*

[munto omoraʝa omwiro akweʝa]

Mtu **mrefu mweusi** amekuja.

Huu ni mfano mmoja wa ruwaza ya vivumishi viwili vya sifa vikitokea pamoja katika sentensi. Kivumishi **ũmũraja** [omoraja] (mrefu) kinatokea kabla ya **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi) kwa sababu kinaonyesha kimo cha mtu. Hali ya sifa za kisemantiki au maana za vivumishi kama hivyo inatiliwa mkazo (Vendler, 1968; Quirk na Wenzie, 1985) katika kuamua mfuatano wa vivumishi vyovyote vile vya sifa. Hali ya kivumishi cha kuonyesha kiwango kutangulia kile cha kuonyesha rangi inasisitizwa zaidi na Belk (2011) anapotoa mfano kama huu katika lugha ya Kiingereza: *The big brown bag.* Anasisitiza kuwa mpangilio huu wa vivumishi ndio unapendelewa kuliko, *The brown big bag.*

Pia, kivumishi cha sifa kinaweza kutangulia kivumishi cha a - unganifu vinapotumika vyote viwili katika sentensi moja. Hali hii inajitokeza katika sentensi zifuatazo:

(47) (i) *Mũtanocia ena gĩcuncĩ* ***gĩkĩnene kĩa*** *munda.*

[motanɔcia ɛna gecunce gekenɛnɛ kea munda]

Kakangu ana sehemu **kubwa ya** shamba.

(ii) *Ngũũ* ***ĩnthongi ya*** *mwana ĩkũgũrwa.*

[ŋgo: enθɔŋgi ja mwana ekogorwa]

Nguo **nzuri ya** mtoto imenunuliwa.

(iii) *Kwĩna nyomba* ***ĩnene ya*** *mũcemanio.*

[kwena ɲɔmβa enɛnɛ ja mocɛmaniɔ]

Kuna nyumba **kubwa ya** mkutano.

(iv) *Muntũ* ***ũmũthũku wa*** *gwĩtĩkia atĩbui.*

[munto omoθoku wa gwetekia ateβui]

Mtu **mbaya wa** kuamini hafai.

(v) *Mbeũ* ***ngeni ya*** *ikwacĩĩ ya kũanda nĩkwendua nandĩ.*

[mβɛo ŋgɛni ja ikwace: ja koanda nekwɛndua nande]

Mbegu **mpya ya** viazi ya kupanda inauzwa sasa.

Katika hali nyingine kivumishi cha sifa hutangulia kivumishi kiashiria. Sentensi hizi hudhihirisha hali hiyo:

(48) (i) *Mũcemanio* ***jũmũnene jũrĩa*** *jũrarĩ Nakuru ijũrarĩ na antũ babaingĩ cana.*

[mocemaniɔ ɟomonɛnɛ ɟorea ɟorare Nakuru iɟorare na anto βaβaiŋge cana]

Mkutano **mkubwa ule** uliokuwa Nakuru ulihudhuriwa na watu wengi.

(ii) *Ntũkũ ya kiumia aritwa bakaina ndwĩmbo* ***injeru irĩa*** *baciritanĩte.*

[ntoko ja kiumia aritwa βakaina ndwemβɔ inɟɛru irea βaciritanetɛ]

Siku ya Jumapili wanafunzi wataimba nyimbo **mpya zile** wamejifunza.

(iii) *Mũbundi akabakĩra nyomba **injega irĩa** ikabagwĩria*.

[moβundi akaβakera ɲɔmβa inɟɛga irea ikaβagweria]

Fundi atawajengea nyumba **nzuri zile** zitawafurahisha.

(iv) *Jaja nĩ mantũ **jamathũku jarĩa** jatĩbui.*

[ɟaɟa ne manto ɟamaθoku ɟarea ɟateβui]

Haya ni mambo **mabaya yale** hayafai.

(v) *Twana twawe tũmwĩraga mantũ **jamerũ jarĩa** tũthomere cukuru.*

[Twana twawɛ tomweraga manto ɟamɛro ɟarea tuθɔmɛrɛ cukuru]

Watoto wake humwambia mambo **mapya yale** walisoma shule.

Sheria moja huweza kutumika kueleza ruwaza tatu katika 46, 47 na 48 zinazohusiana na kivumishi cha sifa. Tunaieleza kuwa kivumishi cha sifa hutangulia kingine cha sifa, a - unganifu au kiashiria katika sheria ifuatayo:

(49) *Kivumishi cha sifa; kivumishi cha a – unganifu; kivumishi kiashiria.*

Wakizungumzia mkururo wa vivumishi vya sifa katika sentensi moja, Philipo (2017); Philipo na Kuyenga (2017) wanasema vivumishi vitatu vya sifa huweza kuandamana katika sentensi moja kuvumisha nomino. Wanadai kuwa hii ni sifa moja ya vivumishi vya Kiswahili. Hata hivyo, hali ya vivumishi vitatu vya sifa kufuatana haikudhihirika katika Kiimenti.

### 5.5.6 Ruwaza za Kivumishi cha Jina na Kivumishi Kingine

Kivumishi cha jina hutangulia kile cha sifa ili kuunda ruwaza katika sentensi husika. Hali hii inadhihirika katika sentensi hii:

(50) *Mũthaka **mũrĩmĩ ũmwega** akwĩja.*

[moθaka moreme omwɛga akweɟa]

Kijana **mkulima mzuri** amekuja.

Aidha, kimilikishi hufuata kivumishi cha jina na kuunda ruwaza inayobainika katika sentensi hii:

(51) *Amerũ bendete muntũ ũrĩ na* ***into biawe.***

[Amɛro βɛndɛtɛ munto ore na into βiawɛ]

Wameru hupenda mtu mwenye **mali yake**.

Ruwaza ya mwisho ni pale ambapo kivumishi cha jina kinatangulia kivumishi cha pekee. Sentensi hii inaweza kutumika kueleza hali hiyo:

(52) *Ĩta kĩrĩ abagu* ***mũgũciari wengwa.***

[eta kere aβagu mogociari wɛŋgwa]

Enda kwa baba **mzazi mwenyewe**.

Ruwaza tatu katika 50, 51 na 52 zinazohusiana na kivumishi cha jina zinaweza kuelezwa kutumia sheria moja katika 53. Maelezo yake ni kuwa kivumishi cha jina hutangulia kivumishi cha sifa, kivumishi kimilikishi au kivumishi cha pekee katika sentensi.

Sheria inayojitokeza ni:

(53) *Kivumishi cha jina; kivumishi cha sifa; kivumishi kimilikishi; kivumishi cha pekee.*

### 5.5.7 Ruwaza za Kiashiria na Kivumishi Kingine

Kiashiria hutangulia vivumishi vingine katika sentensi na kuibua ruwaza saba. Kwanza, kinatangulia kiashiria kingine kama inavyoonekana katika sentensi hizi:

(54) (i) *Ngono* ***iji irĩa*** *ũgũtũgonera ni injega.*

[ŋgɔnɔ iji irea ogotogɔnɛra ni inɟɛga]

Hadithi **hizi zile** unatuhadithia ni nzuri.

(ii) *Mpendaga mantũ* ***jaja jarĩa*** *ũtwĩraga ntũkũ cionthe.*

[Mpɛndaga manto ɟaɟa ɟarea otweraga ntoko ciɔnθɛ]

Napenda mambo **haya yale** unatuambia siku zote.

(iii) *Nĩmpendete ntũũra iji irĩa twaciarĩrwe.*

[Nempɛndɛtɛ nto:ra iɟi irea twaciarerwɛ]

Napenda vijiji **hivi vile** tulizaliwa.

Pili, kivumishi kiashiria hutokea kabla ya kivumishi cha a - unganifu. Mfano wa sentensi zifuatazo unaweza kutumiwa kueleza hali hii:

(55) (i) *Mũrugĩre* ***jũjũ jwa*** *nyama jũtĩbui.*

[morugerɛ ɟoɟo ɟwa ɲama ɟoteβui]

Upikaji **huu wa** nyama haufai.

(ii) *Rũgono* ***rũrũ rwa*** *mpaka rũkũgwĩria twaana twa cukuru.*

[Rogɔnɔ roro rwa mpaka rokogweria twa:na twa cukuru]

Hadithi **hii ya** paka imefurahisha wanafunzi wa shule.

(iii) *Jũũjũ agatũgonera rũgono rwa mantũ* ***jau ja*** *ũtheru.*

[ɟo:ɟo agatogɔnɛra rogɔnɔ rwa manto ɟau ɟa oθɛru]

Nyanya ametuhadithia hadithi ya mambo **hayo ya** usafi.

(iv) *Ũritani* ***bũũ bwa*** *ũtheru bũgatethia mũgongo jũjũ.*

[oritani βo: βwa oθɛru βogatɛθia mogɔŋgɔ ɟoɟo]

Ufunzaji **huu wa** usafi utasidia jamii hii.

(iv) *Mwekũrũ ũũ nĩabagoneree rũgono* ***rũrũ rwa*** *nkũnkũni ijĩrĩ.*

[Mwɛkoro o: neaβagɔnɛrɛ: rogɔnɔ roro rwa nkonkoni iɟere]

Mwanamke huyu aliwahadithia hadithi **hii ya** kunguni wawili.

Tatu, kivumishi cha pekee hufuata kiashiria kama inavyobainika hapa chini:

(56) (i) *Mũtũma agũtũnya kũrũ* ***ĩu ĩngĩ*** *nyama.*

[motoma agotoɲa koro eu eŋge ɲama]

Mutuma amempokonya mbwa **huyo mwingine** nyama.

(ii) *Antũ barĩa bangĩ bakwĩja thaa iji.*

[Anto βarea βaŋge βakweɟa θa: iɟi]

Watu **wale wengine** wamefika saa hii.

(iii) *Mantũ* ***jarĩa jonthe*** *jakwendeka jakathithua mbere ya mwaka jũthira*.

[Manto ɟarea ɟɔnθɛ ɟakwɛndɛka ɟakaθiθua mβɛrɛ ja mwaka ɟoθira]

Mambo **yale yote** yanahitajika jatafanywa kabla ya mwaka kuisha.

(iv) *Antũ* ***bau bonthe*** *bakũrũkĩre aja.*

[Anto βau βɔnθɛ βakorokerɛ aɟa]

Watu **hao wote** walipitia hapa.

(v) *Irio* ***biu bionka*** *bĩtĩng'ana.*

[iriɔ βiu βiɔnka βeteɲana]

Chakula **hicho pekee** hakitatosha.

(vi) *Antũ* ***bau bonka*** *nĩbo barĩre nyama cia mpaka.*

[Anto βau βɔnka neβɔ βarerɛ ɲama cia mpaka]

Watu hao pekee ndiyo walikula nyama ya paka.

Nne, kiashiria ndicho hutokea kabla ya kimilikishi katika sentensi kama inavyoonekana katika sentensi hizi:

(57) (i) *Mũgongo* ***jũjũ jwetũ*** *jwĩna nkuma ĩnjega.*

[mogɔŋgɔ ɟoɟo ɟwɛto  ɟwena nkuma eɲɟɛga]

Jamii **hii yetu** ina sifa nzuri.

(ii) *Nthĩgũrũ **ĩjĩ yetũ** ĩna thĩna mono.*

[Nθegoro iɟi jɛto ena θena mɔnɔ]

Nchi **hii yetu i**na shida sana.

(iii) *Menyeera njaũ **ĩjĩ yakwa.***

[Mɛɲɛ:ra nɟao eɟe jakwa]

Chunga ndama **huyu wangu.**

(iv) *Nĩmbi ũkũria mwana **ũjũ  wakwa?***

[Nemβi  okoria mwana oɟo wakwa?]

Unauliza mtoto **huyu wangu** nini?

(v) *Nũũ ũrĩ  mundene **jũjũ jwakwa?***

[No: ore mundɛnɛ ɟoɟo ɟwakwa?]

Nani yuko kwenye shamba **hili langu**?

Tano, kiashiria hukalia nafasi ya kwanza katika sentensi na kisha kivumishi cha idadi.

Sentensi zifuatazo zinaweza kutumika kuonyesha hali hiyo:

(58) (i) *Antũ **baba bobaĩrĩ** batĩbui.*

[Anto βaβa βɔβaere βateβui]

Watu **hawa wawili** si wazuri.

(ii) *Citima **irĩa nyingĩ**  ndene ya nthĩgũrũ  yetũ ciũmĩte rũũjine rwa Thagana.*

[citima irea ɲiŋge ndɛnɛ ja nθegoro jɛtu ciumetɛ ro:ɟinɛ rwa θagana]

Stima **zile nyingi** nchini zimetoka Mto Thagana.

(iii) *Ekũrũ* ***barĩa baingĩ*** *nĩbakũũrwa ni arũme nthĩgũrũne.*

[ɛkoro βarea βaiŋge neβako:rwa ne aromɛ nθigoronɛ]

Wanawake **wale wengi** wanachapwa na wanaume nchini.

(iv) *Mĩtĩ* ***ĩrĩa mingĩ*** *gekũma.*

[Mete erea miŋge gɛkuma]

Miti **ile mingi** inakauka.

(v) *Mauku* ***jarĩa maingĩ*** *jakũgũrwa.*

[Mauku ɟarea maiŋge ɟakogorwa]

Vitabu **vile vingi** vimenunuliwa.

Sita, kiashiria hufuatwa na kivumishi cha sifa na kuunda ruwaza hiyo. Kwa maoni ya Miricho na Wenziwe (keshatajwa) ruwaza kama hii hujitokeza hata katika lugha ya Kiswahili. Sentensi hizi zinadhihirisha ruwaza hiyo:

(59) (i) *Muntũ* ***ũrĩa mũthũku*** *agwĩta.*

[munto orea moθoku agweta]

Mtu **yule mbaya** ameenda.

(ii) *Ng'ombe* ***ĩu njerũ*** *nĩ yetũ.*

[ŋɔmβɛ eu ɲɟɛro ne jɛto]

Ng'ombe **huyo mweupe** ni wetu.

(iii) *Kaana* ***kau kanene*** *nĩ kao.*

[ka:na kau kanɛnɛ ni kaɔ]

Mtoto **huyo mkubwa** ni wao.

(iv) *Mwitũ* ***jũrĩa mũnene*** *ijũgũtemwa.*

[Mwito ɟorea monɛnɛ iɟogotɛmwa]

Msitu **ule mkubwa** unakatwa.

(v) *Kĩatho **gĩkĩ kĩnene** ũjũ gĩkejĩwa nĩ antũ babanene thirikarĩne.*

[keaθɔ geke kenɛnɛ oɟo gekɛɟewa ne anto βaβanɛnɛ θirikarenɛ]

Sherehe **hii kubwa** hivi itahudhuriwa na watu wakubwa serikalini.

(vi) *Mantũ **jaja jamerũ** jagatethia mũrĩmi wa merũ.*

[Manto ɟaɟa ɟamɛro ɟagatɛθia moremi wa Mɛro]

Mambo **haya mapya** yatasaidia mkulima wa Meru.

Ruwaza sita zinazopatikana katika 54 – 59 wakati kiashiria kinapotangulia kivumishi kingine katika sentensi huweza kuunda ruwaza moja ambayo inaweza kuelezwa kwa sheria katika 60. Maelezo yake ni kuwa kiashiria hutangulia mojawapo ya vivumishi hivi katika sentensi: kiashiria, a – unganifu, pekee, kimilikishi, idadi au sifa. Sheria husika ni:

(60) *kiashiria; kivumishi cha a – unganifu; kivumishi cha pekee; kimilikishi; kivumishi cha idadi; kivumishi cha sifa.*

Kuna uwezekano wa kiashiria kutumika pamoja na vivumishi vingine viwili na kuunda ruwaza mbalimbali za mfuatano wa vivumishi katika tungo za Kiimenti. Kwa ujumla ruwaza kumi na tano hujitokeza huku kiashiria kikitangulia kila ruwaza. Ruwaza ya kwanza inahusu kiashiria kikitangulia kimilikishi na kivumishi cha a – unganifu kikitokea nafasi ya mwisho wa sentensi. Sentensi hizi zinaonyesha ruwaza hiyo:

(61) (i) *Mĩtĩ **ĩjĩ yetũ ya** ntwĩre ĩna baita cana.*

[mete eɟe jɛto ja ntwerɛ ena βaita cana]

Miti **hii yetu ya** asili ina faida sana.

(ii) *Mũka **ũjũ wakwa wa** mbere ntĩkũmwenda.*

[Moka oɟo wakwa wa mβɛrɛ ntekomwɛnda]

Mke **huyu wangu wa** kwanza simtaki.

Ruwaza ya pili inahusisha mfuatano wa kiashiria, kivumishi cha idadi na kivumishi cha a –unganifu. Sentensi hizi zinadhihirisha ruwaza hiyo:

(62) (i) *Antũ* ***baba bathatũ ba*** *nthukĩ ĩmwe I bendene.*

[Anto βaβa βaθato βa nθuke emwɛ I βɛndɛnɛ]

Watu **hawa watatu wa** rika moja wanapendana.

(ii) *Ngarĩ* ***iji ithatũ cia*** *mbere ikathambua*.

[ɲgare iɟi iθato cia mβɛrɛ ikaθamβua]

Magari **haya matatu ya** kwanza yataoshwa.

Ruwaza ya tatu ni mfuatano wa kiashiria, kivumishi cha pekee na kivumishi cha a –unganifu kama inavyobainika katika sentensi hii:

(63) *Kĩama* ***kĩrĩa kĩngĩ kĩa*** *arĩmĩ kĩgukinya.*

[keama kerea keŋge kea areme kegukiɲa]

Chama **kile kingine cha** wakulima kimefika.

Ruwaza ya nne ni mkururo wa kiashiria, kivumishi cha sifa na kivumishi cha pekee. Sentensi hizi zinathibitisha hali hiyo:

(64) i) *Ngũgĩ* ***irĩa nene cionthe*** *ciarĩ cia arũme.*

[ngoge irea nɛnɛ ciɔnθɛ ciare cia aromɛ]

Kazi **zile muhimu zote** zilikuwa za wanaume.

ii) *Auni mawatho* ***jarĩa manene jonthe*** *ndene ya Kenya tĩ antũ babega.*

[auni mawaθɔ ɟarea manɛnɛ ɟɔnθɛ ndɛnɛ ya Kɛɲa te anto babɛga]

Wanaovunja sheria **zile muhimu zote** nchini Kenya si watu wazuri.

Ruwaza ya tano ni pale kiashiria hutokea kabla ya kimilikishi huku kivumishi cha sifa kikitokea kikiwa cha mwisho. Sentensi hizi zinaonyesha ruwaza hiyo:

(65) (i) *Ngũũ **ĩu yawe ĩndaja** nĩ ya mbeca inyingĩ.*

[ŋgo: eu jawɛ endaɟa ne ja mβɛca iɲiŋge]

Nguo **hiyo yake ndefu** ni ya pesa nyingi.

(ii) *Mbogo ĩgũkũrũkia nja ngoci **irĩa ciayo indaja** mũka nakĩrĩre nyomoo ĩu.*

[Mβɔgɔ egokorokia ɲɟa ŋgɔci irea ciajɔ indaɟa moka nakererɛ ɲɔmɔ: eu]

Mbogo alipoingiza nyumbani pembe **zile zake ndefu** mwanamke aliogopa mnyama huyo.

(iii) *Twaana **tũria tũniini tũnthe** tũkamuntwa cindano.*

[Twa:na toria toni:ni tunθɛ tokamuntwa cindanɔ]

Watoto **wale wadogo wote** watachanjwa.

Ruwaza ya sita kiashiria hupatikana kabla ya kivumishi cha sifa na cha a - unganifu. Mfano wa sentensi hizi unaweza kutumika kuionyesha ruwaza hiyo:

(66) (i) *Iuku **rĩrĩ rĩrĩerũ rĩa** maromba rĩgũtũgwĩria.*

[iuku rere rereɛro rea marɔmβa regotogweria]

Kitabu **hiki kipya cha** maombi kimetufurahisha.

(ii) *Rũũjĩ **rũria rũnene rwa** Kenya rwĩtagwa Thagana.*

[Ro:je rorea ronɛnɛ rwa Kɛɲa rwetagwa θagana]

Mto **ule mkubwa wa** Kenya unaitwa Thagana.

(iii) *Antũ bakaritanwa mantũ **jaja jamerũ ja** ũtheru.*

[Anto βakaritanwa manto ɟaɟa ɟamɛro ɟa oθɛru]

Watu watafundishwa mambo **haya mapya ya** usafi.

(iv) *Mantũ* ***jau jamathũku ja*** *gwikumia jatĩbui*.

[manto ɟau ɟamaθoku ɟa gwikumia ɟateβui]

Mambo **hayo mabaya ya** kujivuna hayafai.

Ruwaza ya saba inaundwa kwa kiashiria kutangulia kivumishi cha pekee na kiashiria. Sentensi hii inaweza kutumiwa kudhihirisha ruwaza hiyo:

(67) *O amwe na mantũ* ***jau jonthe jarĩa*** *mwĩjĩ athagwa, naragũragĩrwa I mũgaa.*

[ɔ amwɛ na manto ɟau ɟɔnθɛ ɟarea mweɟe aθagwa naragoragerwa I moga:]

Pamoja na mambo **hayo yote yale** mvulana alifundishwa, aliaguliwa na mganga.

Ruwaza ya nane kiashiria hutokea kabla ya kimilikishi na hatimaye kivumishi cha pekee. Mfano wa sentensi ifuatayo unaweza kutumika kuionyesha:

(68) *We nakũmenyekana ntũrene* ***ĩu yao yonthe.***

[Wɛ nakomɛɲɛkana ntorɛnɛ iu jaɔ jɔnθɛ]

Yeye anajulikana katika kijiji **hicho chao chote**.

Ruwaza ya tisa inahusisha kiashiria kikiandamana na kivumishi cha pekee na kimilikishi. Mfano wa sentensi ifuatayo unadhihirisha ruwaza hiyo:

(69) *Mbeca* ***iu cionthe ciao*** *ikarĩwa.*

[Mβɛca iu ciɔnθɛ ciaɔ ikarewa]

Pesa **hizo zote zao** zitalipwa.

Ruwaza ya kumi ni safu ya kiashiria, kivumishi cha idadi na kiashiria. Hali hii ni dhahiri katika sentensi hii:

(70) *Ũkamwĩra mantũ* ***jau jamaingĩ jarĩa*** *jakamũtanga.*

[okamwera manto ɟau ɟamaiŋge ɟarea ɟakamotaŋga]

Usimwambie mambo **hayo mengi yale** yatamkanganya.

Ruwaza ya kumi na moja inahusu kiashiria, kimilikishi na hatimaye kiashiria. Mfano wa ruwaza hii unawekwa wazi katika sentensi hii:

(71) *Impendete ntũũra **ĩjĩ yetũ ĩrĩa** ndaciarĩrwe.*

[Impɛndɛtɛ nto:ra eɟe jɛto erea ndaciarerwɛ]

Napenda kijiji **hiki chetu kile** nilizaliwa.

Ruwaza ya kumi na mbili kiashiria huandamwa na kivumishi cha pekee na kisha kivumishi cha sifa. Sentensi zifuatazo zinaonyesha mpangilio huo:

(72) (i) *Miitũ **ĩrĩa ĩngĩ ĩmĩnene** nĩ ya Merũ.*

[Mi:to erea eŋge emenɛnɛ ne ya Mɛro]

Misitu **ile mingine mikubwa** ni ya Meru.

(ii) *Mantũ **jau jangĩ jamaingĩ** ijamũtetherie.*

[manto ɟau ɟaŋge ɟamaiŋge iɟamotɛθɛriɛ]

Mambo **hayo mengine mengi** yalimsaidia.

(iii) *Nyomoo **iu ingĩ niini** iciaĩgĩrue mpara.*

[ɲɔmɔ: iu iŋge ni:ni iciaegeruɛ mpara]

Wanyama **hao wengine wadogo** walihisi njaa.

(iv) *Mĩĩtĩ **ĩjĩ yonthe ĩmĩerũ** yaandi nĩ antũ barĩa.*

[Me:te eɟe jɔnθɛ emeɛru ya:ndi ne anto βarea]

Miti **ile yote mipya** imepandwa na watu wale.

Ruwaza ya kumi na tatu kiashiria huchukua nafasi ya kwanza na kufuatwa na vivumishi viwili vya pekee. Sentensi hizi zinaweza kushadidia hali hiyo:

(73) (i) *Into **biu bingĩ bionthe** nĩ biawe.*

[Intɔ βiu βiŋge βiɔnθɛ ne βiawɛ]

Vitu **hivyo vingine vyote** ni vyake.

(ii) *Nyomoo* ***iji ingĩ cionthe*** *nĩciejĩre mucemanio jwa nyomoo.*

[ɲɔmɔ: iɟi iŋge ciɔnθɛ neciɛɟerɛ mucɛmaniɔ ɟwa ɲɔmɔ:]

Wanyama **hawa wengine wote** walifika kwenye mkutano wa wanyama.

(iii) *Muntũ ũũ endi nkũrũki ya antũ* ***barĩa bangĩ bonthe.***

[Munto o: ɛndi nkoroki ja anto βaria βaŋge βɔnθɛ]

Mtu huyu anapendwa kuliko watu **wale wengine wote**.

(iv) *Gĩkundi kĩu kĩaijĩkene nkũrũki ya ikundi* ***birĩa bingĩ bionthe.***

[Gekundi keu keaijekɛnɛ nkoroki ja ikundi βirea βiŋge βiɔnθɛ]

Kikundi hicho kilijulikana kuliko vikundi **vile vingine vyote**.

(v) *Mũcũnkũ naretere mawega* ***jarĩa jangĩ jonthe***.

[moconko narɛtɛrɛ mawɛga ɟarea ɟaŋge ɟɔnθɛ]

Mzungu alileta mazuri **yale mengine yote**.

(vi) *Antũ* ***barĩa bangĩ bonthe*** *nĩbaunĩre ĩria*.

[Anto βarea βaŋge βɔnθɛ neβaunerɛ eria]

Watu **wale wengine wote** walivuka ziwa.

Ruwaza ya kumi na nne kiashiria hutokea kabla ya kivumishi cha pekee na kisha kivumishi cha idadi. Mfano wa sentensi hii unaonyesha ruwaza hiyo:

(74) *Mĩrĩga* ***ĩu yonthe kenda*** *yatũraga atĩa?*

[Merega eu jɔnθɛ kɛnda jatoraga atea?]

Koo **hizo zote tisa** ziliishi aje?

Ruwaza kumi na nne zinazopatikana katika 61 – 74 ambapo kivumishi kiashiria hutangulia vivumishi vingine huweza kutumika kuunda ruwaza zinazoelezwa kupitia sheria tano zifuatazo:

(75) (a) *Kiashiria; kimilikishi; kivumishi cha sifa; kivumishi cha a - unganifu; kivumishi cha pekee; kiashiria.*

(b) *Kiashiria; kivumishi cha pekee; kivumishi cha sifa; kimilikishi; kivumishi a – unganifu.*

(c) *Kiashiria; kivumishi cha pekee; kivumishi cha idadi; kivumishi cha a – unganifu.*

(d) *Kiashiria; kivumishi cha pekee; kivumishi cha pekee.*

(e) *Kiashiria; kivumishi cha idadi; kiashiria.*

**5.6 Hitimisho**

Sura hii imeangazia michakato ya kifonolojia na mofolojia ambayo hujitokeza katika muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Vivumishi husika vinapoundwa hupitia michakato mbalimbali ya kifonolojia. Michakato husika imeainishwa na sheria zinazobainika katika kila mchakato wa kifonolojia. Aidha, mchakato wa uradidi umegusiwa ambao ni wa kimofolojia na ni muhimu katika miundo mbalimbali ya vivumishi vya Kiimenti. Hatimaye, ruwaza zinajitokeza vivumishi vya Kiimenti vinapotumika katika tungo mbalimbali zimeelezwa. Ruwaza hizi zilifaa katika uandikaji wa sheria zinazodhibiti mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia masuala kuhusu hitimisho la utafiti huu. Masuala yaliyoangaziwa ni muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## 6.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni manne. Madhumuni ya kwanza yalikuwa kubainisha aina za vivumishi zinazopatikana katika lahaja ya Kiimenti. Utafiti huu umebainisha kuwa kuna aina kumi za vivumishi vya Kiimenti. Vivumishi hivi ni:

i). Vivumishi vya sifa kama **ũmũraja** [omoraja] (mrefu), **gĩkĩega** [gekeɛga] (kizuri), **babathũku** [βaβaθoku] (wabaya) na **bibioru** [βiβiɔru] (vilivyooza).

ii)Vivumishi vingine ni vile vya idadi. Vivumishi vya idadi ni vya aina mbili. Aina hizi ni idadi kamili inayowakilishwa na maneno kama **ũmwe** [omwɛ] (mmoja), **baĩrĩ** [βaere] (wawili), na **ĩkũmi** [ekomi] (kumi). Vivumishi hivi hutaja idadi kamili ya nomino inayovumishwa. Aina nyingine ya vivumishi ni vile ambavyo huonyesha idadi isiyo kamili. Hivi ni kama **babaingĩ** [βaβaiŋge] (wengi), **bikai** [βakai] (vichache), **bamwe** [βamwɛ] (baadhi yao) na **inga'anona** [iŋanɔna] (wastani).

iii) Vivumishi viulizi ambavyo ni kama **king'ana**?[kĩŋana] (kiasi gani?), **ũrĩkũ** [oreko] ? (yupi?) na **baũ**? [βao] (kina nani).

iv) Vivumishi vimilikishi kama w**akwa** [wakwa] (wangu), **wetũ** [wɛto] (wetu), **waku** [waku] (wako), **wenu** [wɛnu] (wenu), w**awe** [wawɛ] (wake) na **yao** [jaɔ] (yao).

v) Vivumishi vya pekee kama **bingĩ** [βiŋge] (vingine), **bonthe** [βɔnθɛ] (wote), **wenka** [wɛnka] (pekee yake), **jongwa** [ɟɔŋgwa] yenyewe) na **mwene** [mwɛnɛ] (mwenyewe).

vi) Vivumishi viashiria kama **ũjũ** [oɟo] (huyu), **ũu** [ou] (huyo) na **ũrĩa** [orea] (yule).

vii) Vivumishi vya majina. Haya ni majina ya Kiimenti ambayo huwa na uamilifu wa vivumishi katika matumizi kwenye tungo. Kwa mfano, katika virai nomino vifuatavyo; nomino ya pili ina utendakazi wa kivumishi katika kila kirai nomino. Virai nomino hivyo ni: **muntũ mũka** [munto moka] (mtu mwanamke], **muntũ mũrũme** [munto morome] , **mbũri ntũrũtũ** [mβori ntoroto] (mbuzi msumbufu] na **mwarĩ mũthao** [mware mũθaɔ] (msichana mvivu].

viii) Vivumishi vya a – unganifu kama **wa** [wa] (wa), **jwa** [ɟwa] (wa), **ba** [βa] (wa), **ja** [ɟa] (ya) na **kwa** [kwa] (kwa).

ix) Vivumishi viradidi visisitizi kama **wewengwa** (kusisitiza mwenyewe zaidi), **bobongwa** [βɔβɔŋgwa] (kusisitiza wenyewe zaidi) na **yoyongwa** [jɔjɔŋgwa] (kusisitiza yenyewe zaidi).

x) Visisitizi vilinganishi kama **ũmũrajaraja** [omorajaraja] (mrefu zaidi), **ũmũkuakuĩ** [omokuakue] (mfupi zaidi) na **ũmũkũrakũrũ** [omokorakoro] (mzee zaidi).

Madhumuni ya pili yalikuwa kuchunguza miundo ya vivumishi vya Kiimenti na jinsi usarufi unavyowakilishwa katika maumbo ya vivumishi. Utafiti huu ulibainisha kuwa vivumishi vya Kiimenti huzingatia miundo mitatu mbalimbali. Miundo hii ni kama:

i) Mz

Kuna vivumishi hasa vya mkopo vinavyoingia katika lahaja ya Kiimenti kama **maritati** [maritati] (maridadi), **atarĩ** [atare] (hatari) na **maarumu** [ma:rumu] (maalum).

ii) KA + Mz

Vivumishi vingine huundwa wakati mzizi wa kivumishi huambishwa kiambishi kimoja awali au zaidi ya kimoja. Kwa hivyo, tuna aina tatu za vivumishi hivi.

a) Kip + Mz

Vivumishi vyenye muundo huu ni vile ambavyo mzizi wa kivumishi huambishwa kipatanishi pekee. Hivi ni kama **ũrĩkũ** [oreko] (yupi), **wetũ** [wɛto] (wetu), **inya** [iɲa] (nne), **bonthe** [βɔnθɛ] (wote), **aja** [aɟa] (hapa) na **irĩa** [irea] (zile).

b) Kip + Kip +Mz

Vivumishi vyenye muundo huu ni vile ambavyo mzizi wa kivumishi huambishwa vipatanishi viwili. Hivi ni kama **babathũku** [βaβaθoku] (wabaya), **babanoru** [βaβanɔru] (wanono), **babairũ** (weusi) [βaβairo], **bibiega** [βiβiɛga] (vizuri), **bibingĩ** [βiβiŋge] (vingi) na **bibikai** [βiβikai] (vichache).

c) Kip + KiN +Mz

Vivumishi vyenye muundo huu ni vile huambishwa kipatanishi na kiambishi cha ngeli kama viambishi awali katika mzizi wa kivumishi. Mfano wa vivumishi hivi ni kama: **inyanya** [iɲaɲa] (nane), **ũmũthũku** [omoθoku] (mbaya), **ũmwega [**omwɛga] (mzuri), **jũmũkuĩ** [jomokue] (mfupi) na **ũmwirũ** [omwiro] (mweusi).

iii) KA + Mz + I (Kip)

Vivumishi vyenye muundo huu ni vile ambavyo mzizi wa kivumishi huambishwa kipatanishi kama kiambishi awali na irabu ya kipatanishi ikiwa kiambishi tamati. Mifano ni kama **ũjũ** [oɟo] (huyu), **iji** [iɟi] (hizi), **aja** [aɟa] (hapa), **bũbũ** [βoβo] (huu), **ĩjĩ** [eje] (hii), jũjũ [ɟoɟo] (huu) na **jaja** [ɟaɟa] (haya).

Vilevile, utafiti umeonyesha michakato ya kifonolojia inayoathiri vivumishi vya Kiimenti. Kwa ujumla michakato kumi ilibainishwa na sheria zilizodhibiti kila mchakato kuelezwa. Michakato hiyo ni: uyeyushaji, uimarikaji wa fonimu, usilimisho nyuma, udondoshaji wa irabu, udondoshaji na uchopekaji wa irabu, mvutano wa irabu, uwiano wa irabu, udondoshaji wa konsonanti, uchopekaji wa konsonanti na ukaakaishaji. Mchakato wa uradidi na umuhimu wake pia umeelezwa kwa sababu una nafasi muhimu katika muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Imebainika kuwa fonolojia na mofolojia hutagusana ili kukamilisha muundo wa vivumishi vya Kiimenti.

Pia, utafiti ulidhihirisha kuwa vivumishi vya Kiimenti kama tulivyotaja hapo juu huanisha mofu zenye usarufi. Kwa hivyo, vilipochanganuliwa mofimu zifuatazo ziliainishwa. Hizi ni kama zile za ngeli za mofolojia za Kiimenti, ngeli za sintaksia, vipatanishi na idadi (umoja na wingi). Aidha, mofu jenzi, mofu kapa, mzizi na irabu za vipatanishi.

Madhumuni ya tatu yalikuwa kupambanua ruwaza za usarufi katika vivumishi vya Kiimenti.
Usarufi katika vivumishi vya Kiimenti huzingatia ruwaza mahsusi. Kwa hivyo, ruwaza sita zimebainishwa na kuelezwa. Ruwaza hizo zinaweza kuunda sheria mbalimbali za kueleza usarufi katika vivumishi vya Kiimenti.

Madhumuni ya nne yalikuwa kutathmini sheria za mpangilio wa vivumishi katika tungo za Kiimenti. Utafiti huu ulibainisha kuwa vivumishi vya Kiimenti huzingatia mpangilio mahsusi katika tungo za Kiimenti. Kwa hivyo, havipangiliwi kiholela bali mikururo yavyo huzingatia ruwaza fulani. Ruwaza hizo huunda sheria za kijumla za kuongoza mpangilio wa vivumishi vya Kiimenti katika tungo zake.

## 6.3 Mahitimisho

Kulingana na matokeo ya utafiti mahitimisho yafuatayo yanaweza kuelezwa kutegemea madhumuni ya uchunguzi huu. Ilibainika kuwa lahaja ya Kiimenti huwasilisha aina kumi ya vivumishi. Sawa na lugha nyingine lahaja ya Kiimenti huathiriwa na lugha nyingine zinapotagusana. Kwa hivyo, Kiimenti hukopa hata vivumishi kutoka lugha mbalimbali. Vivumishi vingine huingia katika lahaja ya Kiimenti moja kwa moja kulingana na matumizi ya lugha na watu. Hata hivyo, kuna vingine vinavyoingia katika Kiimenti baada ya kuingia katika lugha nyingine kama Kiswahili na kisha Kiimenti. Mfano ni vivumishi vya kigeni kama vya Kiarabu vinavyoingia katika lugha ya Kiswahili na kisha kukopwa na Kiimenti.

Aidha, vivumishi vya Kiimenti huwasilisha muundo mahsusi na vina maumbo yenye usarufi. Baadhi ya usarufi uliojitokeza ni kama idadi, ngeli, udogo na ukubwa, kipatanishi, mzizi, kiishio na usarufi mwingine. Usarufi katika vivumishi husika huzingatia ruwaza maalumu ambayo huweza kuelezwa kupitia sheria za kiisimu. Michakato ya kifonolojia na mofolojia hushirikiana katika kufanikisha muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Kwa hivyo, nadharia ya SGUZ ilfaa sana kueleza hali ya usarufi katika vivumishi husika. Aidha, nadharia ya FZA ilikuwa muhimu kueleza michakato ya kifonolojia inayoathiri muundo wa vivumishi vya Kiimenti. Muundo wa vivumishi vya Kiimenti huathiriwa na ngeli za kimofolojia za Kiimenti ambazo huathiri viambishi awali katika vivumishi husika.

Vivumishi vya Kiimenti vinapotumika katika sentensi huweza kupatikana kwa mkururo. Mkururo wa vivumishi hautokei kiholela bali vivumishi huzingatia mpangilio fulani.

Mipangilio tofauti ya vivumishi huunda ruwaza za mbalimbali ambazo huweza kuandikwa sheria za kijumla.

